"Katika hali hii naweza kukithibitisha kwa kiwango cha juu kitabu kipya cha Dk. Thomas Schirrmacher. Kinaweka mambo wazi na kwa mantiki juu ya maswali mengi hata ambayo watu wanaojichukulia kuwa si watu wa dini, sasa wanauliza. Kinaweza kusomwa vizuri na Biblia ikiwa imefunguliwa na baadhi ya magazeti ya kila siku. Kitaweza kutoa mambo mapya ya kushangaza juu ya inamaanisha nini kuishi katika "kipindi kama hiki."

(Kutoka katika Dibaji ya Mhashamu Mch. Johan Candelin, Mkurugenzi wa Kamisheni ya Uhuru wa Kuabudu ya Muungano wa Kiinjili Ulimwenguni)

Mateso huja kwa njia nyingi lakini moja ya tunachoambiwa na Maandiko ni kuwa Wakristo wategemee mateso yatokanayo na imani. Kama funzo la Theolojia la Thomas Schirrmacher litakavyoonesha, Biblia ina mambo mengi ya kutufundisha kuhusu mateso. Bila uelewa wa Biblia kuna uwezekano wa kutoelewa asili ya vita vya kiroho, wala ina maana gani kuwa kondoo miongoni mwa mbwa mwitu na wakati huo huo kuwa nyoka mwerevu na kama hua. Maajabu ya teknolojia yameniwezesha mimi kufanya kazi na Thomas Schirrmacher juu ya mambo ya uhuru wa Kidini katika mazingira ya Ulaya na chini ya mwavuli wa Tume ya Uhuru wa kidini ya Ushirika wa Kiinjili Ulimwenguni. Mawasiliano ya kielektroniki yanaliwezesha kanisa la kiulimwengu kushirikishana taarifa, kutoa ushauri na kuzungumza kwa sauti ya umoja kwa niaba ya Wakristo wanaoteseka, lakini kama tungejua namna ya kuomba, kuongea na kutenda, tunapaswa kutegemea Maandiko. Hivyo basi ninafurahi kuwa kitabu hiki kinaweka katikati mafundisho ya Biblia juu ya mateso.

(Kutoka katika Dibaji ya Julia Doxat-purser, Mwakilishi wa Siasa-jamii na Mratibu wa Uhuru wa Kuabudu wa Muungano wa Kiinjili wa Ulaya).

Thomas Schirrmacher alipata Shahada ya Udaktari (Uzamivu) katika Umisheni mwaka 1985 (Dr. theol.), katika Cultural Anthropology mwaka 1989 (PhD), na katika Elimu ya Maadili(Ethics) mwaka 1996 (ThD). Alitunukiwa Shahada ya heshima mwaka 1997 (DD). Ni Profesa wa Maadili, Misheni na Maendeleo ya Kimataifa katika Vyuo Vikuu na Seminari mbalimbali huko Marekani, Ujerumani, Africa Kusini na India na ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Martin Bucer Seminari huko Bonn Ujerumani. Ni Katibu wa Tume ya Uhuru wa Kidini ya Tume ya Shirikisho la Kiinjili la Ujerumani na Mwanachama wa Shirikisho la Kiinjili Ulimwenguni na Mwenyekiti ya Bodi ya Wadhamini ya Mikono Itoayo (Giving Hands) gGmbH, ambayo ni taasisi ya kimataifa yenye miradi katika maeneo yenye majanga ambapo haki za binadamu zinakiukwa.

ISBN 9976 906 97 X
ISBN 978-3-928936-62-0

inland press
Email: inlandpress@yahoo.com

Toleo la Kiswahili 2008
Schirrmacher Mateso ya Wakristo Toleo la Kiswahili 2008
Toleo la Kiswahili 2008

Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote

Thomas Schirrmacher

Kuelekea Theolojia ya Mauaji wa Mashahidi wa Imani

Juzuu 70 za Kibiblia na Kitheolojia zilizoandikwa kwa ajili ya Shirikisho la Kiinjili la Ujerumani na Tume ya Uhuru wa Kidini

Dibaji imeandikwa na John Candelin, Shirikisho la Kiinjili la Ulimwengu, na Julia Doxat-Purser, Shirikisho la Kiinjili la Ulaya

Thomas Schirrmacher

Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote

RVB International

1	Thomas Schirrmacher:	GOD Wants You to Learn Labor and Love
2	Thomas Schirrmacher:	Legends About the Galileo-Affair
3	Thomas Schirrmacher:	World Mission – Heart of Christianity
4	Thomas Schirrmacher:	Law or Spirit – an alternative View of Galatians
5	Thomas Schirrmacher:	Human Rights Threatened in Europe
6	Thomas Schirrmacher:	Be keen to get going – William Carey's Theology
7	Thomas Schirrmacher:	Love is the Fulfillment of the Law
8	Thomas Schirrmacher:	Studies in Church Leadership
9	Monte Wilson:	The Most Important Rule for Living
10	Monte Wilson:	Principles of Success in Business
11	Th. Schirrmacher (Ed.):	A Life of Transformation – From Politician to Good Samaritan – A Festschrift for Colonel Doner
12	Thomas Schirrmacher	DIOS Quiere Que tu Aprendas, Trabajes y Ames
13	Christine Schirrmacher	La Vision Islamica de Importantes Enseñanzas Cristianas
14	Thomas Schirrmacher	Sheria au Roho
15	Thomas Schirrmacher	Upendo ni Utimilifu wa Sheria
16	Thomas Schirrmacher	Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote
17	Monte Wilson	Sheria Muhimu Zaidi katika Kuishi

Thomas Schirrmacher

Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote

Kuelekea Theolojia ya Mashahidi wa Imani

Kimetafsiriwa na Joseph SM Ipimilo

RVB
International

Die Deutsche Bibliothek – CIP

Bibliografische Information Der Deutschen Bibliothek

Die Deutsche Bibliothek verzeichnet diese Publikation in der Deutschen Nationalbibliografie; detaillierte bibliografische Daten sind im Internet über http://dnb.ddb.de abrufbar.

Bibliographic information published by Die Deutsche Bibliothek

Die Deutsche Bibliothek lists this publication in the Deutsche Nationalbibliografie; detailed bibliographic data are available in the Internet at http://dnb.ddb.de

ISBN 978-3-928936-62-0

© Copyright 2001, 2008 by
Reformatorischer Verlag Beese
www.rvbeese.de / info@rvbeese.de
Printed in Germany

ISBN 9976 906 93 5

© Kwa Toleo la Kiswahili, 2008
2nd edition 2009
Trans-Africa Swahili Christian Ministries
P.O. Box 772, Mwanza, Tanzania
Toleo la Kwanza, 2008 Nakala 2,500

Kimetolewa na Inland Publishers, S.L.P. 125, Mwanza, Tanzania
E-mail: ipublishers@hotmail.com

Toleo Asilia: The Persecutions of Christians Concerns Us All – Towards a Theology of Martyrdom, VKW, Bonn, 2001, ISBN 3-932829-41-7.

Maandiko Matakatifu: The Holy Bible in Kiswahili Union Version, 1994

Mistari ya Biblia iliyokolezwa ni tafsiri ya mwandishi mwenyewe kutoka katika Maandiko Matakatifu asilia ya Kigriki.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kurudufu au kutoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini ya VKW International na Trans-Africa Swahili Christian Ministries, Idara ya Maandiko.

Kimepigwa Chapa na: Inland Press, P.O. Box 125, Mwanza, Tanzania (East Africa) TEL. +255 28 2560175 inlandpress@yahoo.com

Tabaruku kwa

Peter Beyerhaus

kwa ushiriki wake wa muda mrefu kwa ajili ya kanisa linaloteswa

Yaliyomo

Yaliyomo 7

Mizizi ya Kikristo ya Haki za Binadamu; Dibaji na Mhashamu Mch. Johan Candelin 11

Dibaji na Julia Doxat-Purser, Mwakilishi wa Siasa-jamii na Mratibu wa Uhuru wa Kidini kwa Muungano wa Kiinjili wa Ulaya 11

Dibaji na Mch. Rudolf Westerheide, Muungano wa Kiinjili kwa Ulaya na Ujerumani 12

A. Hali ya Sasa 15

1. Sababu za Mchango Huu 15
2. Theolojia ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani 21
3. Makundi Makubwa ya Wakristo Yamekuwa Yakiteswa 24
4. Theolojia ya Kanisa la Kwanza ilighushiwa na Mauaji ya Mashahidi wa Imani 25
5. Suala la Mateso ya Wakristo Halikomei Tu kwa Kanisa la Kwanza 26
6. Sababu Zenye Sura Mbalimbali za Mateso 29
7. Shahidi wa Imani ni Nani? 29

B. Dhamira Muhimu ya Kibiblia 30

8. Maandiko Yamechukuliwa Nje ya Mazingira na Kudunishwa 30
9. Sehemu kubwa ya Maandiko hujishughulisha na Mateso 31
10. Msaada Katika Ufunuo 34
11. Ukosoaji wa Kihistoria na Matatizo Yake kwa Vifungu vya Mashahidi wa Imani katika Agano Jipya 35
12. Mwanadamu wa Kwanza Kufa Alikuwa Shahidi wa Imani 36
13. Manabii wa Agano la Kale Waliteswa 37
14. Watu wa Mungu Huwatesa Watu wa Mungu 40
15. Wakristo Pia Huwatesa Wakristo Wenzao Pamoja na Wengine 41
16. Mateso ni Suala la Kanisa la Kikristo Kiulimwengu (Kiekumenika) 44
17. Shahidi wa Imani wa Kwanza Aliye Mkristo 45

C. Kuzungumuza juu ya Kristo ni Kuzungumuza juu ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani 46

18. Yesu ni Kielelezo cha Shahidi wa Imani 46
19. Kufa kwa Ajili ya Marafiki ni Hali ya Juu Kabisa ya Upendo 47
20. Kwa Uhalisia, Mateso Yote Huelekezwa kwa Yesu 47
21. Mwendelezo wa Mateso ya Kristo 47
22. Yesu kama Kielelezo cha Kuigwa - Mashahidi wa Imani kama Vielelezo vya Kuigwa 48
23. Theolojia ya Msalaba ('theolojia crucis') 49

D. Kanisa chini ya Mateso 51

24. Hakuna Kanisa bila Mauaji ya Mashahidi wa Imani 51
25. Chuki Dhidi ya Mungu 52
26. Chuki ya Ulimwengu kwa Mungu ina Asili Katika Chuki ya Shetani 52
27. Roho Mtakatifu - Faraja Katika Mateso 54
28. Furaha katika Mateso 56
29. Kumtumaini Mungu Pekee 56

E. Tabia Chini ya Mateso 57

30. Kamwe Usipanie Mateso 57
31. Ni Halali Kukimbia Mateso 59
32. Si Mateso Yote ni kwa Ajili ya Kristo 61
33. Msaada kwa Wadhaifu 61
34. Kuomba kwa Ajili ya Mtesaji 63
35. Wauaji Huwa Waamini 64

F. Umisheni na Mauaji ya Mashahidi wa Imani 64

36. Matunda ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani 64
37. Matunda si Kitu cha Kuja Chenyewe Tu 67
38. Mauaji ya Mashahidi wa Imani Huambatana na Umishenari wa Ulimwengu 68
39. Shahidi wa Imani kama "Shahidi"; Ushuhuda wa Mashahidi wa Imani 69

40. Ushindi na Kushindwa kwa Manabii Vyote Huenda pamoja 74
41. Udhaifu wa Mkristo ni Nguvu Zake 75
42. Kufunuliwa kwa Wana wa Mungu 75
43. Kilio kwa Ajili ya Haki 76
44. Kwa Nini Wasio na Mungu Hufanikiwa Sana? 77

G. Dhidi ya Dini ya Mafanikio 78
45. Ukristo si Dini ya Mafanikio (Warumi 5:1-5) 78
46. Theolojia ya Injili ya Utajiri na Afya ni ya Kuhojiwa 79
47. Kujikana na Kuteseka 80
48. Pigana Vita Vizuri vya Imani 80
49. Mauaji ya Mashahidi wa Imani ni Upinzani Dhidi ya Mashambulizi ya Roho 81
50. Tamasha Mbele ya Ulimwengu Usioonekana 81
51. Maono ya Makao Mbinguni 81
52. Maandiko Hayaweki Mpaka Kuwa Mateso Lazima Yatokee katika 'Siku za Mwisho' Tu 83

H. Serikali na Mateso 84
53. Kuna Aina Nyingi za Mateso 84
54. Istilahi ya Mashahidi wa Imani Haipaswi Kutumiwa Vibaya Kisiasa 85
55. Dhidi ya Ukamilifu wa Mamlaka 86
56. Raia Waaminifu 87
57. Kuomba kwa Ajili ya Maisha ya Amani 89
58. Kupinga Serikali 90
59. Mateso ya Wakristo Yanaweza Kukua kuwa Mauaji ya Kimbari 93
60. Mateso ya Wakristo Mara Nyingi Yamekuwa Sehemu ya Mauaji ya Halaiki 93
61. Mateso ya Wakristo chini ya Ujamaa wa Kitaifa 94

I. Huruma ya Kivitendo 96
62. Wakati Mmoja Anapoteseka... 96
63. Kujipenyeza kwa Mwili wa Kristo kwa Ajili ya Mashahidi Wake wa Imani Hufunua Hali Yake Wenyewe 98

64. Ushirika ni Sehemu Halisi ya Kukumbuka Waamini Wanaoteseka 98
65. Kuwakumbuka Mashahidi wa Imani Katika Ibada 98
66. Elimu juu ya Mateso 101
67. Tunahitaji Wakiri Imani 101
68. Ustahimilivu ni Muhimu 102
69. Muundo wa Kanisa na Mateso 102
70. Tunahitaji Mawazo Yenye Uhalisia 102
Kiambatanisho 1. Haki za Binadamu na Imani ya Kikristo 105
Kiambatanisho 2. Imani ni Haki ya Binadamu 113
Vitabu vya Rejea juu ya Mateso ya Wakristo 118

Anuani za Mtandao 151

Tume ya Uhuru wa Kidini 152

Mizizi ya Kikristo ya Haki za Binadamu

Dibaji na Mhashamu Mch. Johan Candelin, Mkurugenzi wa Tume ya Uhuru wa Kidini ya Muungano wa Kiinjili Ulimwenguni

Kuna hadithi inayozungumzwa juu ya Profesa Albert Einstein. Aliandaa maswali kwa baadhi ya wanafunzi pale ambapo katibu muhtasi wake alisema: "Lakini, Profesa, haya ni maswali yale yale uliyoyatoa kipindi kilichopita", "Najua! Alisema Einstein, "Lakini nimebadilisha majibu!" Tunaishi katika kipindi ambapo majibu ni mapya kwa maswali ya zamani. Dunia si sawa kama ilivyokuwa miaka kadhaa iliyopita. Wakati ule ule baadhi ya maswali na majibu hayabadiliki. Tunapaswa kujua yapi yamebadilika na yapi bado.Tunapaswa kufanya hivi katika ulimwengu tunamoishi ambao unakanganya ambamo kuna mvutano kati ya sera za kigeni, utandawazi na dini ambazo zinabeba mapya juu ya dini hasa Uislamu na uhusiano wake na Ukristo. Tunahitaji kulinda uhuru kwa ajili ya Waislamu waliopo Magharibi lakini pia kulinda uhuru wa Wakristo katika Ulimwengu wa Kiislamu. Mara zote wanajisikia wamesahauliwa na sisi.

Katika hali hii naweza kuthibitisha kwa kiwango cha juu kitabu kipya cha Dk. Thomas Schirrmacher. Kinaweka mambo wazi na kwa mantiki katika maswali mengi yanayoulizwa sasa hata na watu wanaojichukulia kuwa si watu wa dini. Kinaweza kusomwa vizuri na Biblia ikiwa wazi na baadhi ya magazeti ya kila siku. Kitaweza kutoa mambo mapya ya kushangaza juu ya inamaanisha nini kuishi katika "kipindi kama hiki."

Dibaji na Julia Doxat-Purser, Mwakilishi wa Siasa-jamii na Mratibu wa Uhuru wa Kidini kwa Muungano wa Kiinjili wa Ulaya

Wakristo wana ndugu zao wa kike na kiume kutoka kila utamaduni. Kuwa ndani ya familia kunaleta wajibu. Biblia inaweka wazi sehemu nyingi kuwa Kanisa linapaswa kuungana, kutenda kama mwili mmoja na mwingine na kusimama katika mshikamano pale mateso yanapokuja huja kama sehemu ya muhimu ya mambo awapayo Mungu watoto wake.

Mateso huja kwa njia nyingi lakini moja tunachoambiwa na Maandiko ni kuwa Wakristo wategemee mateso yatokanayo na imani. Kama funzo la Theolojia la Thomas Schirrmacher litakavyoonesha, Biblia ina mambo mengi ya kutufundisha kuhusu mateso. Bila uelewa wa Biblia kuna uwezekano wa kutoelewa asili ya vita vya kiroho, wala ina maana gani kuwa kondoo miongoni mwa mbwa mwitu na wakati huo huo kuwa nyoka mwerevu na kama hua.

Kama mratibu wa uhuru wa kuabudu wa Ushirika wa Kiinjili wa Ulaya ni bahati njema ya kufanya kazi na Wakristo Ulaya yote. Wengine wanajua ukweli wa mateso katika hatua ya kukutana nayo. Wengine kama mimi tuna ufahamu

usio wa moja kwa kwa moja. Lakini tunaweza kujifunza toka mmoja hadi mwingine. Na kwa pamoja, tunaweza kuleta tofauti kwa kanisa lililo katika mateso wakati tunapoomba, kutoa msaada wa vitendo na kupaza sauti kwa niaba ya wale wasio na sauti mbele za umma. Kwa sasa Wakristo wengi wa Ulaya wanafaidi nafasi ya kupumzika, pale inapokuja kwenye mateso makubwa. Hii haimaanishi hata hivyo kuwa hatupaswi kuwa na busara na hadhari pale inapotupasa kujibu maelezo ya mashinikizo ambayo yangeweza kuishia kuzuia kanisa kushuhudia kama linavyopaswa kufanya. Kama raia wa nchi ambamo tuko huru kujadiliana na viongozi wa kisiasa, tunao wajibu maalumu kuwa mawakili wa Wakristo wanaoteseka wanaoishi chini ya aina fulani mbalimbali za kisiasa.

Maajabu ya teknolojia yameniwezesha mimi kufanya kazi na Thomas Schirrmacher juu ya mambo ya uhuru wa kidini katika mazingira ya Ulaya na chini ya mwavuli wa Tume ya Uhuru wa kidini ya Ushirika wa Kiinjili Ulimwenguni. Mawasiliano ya kielektroniki yanaliwezesha kanisa la kiulimwengu kushirikishana taarifa, kutoa ushauri na kuzungumuza kwa sauti ya umoja kwa niaba ya Wakristo wanaoteseka, lakini kama tungejua namna ya kuomba, kuongea na kutenda, tunapaswa kutegemea Maandiko. Hivyo basi ninafurahi kuwa kitabu hiki kinaweka katikati mafundisho ya Biblia juu ya mateso.

Dibaji na Mch. Rudolf Westerheid, wa Muungano wa Kiinjili wa Ujerumani na Ulaya

Ni miaka michache iliyopita, taarifa kuhusu Wakristo wanaoteseka zilionekana siyo kweli. Tulishituliwa na maelezo ya ukatili usiofikirika uliokuwa ukifanywa magerezani na kwenye kambi za mateso – maeneo ya mbali huko Siberia, labda – lakini kwa ujumla ilikuwa sawa na maelezo ya Ulimwengu wa kigeni. Taarifa za Mashahidi wa imani na uvumilivu wao chini ya mateso ya kutisha zimetuvuta – na hasa kwa sababu zimetukumbusha tofauti zetu.

Kufuatia kuanguka kwa Pazia la Chuma*, hali imebadilika kwa namna mbili. Kwa upande mmoja, sehemu kubwa ya Kambi ya Mashariki ya hapo awali wanafurahia uhuru wa kidini – Bwana asifiwe! Kwa upande mwingine, uwezekano mpya wa kusafiri unatupa nafasi ya kukutana na waumini waliopitia kambi za mateso. Katika mikutano ya kimataifa ya Muungano wa Kiinjili, Wakristo vijana matajiri kutoka Ujerumani walikaa kando ya Wakristo wazee toka Rumania ambao wametumikia kifungo jela kwa miaka kwa sababu ya imani zao. Mateso ya wateswao yanachukua nafasi na huwa ndiyo uhalisia na uelewa mzuri kuwa watu hawa waume kwa wake waliojithibitisha wenyewe katika moto bado wako katika hatari kwa udhaifu na ubatili wa mwanadamu.

Wakati ule ule tunapaswa kukabiliana na ukweli kuwa, vitisho vya uvumilivu wa kidini na kitaifa dhidi ya Wakristo imekuwa sehemu ya uhalisia wa Ulaya. Katika nchi iliyo mapumzikoni ya Ugiriki, msimamo wa kimishenari wa waumini wa Kiinjili umewafanya kukabiliana na mamlaka na inaweza kuwafanya wahanga wa matatizo kazini na vifungo. Uzoefu wa waumini wenzetu wa Kituruki

unatukumbusha kuwa ugandamizaji wa nguvu wa Kiislamu tayari umefika Ulaya.

Hali hii mpya imechanganywa na hadithi za vitisho toka sehemu zingine za dunia, haikwepeki inatulazimisha kukabiliana na suala la mateso ya Wakristo. Tunatambua kuwa wale wanaoteseka kwa ajili ya imani yao siyo wengine bali ni mwili wa Kristo. Tunahusika pale ambapo wanawake wanauzwa Sudani - hatuwezi kukwepa wajibu wa kubeba mzigo katika maombi na dua kwa Mungu awalinde katika namna ya pekee. Kwa wakati ule ule tunapaswa kutambua ukweli wa uonevu na mateso kama kipengele awali cha uwepo wa Ukristo na kukubali kuwa uhuru wetu kamili ni wa kipekee katika kanuni hiyo.

Tume ya Muungano wa Kiinjili wa Ujerumani imejikita kwa kazi hii ya maandalizi ya Siku ya Maombi kwa ajili ya Kanisa lililo katika mateso. Ni hivi karibuni imegundulika kuwa kujulikana kwa ukweli ilikuwa haitoshi; kuwa tunahitaji mtizamo mpya wa Kibiblia – kitheolojia na kikanisa wa somo la Profesa, Dk. thomas Schirrmacher, Rais wa Martin Bucer Seminary huko Bonn, anatuletea somo lifuatalo. Kimsingi na kihistoria, mateso ya Wakristo ni dhamira za kimsingi zaidi katika Muungano wa Kiinjili. Pamoja na uwasilishaji nyaraka hizi, tungependa hasa waumini wa Kiinjili kulichukulia suala hili kwa undani na hadhari.

Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote

Kuelekea Theolojia ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani

Juzuu 70 za Kibiblia na Kitheolojia zilizoandikwa kwa ajili ya Muungano wa Kiinjili wa Ujerumani na Tume Yake ya Uhuru wa Kidini

A. Hali ya Sasa

1. Sababu ya Mchango Huu

Sehemu ya Kanisa ambayo haimo katika mateso haiwezi kupuuza idadi kubwa ya Wakristo waliomo katika mateso makali na hata kitisho cha kifo, bali ni lazima ichukue hatua kwa kuwa "Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho ..." (1 Kor. 12:26). Tunapaswa kuomba, kutoa, kutubu na kuhamasisha vyombo vya habari na wanasiasa kuhusika kikamilifu katika suala hili. Katika kufanya hivyo tunatii amri ya Biblia, "Wakumbukeni hao waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao; na hao wanaodhulumiwa, kwa vile ninyi nanyi mlivyo katika mwili" (Waebrania 13:3).

Kanisa lilitokea katika mateso kipindi cha Agano Jipya na kuendeleza theolojia yake ya awali chini ya mbinyo wa mateso na manyanyaso. Kurasa zifuatazo zinataka kudhihirisha kwamba mauaji ya mashahidi wa imani sio matokeo yenye kusumbua ya Ukristo, bali ni chembe muhimu ya imani ya Agano la Kale, ya Agano Jipya, ya Kiyahudi na ya Kanisa la Mwanzo. Wakati ule ule, tutaona kwamba juhudi za kujitoa kusaidia Wakristo wanaoteswa haziwezi kuachwa kwa wakereketwa wachache, bali kwa kufuatana na Agano Jipya, ni wajibu wa msingi wa Kanisa la Kikristo.

Kanisa Katoliki hapa Ujerumani lilifanya siku za maombi ya kitaifa kwa ajili ya kanisa lililoteswa tangu 1977 hadi 1994,[1] lakini limeachana na mpango huo

---

1 Tazama; Christen unter dem Kreuz. Arbeitshilfen 8. Sekretariat der Deutschen Bischofskonferenz: Bonn, 1976; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche. Arbeitshilfen 13. Ibid. 1980; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1984. Arbeitshilfen 35. Ibid, 1984; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1985. Arbeitshilfen 38. Ibid. 1985; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1986. Arbeitshilfen 43. Ibid., 1986; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1987. Arbeitshilfen 49. Ibid., 1987; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1988. Arbeitshilfen 58. Ibid., 1988; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1989. Arbeitshilfen 63. Ibid. 1989; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1990. Arbeitshilfen 78. Ibid. 1990; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1991. Arbeitshilfen 85. Ibid. 1991; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1992. Arbeitshilfen 99. Ibid., 1992; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1993: China. Arbeitshilfen 105. Ibid. 1993; Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1994. Arbeitshilfen 119. Ibid. 1994. See also the article "Gebetstag fuer die verfolgte Kirche - Grundsaetzliche UEberlegungen". p. 7-14 in: Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1993: China. op. cit.

baada ya kuvunjika kwa Ukomunisti,[2] yawezekana ni kutokana na kukosekana kwa msukumo ambao ulichochewa na huruma ya wale ambao hawakuupenda Ukomunisti na hata miongoni mwa wale wa Kiinjili. Mateso katika baadhi ya nchi yamekuwa hayatiliwi maanani,[3] na hivyo Wakristo wengi wa Magharibi hawafahamu kabisa kuwa waumini wenzao wengi wakiwemo wale wanaoathirika na mateso hawaishi 'Mashariki' au 'Magharibi' bali katika nchi za Dunia ya Tatu. Shirikisho la Kiinjili la Ujerumani na Uswisi limeuchukua mradi kwa maeneo yanayozungumza Kijerumani[4] katika mwaka 1998, pale walipoichukua 'Siku ya Kimataifa ya Maombi kwa Kanisa Linaloteswa', ambayo ilianzishwa na Ushirika wa Kiinjili wa Ulimwengu[5] katika mwaka 1996.[6] Ujumbe wa dunia nzima unaandikwa kwa Kijerumani, na ulisomwa katika Ibada Kuu ya Maombi ya Kimataifa huko Stuttgart. Siku ya Maombi ya Kidunia imeidhinishwa na kuungwa mkono na Bunge la Marekani[7] na makanisa mengi ya Marekani na mengi kati ya hayo siyo ya Kiinjili. Shirikisho la Kiinjili liliundwa mwaka 1846

---

2 Hoja muhimu za maamuzi kwa ajili ya uamuzi wa Tume ya Kusimamia zilikuwa ni mfano wa kuanguka kwa serikali zilizowatesa Wakristo katika nchi za awali za Kikomunisti, na ugumu wa kutafuta na kuwasilisha mfano wa nchi kwa ajili ya Siku ya Maombi, pasipo kupoteza matakwa ya waaminifu kupitia kuchoka." (P. Gerhard Mockenhaupt MSF, Zentralstelle Weltkirche der Deutschen Bischofskonferenz: mwenyekiti, kwa Thomas Schirrmacher, Nov.11,1999).

3 Paul A. Marshall. Their Blood Cries out. op. cit., p. 72.

4 (Thomas Schirrmacher, Rudolf Westerheide). Weltweiter Gebetstag fuer verfolgte Christen. Deutsche Evangelische Allianz: Stuttgart, 1998. 12. p.; (Thomas Schirrmacher, Rudolf Westerheide). Weltweiter Gebetstag fuer verfolgte Christen. Ibid. 1999. 12. p. Vifungu hivi vyaweza pia kupatikana katika katika wovuti www.ead.de/gebet/weitere/verfolgte.htm na www.each.ch/veranst.htm#verfolgte na www.worldevangelical/idop/contents.htm

5 WEF ni "Taasisi isiyo ya kiserikali yenye hadhi maalum ya ushauri kwa kushirikiana na Baraza la Kijamii na Uchumi la Umoja wa Mataifa (Economic and Social Council of the United Nations)".

6 Kwa ajili ya usuli*, tazama; Nina Shea. In The Lion's Den. op. cit., pp. 8-9+87-88. Uanzilishi wa Siku ya Maombi ulitoka kwa Ushirika wa Kitaifa wa Kiinjili (National Association of Evangelicals) (Ibid., p. S. 9-10), ambao tamko lake la 1996 lilichukuliwa rasmi kwa uduni na makanisa ya Kiinjili na kikamilifu na makanisa ya 'kiliberali', kama vile Southern Baptist Convention, the Episcopal Church, United Methodist Church and the United Presbyterian Church (USA) (tazama kumbukumbu hapo juu, Ibid., pp. 103-110).

7 Senate Resolution Sept. 17, 1996 na House Resolution Sept 24, 1996. Toleo lilirudiwa tena katika Nina Shea. In The Lion's Den. op. cit., pp. 111-116, (kipekee pp.113+112) Tazama pia Paul A. Marshall. Their Blood Cries out. op. cit., p. 230. Serikali ya Marekani kwa kina imekuwa ikijihusisha juu ya mambo yanayodhalilisha uhuru wa kidini. (Tazama 'United States' katika vitabu teule vya rejea). Hata hivyo, Chuck Colson, katika "Utangulizi" wake pp. ix-xii katika: Nina Shea. In The Lion's Den: A Shocking Account of Persecution and Martyrdom of Christians Today and How We Should Respond. Broadman & Holman: Nashville (TN), 1997 anapinga kwamba Serikali ya Marekani na Balozi za Marekani ghafla huwa kimya, wakati wakimbizi wanapoomba uhifadhi kutokana na sababu za kidini, kamauifanyavyo umma wa kisekyula, ambao mara nyingine hujishughulisha na haki za binadamu! (Tazama pia Paul A. Marshall. Their Blood Cries out. op. cit., pp. 181-209).

huko London ili kupanda na kudai haki ya uhuru wa kidini,[8] kwa wafuasi wa imani zingine na vikundi vya Kikristo.[9] Somo langu linaendeleza utamaduni huu.

Kutokana na hisia zilizo vigumu kuthibitishwa za David Barrett, katika mwaka 1970 takribani Wakristo 230,000 wa madhehebu yote walikufa kutokana na imani zao, katika mwaka 1988 takribani 300,000. Hata hivyo, utabiri wa ongezeko zaidi la idadi limethibitishwa kuwa na makosa.[10] Ni takribani mashahidi wa imani 164,000 'tu' walikufa katika mwaka 1999.[11] Ukizingatia kuwa idadi ya watu duniani imeongezeka toka mwaka 1970 hata leo kutoka bilioni 3.7 hadi bilioni 6, idadi ya mashahidi wa imani waliouawa imepungua si tu katika maneno ya jumla bali imepungua sana kwa uwiano.[12] Juu ya yote maendeleo haya yanatokana na kuanguka kwa Ukomunisti wa kimataifa na kuanguka kwa madikteta wengi.[13] Hata hivyo, idadi ya mashahidi wa imani wanaouawa inaongezeka tena; kila mwaka ikiwa ni matokeo ya kupanuka kwa Waislamu wanasili* kukua kwa Uhindu wa kisiasa na kuibuka kwa udikteta mpya

---

8 Tazama; Christoph Johannes Riggenbach (Ed.). Siebente Hauptversammlung der Evangelischen Allianz gehalten in Basel ... 1879: Berichte und Reden. Vol. 2. Bahnmaier's Verlag/H. Georg: Basel, 1880. pp. 999-1004. Werner Beyer. Einheit in der Vielfalt: Aus 150 Jahren Evangelischer Allianz. R. Brockhaus: Wuppertal, 1995 anamtaja mjumbe aliyetumwa kwa Mfalme wa Prussia ili kupinga adhabu ya kifo kwa Waturuki walioamini (kr. 45-46) na pia dhidi ya adhabu za kitumwa kwa Waprotestanti wa Kihispania (kr. 78-80).

9 Tazama; Christoph Johannes Riggenbach (Ed.). *Siebente Hauptversammlung der Evangelischen Allianz gehalten in Basel ... 1879*: Berichte und Reden. Vol. 2. Bahnmaier's Verlag/H. Georg: Basel, 1880. pp. 999-1004. Werner Beyer. *Einheit in der Vielfalt: Aus 150 Jahren Evangelischer Allianz.* R. Brockhaus: Wuppertal, 1995 anamtaja mjumbe aliyetumwa kwa Mfalme wa Prussia ili kupinga adhabu ya kifo kwa Waturuki walioamini (kr. 45-46) na pia dhidi ya adhabu za kitumwa kwa Waprotestanti wa Kihispania (kr. 78-80).

10 Tazama maandiko yaliyoorodhesha katika: Thomas Schirrmacher. *Theodor Christlieb und seine Missionstheologie*, Telos – Evangelikale Theologie. EgfD: Wuppertal: 1985, kk. 49 kk na 108 kk.

11 Idadi kubwa ya kidunia kwa takwimu za kanisa na misheni, zikijumuisha idadi ya mashahidi wa imani, imekuwa ikichunguzwa kila mwaka na David B. Barrett na Todd M. Johnson, Taarifa ya mwisho; David B. Barrett, Todd M. Johnson. "Annual Statistical Table on Global Mission: 1999". International Bulletin of Missionary Research 23 (1999) 1 (Jan): 24-25, pia ilichapwa katika World Evangelization (Lausanne Committee) Aprili 1999. The International Bulletin of Missionary Research ni gazeti la kikanisa chini ya uongozi wa Kikatoliki, na hivyo haliakisi mtazamo wa kichunguzi wa Kiinjili pekee. Idadi hiyo pia hujumuisha waamini waliouawa katika mazingira yanayoweza kusemwa kuwa ya kisiasa, kwa mfano kati ya Waislamu na Wakristo huko Sudan.

12 Bong Rin Ro (Ed.). Christian Suffering in Asia. *op. cit.* na David B. Barrett. Our Globe and How to Reach it. New Hope: Birmingham (AL), 1990. uk. 18. Tangu Kusulubiwa kwa Yesu hadi mnamo 1990, takribani Wakristo 40,725,000 ni mashahidi wa imani waliouawa. Kwa sasa idadi inakaribia 43,100,000.

13 Cuba, China, Vietnam na Korea ya Kaskazini bado zinabaki kuwa serikali za Kikomunisti zinazotesa Wakristo. Tazama: Paul A. Marshall. Their Blood Cries out. *ob. cit.,* uk. . 71-96. Paul Marshall. "Persecution of Christians in the Contemporary World". International Bulletin of Missionary Research 22 (1998) 1 (Jan): 2-8, uk. 3 anaonesha kuwa robo ya idadi ya watu wote duniani huishi katika nchi za Kikomunisti za Asia.

barani Afrika, Wakristo 3,000 zaidi wanakufa kwa ajili ya imani yao kuliko mwaka uliopita.[14]

Jinsi kupungua kunavyoridhisha, nani anaweza kufurahia juu ya mashahidi wa imani 164,000 wanaouawa? Mia moja na arobaini na sita elfu! Na idadi hii haijumuishi wahanga wanaobaki hai. Ni Wakristo wangapi duniani wameteswa, wamebughudhiwa au wametiwa kifungoni? Hatufahamu. Tena hatuna habari za kutosha hata kwa wale waliohimili maudhi makubwa kutoka kwa wenye mamlaka, kwa mfano, ambao hufunga makanisa au huwanyima vijana wa Kikristo elimu ya juu. Na vipi kuhusu wale wa imani nyingine, wanadamu pia walioumbwa kwa mfano wa Mungu? Wengi lazima wafe kwa kile wanachokiamini.

Dokezo la ziada (2001): Idadi ya Mashahidi wa Imani

Idadi na takwimu za dunia nzima juu ya kanisa na umisheni, zikijumuisha idadi ya mashahidi wa imani, zinakusanywa kila mwaka na David B. Barret na Todd M. Johnson. Takwimu za hivi karibuni kabisa zilionekana katika; David B. Barret na Todd M. Johnson, "Jedwali la Takwimu za Mwaka juu ya Umisheni wa Ulimwengu" (Annual Statistical Table on Global Mission)".International Bulletin of Missionary Research (Jarida la Kimataifa la Utafiti wa Umishenari) 23 (1999) 1 (Jan): 24-25 [164,000]; 24 (2000) 1 (Jan): 24-25 [165,000]; 25 (2001) 1 (Jan): 24-25 [167,000] na katika toleo la Aprili la World Evangelization (Uinjilishaji wa Kiulimwengu) (Lausane Committee/Tume ya Laussane) la kila mwaka. Kama Jarida la Kimataifa la Utafiti wa Umishenari lililo la taasisi ya kiekumenika chini ya uongozi wa Kikatoliki, linaakisi mitizamo mingine kuliko ile ya tafiti za kiinjili na hivyo linajumuisha Wakristowa majina na waamini wanaokufa chini ya unyanyasaji wa kisiasa au katika vitavya kikabila, kama ilivyo katika Sudani.

14 Taarifa za mwisho juu ya uhuru wa kidini uliwenguni pote zilifanywa na Paul A. Marshall (Hg.). Religous Freedom in the World: A Global Report on Freedom and Persecution. Broadman & Holman Publ.: Nashville (TN), 2000 [Tazama pia Paul Marshall. "The Current State of Religious Freedom". International Bulletin of Missionary Research 25 (2001) 2: 64-66] na Kevin Boyle, Juliet Sheen (Ed.). *Freedom for Religion and Belief: A World Report*. Rouledge: London/New York, 1997; kwa ajili ya nchi zilizochaguliwa katika Ushirika wa Kiinjili Duniani (World Evangelical Fellowship). The Geneva Report 2001. Religious Liberty Commission: Kokkola (Finland) & Geneva, 2001. 24 S. (auch unter www.advocatesinternational.org/geneva_report.htm) and Freedom of Religion: Taarifa yenye msisitizo wa kipekee juu ya Haki ya Kuchagua Dini na Mifumo ya Usajili. Forum 18: Oslo, 2001 (auch zum Downloaden unter www.normis.no, dann unten auf "Forum 18" klicken); Tazama pia taarifa ya kila mwaka iliyo muhimu, wakati mwingine pia iliyoegemea upande mmoja ya Tume ya Serikali ya Marekani (www.state.gov/g/drl/irl und www.uscirf.gov - tazama orodha ya wovuti mwishoni);juu ya mateso ya Wakristo, tazama Nina Shea. *In The Lion's Den: Persecuted Christians and What the Western Church Can Do About It*. Broadman & Holman: Nashville (TN), 1997 und Paul A. Marshall. T*heir Blood Cries out: The Untold Story of Persecution against Christians in the Modern World*. Word: Dallas, 1997. Kuhusu hali ya Ujerumani, tazama; Gabriele Martina Liegmann. *Eingriffe in die Religionsfreiheit als asylerhebliche Rechtsgutverletzung religioes Verfolgter*. Nomos: Baden-Baden, 1993. Pia tazama taarifa ya kila mwaka ta tume iliyo chini ya rais wa Marekani: A: www.state.gov/www/global/human_rights/irf/irf_rpt/ 1999/index.html (Bericht der US-Regierung zur Religionsfreiheit).

Kwa utegemezi wa idadi hii, narudia tamko langu kwa Tume ya Uhuru wa Kidini ya Shirikisho la Kiinjili Ulimwenguni: "Ningependa kuwapa makadirio ya mashahidi wa imani waliouawa ya karibuni kabisa yaliyo kwenye mjadala. Kwa sasa kuna takribani 165,000 kila mwaka (tunatarajia takribani 167,000 ifikapo mwaka 2001). Tafadhali angalia katika ukurasa wa mtandao http://gem-werc.org/line 31 kwa taarifa za hivi karibuni kabisa.

Makisio yaliyoonekana katika jedwali la "Hali ya Umisheni Ulimwenguni" lililoandaliwa na David Barret na Todd M. Johnson, "kwa ajili ya Jarida la Uekumenika la Kikatoliki (Catholic Ecumenical Journal), "Jarida la Kimataifa la Utafiti wa Umishenari" (International Bulletin of Missionary Reaserch). Pamoja na makisio mengine, jedwali hili limenukuriwa na WEF mara nyingi miongoni mwa nukuu nyingine, na ni chanzo cha makisio mengine zaidi katika maendeleo ya kimataifa katika jarida la *Idea*.

Kama ilivyo kwa wanatakwimu wengi juu ya masuala ya kidini, kama vile Patrick Johnstone, mara nyingi nimemrejea Barret, ili kutazama katika benki ya kumbukumbu zake juu ya idadi ya mashahidi wa imani waliouawa au kupata orodha ya mgawanyo wa mashahidi wa imani toka nchi mbali mbali. Ensaklopidia ya Ukristo Ulimwenguni (The World Christian Encyclopaedia) imejumuisha idadi ambayo haitawekwa wazi kabla ya kitabu kuchapwa. Inajumuisha kumbukumbu juu ya mashahidi wa imani katika karne zilizopita na fasili pana zaidi ya istilahi "Mashahidi wa Imani", lakini haijumuishi orodha ya nchi shiriki, ingawa maelezo mengi yameambatanishwa kwa kila moja**.** Pindi nilipotambua kwamba idadi iliyoahidiwa haikujumuishwa, Barret alinirejesha kwenye namba za kurasa husika, lakini taarifa zilikuwa zimekwishaondolewa. Sasa Barret amekwishanifahamisha kuwa kitabu juu ya mashahidi wa imani chenye taarifa zinazotakiwa kitatoka mwaka 2002. Toleo jipya ni: David Barret, George T. Kurian, Todd M. Johnson, Ensaklopidia ya Kikristo Ulimwenguni: Utafiti Linganishi wa Makanisa na Dini katika Ulimwengu wa Sasa.Vit. 2 (New York and Oxford: Oxford University Press, 2001) kk. 876+823 (Toleo Unganifu $ 250.00). Kurasa 834-835 za Kitabu 1 hujishughulisha na mateso ya Wakristo; wasilisho hujumuisha: safu za 56-69 (hali za nchi moja moja) (World Christian Encyclopaedia: A Comparative Survey of Churches and Religions in the Modern World. 2 Vols. (New York and Oxford: Oxford University Press, 2001), Ukurasa wa 856 (Ramani ya 7 ya Dunia), ukurasa wa 11 "Mchoro wa 6 wa Dunia" (mtawanyiko wa mauaji ya mashahidi wa imani katika makundi makundi katika miaka 2000 ya mwisho). Pitio langu la kitabu hiki laweza kuonekana katika gazeti la 'Evangelikale Missiologie': "Katika mwaka 1l68, wanatakwimu wa kanisa na huduma za misheni waliunganisha nguvu chini ya uongozi wa David Barret aliye mtaalamu wa Kiinjili kwa huduma ya umisheni, ili kuanzisha mradi mkubwa sana, uliosababisha kupatikana kwa toleo la kwanza la WCE la mchapishaji maarufu kitaaluma mnamo mwaka 1981. Pamoja na usajili wake wa dini zote na madhehebu ya Ulimwengu, kitabu kilivuta hisia nje ya Uliwemgu wa Kikristo, na haraka kikawa tunu ya takwimu za kidini, kama kilivyojumuisha data za pekee za nchi nyingi.

Toleo la pili lililosubiriwa kwa hamu kubwa limeenda mbali zaidi, kwa vile mambo mengi yamefanyika katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita. Takwimu za kiinjili za Umisheni zimekuja mahali penyewe, na zimekuwa mota (injini) ya mipango, ya motisha na ya maombi. Vitabu vilivyopo vinawasilisha kiasi kikubwa cha data katika mambo yote yanayohusu Ukristo na dini nyingine. Unahitaji kujua nini? Kiasi gani cha fedha kinachofujwa huko Honduras kila mwaka? Kuna wafanyakazi wangapi wa kanisa wanaofanya kazi muda wote katika Hawaii? Kiasi gani cha fedha kinatumiwa kwa ajili ya vyombo vya habari vya Kikristo huko Ujerumani kila mwaka?

Ni kwa kiasi gani Mkristo wa Uswisi hutoa kwa ajili ya umisheni kuliko Mjerumani? Je, Uislamu unakuwa kwa kuwaongoa watu au kwa kuzaliana huko Indonesia?

Kuna madhehebu ya Kikarismatiki au Kipentekoste mangapi na makundi yaliyomeguka huko Kanada? Ni mashahidi wa imani wangapi wamepata kuwapo katika historia? Ni Wa-kiinjili wangapi wanaoishi huko Cologne? Ni lini kanisa la Methodisti lilianzishwa katika Paraguay?

Lakini data hizi zinaaminika kwa kiasi gani? Mbali na orodha ndefu ya wachangiaji na vitabu vingi vya bibliografia (kwa kila nchi), haiwezekani kurudia njia zilizo msingi wa data hizi kila wakati. Cha kusikitisha, Barret, anayejulikana kwa ukosefu wa utayari wake wa kushirikisha au kujadili data zake, ameshindwa kutoa taarifa za kuridhisha juu ya njia zake za takwimu; tofauti na timu ya waandishi ya 'Operesheni ya Dunia' (Operation World) ya Patrick Johnstone. Tangu taasisi kubwa ya Barrett ilipokusanya data kutoka karibu kila somo la takwimu juu ya kanisa au dini ambayo haijapata kuwepo, tunapaswa kumtegemea, kwa vile hakuna data zingine zilizopo. Hata hivyo, utangulizi unaodai kuwa kitabu kimejumuisha kweli tupu bila tafsiri hauwezi kukubaliwa. Makisio ya idadi ya "Wakristo wa Agizo Kuu" (Wale ambao kibinafsi hupokea wito wa Agizo Kuu) lina madhanio ya aina fulani ya tafsiri, kwa kuwa hakuna hata mchungaji anayeweza kukisia hesabu ya watu kwa kanisani lake mwenyewe. Tangu hapo kitabu cha William Carey cha mwaka 1792 juu ya Umisheni - na takwimu za kidini kilipoanzisha enzi mpya ya takwimu za Kiinjili za Umisheni, uwanja huu umekuwa usiotengwa, lakini haupaswi kuzidisha makisio ya umuhimu wake wenyewe na kujifanyia kiwango cha ukweli usiofikiwa katika ulimwengu mchanganyiko na wenye kubadilika kama huu.

Miswada ifuatayo inajishughulisha tu na mauaji ya mashahidi wa imani ya Kikristo, ambao ni mtazamo mmojawapo wa somo jumuishi zaidi la uhuru wa kidini na haki za binadamu.[15] Mpaka huu kwa kiasi fulani unahalalishwa, kwa

15 Tazama: makala yangu juu ya uhuru wa kidini katika the Jarida la Kijerumani la Amnesty International: "Glauben ist ein Menschenrecht" (Titel). ai-Journal 8/2000: 6-9; vilevile tazama Thomas Schirrmacher. "Christlicher Glaube und Menschenrechte". Querschnitte 12 (1999) 3 (Mrz): 1-6; Thomas Schirrmacher. "Christlicher Glaube und Menschenrechte" (Russisch). POISK: Ezemedel'naja Vsesojuznaja Gazeta [Publication of the Russian Academy of Sciences]. Nr. 48 (446) 22.-28. November 1997. p. 13., Thomas Schirrmacher. "Christlicher Glaube und Menschenrechte"

kuwa mateso kwa misingi ya kidini huwaangukia zaidi Wakristo; hakuna imani nyingine iliyoteswa kwa nguvu kiasi hicho zaidi ya Kanisa la Kikristo[16] - jambo ambalo limekuwa si jambo la kuzungumziwa. Rabi* mkuu wa kwanza wa Jamii ya Kiyahudi katika Uingereza hivi karibuni amenukuliwa akisema kuwa, kwa mara ya kwanza katika historia, hakuna mahali popote duniani ambapo Wayahudi wanateswa kwa ajili ya Uyahudi wao.[17]

2. Theolojia ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani

Hoja : Kwa kiasi kikubwa tunakosa theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani.[18]

(Russian). Utschitjelskaja Gazeta (Gazeti la Kirusi kwa ajili ya walimu). No. 2 (9667) 3.1.1998. uk. 21 + No. 3 (9668) 20.1.1998. p. 21 + No. 4 (9669) 3.2.1998. p. 22.

16 Nina Shea. In The Lion's Den, *op. cit.*, p. 4.

17 Friede ueber Israel 82 (1999) 2: 75 [katika *Idea* Nov. 18,1998]. Kwa ujumla tamko liko sahihi, lakini kuna uwezekano wa hadhari* katika ulimwengu wa Kiislamu.

18 Michango iliyo bora kabisa niliyoifahamu mimi ni:
Ya Kilutherani: Otto Michel. Prophet und Maertyrer. Beitraege zur Foerderung christlicher Theologie 37 (1932), Vol. 2. Bertelsmann: Guetersloh, 1932; Dietrich Bonhoeffer. Nachfolge. Chr. Kaiser: Muenchen, 1950[3]; 1987[16]; [1937]; repr. Dietrich Bonhoeffer Werke, Vol. 4. Guetersloher Verlagshaus: Guetersloh, 1989[1]; 1994[2]; Medardo Ernesto Gómez. Fire against Fire: Christian Ministry Face-to-Face with Persecution. Augsburg Publ.: Minneapolis (MN), 1990 [Original: Fuego contra fuego. Ediciones Liberación: o. O. (El Salvador), 1990]; Robert Kolb. For all the Saints. Changing Perceptions of Martyrdom and Sainthood in the Lutheran Reformation. Mercer University Press: Macon (GA), 1987;
Ya Kimatengenezo*:* A.lfred de Quervain. Die Heiligung. Ethik Erster Teil. Evangelischer Verlag: Zollikon, 1946[2] [1942[1]]. pp. 151-221 (Ch. III. "Das Kreuz im christlichen Leben");
Ya Kiinjili*:* Peter Beyerhaus. Die Bedeutung des Martyriums fuer den Aufbau des Leibes Christi (Eph. 1,22-23). Orthodoxe Rundschau 16 (1984): 4-24 (Special Issue); revised as: Die Bedeutung des Martyriums fuer den Aufbau des Leibes Christi. Diakrisis 25 (1999) 3: 131-141; Peter Beyerhaus. Martyrdom - Gate to the Kingdom of Heaven". p. 163-179. God's Kingdom and the Utopian Error. Tyndale: Wheaton (IL), 1992; Christof Sauer. Mission und Martyrium: Studien zu Karl Hartenstein und zur Lausanner Bewegung. edition afem - missions scripts 5. Verlag fuer Kultur und Wissenschaft Schirrmacher: Bonn, 1994; Josef Tson. Suffering, Martyrdom, and Rewards in Heaven. University Press of America: Lanham/New York, 1998 [Diss. Heverlee (B), 1996]; Paul A. Marshall. Their Blood Cries out: The Untold Story of Persecution against Christians in the Modern World. Word: Dallas, 1997; Herbert Schlossberg. A Frangrance of Oppression: The Church and Its Persecutors. Crossway Books: Wheaton (IL), 1991. p. 115-134 (Biblical-theological section);
Ya Kikatoliki*: :* Karl Rahner. Zur Theologie des Todes. Quaestiones disputatae 2. Herder: Freiburg, 1958, particularly. "Exkurs ueber das Martyrium". p. 73-106 [*Ibid.*, . 1965[5]]; Oda Hagemeyer. "Theologie des Martyriums". Benediktische Monatsschrift 60 (1984) 309-315; Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. Muensterische Beitraege zur Theologie 45. Aschendorff: Muenster, 1980; Ivo Lesbaupin. Blessed are the Persecuted: The Early Church Under Siege. Orbis Books: Maryknoll (NY), 1987 [Original Portugiesisch]; Spire (Hodder & Stoughton): Sevenoaks (GB), 1988; Georg Stoll. "Gefahr fuer Leib und Leben". Stadt Gottes: Familienzeitschrift der Steyler Missionare 122 (1999) 9 (Sept): 8-10;
Maandiko Mchanganyiko: Jan Pit (Ed.). Jeden Tag geborgen: 366 Andachten verfolgter Christen. Haenssler: Neuhausen, 1998; William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. University Press of America: Washington D.C., 1981 [Diss. Basel, 1977]; Harry W. Tajra. The Martyrdom of St. Paul: Historical and Judicial: Context, Traditions, and Legends. Wissenschaftliche Untersuchungen zum Neuen Testament 67. Mohr Siebeck: Tuebingen, 1994; John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. Journal for the Study of the New Testament Supplement Series 6. JSOT Press: Sheffield, 1985; Scott Cunningham. Through Many Tribulations: The Theology of

Theolojia ya kitaaluma[19] imejishughulisha na suala la mauaji ya mashahidi wa imani katika mazingira ya historia ya kanisa la kwanza (karne tatu za mwanzo BK.) tu, kama si kutojishughulisha kabisa.[20] Kwa ujumla, theolojia ya Kiinjili hailijali suala hili, ikiliacha mikononi mwa bodi maalumu za umisheni na vituo

---

Persecution in Luke-Acts. Journal for the Study of the New Testament Supplement Series 142. Sheffield Academic Press: Sheffield (GB), 1997; Daniel Boyarin. Dying for God: Martyrdom and the Making of Christianity and Judaism. Stanford University Press: Stanford (CA), 1999; Norman H. Hjelm (Ed.). Out of the Ashes: Burned Churches and the Community of Faith. NelsonWord: Nashville (TN), 1997; Nina Shea. In The Lion's Den: Persecuted Christians and What the Western Church Can Do About It. Broadman & Holman: Nashville (TN), 1997; Ready for the End Battle. Open Doors: Johannesburg (South africa), n. d. (ca. 1980), repr. Jan Pit. Persecution: It Will Never Happen Here? Open Doors: Orange (CA), 1981; John Rutherford. "Persecution". Sp. 23-24 in: James Orr (Ed.). The International Standard Bible Encyclopedia. 5 Vols., Vol. 4. Wm. B. Eerdmans: Grand Rapids (MI), 1957 [1939]; Merill Tenney. "Persecution". p. 403 in: Everett F. Harrison. Baker Dictionary of Theology. Baker Book House: Grand Rapids (MI), 1975;
Ya Kiasia: **.....**
Ya Kiafrika*:* Festo Kivengere (1921-1988). The Spirit is Moving. Africa Christian Press: Nairobi (Kenia) & Lagos: London, 1976; Festo Kivengere. I Love Idi Amin: The Story or Triumph under Fire in the Midst of Suffering and Persecution in Uganda. Marshall, Morgan and Scott: London, 1977; Revell: Old Tappan (NJ), 1977; ; Festo Kivengere. Ich liebe Idi Amin: Uganda heute, Triumph der Liebe mitten in Leiden und Verfolgung. Haenssler: Neuhausen, 1978[1]; 1979[3]; Festo Kivengere. Revolutionary Love. African Evangelistic Enterprise: Nairobi (Kenia), 1981; Tokunboh Adeyemo. "Persecution: A Permanent Feature of the Church". Evangelical Ministries/Ministères Evangélique (Association of Evangelicals of Africa and Madagascar) Mar-Aug 1985: 3-9; Tokunboh Adeyemo. De gemeente zal altijd vervolgd worden. n. d.; Tortured for Christ. Themenheft Evangelical Ministries/Ministères Evangélique (Association of Evangelicals of Africa and Madagascar) Mar-Aug 1985, particularly . Herman Boonstra. "La Persecution: Formule de Dieu pour la Croissance". p. 11-13; Philip Makau Kavuo. "Unchain My Brethren". p. 14-15; Emmanuel S. A. Ayee. "Persecution: A Bible Study Guide". S. 1925; Brother Andrew (Ed.). Destined to Suffer? African Christians Face the Future. Open Doors: Orange (CA), 1979; particularly . Tokunboh Adeyemo. "Persecution: A Permanent Feature of the Church". p. 23-36 und Dan Kyanda. "The Attitude of the Prepared Christian". p. 97-104; Ready for the End Battle. Open Doors: Johannesburg (South africa), n. d. . (ca. 1980), repr. Jan Pit. Persecution: It Will Never Happen Here? Open Doors: Orange (CA), 1981; Daniel Kyanda. "Mission and Persecution". Arbeitspapier der gleichnamigen Arbeitsgruppe auf der World Consultation on Frontier Mission, Edinburgh 1980.unpublished paper; Idoti und David M. Davies. With God in Congo Forests During the Persecution Under Rebel Occupation as Told by an African Pastor. Worldwide Evangelization Crusade: Bulstrode, Gerrards Cross (GB), 1971;
Lexica*:* Wilhelm Schneemelcher. "Christenverfolgungen". Col. 257-260 in: Hermann Kunst, Siegfried Grundman (Ed.). Evangelisches Staatslexikon. Kreuz Verlag: Stuttgart, 1966[1]; Wilhelm Schneemelcher. "Christenverfolgungen". Col. 324-327 in: Hermann Kunst (Ed.). Evangelisches Staatslexikon. Kreuz Verlag: Stuttgart, 1975[2] (See also the bibliography); Eduard Christen. "Martyrium III/2.". p. 212-220 in: Gerhard Krause, Gerhard Mueller (Ed.). Theologische Realenzyklopaedie. Vol. 22. Walter de Gruyter: Berlin, 1992; Rudolf Freudenberger u. a. "Christenverfolgungen". p. 23-62 in: Gerhard Krause, Gerhard Mueller (Ed.). Theologische Realenzyklopaedie. Vol. 8. Walter de Gruyter: Berlin, 1981.

19 Katika Ujerumani, theolojia ya kitaaluma inatawaliwa na kanisa Katoliki la Rumi (Roman Catholic) na kanisa la kiserikali la Kilutheri (Lutheran State church) na vitivo vyao katika vyuo vikuu vya serikali. Seminari za Kiinjili hazitambuliwi na vyuo vikuu vya Ujerumani na makanisa ya kiserikali.

20 Hali imezidi kuwa mbaya zaidi. The Evangelische Staatslexikon ilijumuisha makala juu ya "Christenverfolgungen" katika matoleo yao mawili ya awali (Wilhelm Schneemelcher. "Christenverfolgungen". Col. 257-260 in: Hermann Kunst, Siegfried Grundman [Ed.]. Evangelisches Staatslexikon. Kreuz Verlag: Stuttgart, 1966[1]; repr. Col. 324-327 in: Hermann Kunst [Ed.]. Evangelisches Staatslexikon. Kreuz Verlag: Stuttgart, 1975[2]), lakini toleo-rudufu la mwisho (1987[3]) limeondoa mchango pasipo kuujaza na majadiliano yoyote ya kina juu ya somo lenyewe, ingawa linashiriki jukumu muhimu katika suala la mahusiano kati ya Kanisa na Serikali.

vyao vya uchapaji. Hata hivyo, mfululizo wa mikutano katika miaka ya 1970 na 1980[21] na mafanikio ya Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Wakristo Wanaoteswa, ambapo makanisa takribani 300,000 yalishiriki, yakichochea matumaini ya mabadiliko.

Eduard Christen ameonesha kuwa nafasi inayohusu mateso ya Wakristo hadi 311 BK. kiungwana imekuwa ikikubaliwa, lakini ni kwamba hakuna tathmini ya kibiblia kuhusu somo hili au mateso tangu 311 BK. hadi sasa, na ya kuwa tumeondolewa kupelekwa mbali na uwekaji kumbukumbu – pangilivu wenye kuhitajiwa sana juu ya somo au ‘ Theolojia ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani.’[22] Ukosefu wa mafundisho ya Kibiblia na Kitheolojia na tafakari juu ya somo hili ni wenye kuonekana bayana, hata katika Uinjili wa Marekani (American Evangelicalism), ambao kwa ujumla ndio husambaza taarifa juu ya mateso ya kimataifa. Ninaweza kukubaliana tu na utetezi wa Patrick Johnstone kwa ajili ya maendeleo na usambazaji wa somo la Mauaji ya Mashahidi wa Imani, yaani mafundisho ya mateso.[23]

---

21 Makongamano ya Kiinjili yaliyo muhimu zaidi juu ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani yamekuwa ni haya:
***1977**:* Ingrid Kastelan. “Verfolgung ist letztendlich Verheissung”. idea 45/1977 (7.11.). p. I-II (No report);
Konferenz der AEM “Gemeinde in Bedraengnis” 2.-6, Nov. 1977 in Burbach-Holzhausen;
***1978**:* Love Africa ‘78 Congress in Blantyre, Malawi, Mai 1978: Brother Andrew (Ed.). Destined to Suffer? African Christians Face the Future. Open Doors: Orange (CA), 1979;
***1978**:* AEPM/EFMA/IFMA Konferenz Overland Park (Kansas) 25.-29, Sept. 1978: Edwin L. Frizen, Wade T. Coggins (Ed.). Christ and Caesar in Christian Missions. William Carey Library: Pasadena (CA), 1979;
***1980**:* Daniel Kyanda. “Mission and Persecution”. Taarifa ya kundi lenye jina sawa na hili katika World Consultation on Frontier Mission, Edinburgh 1980. haikuchapwa;
***1983**:* “The Yakunin Hearing July 22-26, 1983 Vancouver ...” (Christian Solidarity International). Mpango, lakini hakuna taarifa;
***1984**:* 4. Theologische Konsultation der Asia Theological Association (ATA) in Hong Kong, 1984: Christian Suffering and Persecution. Asian Perspectives, Nr. 9. (The Declaration of the 4th ATA Theological Consultation in Hong Kong. Asia Theological Association (ATA): Taichung (Taiwan), 1984;
***1984**:* Meeting of the Theologischen Kommission der World Evangelical Fellowship / Weltweiten Evangelischen Allianz in St. Chrischona / Basel, Result of the so-called. “Baseler Brief”: “The Basel Letter” Col. 8-18 in: Christian Suffering and Persecution. Asian Perspectives, NR. 9. (The Declaration of the 4th ATA Theological Consultation in Hong Kong. Asia Theological Association (ATA): Taichung (Taiwan), 1984;
***1988**:* AfeM-Jahrestagung 1988: Urgemeinde und Endzeitgemeinde - Missionarische Existenz in Zeugnis und Leiden: Vier Referate der Jahrestagung des Arbeitskreises fuer evangelikale Missiologie (AfeM). Idea Dokumentation 3/1988;
1988: Konferenz der Asiatischen Evangelischen Allianz / Evangelical Fellowship of Asia “Die Kirchen inmitten des Leides” Hong Kong 24.-27.2.1988: Bong Rin Ro (Ed.). Christian Suffering in Asia. Evangelical Fellowship of Asia: Taichung (Taiwan), 1989; “A Theology of Suffering”. Themenheft Asia Theological News 14 (1988) 3, particularly . “A Letter to the Churches in Asia”. pp. 4-5 and on the reason for the Conference, John Richard. “Preparing for Suffering”. p. 8-9; Tazama pia taarifa za: “Prepare for Sufferings Says a Letter to Asia’s Churches”. Evangelical World May 1988: 1-2 na katika *Idea* 24/1988 (16.3.). p. 2-3

22 Eduard Christen. “Martyrium III/2.”. *op. cit.*, p. 212.

23 Patrick Johnstone. “Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution”. Worldwide Thrust (WEC USA) Nov/1978: 3-7, here p. 3.

3. Makundi Makubwa ya Wakristo Yamekuwa Yakiteswa

Hoja: Asilimia kubwa ya Wakristo leo, kipekee Wakristo wa Kiinjili, hawaishi tena katika mafanikio wala ulinzi wa sheria bali chini ya mateso. Wakristo hawa wanayaelewa Maagano yote ya Kale na Jipya kwa uhalisia zaidi kuliko Wakristo wa Magharibi.

"Mauaji ya mashahidi wa imani ya Kanisa la Kristo yamefikia kilele kipya katika karne hii"[24] na Kanisa la Magharibi na upungufu wake mkubwa katika theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani linahitaji kujifunza kutoka kwa waamini wenzao marafiki kutoka katika nchi na katika mazingira yaliyo chini ya mateso, aidha kwa mawasiliano na watu binafsi walioko huko au kupitia maandishi yao.[25]

---

24 Peter Beyerhaus. Die Bedeutung des Martyriums fuer den Aufbau des Leibes Christi. Diakrisis 25 (1999) 3: 131-141, here p. 134; See also: Andrew Chandler (Ed.). The Terrible Alternative: Christian Martyrdom in the Twentieth Century. Cassell: London, New York, 1998; Ann Ball mit Paul Marx, Stephen Dunham. The Persecuted Church in the Late Twentieth Century. Maginificat Press: Avon (NJ), 1990 (Catholic point of view); on a part of the world seldom discussed in this respect: Martin Lange, Reinhold Iblacker (Ed.). Christenverfolgung in Suedamerika: Zeugen der Hoffnung. Herder: Freiburg, 1980; in English; Martin Lange, Reinhold Iblacker (Ed.). Witnesses of Hope: The Persecution of Christians in Latin America. Orbis Books: Maryknoll (NY), 1981.

25 ***Kwa mfano, Asia****:* Petrus Oktavianus. "Die Narde ausschuetten". p. 120-128 katika: Otto Riecker (Ed.). Ruf aus Indonesien, Haenssler: Neuhausen, 1973[3] [1971[1]]; Chua Wee Hian, Frank Saphir Khair-Ullah, Subodh Sahu. "Evangelism in the Hard Places of the World". p. 464-473 in J. D. Douglas (Ed.). Let the Earth Hear His Voice: International Congress on World Evangelization Lausanne, Switzerland. World Wide Publ.: Minneapolis (MN), 1975; Bong Rin Ro (Ed.). Christian Suffering in Asia. Evangelical Fellowship of Asia: Taichung (Taiwan), 1989 (8 general contributions 15 reports), particularly; Ken R. Gnanakan. "A Biblical Perspective on Suffering" p. 23-30 and Jonathan Chao. "Witness in Suffering". p. 43-54; "Christian Suffering and Persecution". Asian Perspectives, Heft 9. (The Declaration of the 4th ATA Theological Consultation in Hong Kong. Asia Theological Association (ATA): Taichung (Taiwan), 1984; Met Q. Castillo. The Church in Thy House. Alliance-Publishers: Malina (Philippinen), 1982;
Afrika *:* Preparing Believers for Suffering and Persecution: A Manual for Christian Workers. Hope: Bulawayo (Simbabwe), n. d. (ca. 1979). 15 S.; Ready for the End Battle. Open Doors: Johannesburg (South africa), n. d. (ca. 1980), repr. Jan Pit. Persecution: It Will Never Happen Here? Open Doors: Orange (CA), 1981; Brother Andrew. Destined to Suffer? African Christians Face the Future. Open Doors: Orange (CA), 1979, particularly . Tokunboh Adeyemo. "Persecution: A Permanent Feature of the Church". p. 23-36 and Dan Kyanda. "The Attitude of the Prepared Christian". p. 97-104; Daniel Kyanda. "Mission and Persecution". Arbeitspapier der gleichnamigen Arbeitsgruppe auf der World Consultation on Frontier Mission, Edinburgh 1980. unpublished. Peter Hammond. Faith under Fire in Sudan. Frontline Fellowship: Newlands (South africa), 1996; Peter Hammond. In the Killing Fields of Mozambique. Frontline Fellowship: Newlands (South Africa), 1998; See also Brother Andrew. Battle for Africa. Revell: Old Tappan (NJ), 1977 and Patrick Johnstone. "Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution". Worldwide Thrust (WEC USA) Nov/1978: 3-7
Amerika ya Kusini*:* Medardo Ernesto Gómez. Fire against Fire: Christian Ministry Face-to-Face with Persecution. Augsburg Publ.: Minneapolis (MN), 1990 [Original: Fuego contra fuego. Ediciones Liberación: (El Salvador), 1990] (Lutheran); Ivo Lesbaupin. Blessed are the Persecuted: The Early Church Under Siege. Orbis Books: Maryknoll (NY), 1987 [Original Portuguese]; Spire (Hodder & Stoughton): Sevenoaks (GB), 1988 (Brasilian; Catholic);
Former Iron Curtain; Josef Tson. Suffering, Martyrdom, and Rewards in Heaven. University Press of America: Lanham/New York, 1998 [Diss. Heverlee (B), 1996]; Ivan Vasiljevitch Moisejev. Eine Maertyrergeschichte. Aktionskomitee fuer verfolgte Christen: Rheinbach, 1982[5]; See also. Manfred Fermir. Christen in der Verfolgung. Anregungen: Arbeitshefte fuer den Religionsunterricht ... 3. R.

Maandishi na mafundisho mengi ya Kijerumani juu ya Somo la Mauaji ya Mashahidi wa Imani, kwa kawaida yaliandikwa katika kipindi cha Utawala wa Tatu (Third Reich). Miongoni mwa yale yaliyo maarufu sana ni ya: Waprotestanti Otto Michel (1932), Hans Freiherr Von Campehausen (1936), Dietrich Bonnhoeffer (1937), Hellmuth Frey (1938), Hans-Weren Surkau (1938), Ethelbert Stauffer (1933 na 1941), Ernst Guenther (1941), Alfred de Quervain (1942), Friedrich Graber (1943) na katika Ufaransa ni Andrá Graber (1943), na Mkatoliki Albert Ehrhard (1932).[26]

4. Theolojia ya Kanisa la Kwanza Ilighushiwa na Mauaji ya Mashahidi wa Imani

Hoja: Mateso yaliyowasibu Wakristo chini ya Dola ya Kirumi hadi 311 BK. yamekuwa na matokeo ya kudumu katika Theolojia ya Kanisa.[27] "Ingawa yalichukua idadi ndogo ya waathirika kinyume na muda mrefu yaliyochukua, mateso haya yamefinyanga muundo na theolojia ya Kanisa inayokua kuliko sababu nyingine yoyote."[28] Kwa sababu Kanisa la Agano Jipya liliibuka tokea matesoni na kukuza theolojia yake katika karne za kwanza za uwepo wake chini ya mbinyo wa mteso na ugandamizaji, ni jambo la maana kusoma tena urithi wa kimaandiko wa kanisa lililoteswa.[29] "Kuna maandiko tele ya kipindi baada ya mitume na kipindi cha mababa wa Kanisa juu ya mauaji ya mashahidi wa imani, kipekee kumbukumbu juu ya mashahidi wa imani waliouawa na mateso yao,[30] vile vile maandishi rasmi ya mashitaka yao na taarifa

Brockhaus, 1979; G. P. Wiens [= Georgii Petrovich Vins]. Zeugnis vor der Kommission fuer Sicherheit und Zusammenarbeit in Europa 7 Juni 1979. Missionswerk Friedensstimme: Koeln, n. d. [1979]; Georgi Vins. Auf dem Pfad der Treue. Missionswerk Friedensbote: Gummersbach, 1999; Georgii Petrovich Vins. Let the Wars Roar: Evanglists in the Gulag. Baker Book House: Grand Rapids (MI), 1989; Georgii Petrovich Vins. Chronique de la persécution religieuse. Éditions des Catacombes: Courbevoie (F), 1975; Georgii Petrovich Vins. De Kerk leeft nog! De Situatie van de Hervormde Baptisten in Rusland. Ed. von Henk Wolzak. J. H. Kok: Kampen, 1981; Georgii Petrovich Vins. Konshaubi: A True Story of Persecuted Christians in the Soviet Union. Baker Book House: Grand Rapids (MI), 1988; Georgii Petrovich Vins. Three Generations of Suffering. Hodder & Stoughton: London, 1976; Georgii Petrovich Vins. Testament from Prison. ed. by Michael Bordeaux. D. C. Cook Publ.: Elgin (IL), 1975.

26 Tazama Bibliografia.

27 Tazama: Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 1; Theofried Baumeister. "Maertyrer und Verfolgte im fruehen Christentum". *op. cit.*, p. 169 und Albert Ehrhard. Die Kirche der Maertyrer. a. *op. cit.*, p. 117-121 na kitabu kizima. Jambo hili ni kweli katika mtazamo chanya, lakini pia ni kweli katika mtazamo hasi, kama kifungu kinavyoonesha.

28 Rudolf Freudenberger et. al. "Christenverfolgungen". *op. cit.* p. 23.

29 Kama utangulizi, ningependekeza Waraka kwa Makanisa ya Viena na Lioni [the Epistle of the Churches of Vienne and Lyon (177 A. D.)], katika Eusebius of Caesarea (Yusibiasi wa Kaisaria). Kirchengeschichte. Wissenschaftliche Buchgesellschaft: Darmstadt, 1984 [Lizenz von Koesel: Muenchen, 1981²]. p. 233-245 [5th Vol. Ch. 1-2] and Lactantius. De mortibus persecutorum. ed. by J. L. Creed. Clarendon Press: Oxford, 1984. Yenye thamani ya kipekee ni maelezo ya mwenendo ya mababa wa kanisa* akina Laktanti, Sipriano, Agostino na Yusibiasi (Laktantius, Cyprian, Augustinus und Eusebius) wakati wa mateso.

30 Kwa upangaji mzuri wa maandiko haya, tazama: Herbert Musurillo (Ed.). The Acts of Christian Martyrs. Clarendon Press: Oxford, 1972. pp. lii-liii in "Introduction" pp. xi-lxxiii. Tazama pia

zenye kuaminika za mashahidi walioona kwa macho."[31] Ethelbert Stauffer amedokeza kuwa Historia ya Kanisa ya Eusebius, ya kwanza na ya aina yake, iliandikwa kutoka katika mtazamo wa Mafundisho ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani[32] (kielelezo kwa nyakati hizi!).

Hata hivyo tunapaswa kuwa na tahadhari katika kuhamasisha *kiu* kwa mateso ya mashahidi wa imani na ingawa baadhi ya maendeleo yalikuwa yenye kutia mashaka,[33] Kanisa la Kwanza lilielewa kwa usahihi, kwamba nadharia na vitendo vya mateso na mauaji ya mashahidi wa imani katika karne za kwanza za uhai wake vilikuwa mwendelezo wa moja kwa moja wa mafundisho na uzoefu wa Kanisa la Agano Jipya. Makanisa yale yaliyoishi pasipo kujali mateso na mauaji ya mashahidi wa imani kwa nguvu yanaondoka kutoka katika Agano Jipya kuliko yale makundi yaliyoteswa ya karne za kwanza ambayo, kwa kuteseka mauaji ya mashahidi wa imani na kulithamini jambo hilo kwa kiwango cha juu, kulisababisha kuifikia Dola ya Kirumi na Injili.

5. Suala la Mateso ya Wakristo Halikomei kwa Kanisa la Kwanza

Hoja: Mauaji ya Mashahidi wa Imani na mateso ya waamini hayahusu tu Kanisa la Kwanza, kwa kuwa daima yameambatana na Ukristo katika historia yake yote.[34] "Mateso ya Wakristo na mauaji ya mashahidi wa imani yalitokea katika kila karne."[35] Hili linapaswa kujulikana kwa wanafunzi wa Historia ya Kanisa. Machapisho mengi ya kitheolojia yajishughulisha na somo hili kana kwamba mateso yalikoma katika karne za mwanzo za historia ya Ulaya. Mafupisho mengi ya historia hukomea katika

---

makusanyo mbalimbali, *Ibid*., (Tafsiri za Kigriki/Kilatini na Kiingereza); Rudolf Knopf, Gustav Krueger (Ed.). Ausgewaehlte Maertyrerakten. Sammlung ausgewaehlter kirchen- und dogmengeschichtlicher Quellenschriften 3. J. C. B. Mohr: Tuebingen, 1929; kilifanyiwa urudufu na Gerhard Ruhbach *Ibid*., 1965 (Greek Originals); Andreas Schwerd. Lateinische Maertyrerakten. Humanitas christiana 1. Koesel: Muenchen, 1960; Gerhard Rauschen. Fruehchristliche Apologeten und Maertyrerakten. 2 Vols. Bibliothek der Kirchenvaeter. Koesel: Kempten, n. d. (German); Hugo Rahner. Die Maertyrerakten des zweiten Jahrhunderts. Zeugen des Wortes 32. Herder: Freiburg, 1954. See the list of German translations of sources Hans Dieter Stoever. Christenverfolgung im roemischen Reich. Econ: Duesseldorf, 1983; Bechtermuenz: Eltville am Rhein, 1990 (Edition 1983. p. 290-294).

31 I. Bria. "Martyrium". *op. cit*., p. . 267. Daneben gehoeren natuerlich im weiteren Sinne noch Passionsdarstellungen und Maertyrerlegenden dazu; See also. Gerhard Ruhbach. "Maertyrerakten". p. 1303 in: Helmut Burkhardt, Uwe Swarat (Ed.). Evangelisches Lexikon fuer Theologie und Gemeinde. Vol. 2. Brockhaus: Wuppertal, 1993.

32 Ethelbert Stauffer. "Maertyrertheologie und Taeuferbewegung". Zeitschrift fuer Kirchengeschichte 52 (1933): 545-598, here p. 548.

33 Tazama mchango juu ya ibada ya watakatifu hapo chini, lakini tahadhari inashauriwa. Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit*., pp. 252-257, ameonesha kuwa Kanisa la Kwanza, kipekee lile la "Mchungaji wa Herma" limekuwa likilaumiwa kimakosa kwa kufundisha 'Thawabu', mafunzo ya malipo juu ya ushahidi wa imani.

34 Kwa ajili ya ufupisho mzuri, tazama: Jonah Spaulding. A Summary History of Persecution from the Crucifiction of Our Saviour to the Present Time. S. K. Gilman: Hallowell (ME), 1819.

35 Gerhard Ruhbach. "Maertyrer". p. 1303 in: Helmut Burkhardt, Uwe Swarat (Editors.). Evangelisches Lexikon fuer Theologie und Gemeinde. Vol. 2. Brockhaus: Wuppertal, 1993.

utawala wa Constantine,[36] hii si tu kutupilia mbali na kuyafanya mateso makubwa ya Karne ya Ishirini kuwa kitu kisicho na uzito,[37] ambacho kwacho Chuck Colson anaandika "Wakristo wengi wamekwishauawa kwa ajili ya imani yao katika karne hii pekee kuliko katika karne kumi na tisa zilizotangulia ukiziweka pamoja."[38] Taarifa hizi pia hazitilii maanani ukweli kuwa mateso yameshiriki jukumu katika Historia ya Kanisa na Elimu ya Umisheni,[39] kwa kuwa, "Historia ya Kanisa pia ni historia ya mateso yake."[40] Kutolitilia maanani somo hili ni kuyapuuza mateso[41] yaliyofanywa katika vita vyote vya kidini na mashindano, matokeo ya Mapinduzi ya Ufaransa,[42] Wakristo katika Dunia ya Kiislamu,[43] vile vile mauaji ya umma ya Wakristo wengi huko Asia; kipekee huko

---

36 Kwa mfano, tazama, Albert Ehrhard. Die Kirche der Maertyrer: Ihre Aufgaben und ihre Leistungen. J. Koesel & F. Pustet: Muenchen, 1932; H. Last. "Christenverfolgung II (judicial)". Col. 1208-1228 and J. Vogt. "Christenverfolgung I (historical)". Col. 1159-1208 in: Reallexikon fuer Antike und Christentum. Vol. 2. Hirsemann: Stuttgart, 1954. *Ibid.*, p. 1159 anafasili kwa urahisi mateso ya Wakristo kama mateso ya Warumi (na kwa sehemu, ya Wayahudi katika Dola ya Rumi)! Uwekaji mpaka wa mambo kama huu unatokea pia kwa Geoffrey W. Bromiley. "Persecute". p. 771-774 in: Geoffrey W. Bromiley (Ed.). The International Standard Bible Encyclopedia. Vol. 3. Wm. B. Eerdmans: Grand Rapids (MI), 1986; John Rutherford. "Persecution". p. 23-24 in: James Orr (Ed.). The International Standard Bible Encyclopedia. 5 Vols. Vol. 4. Wm. B. Eerdmans: Grand Rapids (MI), 1957 [1939] oder I. Bria. "Martyrium". *op. cit.*, oder Michael Slusser. "Martyrium III/1.". p. 207-212 in: Gerhard Krause, Gerhard Mueller (Ed.). Theologische Realenzyklopaedie. Vol. 22. Walter de Gruyter: Berlin, 1992.

37 Tazama: James C. Hefley, Marti Hefley, James Hefley. By Their Blood: Christian Martyrs of the Twentieth Century. Baker Book House: Grand Rapids (MI), 1994 und Johannes Herzog. "Maertyrer". pp. 166-167 in: Friedrich Keppler (Ed.). Calwer Kirchenlexikon. Vol. 2. Calwer Verlagsb.: Stuttgart, 1941. p. 166-167.

38 Chuck Colson. "Foreword". S. ix-xii in: Nina Shea. In The Lion's Den: A Shocking Account of Persecution and Martyrdom of Christians Today and How We Should Respond. Broadman & Holman: Nashville (TN), 1997. p. ix.

39 Bernard Ruffin. The Days of Martyrs: A History of the Persecution of Christians from Apostolic Times to the Time of Constantine. Our Sunday Visitor: Huntington (IN), 1985; See also the contributions in Diana Wood (Ed.). Martyrs and Martyrologies. Taarifa zilizosomwa katika majira ya joto 1992 na Mkutano wa majira ya baridi 1993... Ecclesiastical History Society. B. Blackwell: Oxford, 1993 and W. J. Sheils (Ed.). Persecution and Toleration. Taarifa zilizosomwa katika... Ecclesiastical History Society. B. Blackwell: Oxford, 1984.

40 Franz Kardinal Hengsbach. "Vorwort". pp. 5-6 in: Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1991. Arbeitshilfen 85. Sekretariat der Deutschen Bischofskonferenz: Bonn, 1991. p. 6.

41 Juu ya vipindi mbalimbali vya Historia ya Ulaya, tazama: Brad Stephan Gregory. Salvation at Stake: Christian Martyrdom in Early Modern Europe. Harvard Historical Studies 134. Harvard University Press: Cambridge (MA), 1999; Lutz E. von Padberg. Die Christianisierung Europas im Mittelalter. Reclam: Stuttgart, 1998; Lacey Baldwin Smith. Fools, Martyrs, Traitors: The Story of Martyrdom in the Western World. A. A. Knopf: New York, 1997; Northwestern University Press: Evanston (IL), 1999[Tb] (teilweise weltlich); Joseph N. Tylenda. Jesuit Saints and Martyrs. Loyola University Press: Chicago 1984[1]; Loyola Press: Chicago, 1998[2]; F. Graeme Smith. Triumph in Death: The Story of the Malagasy Martyrs. Evangelical Press: Welwyn (GB), 1987; 1994[Tb]

42 Rudolf Freudenberger et. al. "Christenverfolgungen". *op. cit.*, pp. 45-48.

43 *Ibid.*, pp. 35-38 . Tazama pia mfano wa Misri katika Martyrs and Martyrdom in the Coptic Church. Saint Shenouda the Archimandrite Coptic Society: Los Angeles (CA), 1984; John Eibner (Ed.). Christians in Egypt: Church under Siege. Institute for Religious Minorities in the Islamic World: Zuerich, Washington, 1993; kuhusu hali ya sasa, tazama Herbert Schlossberg. A Frangrance of

Japani (1587-1635), China (1617,1665,1723,1724,1736,1811,1857,1900-1901) na Korea (1784, 1791,1801,1815,1827,1839,1846,1866,1881,1887), kwa kutaja mifano michache. Hata kabla ya Karne ya Ishirini, mataifa mengi yalizuia na kuigandamiza imani ya Kikristo (kwa mfano, Japani 1635-1854, Madagasca tangu 1835, na daima huko Saudi Arabia).[44]

Makanisa madogo yaliyoteswa kishenzi mara kwa mara na mavuguvugu ya Kianabaptisti yametambua kuwa historia nzima ya Kanisa imefinyangwa kwa mateso, kama ambavyo Stauffer ameeleza: kuwa cha kusikitisha, maafa na mateso ya mashahidi wa imani katika Ufunuo hayakutokea katika makanisa yaliyokuwepo bali katika 'vikundi vya ushirika vya kizushi',[45] kama Waldensia au Waprotestanti katika kukabiliana na Kanisa Katoliki, Wabaptisti wakikabiliana na Wakatoliki na Waprotestanti, au Wabaptisti na Wamenonaiti dhidi ya Kanisa la Othodoksi katika nchi za mwanzo za Pazia la Chuma. Waanabatisti walitambua kila kitu walichopaswa kukijua: 'Kundi (Kanisa, nyongeza ya mtafsiri) la Waamini wa kweli daima limekuwa kundi la mashashidi wa imani. Hili ndilo wazo la msingi la historia ya Theolojia ya Kibaptisti."[46]

Oppression: The Church and Its Persecutors. Crossway Books: Wheaton (IL), 1991. pp. 25-50; Andrea Morigi, Vittori Emanuele Vernole, Priscilla di Thiene. Die Religionsfreheit in den Laendern mit ueberwiegend islamischer Bevoelkerung. Schriftenreihe von 'Kirche in Not/Ostpriesterhilfe'. KIN/OPH: Muenchen/Luzern/Wien, 1999 (hasa hasa wahanga wa Kikatoliki); Eberhard Troeger. "Verachtung, Bachteile - Unrecht, Tod? Christsein in islamischen Laendern". Confessio Augustana 1/2000: 29-33; "Facing the Fire: Christians Under Persecution". Crossroads (Middle East Christian Outreach) Nr. 70: March 1988: 2-9; Abram J. Wiebe. "Special Problems with Islamic Governments": p. 95-102 in: Edwin L. Frizen, Wade T. Coggins (Ed.). Christ and Caesar in Christian Missions. William Carey Library: Pasadena (CA), 1979 and Christine Schirrmacher. "Human Rights and the Persecution of Christians in Islam". Chalcedon Report No. 375 (Oct 1996): 13-15; Christine Schirrmacher. "Menschenrechte und Christenverfolgung in der islamischen Welt". Querschnitte 12 (1999) 4/5 (Apr/Mai): 1-8; Christine Schirrmacher. "Menschenrechte und Christenverfolgung in der islamischen Welt". S. 24-35 in: Max Klingberg (Hg.). Maertyrer heute. Schulte & Gerth: Asslar, 2000; Christine Schirrmacher. "Wenn Muslime Christen werden - Glaubensabfall und Todesstrafe im Islam". S. 36-49 in: Max Klingberg (Hg.). Maertyrer heute. Schulte & Gerth: Asslar, 2000; Lorenz Mueller. Islam und Menschenrechte. Diss. Hamburg, 1996.

44 Tarehe zimechukuliwa kutoka katika "Christenverfolgungen". Col. 1115-1120 in: Josef Hoefer, Karl Rahner (Ed.). Lexikon fuer Theologie und Kirche. Vol. 2. Herder: Freiburg: 1986 (toleo-rudufu tangu 1958). p. 1120 (limetawaliwa na mashahidi wa imani wa Kikatoliki); Tazama pia. Rudolf Freudenberger et. al., . "Christenverfolgungen". *op. cit.*, pp. 38-44 kuhusu China, Japani, Korea na Vietnam.

45 Ethelbert Stauffer. "Maertyrertheologie und Taeuferbewegung". *op. cit.*, p. 553.

46 *Ibid.*, p. 560.

6. Sababu Zenye Sura Mbalimbali za Mateso

Hoja: Sababu za mateso ya Wakristo mara nyingi ni zenye sura nyingi na mara chache zinakuwa za kidini kabisa.[47] Utashi wa kisiasa, kitamaduni, kitaifa, kiuchumi na kibinafsi pia waweza kuchangia.

Agano la Kale linadhihirisha hili kwa uwazi kabisa. Chuki ya malkia Yezebeli kwa Mungu na manabii wake ilichangayika na tamaa ya mamlaka, vile vile kwa ajili ya faida binafsi (1 Wafalme 16-19). Katika Ufunuo wa Mt. Yohana utaona chuki dhidi ya Kanisa inatiwa nguvu na masuala ya siasa na uchumi. Mfano mwingine ni ule wa mafundi stadi (wafua vyuma) wa Efeso waliochochea vurugu kwa sababu waliuona ujumbe wa Paulo kuwa kitisho kwa mambo yao (Matendo ya Mitume 19:23-29). Katika Matendo 16, Paulo na Sila wanatiwa gerezani baada ya kumfungua binti aliyekuwa na pepo wa uaguzi, kwa sababu wamiliki wake wana hasira kwa kupoteza faida yao (Matendo ya Mitume).

Tunakosa nafasi ya kushughulika na utashi mbalimbali na sababu zilizo nyuma ya mawimbi ya mateso katika kina chote cha kihistoria na kijiografia. Hata hivyo, ni lazima tujue kwamba daima kuna muungano wenye kuchanganya wa mahitaji ya kidini na matatizo ya kitamaduni na kijamii.

7. Shahidi wa Imani ni Nani?

Hoja: Shahidi wa imani ni Mkristo anayeteseka hadi kifo kwa dhamiri yake mwenyewe, kama adhabu kwa ukiri wa imani yake au ukataaji wa kuikana imani au moja ya mafundisho yake ya kidogma*, kanuni au vitendo vyake.[48] 'Mauaji ya Mashahidi wa Imani, kama tunavyoitumia istilahi hiyo siku hizi, humaanisha kifo kwa ajili ya imani ya Kikristo au desturi za Kikristo.'[49] Ukweli ni kwamba, hakuna tofauti kati ya wale 'walioteswa kwa sababu ya imani yao' na wale waliteswa kwa sababu ya 'utetezi wao ulio hai wa haki';[50] Kitabu cha Ufunuo hudhihirisha wazi kuwa mateso kwa sababu ya kutenda au desturi yanaweza kutazamwa kama mateso kamili.[51] Serikali ya Mpiga Kristo (Mnyama) huwagandamiza "watakatifu: hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." (Ufunuo 14:12) na hakika itashindwa. Ufunuo 12:17 huwaelezea wale walioteswa na Joka kwa njia ile ile. Kwa kawaida, Wakristo wameelezwa kwanza kama wale wanaotii amri za Mungu, na tena kama wale tu walio wa Yesu Kristo, ambacho ni kitu kile kile. Yote kwa usawa huvuta hasira za waovu.

---

47 Gerhard Ruhbach. "Christenverfolgung/-en". *op. Cit.*

48 David B. Barrett. World Christian Encyclopedia. Nairobi etc.: Oxford University Press, 1982. p. 833.

49 Karl Rahner. Zur Theologie des Todes. Quaestiones disputatae 2. Herder: Freiburg, 1958, particularly. "Exkurs ueber das Martyrium". pp. 73-106 [*Ibid.* 1965[5]]. p. 73.

50 Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1993: China. *op. cit.*, p. 11.

51 Otto Michel. Prophet und Maertyrer. Beitraege zur Foerderung christlicher Theologie 37 (1932), Vol. 2. Bertelsmann: Guetersloh, 1932. p. 42.

B. Dhamira Muhimu ya Kibiblia

8. Maandiko Yamechukuliwa Nje ya Mazingira na Kudunishwa

Hoja: Tumedunisha mistari mingi sana kwa kuichukua nje ya mazingira ya mateso na maumivu. Ni lazima kujifunza upya kuyaelewa haya kinyume cha usuli wake.

Mfano halisi ni usihi wa Bwana Yesu kuwa Wakristo ni lazima wawe *Chumvi ya Dunia*, neno ambalo hutukumbusha kuwa uharibifu wa dunia yetu lazima uwe ni kitu muhimu kwetu. Hata hivyo, kwa kiasi kidogo tunaonesha matokeo dhahiri ya imani, ambayo Yesu anayaelezea kama utayari wa kufa! Manabii wa Agano la Kale walikuwa chumvi ya dunia, kama tunavyopaswa kuwa sasa: "**Wamebarikiwa wale wateswao kwa ajili ya haki; kwa maana ufalme wa mbinguni ni wao. Ninyi ni wenye baraka, wakati watu watakapowatukana, na kuwatesa, na kuwanenea mambo yote maovu kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kuzidi katika shangwe; kwa maana zawadi yenu ni kubwa huko mbinguni; kwa kuwa ndivyo walivyowatesa manabii waliokuwepo kabla yenu. Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini ikiwa chumvi imepoteza ladha yake, kwa njia gani itakolezwa? Hivyo haifai kitu bali kutupwa, na kukanyagwa na watu.**" (Mathayo 5:10-13).

Mfano mwingine wa usihi wa kumtazama Yesu, "... mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Maana mtafakarini sana yeye aliyestahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkazimia mioyoni mwenu. Hamjafanya vita hata kumwaga damu, mkishindana na dhambi; tena mmeyasahau yale maonyo, yasemayo nanyi kama kusema na wana, Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana, wala usizimie moyo ukikemewa naye". (Ebr. 12:2-5) ambao unaonesha uvumilivu wa Bwana katika mateso na kifo kama kielelezo kwa ajili yetu. Kumtazama Yesu, ambako kunatuwezesha kuvumilia, si tu suala la utimizaji wajibu au kufanya tafakuri, bali ni majumuisho dhahiri kuwa Yesu aliteswa, kwa sababu alijua kilichokuwa kikimsubiri mbele yake, na uigaji wa kielelezo chake. Mwandishi wa Waebrania alikuwa na mateso akilini mwake alipokuwa akiandika maneno haya, kwa kuwa ametaja "wingu la mashahidi" (12:1), ambalo amelijadili kwa undani katika sura ya 11.

Wakati Yesu atuitapo tujikane nafsi zetu, na kutupa changamoto ya kubeba msalaba wetu, si tu anazungumza katika maneno ya kisaikolojia[52] - - kujitazama

---

52 Ushirika wa upendo na amri za Mungu huelezea usihi ufuatao, "Mpende jirani yako kama nafsi yako." Baadhi huielewa sentensi hii kama wazo la kisaikolojia, kwamba mtu anaweza tu kuwapenda wengine, wakati mtu anapoipenda nafsi yake. Wengine huelewa kujipenda nafsi yako kuwa kinyume kabisa na kujikana nafsi yako jambo ambalo Yesu hulihitaji (Mat. 16:24; Mk 8:34; Lk 9:23) na huelewa 'kama nafsi yako' kuwa ruhusa ya ubinafsi wa mwanadamu. Pindi tusomapo Amri za Mungu mawazo yote mawili yanalingana katika ukweli na katika makosa. Kwa kuwa Mungu anataka tuzijali nafsi zetu na kufurahia, tamko la Yesu haliwezi kudai kujikana nafsi kwa asili. Wakati

kama mtu duni au kujiona hufai - lakini kwa urahisi anamaanisha utayari wa kuteseka mauaji ya mashahidi wa imani. "Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona" (Mathayo 16:24-25). Kumbuka kuwa maandiko haya ni sehemu ya Mahubiri yake makuu juu ya Mateso yake katika Mathayo 10:16-42. Neno 'Msalaba" na "Mateso" yote ni sawa kwa malengo ya utendaji.

9. Sehemu Kubwa za Maandiko Hujishughulisha na Mateso

Hoja: Sehemu kubwa za maandiko zinaweza tu kueleweka katika mazingira ya mauaji ya mashihidi wa imani yaliyopita au yanayotarajiwa.

Otto Michel akiandika juu ya Agano Jipya, asema, "Lugha ya mauaji ya mashahidi wa imani, fikra nzito juu ya mauaji ya mashahidi wa imani na historia juu ya mauaji ya mashahidi wa imani ni sehemu muhimu ya utamaduni wa mwanzo wa Kikristo, ni dhamira zinazojitokeza mara kwa mara. Hakuna kati ya maandiko ya mwanzo ya Kikristo ambayo hayaguswi na somo hili; kwa upande mwingine, hakuna kati ya maandiko ya mwanzo ya Kikristo yanayoweza kueleweka kabisa pasipo somo hili."[53] Michel anabuni Waraka kwa Waebrania, 1 Petro[54] na Ufunuo wa Mt. Yohana kama "Maandiko ya Mashahidi wa Imani'[55] kwa maana halisi ya neno, kwa kuwa makusudio ya vitabu hivyo ni kuandaa makundi ya Mungu (makanisa, *nyongeza ya mtafsiri*) kwa ajili ya mauaji ya mashahidi wa imani au kuwafariji katika mateso hayo. Kushindwa kuliewa hili mara nyingi hutuongoza katika kuuelewa kimakosa Waraka kwa Waebrania.[56] "Soma kwa kuzingatia usuli wa theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani,

---

atuambiapo tujichumie maisha yetu au kufurahia chakula chetu, vitu hivyo haviwezi kuwa ni makosa. Amri yake ya kujali matakwa ya wengine kabla ya yale ya kwetu, haiwezi kutanguliwa na nadharia za kisaikolojia. Biblia haiomwonei huruma mtu binafsi dhidi ya jamii, au mahitaji ya mtu binafsi dhidi ya yale ya wengine; vilevile (Biblia) si ya kibinafsi au ya kijamii, bali hulinda mambo ya mtu binafsi pasipo kumweka huru mbali na wajibu wa kijamii. Kanuni ya Dhahabu katika Mathayo 7:12 huunganisha kujipenda nafsi na upendo kwa wengine bila kutenganisha: "Basi yoyote mtakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii." Lengo kuu l amwanadamu, uzima wa milele na ushirika wa milele pamoja na Mungu una msingi katika kanuni mbili; Mungu huchukua kwanza nafasi katika maisha yetu, na mwanadamu hujinyenyekeza kwa utii kwake, na atamsifu yeye milele kama Bwana na Mwokozi. Kwa upande mwingine, hili ni jambo bora kabisa mtu awezalo kufanya kwa ajili yake mwenyewe.

53 Tazama Otto Michel. Prophet und Maertyrer. Beitraege zur Foerderung christlicher Theologie 37 (1932), Vol. 2. Bertelsmann: Guetersloh, 1932. p. 42.

54 *Ibid.*, p. 40-42; Tazama pia Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 204-209 na William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. University Press of America: Washington D.C., 1981 [Diss. Basel, 1977]. p. 63-69.

55 Otto Michel, Prophet und Maertyrer, *op. cit.*, p. 36.

56 *Ibid.*, pp. 37-40.

Waebrania hupoteza udhahania wake na huwa na ukweli halisi katika maisha."[57] Hususani Ufunuo, ambacho tutakizungumzia baadaye, mara nyingi hudhurika kutokana na waamini wa Magharibi kushindwa kutambua suala la msaada kwa ajili ya Kanisa lililo katika mateso.[58]

Ni vitabu vitatu tu vya Agano Jipya visivyotaja mateso. Hususani vitabu vinne viliandikwa kuwatia moyo Wakristo walioteswa na mateso ilikuwa mada kubwa katika mafundisho ya Yesu, Paulo, Petro, na Yohana.[59] Vitabu vingine vyote viliandikwa kwa Wakristo waliokuwa katika mateso, hususani 1 Timotheo, 1 Petro na Ufunuo.[60] Kitabu cha Matendo ya Mitume[61] kina sura mbili tu ambazo hazitaji mateso.[62] Shughuli zote za kimishenari na Theolojia za Paulo[63] zinaghubikwa na mauaji ya mashahidi wa imani, kama tutakavyoona.[64] Paulo aliweza kujiona yeye mwenyewe kama shahidi wa imani tu.[65]

---

57 *Ibid.*, p. 39; Tazama pia Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 200-204 na William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. University Press of America: Washington D.C., 1981 [Diss. Basel, 1977]. pp. 69-71.

58 *Ibid.*, p. 39; Tazama pia Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. a. a. O. pp. 211-228, kipekee 219-227, na William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. a. a. O. p. 73-78, na mlolongo wa mistari hapo chini juu ya mambo yaliyochukuliwa kutoka sehemu nyingine yahusuyo 'shahidi wa imani'.

59 Imechukuliwa kutoka Patrick Johnstone. "Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution". *op. cit.*, p. 4.

60 Imechukuliwa kutoka Preparing Believers for Suffering and Persecution: A Manual for Christian Workers. Hope: Bulawayo (Zimbabwe), n. d. (ca. 1979). 15 pp. p. 6.

61 Juu ya theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani katika Matendo ya Mitume, tazama: Scott Cunningham. Through Many Tribulations: The Theology of Persecution in Luke-Acts. Journal for the Study of the New Testament Supplement Series 142. Sheffield Academic Press: Sheffield (GB), 1997. Apg 186-294 + 295-342; William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 31-43; Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, 119-137.

62 Preparing Believers for Suffering and Persecution: A Manual for Christian Workers. Hope: Bulawayo (Zimbabwe), n. d. . (ca. 1979). 15 pp., p. 6.

63 Juu ya theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani katika maandiko ya Paulo, tazama John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. Journal for the Study of the New Testament Supplement Series 6. JSOT Press: Sheffield, 1985; Harry W. Tajra. The Martyrdom of St. Paul: Historical and Judicial: Context, Traditions, and Legends. Wissenschaftliche Untersuchungen zum Neuen Testament 67. Mohr Siebeck: Tuebingen, 1994. pp. 1-117 (pp. 118-197 juu ya mauaji ya mashahidi wa imani ya Paulo kutoka katika vyanzo vya baada ya nyakati za Biblia); Harry W. Tajra. The Trial of Paul. Mohr Siebeck: Tuebingen, 1989; William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 43-63; Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 156-200

64 Tazama pia: Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 161-164 (juu ya Wagalati), kr. 164-169 (juu ya 1 Kor.)

65 Tazama John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. *op. cit.*, pp. 93-106.

Mifano ya Kibiblia ya Mateso
Agano la Kale
*Abel aliuawa na Kaini (Mwa. 4:2-10; Mat. 23:5; Luka 11:51; Ebr. 11:4; 12:24)[66] *Isaka aliteseka kutokana na husuda ya Wafilisti, akiongoza kukoma kwa mateso (Mwa. 26:12-33) *Israeli [wanateswa] na Farao na Wamisri. Matokeo: Mungu anawakomboa kutoka utumwa (Kutoka 1-15) *Daudi [anateswa] na Sauli – Matokeo: Daudi analindwa, anakingwa na Mungu (1 Sam. 18-27); Zab. 31:13; 59:1-4) *Makuhani 58 wa Nobu waliuawa na Sauli na Doegi (1 Sam. 22) *Manabii waliuawa na Malkia Yezebeli (1 Fal. 18:3-4) *Eliya aliteswa na Ahabu na Yezebeli, ikisababisha wokovu wake kwa kukimbia (1 Fal. 18:10-19:2) *Nabii (mwenza wa Eliya) aliuawa na Malkia Yezebeli (1 Fal. 19:14+10) Elisha alitishiwa kifo na mfalme (2 Fal. 6:1). Matokeo - mmoja wa maafisa wa mfalme akafa kwa kukanyagwa (2 Fal. 17-20) *Nabii Hanani aliwekwa jela na Mfalme Asa (2 Nya. 16: 7-10) *Nabii Zekaria aliuawa kwa amri ya Mfalme Yoashi (2 Nya. 24:20-22). *Nabii Uria aliuawa na Mfalme Yehoyakimu (Yeremia 26: 20-23) *Yeremia alifungwa mara kadhaa, mara ya mwisho ni katika nyumba ya shimo, ikisababisha ukombozi unaojirudia (Yeremia 26:7-19; 37:1-38:13,; Pia tazama ukombozi wa mwanzo na ule uliofuata (Yeremia 20:24; 39:18) *Shadraka, Meshaki na Abednego katika tanuru la moto, ikisababisha ukombozi wa kimiujiza uliofanywa na malaika (Danieli 3) * Daniel katika tundu la simba, ikisababisha ukombozi wa kimiujiza uliofanywa na Mungu (Danieli 6)
Agano Jipya
*Yesu akiwa mtoto mchanga, lakini aliokolewa na kwa kukimbilia Misri (Mathayo 2:13-23)
*Yohana Mbatizaji alitiwa gerezani na kukatwa kichwa na Herode (Mathayo 14:3-13) *Stefano alipigwa mawe chini ya amri ya Sauli (Matendo 6:8-8: 3) *Wakristo kadhaa waliteswa na Herode (Matendo 12:1) *Yakobo aliuawa na Herode (Matendo 12:2) *Petro na Yohana gerezani, ikisababisha ukombozi uliofanywa na malaika (Matendo 4:1-31) *Paulo: Tazama hapo chini *Yohana alifungwa huko Patmo (Ufu. 1:9)

66 Tazama hapo chini.

10. Msaada katika Ufunuo

Hoja: Ufunuo wa Yohana una ujumbe wenye nguvu,[67] ambao daima huwatia moyo Wakristo katika mazingira mapya ya historia. Vyovyote tutafasilivyo maelezo ya Ufunuo, tunapaswa kukubaliana katika jambo moja: Kanisa hupanuka si kwa nguvu, utajiri au ulazimishi, bali kwa kupitia mamlaka ya Yesu, kwa Neno la Mungu, kwa Roho Mtakatifu na kwa maombi.

Hata Mungu anaporuhusu mamlaka ya kidini na kiserikali kuunganisha nguvu zao dhidi ya Mwili wa Kristo, mwonekano hudanganya – Kanisa la uongo na Serikali iliyopotoka kamwe havitaweza kuufuta Mwili wa Kristo bali wanajichimbia makaburi yao wenyewe. Mwishowe, Mungu atawafanya wagombane wao kwa wao, hivyo basi Serikali huwaharibu wapinzani wa kidini wa Kanisa, kama ilivyo katika Ufunuo, ambamo nguvu ya kidunia ya Mnyama ghafla inatimiza hukumu ya Mungu kwa Kahaba wa Babeli.

Yesu aliahidi, "... Nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda" (Mathayo 16:18). Ufalme wa Mungu hukua bila habari dhidi ya upinzani wote kutoka nguvu za kidini, kifalsafa, kiuchumi na kisiasa za dunia hii, kanuni ionekanayo vema katika Agano la Kale, na hasa katika kitabu cha Danieli[68]. Je, Yesu hakurudia tamko hili katika mifano yake yote kuhusu shamba la ngano na mizabibu, vile vile katika Utume Mkuu? Je, hakutuhakikishia kuwa milango ya kuzimu haitaweza kulishinda Kanisa lake? Historia hujirudia rudia kuthibitisha ahadi ya Yesu. Je, iko wapi Dola ya Kirumi, uko wapi Umanikaisimu*? Ziko wapi dini zote za zamani zilizosambaa dunia nzima, ambazo zote ziliushambulia Ukristo, lakini sasa zinafahamika na Wanahistoria tu? Yako wapi mapinduzi ya kiulimwengu yaliyoahidiwa na Unazi au Ukomunisti?

Je, hatuwezi kujifunza kutoka katika Ufunuo wa Yohana, kwamba Uislamu na Ukomunisti wa Kichina utashindwa pia, wakati Mungu kwa hekima yake anapoamuru hili? Paulo akizungumza juu yake mwenyewe, mara moja alisema, "Nami katika hiyo nimeteswa hata kufungwa kama mtenda mabaya; lakini neno la Mungu halifungwi" (2 Timotheo 2:9). Je, kauli yake hii si sawa na ukweli wa kusambaa kwa Injili; waamini binafsi wanaweza kufungwa na kudhibitiwa, lakini siyo Neno la Mungu au kanisa. "Mauaji ya Mashahidi wa Imani siku zote ni

67 Juu ya theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani katika katika Ufunuo, tazama: Hans von Campenhausen. Die Idee des Martyriums in der Alten Kirche. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1936[1]; 1964[2]. pp. 42-46.; Hans von Campenhausen. "Das Martyrium in der Mission". pp. 71-85 in: Heinzguenter Frohnes, Uwe W. Knorr (Ed.). Die Alte Kirche. Kirchengeschichte als Missionsgeschichte 1. Chr. Kaiser: Muenchen, 1974. p. 74-76; Bo Reicke. "The Inauguration of Catholic Martyrdom According to St. John the Divine". Augustinum (Rom) 20 (1980): 275-283 and Ivo Lesbaupin. Blessed are the Persecuted: The Early Church Under Siege. Orbis Books: Maryknoll (NY), 1987 [toleo laasili katika Kireno]; Spire (Hodder & Stoughton): Sevenoaks (GB), 1988. p. 62-95. Juu ya masomo haya na juu ya swali ni wimbi lipi la mateso linalorejewa, tazama: Thomas Schirrmacher. "Gruende fuer die Fruehdatierung der Offenbarung vor 70 n. Chr." pp. 129-154 in: David Chilton. Die grosse Truebsal. Reformatorischer Verlag Beese: Hamburg, 1996; pia katika Anstoesse Nr. 17. pp. 1-4 (Supplement to Neues vom Euroteam 1/1998).

68 Kwa maelezo zaidi tazama hoja ya 55

muhimu kama alama na ushuhuda wa imani, wakati dunia inajaribu kuwanyamazisha au kuwafunga minyororo watu wa Mungu. Wakati ambapo hawawezi tena kushuhudia kwa maneno au matendo ya imani na upendo, hawana kilichobakia bali ni ushuhuda wa mateso na kitendo cha kufa."[69]

11. Ukosoaji wa Kihistoria na Matatizo Yake kwa Vifungu vya Mashahidi wa Imani katika Agano Jipya

Hoja: Ukosoaji wa kihistoria wa kunukuu tarehe za baadaye (za mbele) kwa Agano Jipya unakanganya uundaji wa Theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani.

Ukosoaji wa Kihistoria huvipa vifungu vya Agano la Kale vinavyohusu mauaji ya mashahidi wa imani tarehe za baadaye (za mbele) sana. Kwa mfano, kitabu cha Danieli kilipaswa kiwe kimekwishaandikwa katika karne ya 2 KK. katika wakati wa mateso chini ya mfalme wa Ashuru, Antiokasi Epifenesi wa IV (175 –164 B.C). Vitabu vya Agano la Kale vya Apokrifa* kama vile nyongeza ya kitabu cha Danieli au Makabayo 1 na 2 vilitungwa katika kipindi hiki.[70] Nyaraka za Mashahidi wa Imani za Paulo,[71] kama vile Nyaraka za Kichungaji au – kutegemea na mwandishi - Wakolosai na Waefeso zinachukuliwa kama nyaraka za hivi karibuni zilizoghushiwa, vilevile na Ufunuo wa Mt. Yohana, ambao unadhaniwa kuwa haukuandikwa na mtume wala haukuandikwa kabla ya matukio unayoyaelezea.[72] Kama nadharia hizi zingekuwa sawa, basi Wayahudi na Kanisa la Kwanza wangekuwa tu na mkusayiko wa kumbukumbu-gushi zilizoandikwa na waamini wa baadaye wasiojulikana ili kuwafariji.

Zaidi ya yote matokeo ya kunukuu tarehe za baadaye yanamhusu Yesu, lakini watafiti wengi wanadhani kwamba Yesu hakutegemea kuuawa wala hakuamini yeye mwenyewe kuwa na kazi yoyote ya ukombozi.[73] Kwa mfano, somo muhimu kuhusu Mauaji wa Mashahidi wa Imani katika Kanisa la Kwanza hutuambia, "Mbali na mjadala wa miaka michache iliyopita, suala ya kwamba alielekeza kazi yoyote ya ukombozi kwa kifo chake haliwezi kupatiwa

---

69 Friedrich Graber. Der Glaubensweg des Volkes Gottes: Eine Erklaerung von Hebraeer 11 als Beitrag zum Verstaendnis des Alten Testamentes. Zwingli Verlag: Zuerich, 1943. p. 262.

70 Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 13-24; Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp.; Ernst Haag. "Die drei Maenner im Feuer nach Dan. 3:1-30". p. 20-50 und Ulrich Kellermann. "Das Danielbuch und die Maertyrertheologie der Auferstehung". p. 51-75 in: J. W. Van Henten (Ed.). Die Entstehung der juedischen Martyrologie. Studia Post-Biblica 38. E. J. Brill: Leiden, 1989 (Vifungu hivi vnatupatia mapitio mazuri ya theolojia ya Danieli ya mauaji ya mashahidi wa imani)

71 Z. B. Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 191-200

72 Tazama: Thomas Schirrmacher. "Gruende fuer die Fruehdatierung der Offenbarung vor 70 n. Chr." pp. 129-154 in: David Chilton. Die grosse Truebsal. Reformatorischer Verlag Beese: Hamburg, 1996 na maandiko yaliyonukuliwa kwa ajili ya ukanushi.

73 Tazama; Hans F. Bayer. Jesus' Predictions of Vindication and Resurrection. J. C. B. Mohr: Tuebingen, 1986, kwa ajili ya ukanushi bora kabisa, ambao unadhihirisha kwamba nabii zote za Kusulubiwa katika vitabu vya Injili vyaweza kurejewa katika Yesu na kwamba zilikuwa kiini cha ujumbe na mafundisho yake.

ufumbuzi."[74] "Hatupati viashiria vya wazi vya umuhimu ambavyo Yesu mwenyewe alivielekeza kwa kifo chake."[75]

Otto Michel amejumuisha kuwa, wasomi huwa na tabia ya kukataa matamko ya "awali" ya Yesu ambayo yanaonesha kuwa alikichukulia kifo chake kuwa cha muhimu, na wanaweka yafuatayo dhidi ta tamko lake " Kifo huthibitisha haki zake"[76] au "Nabii wa kweli hukamilishwa kwa kifo katika Yerusalemu (Luka 13:32-33)",[77] Michel analenga katika lugha ya mashahidi wa imani - kama vile " kikombe cha mateso" (Marko 10:39; 14:36) au "ubatizo wa mauti" (Marko 10:39; Luka 12:50) ambayo hupenyeza katika huduma yote ya Kristo.

12. Mwanadamu wa Kwanza Kufa Alikuwa Shahidi wa Imani

Hoja: Fasili za Agano Jipya zinamtangaza Habili, mwanadamu wa kwanza aliye kufa au aliyeuawa, shahidi wa imani aliyeuawa kwa sababu ya imani yake.[78]

Yesu alimchukulia Habili kama shahidi wa imani wa kwanza katika historia (Mat. 23:35; Luka 11:51) na mauaji yake kuwa ya kwanza katika mlolongo mrefu wa mateso ya manabii yaliyofanywa na wale waliofundisha Sheria lakini wakiitii kwa nje tu (Luka 11:50). Baba wa Kanisa Aurelius Augustinus aliandika, "Kutoka kwa Habili hadi mwisho wa dunia, safari ya Kanisa hupiga hatua kubwa kuelekea mbele kati ya mateso ya dunia na faraja ya Mungu."[79]

Dhabihu ya Kaini ilikuwa sawa katika hali yake ya nje kama ya Habili lakini Habili alitoa dhabihu "kwa imani" (Ebr. 11:4), wakati dhabihu ya Kaini ilibatilishwa kwa wivu wake na uasi wake dhidi ya Mungu (Mwa. 4:6-7). Akiwa amekasirishwa na Mungu kuipokea dhabihu ya Habili na kukataliwa kwa ile ya kwake, hatimaye Kaini alimuua ndugu yake: "Hivyo Agano la Kale huanza na ushuhuda kwamba dhabihu zilimaanisha kumridhisha Mungu kwa yale yaliyomo katika matendo ya nje ni kitu cha kukemewa, bali ni moyo wa unyenyekevu tu uifanyayo dhabihu kukubalika"[80]

---

74 Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 70.

75 *Ibid.*, pp. 69-70. Tazama pia: Eduard Lohse. Maertyrer und Gottesknecht. Forschungen zur Religion und Literatur des Alten und Neuen Testamentes 64 (NF 46). Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1955.

76 Otto Michel. Prophet und Maertyrer, *op. cit.*, p. 25.

77 *Ibid.*

78 Tokunboh Adeyemo. "Persecution: A Permanent Feature of the Church". p. 23-36 in: Brother Andrew (Ed.). Destined to Suffer? African Christians Face the Future. Open Doors: Orange (CA), 1979. p. 24. Linganisha kichwa cha habari cha kitabu na; George Fox. Cain against Abel: Representing New-England's Church-Hirarchy in Opposition to Her Christian Protestant Dissenters. no publisher.: London (?), 1675. 48 pp.

79 Imenukuliwa na: Zitiert nach Peter Beyerhaus. Die Bedeutung des Martyriums fuer den Aufbau des Leibes Christi. *op. cit.*, 131.

80 Gustav Friedrich Oehler. Theologie des Alten Testaments. J. F. Steinkopf: Stuttgart, 1891^{3}. p. 81.

Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania anaelewa vema kuwa damu ya Yesu "**hunena mambo mema zaidi kuliko ya Habili**" (Ebr. 12:4), lakini anaweka usambamba wa mambo hayo mawili. Katika Waebrani 11:4, anahusisha kifo cha Habili na ushuhuda (mauaji ya mashahidi wa imani) kwamba anaelewa kuwa ni ushuhuda wa haki iliyotolewa na Mungu. "Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki, Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo, ijapokuwa amekufa, angali akinena".

Mateso, kwa njia yoyote ile, mara kadhaa yanachochewa na husuda na wivu. Paulo wakati fulani alisema, "Bali wengine wanamhubiri Kristo kwa fitina, wala si kwa moyo mweupe, wakidhani kuongeza dhiki za kufungwa kwangu" (Flp. 1:17). Ili kuonesha wazo la mauaji ya mashahidi wa imani, Clement wa Rumi[81] anaongeza sehemu ndefu juu ya husuda kwenye barua yake, na anaandika kumhusu Paulo, Petro na mitume wengine, asema, "Kwa sababu ya husuda na wivu, nguzo kubwa na zenye haki sana (yaani, mashahidi wa imani. *Nyongeza ya mtafsiri*) ziliteswa na kupigwa hadi mauti.[82]

13. Manabii wa Agano la Kale Waliteswa

Hoja: Mateso si tu suala la Agano Jipya,[83] bali linajipenyeza hata katika Agano la Kale. Pia watu wanaomhofia Mungu waliteswa katika Agano la Kale katika kipindi chote.

Kufuatana na Yesu, Habili alikuwa shahidi wa kwanza wa Imani (Mat. 23: 35; Luka 11: 51). Shahidi wa imani wa mwisho wa Agano la Kale alikuwa Yohana Mbatizaji (Mat. 14: 1- 12; angalia pia 11: 11 – 13).

Jitihada, mgogoro, mateso na mauaji ya mashahidi wa imani ni sifa za manabii wa kweli. Daudi wakati fulani alisema, "Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini BWANA humponya nayo yote" (Zaburi 34:19). Kwa kuwa ni manabii wachache tu wa Agano la Kale walioachwa bila kuteswa, wao ni mifano halisi ya mauaji ya mashahidi wa imani (Ebr. 11:35-38 + 12:1; Mdo. 7: 51 –53; Mat. 5:12; 23: 31; Yakobo 5: 10; 1 Thes. 2:15). Stephano anauliza "Ni yupi katika manabii ambaye baba zenu hawaku**mtesa**? (Matendo ya Mitume 7: 52). Katika 1 Wathesolanike 2:14-15, Mateso huja kutokana na "**...Wayahudi, ambao walimwua Bwana Yesu, na manabii wao wenyewe, na kututesa sisi; wala hawampendezi Mungu, na wako kinyume na watu wote**". Yesu anawakumbusha wanafunzi wake "**Furahini, na kuzidi katika shangwe; kwa maana zawadi yenu ni kubwa huko mbinguni; kwa kuwa ndivyo**

81 Barua ya Kwanza ya Clemens 5,1 bis 6,2, abgedruckt in "Der Klemensbrief". p. 1-107 in: Joseph A. Fischer (Ed). Die Apostolischen Vaeter. Koesel: Muenchen, 1981[8] p. 30-33 and Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 42-47 (Nr. 21); tazama Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 229-247 und Hermann Strathmann. "martys, martyreo, martyria, martyrion". p. 477-520 in: Gerhard Kittel (Ed.) Theologisches Woerterbuch zum Neuen Testament. 10 Vols. W. Kohlhammer: Stuttgart 1990 (repr of 1933-1979). Vol . IV [1942]. p. 489-492, hier p. 511.

82 Barua ya Kwanza ya Clemens 5,2, "Der Klemensbrief". S. 1-107 katika: Joseph A. Fischer (Ed.). Die Apostolischen Vaeter. Koesel: Muenchen, 1981[8] p. 31.

83 Tazama: Hellmuth Frey. Die Botschaft des Alten Testamentes. Calwer Verlag: Stuttgart, 1938.

walivyowatesa manabii waliokuwepo kabla yenu." (Mat. 5: 12) na anawaonya Mafarisayo na Masadukayo kuwa wanajishuhudia dhidi ya nafsi zao wenyewe, kwamba "ni wana wao waliowaua manabii." (Mathayo 23: 31).[84]

Stauffer anayaeleza mauaji ya mashahidi wa imani ya Agano la Kale ya manabii kama " Utangulizi wa Mateso Makali ya Kristo Msalabani"[85] na mfano wa wakulima dhalimu wa mizabibu (Marko 12: 1-12) kama "muhtasari wa kitheolojia wa mauaji ya mashahidi wa imani ya Historia ya Wokovu"[86] ambamo manabii ni "watangulizi" wa Yesu.[87]

Theolojia ya Kiyahudi iliyofuata katikati ya Malaki na Yohana Mbatizaji, zaidi ya yote katika vitabu vya kiapokrifa, hutilia mkazo juu ya somo la mauaji ya mashahidi wa imani.[88] Tangu karne ya kwanza kabla ya Kristo, wazo kuwa manabii wa kweli ni lazima wateseke na hata kufa, lilikuwa ni sehemu muhimu ya theolojia ya Kiyahudi[89]. Hata hivyo, ingekuwa ni uongo kufikiri kuwa mtazamo

---

84 Tazama, . Johannes Beutler. "martyreo", "martyria", "martys". Col. 958-973 in: Exegetisches Woerterbuch zum Neuen Testament. 2 Vols. Vol. 2. W. Kohlhammer: Stuttgart, 1992[2]. p. 959.

85 Ethelbert Stauffer. Theologie des Neuen Testamentes. Bertelsmann: Guetersloh: 1941[1]. p. 81.

86 *Ibid.*, p. 80.

87 *Ibid.*, p. 81

88 Ethelbert Stauffer. Theologie des Neuen Testamentes. Bertelsmann: Guetersloh: 1941[1]; 1947[4]; 1948[5] amefupisha Septuaginta' (LXX) na kushughulikia somo hili katika Apokrifa, katika 1941[1] S. 314-317; tazama kr. 164-167; Tazama pia: Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 16-24; William H. C. Frend. Martyrdom and Persecution in the Early Church: A Study of a Conflict from the Maccabees to Donatus. Basil Blackwell: Oxford, 1965; Anchor Books: Garden City (NY), 1967; John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. *op. cit.*, pp. 13-46; Daniel Boyarin. Dying for God: Martyrdom and the Making of Christianity and Judaism. Stanford University Press: Stanford (CA), 1999; H. A. Fischel. "Martyr and Prophet: A Study in Jewish Literature". Jewish Quarterly Review 37 (1946/47): 265-280+363-386; William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 3-15; Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 23-65 (Tazama kr. 57-58 juu ya Flavius Josephus); Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 3-15; J. W. Van Henten (Ed.). Die Entstehung der juedischen Martyrologie. Studia Post-Biblica 38. E. J. Brill: Leiden, 1989; Kalman J. Kaplan, Matthew B. Schwartz (Ed.). Jewish Approaches to Suicide, Martyrdom, and Euthanasia. Jason Aronson: Northvale (NJ), 1997; Eugen Weiner, Anita Weiner. The Martyr's Conviction: A Sociological Analysis. Scholars Press: Atlanta (GA), 1990; J. W. Van Henten. The Maccabean Martyrs As Saviours of the Jewish People: A Study of 2 and 4 Maccabees. Supplements to the Journal for the Study of Judaism 57. E. J. Brill: Leiden (NL), 1997; F. W. Gass. "Das christliche Maertyrerthum in den ersten Jahrhunderten, und dessen Idee". Zeitschrift fuer die historische Theologie 29 (1859) 323-392 + 30 (1860) 315-381; H. A. Fischel. "Martyr and Prophet: A Study in Jewish Literature". Jewish Quarterly Review 37 (1946/47): 265-280+363-386; Hans-Werner Surkau. Martyrien in juedischer und fruehchristlicher Zeit. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1938. pp. 9-81; Wolfgang Nauck. "Freude im Leiden". Zeitschrift fuer neutestamentliche Wissenschaft 46 (1955): 68-80, hususani kr. 73-77; Norbert Brox. Zeuge und Maertyrer: Untersuchungen zur fruehchristlichen Zeugnis-Terminologie. Studien zum Alten und Neuen Testament 5. Koesel: Muenchen, 1961. pp. 132-173 + 18-23 und Ephraim Kanarfogel. "Martyrium II: Judentum". pp. 202-207 in: Gerhard Krause, Gerhard Mueller (Ed.). Theologische Realenzyklopaedie. Vol. 22. Walter de Gruyter: Berlin, 1992; Hermann Strathmann. "martys, martyreo, martyria, martyrion". *op. cit.*, pp. 489-492.

89 H. A. Fischel. "Martyr and Prophet: A Study in Jewish Literature". Jewish Quarterly Review 37 (1946/47): 265-280+363-386 und Hans-Joachim Schoeps. "Die juedischen Prophetenmorde". pp.

huu haukuwa na msingi katika Agano la Kale.[90] Maombi ya toba yaliyotolewa na Walawi katika kipindi cha Nehemia hujumuisha maungano ya Waisraeli. "Walakini hawakukutii, wakakuasi, wakaitupa sheria yako nyuma yao, wakawaua manabii wako walioshuhudu juu yako wapate kuwarejeza kwako; wakatenda machukizo makuu" (Nehemia 9:26). Adolf Schlatter amedhihirisha kuwa theolojia iliyofuata baadaye ya mauaji ya mashahidi wa imani ilitokana na theolojia ya Kiyahudi, ambayo iliibuka kutokana na mgogoro wa dini ya Kiyahudi na ulimwengu wa kihelenistiki*.[91]

Hans Von Campenhausen anadhani kwamba wazo la mauaji ya mashahidi wa imani kwa karibu sana lilifungamanishwa na Yesu na kuwa lilianzishwa na dini ya Kiyahudi,[92] lakini anauacha ukweli kwamba mtazamo binafsi wa Yesu juu ya nabii na shahidi wa imani ulikuwa na mizizi katika Agano la Kale.[93] Kielelezo bora kabisa cha mlolongo unaoanzia tangu mitume na wanafunzi wa Agano Jipya na kurudi nyuma kupitia Yesu na manabii wa Agano la Kale kinaweza kupatikana kwa Otto Michel, ambaye anawachukulia manabii wote hawa kuwa muhimu au mashahidi halisi wa imani.[94] Anaandika, "Katika vita ya Mungu na watu wake, katika vita kati ya wateule wa Mungu na nguvu za miungu za dunia hii, katika Uinjilisti wa watu walioitwa na Mungu, nabii hutokeza kama shahidi kwa watu ('Shahidi wa Imani"). Huu ni msingi wa theolojia ya Agano la Kale ya mauaji ya mashahidi wa imani, ambamo utangazaji kwa neno na matendo, vyote kwa pamoja ni ushuhuda kwa Mungu na kweli yake. Katika taratibu za kisheria kati ya Mungu na dunia, nabii anasimama na ushuhuda wake na ungamo lake kwa upande wa Mungu; kifo chake ni kipengele cha mwisho cha ushahidi wake. Asili ya mauaji ya mashahidi wa imani ni ofisi ya unabii."[95]

126-143 katika jambo lilelile. Katika kipindi cha Kanisa la Kwanza; J. C. B. Mohr: Tuebingen, 1950. Tazama pia F. W. Gass. "Das christliche Maertyrerthum in den ersten Jahrhunderten, und dessen Idee". Zeitschrift fuer die historische Theologie 29 (1859) 323-392 + 30 (1860) 315-381. Juu ya mapokeo ya "Mauaji ya Mitume", tazama; Lukas John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. *op. cit.*, pp.108-110.

90 Kutoka katika mtazamo wa Kiprotestanti.

91 Adolf Schlatter. Die Maertyrer in den Anfaengen der Kirche. Beitraege zur Foerderung christlicher Theologie 19 (1915), Vol. 3. Bertelsmann: Guetersloh, 1915.

92 Hans von Campenhausen. Die Idee des Martyriums in der Alten Kirche. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 19361; 19642. pp. 21-29+42-46.

93 Tazama: Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 3 und Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. XI.

94 Otto Michel. Prophet und Maertyrer. Beitraege zur Foerderung christlicher Theologie 37 (1932), Vol. 2. Bertelsmann: Guetersloh, 1932; See also: Marc Lods. Confesseurs et Martyrs: Successeurs des prophètes dans l'église des trois premiers siècles. Cahiers Théologique 41. Delachaux & Niestle: Neuchatel, 1958; Adolf Schlatter. Die Maertyrer in den Anfaengen der Kirche. *op. cit.*, juu ya historia yenye mlengo huu, tazama; Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 6-13.

95 Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 11-12; Kwa ajili ya Matendo ya Mitume na Luka, tazama: Scott Cunningham. Through Many Tribulations: The Theology of Persecution in Luke-Acts. *op. cit.*, pp. 307-313.

Daniel Boyarin anawasilisha mtazamo mpya wa kifungo cha asili kati ya dini ya Uyahudi na Ukristo, ambamo shule na mitazamo mbalimbali ya dini hizo ni vigumu kutenganishwa.[96] Anakataa mawazo yote ya kwamba theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani yalianzia katika dini ya Kiyahudi (mtazamo wa W. H. C. Frend) na msisitizo kwamba iliibukia katika Ukristo chini ya mateso ya Kirumi (mtazamo wa G. W. Bowersock[97]), lakini anaona hali ya daima ya kutoa - na - kupokea kati ya sehemu hizo mbili.

14. Watu wa Mungu Huwatesa Watu wa Mungu

Hoja: Ukianza na Agano la Kale, manabii na waamini wa kweli wamekuwa wakiteswa si tu na serikali ya Kiyahudi au za watu wa mataifa, bali na watu wa Mungu waliojiunga pamoja.

Israeli yenyewe iliwatesa manabii wa Agano la Kale, Yesu na mitume[98] (Yakobo alikuwa shahidi wa imani wa kwanza kati ya mitume.[99] Matendo ya Mitume 2:12. Yesu alimwondoa Yohana pekee kutoka katika mauaji ya mashahidi wa imani Yohana 21:15-20[100]). Bwana aliwakumbusha mara kwa mara watu wa wakati wake juu ya ukweli huu kila alipowalinganisha viongozi wa kiroho wa wakati wake na wale waliowaua manabii wa Agano la Kale (Mat. 5:10-12; 10:23; 23:34; Luka 11:49; 13:34; 21:12; Yohana 5:16; Angalia pia utetezi wa Stefano katika Matendo ya Mitume 7:52 na ule wa Petro katika Matendo ya Mitume 2:23). Mafarisayo na waandishi 'wajishuhudia' wenyewe kuwa "ninyi ni wana wao waliowaua manabii" (Mathayo 23:31).[101] Paulo anawathibitisha Wayahudi kuwa ni chanzo cha mateso. "**Maana ninyi ndugu zangu, mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu katika Kristo Yesu katika Uyahudi; kwa kuwa ninyi pia mmeteseka mambo yaleyale kutoka kwa watu wa taifa lenu wenyewe, kama na wao walivyoyapata kutoka kwa Wayahudi; ambao walimwua Bwana Yesu, na manabii wao wenyewe, na kututesa sisi; wala hawampendezi Mungu, na wako kinyume na watu wote**" (1 Thes. 2:14-15) na anahitimisha "Lakini kama vile siku zile yule aliyezaliwa kwa mwili alivyo**mtesa** yule aliyezaliwa kwa Roho ndivyo ilivyo na sasa" (Gal. 4:29).

Katika Agano Jipya, Wakristo wanateswa si tu na serikali za Mataifa, bali pia na Kanisa Linaloonekana kutotambua lifanyacho, ambalo linawatesa waamini wa kweli kwa jina la Mungu. Kwa pamoja serikali za Mataifa na viongozi wa Kiyahudi wanamtesa, wanamtendea vibaya na kumwua Yesu. Matendo ya

96 Daniel Boyarin. Dying for God: Martyrdom and the Making of Christianity and Judaism. Stanford University Press: Stanford (CA), 1999.

97 Tazama ufupisho wake katika uk. 93.

98 Tazama: Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*

99 Juu ya mauaji ya mashahidi wa imani ya Yakobo, tazama: Hans-Werner Surkau. Martyrien in juedischer und fruehchristlicher Zeit. *op. cit.*, pp. 119-126 kimejikita katika vyanzo vya kibiblia na vya nje ya biblia.

100 Ibid, p. 27.

101 Tazama; Johannes Beutler. "martyreo", "martyria", "martys". *op. cit.*, p. 959.

Mitume na maandiko ya Paulo pia yanahusisha mateso na Wayahudi, watu wa Mungu,[102] ambayo yanaoneshwa kwa uwazi katika Ufunuo, ambapo taasisi za kidini ambazo zinalitesa Kanisa zinaunganishwa na Kahaba wa Babeli. Kauli muhimu kabisa ya Bwana Yesu ni hii, "naam, saa yaja atakapodhania kila mtu awauaye ninyi ya kuwa anamtolea Mungu ibada" (Yohana 16:2).

15. Pia Wakristo Huwatesa Wakristo Wenzao Pamoja na Wengine

Hoja: Hakuna Theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani iwezayo kukanusha ukweli unaothibitishwa mara kwa mara kuwa Wakristo wao wenyewe wameeneza kifo na mateso "katika jina la imani ya Kikristo."[103] Tunahitaji tu kukumbuka uongofu wa kulazimisha kwa nguvu katika Zama za Kati, ukoloni katika Amerika ya Kusini, Vita vya kidini (Crusades), ugandamizaji wa wazushi, Inquisition (kipindi cha baraza la kuhoji wazushi) na mauaji ya kikatili yaliyopangwa ya Wayahudi.[104] Tangu karne ya 4, istilahi 'shahidi wa imani' imepanuliwa kuwajumuisha Wakristo waliouawa na Wakristo wengine wa 'Kiothodoksi'.[105]

Wakati wa Matengenezo ya kanisa, mauaji ya mashahidi wa imani na vitabu vya mashahidi wa imani vilibeba tabia isiyopendeza ya toba. Wakatoliki,[106]

---

102 Scott Cunningham. Through Many Tribulations. *op. cit.*, 301-307.

103 Eduard Christen. "Martyrium III/2.". *op. cit.*, p. 218; tazama insha kamili na Gerhard Ruhbach. "Christenverfolgung/-en". *op. cit.*, p. 370.

104 Tazama: Ephraim Kanarfogel. "Martyrium II: Judentum". *op. cit.*, p. 204-205.

105 Michael Slusser. "Martyrium III/1.". *op. cit.* p. 210 und Hans von Campenhausen. Die Idee des Martyriums in der Alten Kirche. *op. cit.* 1936[1]; 1964[2]. pp. 164-172.

106 Tazama pia bibliografia za Mashahidi wa Imani wa Kikatoliki; John Wagner. The Big Book of Martyrs. Paradox Press: New York, 1997 (Juvenile literature); Bernardo Olivera. How Far to Follow? The Martyrs of Atlas. St. Bebes: Petersham (MA), 1997; Joseph N. Tylenda. Jesuit Saints and Martyrs. Loyola University Press: Chicago 1984[1]; Loyola Press: Chicago, 1998[2]; Asa Hollister Craig. Christian Persecutions. Burlington (WI), 1899 (Anti Protestant); Giancarlo Politi Pime. "Maertyrer in China (I)". China heute 19 (2000) 1/2 (197/198): 27-35 (kwa sehem kubwa ni makuhani/mapadri); Helmut Moll (Ed.). Zeugen fuer Christus: Das deutsche Martyrologium des 20. Jahrhunderts. 2 Vols. in Commision of the German Bisops' Conferenence (Deutschen Bischofskonferenz). Schoeningh: Paderborn, 1999 (Biliografia 700, zikijumuisha Waprotestanti, lakini ni pale walipokufa na Wakatoliki tu), Tazama pia Gernot Facius. "'In unserem Jahrhundert sind die Maertyrer zurueckgekommen'". Die Welt vom 18.11.1999. p. 12 (Katika mwaka 1994, Papa Yohana Paulo II aliamuru Mikutano yote 104 ya maaskofu, kuwasilisha orodha ya Mashahidi wa Imani); Juu ya Utawala wa Tatu (Third Reich), tazama: Walter Adolph (Ed.). Im Schatten des Galgens: Zum Gedaechtnis der Blutzeugen in der nationalsozialistischen Kirchenverfolgung. Morus Verlag: Berlin, 1953 na kuhusu hali ya sasa: Martin Lange, Reinhold Iblacker (Ed.). Christenverfolgung in Suedamerika: Zeugen der Hoffnung. Herder: Freiburg, 1980 [Tafsiri ya Kiingereza:] Martin Lange, Reinhold Iblacker (Ed.). Witnesses of Hope: The Persecution of Christians in Latin America. Orbis Books: Maryknoll (NY), 1981.

Waothodoksi, Waprotestanti[107] Waanglikana,[108] Walutheri.[109] Wakalvini na Wanauzamo (Mapyuritani),[110] wote kwa pamoja waliunda makusanyo ya historia ya mashahidi wa imani[111] lakini kila moja ilijumuisha tu mashahidi wa imani kutoka katika kundi lake, likikanusha ukweli wenye kuuma kwamba madhehebu yote yalikuwa na wahanga wao lakini pia yaliwatesa Wakristo waliokuwa na ushawishi tofauti.[112] Kwa mfano, Kanisa Katoliki la Rumi lilikisia idadi ya mashahidi wa imani wapatao 6,850,000 tangu mwaka wa 1000, lakini lilitekeleza mauaji ya watu 4,580,000 Wakristo wasio Wakatoliki kipindi kile kile.[113] Waanabaptisti, [114]Wakweka na makundi mengine hayana tofauti.[115]

108 John Foxe. Book of Martyrs. W. Tegg: London, 1851 [1563]; matoleo mapya kabisa: John Foxe. Foxe's Book of Martyrs and How They Found Christ: in Their Own Words. Christian Classic Series 3. World Press Library: Springfield (MO), 1998 [1563]; John Foxe. Foxe's Book of Martyrs. Thomas Nelson Publ.: Nashville (TN), 2000 [1563] au ya hivi karibuni: Otto Michaelis. Protestantisches Maertyrerbuch: Bilder und Urkunden der evangelischen Maertyrerkirche aus vier Jahrhunderten. J. F. Steinkopf: Stuttgart, 1917UB261/340 yenye mashahidi wa imani wa Kiprotestanti kutoka katika nchi zote za Ulaya (pasipo Waanabaptisti).

109 Tazama; Helen C. White. Tudor Books of Saints and Martyrs. University of Wisconsin Press: Madison (WI), 1963.

110 Maertyrbuch: Denckwuerdige Reden vnnd Thaten vieler H. Maertyrer ... L. Koenig: Basel, 1597; Ludwig Rabus. Der Heiligen ausserwoehlten Gottes Zeugen, Bekennern vnd Martyrern ... 8 Vols. Balthasar Beck: Strassburg, 1552 & Samuel Emmel: *Ibid*., 1554-1558; Ludwig Rabus. Historien der Maertyrer ... 2 Vols. Josias Rihel: Strassburg, 1571 & 1572; juu ya Rabus, tazama: Gerhard Dedeke. Die protestantischen Maertyrerbuecher von Ludwig Rabus, Jean Crespin, und Adriaen van Haemstede und ihr gegenseitigen Verhaeltnisse. Diss.: Universitaet Halle-Wittenberg, 1924; Robert Kolb. For all the Saints. Changing Perceptions of Martyrdom and Sainthood in the Lutheran Reformation. Mercer University Press: Macon (GA), 1987. pp. 41-84+7 na kitabu kizima juu ya vitabu vya Mashahidi wa Imani wa Kilutheri (Tazama orodha kk. 165-174); kwa mifano ya hivi karibuni; C. J. Fick. Die Maertyrer der Evangelisch-Lutherischen Kirche. Vol. 1. Niedner: Saint Louis (USA), 1854 na Otto Michaelis. Protestantisches Maertyrerbuch. Steinkopf: Stuttgart, 1917; Tazama pia James Michael Weiss. "Luther and His Colleagues on the Lives of the Saints". The Harvard Library Bulletin 33 (1983): 174-195.

111 Tazama. J. C. Ryle. Fuenf Maertyrer: Treu bis in den Tod. CLV: Bielefeld, 1995 und George Fox. Cain against Abel: Representing New-England's Church-Hirarchy in Opposition to Her Christian Protestant Dissenters. no publ.: London (?), 1675. 48 pp. juu ya mateso ya wenye maoni tofauti na Kanisa la Uingereza (Dissenters) yaliyofanywa na Kanisa la Kiserikali la Kianglikana.

112 Tazama orodha hapo juu kwa ajili ya Bibliografia.

113 Mfano halisi ni: James C. Hefley, Marti Hefley, James Hefley. By Their Blood: Christian Martyrs of the Twentieth Century. Baker Book House: Grand Rapids (MI), 1994

114 Bong Rin Ro (Ed.). Christian Suffering in Asia. Evangelical Fellowship of Asia: Taichung (Taiwan), 1989 na David B. Barrett. Our Globe and How to Reach it. New Hope: Birmingham (AL), 1990. p. 18

115 Tazama. Ethelbert Stauffer. "Maertyrertheologie und Taeuferbewegung". *op. cit.*, . Juu ya vitabu vya Mashahidi wa Kianabaptisti, tazama hususani kr. 557 na kuendelea.

116 Hili lilianza mapema sana. Tazama; Thielemann J. (= Janszoon) Braght 1625-1664. Der blutige Schauplatz oder martyrer Spiegel der Tauffsgesinnten oder wehrlosen Christen. Drucks und Verlags der Bruederschafft: Ephrata (PA), 1748/49 (Anabaptists till 1660) = Thieleman J. (= Janszoon) Van Bragt. The Bloody Theater of Martyrs Mirror of the Defenseless Christians. Mennonite Publ. House: Scottdale (SAU), 1951[6.engl.]; Herald Press: Scottdale (USA), 1987[15], 1998[geb] [Toleo asilia, Kiholanzi: Bloedig tooneel, ca. 1660]; Isaac Ienington. Concerning Persecution. Robert Wilson: London, 1661. 31 pp. (on the Quakers), lakini pia kwa sasa; Dave Jackson, Neta Jackson. On Fire for Christ: Stories of Anabaptist Martyrs, Retold from Martyrs Mirror. Herald Press: Scottdale (USA), 1989. Juu ya

Ugandamizaji huu wa pamoja umendelea hadi nyakati za sasa. Kwa mfano, Kanisa la Othodoksi la Urusi liliwatesa wafuasi wa makanisa mengine.[116] Katika mazingira haya, Paulo A. Marshall ameyapinga makanisa ya kiliberali kwa kujali tu Wakristo wanaoteswa wa ushawishi mwingine wa kitheolojia.[117] Ukweli kwamba Wakristo wenyewe wanauana kwa jina la Mungu wa Kikristo, kama inavyotisha sana, si jambo jipya katika Maandiko. Biblia inatupa sababu mbili:

1. Maagano yote mawili yameweka wazi kuwa mbali na utii wa nje wa mifumo ya Kiyahudi au Kikristo, watu wa Mungu waliojipanga vema kama taasisi wanaweza kuwa adui wa Mungu na wote wanaweza kuwatesa manabii na kutenda dhambi mbaya sana ya kuwaua wengine 'kwa jina la Mungu' lakini ni kwa sababu zao wenyewe (linganisha 2 Tim. 3:5, "wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake'). Yesu alisema "Watawatenga na masinagogi; naam, saa yaja atakapodhania kila mtu awauaye ninyi anamtolea Mungu ibada" (Yohana 16:2). Ikiwa Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru, basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki (2 Kor 11:13-14).

2. Hakuna vitabu vitakatifu vya dini nyingine yoyote vimewachora wafuasi wake katika mtazamo hasi namna ile kama Biblia ilivyofanya kwa Wayahudi na Wakristo. Maandiko yanaeleza vizuri mafundisho ya kuwa Wayahudi na Wakristo pia ni wenye dhambi na wawezao kufanya dhambi za kutisha, na yanakataa sio tu uovu mkubwa ufanywao na watu wa Mataifa, bali pia wale wapaswao kuwa watu wa Mungu au watu wa Mungu kelikweli.

Tathmini binafsi inayotia aibu ni sehemu muhimu kwa dini ya Kiyahudi na Ukristo, tofauti na dini nyingine. Hakuna imani nyingine inayojitathmini yenyewe kwa nguvu kiasi hicho kama dini ya Kiyahudi ya Agano la Kale au Ukristo wa Agano Jipya. Maandiko yameweka wazi makosa ya viongozi kwa uwazi sana, na mara kwa mara Mungu hutumia watu wa nje kuwaita tena watu wake ili wamtii. Mwandishi wa Kiyahudi Hannes Stein, anaandika, "Tofauti na maandishi matakatifu ya Mohammed, Biblia ya Kiebrania si kitabu, bali ni maktaba, habari nzuri sana za kuvutia zilizowekwa pamoja, zilizosokotwa pamoja na watu wote kwa kipindi cha karne nyingi. Hakuna tendo hata moja la Israeli limeondolewa, hakuna uovu wa watu maarufu uliofutwa. Paul Badde anaandika, 'kimatendo kila kitabu cha Biblia hadi Agano Jipya kinaweza kuonekana kama kinapingana, kizuizi au komentari yenye kupinga vile vya awali au historia ya sasa'. Ikiwa ni matokeo ya kujidhihirisha katika kweli, jamii ya Uyahudi-Ukristo huthamini kujichunguza yenyewe kama kitu chenye thamani, sifa ya kuwa na

karne ya 20, tazama. Aron A. Toews. Mennonite Martyrs: People Who Suffered for Their Faith: 1920-1940. Kindred Press: Winnipeg (CAN) & Hillsboro (KS), 1990. (Mennonites in the Soviet Union).

117 Paul A. Marshall. Their Blood Cries out.*op. cit.*,. S. 119-143 Ch. "Christen gegen Christen".

117 *Ibid.*, pp. 162-178 na matamko ya Marshall katika Nina Shea. In The Lion's Den. *op. cit.*, pp. 14-15. Tazama pia uungaji mkono uliotolewa na 'makanisa ya kiliberali' huko Marekani kwa ajili ya Siku ya Maombi Duniani kwa ajili ya Wakristo Wanaoteswa na kwa ajili ya Azimio la Ushirika wa Kitaifa wa Kiinjili. (=Worldwide Day of Prayer for Persecuted Christians na Declaration of the National Association of Evangelicals).

uwezo, na si kukubali udhaifu. Katika utamaduni wa Kiislamu, hali hii ni tofauti kwa hali ya juu sana, kuitathmini kwa kuipinga historia yako ni kufuru isiyofikirika, hatari kwa msingi wa mafunuo na tusi kwa Nabii! Hivyo, nchi za Kiislamu haziwezi kuruhusu uhuru wa kuzungumza wala midahalo katika mabunge huru yaliyochaguliwa."[118]

Kamwe Biblia haiweki imani au kutokuamini katika madaraja kwa kigezo cha ujamii* au taifa, bali huwaelezea Mataifa na Wayahudi wasioamini kwa maneno yale yale. Wakati wa kutoka Misri, si tu Wamisri waliwabugudhi Waisraeli, bali pia Wamisri wasioamini na Waisraeli wote waliwapinga Wamisri na Wayahudi walioamini.[119] Kwa sababu hii, Wamisri wale waliosikia maonyo ya Musa waliruhusiwa kuungana na Waisraeli (Kutoka 12:28. Angalia pia Hesabu 11:4; Law. 24:10), wakati Waisraeli wasioamini waliteketezwa baada ya kuabudu Ndama wa Dhahabu (Kutoka 32).

Ukristo huwa kitu cha kuogofya unapokataa nguvu ya kweli ya imani (2 Tim. 3:5, "Wenye mfano wa utawa, lakini wakikana nguvu zake") au unapochukua nafasi ya sheria na amri za mwanadamu na uzifanya badala ya ufunuo wa ki-Mungu (Marko 7:1-3; Isaya 28:13-14). Agano Jipya linawapinga Wayahudi kwa sababu, wakati walipoyasoma Maandiko, walipuuza kipengele muhimu - Yesu (Yohana 5: 39) na wao wenyewe walishindwa kujiweka chini yake (Warumi 10:2-3). Walivutwa na neno la Mungu lakini hawakuishi kwa mujibu wake (Warumi 2).

Kufananishwa kwa Kanisa Katoliki la Rumi na Kahaba wa Babeli, Martin Luther na wasomi wengine wa Kiprotestanti waliielewa kanuni ya Biblia, kuwa Kanisa la kweli linateswa na kanisa la uongo, ingawa miaka 450 baadaye, tunahoji wazo kuwa Kanisa Katoliki la wakati wa Matengenezo limekuwa utimilifu pekee wa historia wa ishara hiyo.

16. Mateso ni Suala la Kanisa la Kikristo Kiulimwengu (Kiekumenika)

Hoja: Mateso ni suala la Kanisa la Kikristo kiulimwengu,[120] cha kusikitisha ni suala lisababishalo ukosefu wa umoja wa dhati miongoni mwa Wakristo.

Ndugu Andrew, Mdachi mtangulizi wa kuhudumia Wakristo wateswao wakati fulani alijiona akilazimishwa kukubali kuwa "Mengi ya mateso katika Kanisa la kiulimwengu yanachochewa na wazo potovu kwamba 'Mwili wa Kristo'

---

118 Hannes Stein. Moses und die Offenbarung der Demokratie. Rowohlt Berlin Verlag: Berlin, 1998. p. 47.

119 Tazama; Jonathan Magonet. "Die Einstellung des Buches Exodus gegenueber AEgypten". Concilium 24 (1988): 439-445, hier pp. 439+441. Kutoka hutofautisha kati ya Farao aliyefanywa kuwa mgumu na wale maofisa wake na watu wake waliomsikiliza Mungu (*Ibid*., uk. 442). Kwa kuwa baadhi ya Wamisri walileta mifugo yao baada ya kusikia hukumu ijayo (Kutoka 9:20), ni lazima walikuwa wamemwamini Musa.

120 "The Yakunin Hearing July 22-26, 1983 Vancouver ..." (Christian Solidarity International). Programmheft.

ni sawa na 'kanisa langu' (kanisa la mtaa, dhehebu, fundisho lipaswalo kuaminiwa bila kupingwa - yaani dogma)."[121]

Ni ukweli wa kusikitisha wa historia ya kanisa kwamba mateso yanaweza pia kuwa chanzo cha mgogoro na mgawanyiko miongoni mwa Wakristo.[122] Tumekwisha kuona kuwa migawanyiko yote katika karne ya kwanza zilisababishwa na mateso na matokeo ya jinsi Kanisa lilivyojihusisha nayo. Kwa usawa, ikiwa ni wenye kuogofya, mfano wa wakati huu ulitokea huko Korea, pale ambapo watawala wa Kijapani (1910-1945) walipowataka Wakorea wote kuabudu kwa kugusisha vichwa vyao mpaka chini ya ardhi kwa madhabahu za Shinto ili kumheshimu Mfalme wa Kijapani na mungu mke - jua. Baada ya upinzani wa muda mrefu, katika mwaka 1937 na 1938, makundi mengi ya Wakristo yalijisalimisha kutokana na ongezeko la mbinyo usiovumilika, lakini yaligawanya vibaya sana (hususani Wapresbaiteria) juu ya umuhimu wa sherehe iliyotakiwa; je ilikuwa ni ibada ya kidini au utamaduni wa kijamii tu? Miaka sitini baadaye, suala lilibaki bila kutatuliwa na ufa bado unadhihirika, ingawa tatizo la kimsingi limekwisha toweka muda mrefu tayari.[123]

17. Shahidi wa Imani wa Kwanza Aliye Mkristo

Hoja: Si kwa bahati, kitabu cha Matendo ya Mitume kinahusisha mauaji ya shahidi wa imani wa kwanza wa Agano Jipya, Stefano[124] (Matendo ya Mitume 6:8 - 8:3[125]) kwa undani mkubwa.

---

121 Bruder Andrew. "Wir brauchen eine neue Sicht der leidenden Kirche". Geoeffnete Tueren. Rundbrief Geoeffnete Tueren (Frutigen, Schweiz). Febr 1980. pp 1-3, here p. 3; sawasawa na; Preparing Believers for Suffering and Persecution: A Manual for Christian Workers. Hope: Bulawayo (Zimbabwe), n. d. (ca. 1979). 15 pp. p. 7+8.

122 Tazama; Albert Ehrhard. Die Kirche der Maertyrer. pp. 122-267. Erhard anadhihirisha kuwa mabishano na migongano mingi ya kidogma ya zamani iliibuka kutokana na vikundi na mavuguvugu ya kizushi katika Kanisa la Kwanza, na mara nyingi yalihusisha mateso.

123 Tazama;. "Der geistliche Kampf um Korea". Supplement to HMK-Kurier M 11403. Xeroxed. Hilfsaktion Maertyrer Kirche: Uhldingen, 1997. 4 pp. und Peter Pattison. Crisis Unaware: A Doctor Examines the Korean Church. OMF Books: Sevenoaks (GB), 1981.

124 Tazama; Hans-Werner Surkau. Martyrien in juedischer und fruehchristlicher Zeit. *op. cit.*, pp. 105-119; Hans von Campenhausen. Die Idee des Martyriums in der Alten Kirche. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1936[1]; 1964[2]. pp. 57-59; Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 123-132; William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 36-43. Jacob Thiessen. Die Stephanusrede: Apg 7,2-53, Verlag fuer Theologie und Religionswissenschaft: Nuernberg, 1999. Thiessen anachunguza na kufasili hotuba ya Stefano kutoka katika Agano la Kale na kutoka katika mtazamo wa Kiyahudi na anatoa kwa kiasi maelezo ya kutosha, lakini hajishughulishi vya kutosha na mitazamo mingine au na somo la mauaji ya mashahidi wa imani.

125 Kwa mujibu wa William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, p. 38, Luka anaonesha kumpa umakini mkubwa Stefano, si kwa sababu alikuwa Shahidi wa kwanza wa imani, bali kwa sababu ya matokeo ya mauaji ya ushahidi wake wa imani (Matendo 8:1), lakini hata kwa mwelekeo huu, suala la mauaji ya mashahidi wa imani bado ni kiini cha kifungu. Pia, Luka hakuhitaji kuelezea sana; anataja kifo cha Yakobo katika sentensi moja (Matendo 12:2), na angeweza kufupisha hotuba ya Stefano, kama alivyofanya kwa nyingine katika Matendo.

Tukio hili si kwa bahati, pia mwonekano wa kwanza wa Sauli wa Taso (Matendo ya Mitume 7:58; 8:1+3; 9:1), aliyeanza kama mtesaji wa Wakristo lakini baadaye yeye mwenyewe akawa mmishenari mteswaji na kushiriki jukumu hilo kubwa katika historia ya umishenari. Kwa usawa kabisa, 1. Stefano anajiona mwenyewe kama mrithi wa manabii wa Agano la Kale (Matendo ya Mitume 7:51-52), na 2. mateso yake hayatokani na Serikali, bali kutoka kwa watu wa Mungu ambao hawakuongozwa vema, kwa nafsi ya viongozi wao, makuhani wakuu na wanatheolojia viongozi, Mafarisayo (kama vile Sauli. Matendo ya Mitume 6:12; 8:1). Kama ilivyo katika mahubiri ya Petro wakati wa Pentekoste (Matendo ya Mitume 2:14-36), Stefano anawatia hatiani watu wa Mungu kwa kumsulubisha Masihi.

C. Kuzungumza juu ya Yesu ni kuzungumuza juu ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani

18. Yesu ni Kielelezo cha Shahidi wa Imani

Hoja: Yesu ni kielelezo-tangulizi cha Shahidi wa imani. "Ukristo wa mwanzo ulifasili kazi ya Kristo katika aina za theolojia ya Mashahidi wa imani, na ulifasili hatima ya mashahidi wa imani kwa mujibu wa hatima ya Kristo."[126] Waraka ulioandikwa kwa makanisa ya Vienne na Lyon mwaka 177 BK. humwita "Kristo mwaminifu na shahidi wa imani wa kweli."[127] Utabiri juu ya kuuawa kwake unaambatanishwa na huduma yake yote hapa duniani tangu mwanzoni kabisa (kwa mfano, Mat. 16:21; 17:22-23; 10:17-19; 26:2). Mateso ya msalaba yanachukua sehemu kubwa ya vitabu vya Injili na yanahusisha usaliti wa Yuda, mashitaka ya uongo, kesi isiyozingatia sheria, mateso na uuaji wa maumivu makali kabisa mikononi mwa viongozi wa Israeli na Serikali ya Rumi, kwa undani mkubwa.[128] Daima Paulo alimwelezea Yesu kama kilelezo-tangulizi cha shahidi wa imani na kama mfano kwa Wakristo wote.[129] Kumbukumbu za Kanisa la Kwanza juu ya mauaji ya mashahidi wa imani[130] zilimwona Yesu kuwa kielelezo-tangulizi cha shahidi wa imani, ambacho hakiwezi kupitwa na kingine chochote.[131]

---

126 Ethelbert Stauffer. "Maertyrertheologie und Taeuferbewegung". *op. cit.* p. 547-548.

127 Katika Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 91; Tazama pia Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, pp. 233-245 [Book 5, Ch. 2-3].

128 Tazama: Hans-Werner Surkau. Martyrien in juedischer und fruehchristlicher Zeit.*op. cit.*, pp. 82-104. Surkau anawasilisha Mateso ya Kristo kama taarifa ya shahidi wa imani. Juu ya wazo la mauaji ya mashahidi wa imani katika vitabu vya Ijnili, tazama; Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 66-119+137-150; juu ya Luka, tazama; Lukas Scott Cunningham. Through Many Tribulations: The Theology of Persecution in Luke-Acts. *op. cit.*, pp. 23-185 + 295-342.

129 Tazama; John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. *op. cit.* 74-92.

130 Tazama maelezo katika tasnifu mbalimbali.

131 Leonardo Boff. "Martyrdom: An Attempt at Systematic Reflection". pp. 12-17 in: Johannes Baptist Metz, Edward Schillebeeckx (Ed). Martyrdom Today.*op. cit.*

19. Kufa kwa ajili ya Marafiki ni Hali ya Juu Kabisa ya Upendo

Hoja: Kutoa maisha yako kwa ajili ya wengine ni hali ya juu kabisa ya upendo katika dunia hii.

Kwa sababu Yesu anafundisha wazi, "Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi. Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake." (Yohana 15:12-13), upendo wa Mkristo daima umeshikizwa kuelekea dhabihu kuu kupita zote ya Yesu, kifo chake pale Msalabani, "mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato." (Efe. 5:2). Kwa sababu hii, mume ni lazima awe tayari kufa kwa ajili ya mke wake; hili ni kanusho la wazo lolote la kidikteta la 'kichwa cha nyumba! "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake;" (Efe. 5:25). Kanisa la kwanza lilifanya vema kuchukulia mauaji ya ashahidi wa imani kwa ajili ya Kristo kuwa uthibitisho mkuu wa upendo wa mtu kwa Mungu.

20. Kwa Uhalisia, Mateso Yote Huelekezwa kwa Yesu

Hoja: Yesu ndiye mlengwa halisi wa mateso yote. Kwa sababu hii Yesu anamwuliza Sauli, "Sauli, Sauli mbona wani**tesa**?" (Matendo ya Mitume 9:4; 22:7; 26:14), na anajitambulisha kama, "... Mimi ndimi Yesu unayeni**tesa** wewe" (Matendo ya Mitume 9:5; 22:8; 26:15).

Sababu ya kweli ya mateso ya Wakristo ni Kristo, ambaye anahalalisha mkanganyo, "Kadiri Kanisa linavyomfahamu Kristo vema na kumshuhudia vema, ndivyo litakavyokumbana na mkanganyiko, mkabiliano na hasira ya Mpinga Kristo."[132] Mara zote Yesu aliwakumbusha wanafunzi wake, kuwa wangeteswa kwa ajili yake (kwa mfano: Mat. 10:22 = Luka 21:17. "Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu"; Mat. 16:25, "Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona."; Luka 21:12, "Lakini, kabla hayo yote hayajatokea, watawakamata na kuwa**tesa**; watawapeleka mbele ya masinagogi, na kuwaua magerezani, mkipelekwa mbele ya wafalme na **viongozi** kwa ajili ya jina langu".)

21. Mwendelezo wa Mateso ya Kristo

Hoja: Mateso ya Mkristo ni ya kipekee kwa sababu yanaendeleza mateso ya Kristo.

Makusanyo mapya ya Golgotha ni ya muhimu katika ufahamu wa mateso ya Kanisa. Howard A. Snyder anauelezea Msalaba kama dhamana ya mateso ya Kanisa, na sio uepukaji wake kutoka katika mateso.[133] Paulo hakuyachukulia

---

132 Martin Luthers Saemtliche Schriften. Ed. by Joh. Georg Walch. Verlag der Lutherischen Buchhandlung H. Harms: Gross Oesingen, 1986 (repr. of 1910²). Vol. V, p. 106.

133 Howard A. Snyder. The Community of the King. IVP: Downers grove (IL), 1977.

mateso yake kama ukombozi,[134] lakini bado anayaelezea kama "Ushirika pamoja na mateso ya Kristo."[135] Katika 2 Wakorintho 1:5 ("Kwa kuwa kama vile mateso ya Kristo yanavyozidi kwetu, vivyo hivyo faraja yetu inazidi kwa njia ya Kristo."), Paulo anahusisha masumbufu chini ya mateso na mateso ya Kristo. Analirudia wazo hilo kwa uwazi zaidi[136] katika Wakolosai 1:24: "Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake." Tena, katika Wagalatia 6:17, anaandika, "Tangu sasa mtu asinitaabishe; kwa maana ninachukua mwilini mwangu chapa zake Yesu," na katika Wafilipi 3:10, anajitakia "ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake". Katika 2 Wakorintho 4:8-10 anaongeza, "**Twasumbuliwa pande zote, hata hivyo hatuhuzunishwi; tunatiwa shaka lakini hatukati tamaa; Tunateswa, lakini hatuachwi; tunatupwa chini, lakini hatuangamizwi; Daima katika miili tunabeba kufa kwa Bwana Yesu, ili kwamba pia maisha ya Yesu yaweze kudhihirishwa katika miili yetu.**"[137] Katika maneno yake kuhusu 'moto' na 'majaribu' Petro anashirikiana na mtazamo wa Paulo, na anaandika "**Lakini furahini, kwa kadri mlivyo washiriki wa mateso ya Kristo; kwamba, wakati wa utukufu wake utakapofunuliwa, mweze kufurahi tena kwa furaha izidiyo sana.**" (1 Pet. 4:13).

22. Yesu kama Kielelezo cha Kuigwa – Mashahidi wa Imani ni Vielelezo vya Kuigwa

Hoja: Kifo cha Yesu cha ushahidi wa imani kinamfanya yeye kuwa kielelezo chetu cha kuigwa wakati tunapopata mateso.

Yesu Kristo mwenyewe aliteseka sawa na mashahidi wa imani wa Kanisa lake, na tena zaidi. "Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa." (Ebr. 2:18'; Ebr. 4:15). Martin Luther aliandika, "Kristo Bwana alipaswa kupata mateso katika mikono ya shetani na dunia: hatupaswi kutamani chochote kilicho bora."[138] Yesu anawakumbusha wanafunzi wake, "Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa walini**tesa** mimi, pia watawa**tesa** ninyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu." (Yohana 15:20). Kwa ajili ya kuelewa mazingira yake soma mistari ya 18-21). Tunaposoma maneno yake, "Angalieni, mimi nawatuma kama vile kondoo kati ya mbwa-mwitu; basi iweni na busara kama nyoka, **na msio na madhara kama njiwa.**" (Mat. 10:16), tunapaswa kukumbuka kuwa yeye ni

134 Auch im Martyrium des Polykarp Herbert Musurillo (Ed.). The Acts of Christian Martyrs. Clarendon Press: Oxford, 1972, 'Martyrium des Polykarp' pp. 2-21. Maelezo ya mauaji ya mashahidi wa imani ya Polycarp (ca. 155-157 A. D.), kwa mfano, hutofautisha kati ya mateso ya ukombozi ya Kristo na mateso ya mashahidi wa imani.

135 Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 31-33.

136 Harry W. Tajra. The Martyrdom of St. *op. cit.*, pp. 52-54.

137 Tazama: William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, p. 51-52.

138 Martin Luthers Saemtliche Schriften. *op. cit.*, Vol. III, p. 691.

Mwana kondoo wa Mungu[139] aliyetumwa miongoni mwa mbwa- mwitu kuteseka na kufa kwa amani kwa ajili ya wengine.

Mfano wake mwenyewe, ambao unafanya jukumu muhimu namna hiyo katika Agano Jipya,[140] unajumuisha mateso yake na kujishughulisha kwake na mateso. Paulo alijua kuwa ukweli wa mateso yake ulikuwa umemfunza Timotheo kukabiliana na hali hizo: "Bali wewe umeyafuata mafundisho yangu, na mwenendo wangu, na makusudi yangu, na imani, na uvumilivu, na upendo na saburi; tena na adha zangu na mateso, mambo yaliyonipata katika Antiokia, katika Ikonio, na katika Listra, kila namna ya **mateso** niliyoistahimili, naye Bwana aliniokoa katika hayo yote. Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wata**teswa**." (2 Tim. 3:10-12). Pia Wathesalonike walikuwa si tu waigaji wa Paulo, Sila na Timotheo chini ya mateso, bali pia kilelezo cha kuigwa kwa waumini katika majimbo ya karibu. "Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi, pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu. Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya." (1 Thes. 1:6-7). "**Maana ninyi ndugu zangu, mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu katika Kristo Yesu katika Uyahudi; kwa kuwa ninyi pia mmeteseka mambo yaleyale kutoka kwa watu wa taifa lenu wenyewe, kama na wao walivyoyapata kutoka kwa Wayahudi; ambao walimwua Bwana Yesu, na manabii wao wenyewe, na kututesa sisi; wala hawampendezi Mungu, na wako kinyume na watu wote.**" (1 Thes. 2:14-15).

23. Theolojia ya Msalaba ('theologia crucis')

Hoja: Bila kwazo la Msalaba kusingekuwa na mateso.

Ethelbert Stauffer, akiandika kuhusu mjadala wa mateso ya Kristo na mitume, anasema "Hii 'Theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani' inapata kiini cha umbo lake na maana yake katika ukweli wa Msalaba."[141] Hivyo Paulo anaandika,[142] "**Nami, ndugu zangu ikiwa ninahubiri habari ya kutahiriwa, kwa nini ningali ninateswa? Basi kwazo la msalaba limefikia ukomo!**" (Gal. 5:11) – pasipo Msalaba, kusingekuwa na mateso. Anawashutumu wapinzani wake kwa kutahiriwa tu ili kukwepa mateso, "**Kama**

---

139 Ludwig Bertsch SJ. "Predigtgedanken". p. 11-15 in: Gebetstag fuer die verfolgte Kirche 1992. Arbeitshilfen 99. Sekretariat der Deutschen Bischofskonferenz: Bonn, 1992. p. 14.

140 Tazama: Thomas Schirrmacher. "Jesus as Master Educator and Trainer". Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 2/2000: 1-4, na toleo refu kwa Kijerumani "Jesus als Meisterpaedagoge". Bibel und Gemeinde 95 (1995): 17-22 = Querschnitte 11 (1998) 11 (Nov): 1-4 = Anstoesse 14. p. 1-4 - Beilage zu Neues vom Euroteam 1/1997 und "Paulus und seine Mitarbeiter: Vom Umgang 'neutestamentlicher Missionare' miteinander". S. 64-81 in: Klaus Brinkmann (Ed.). Missionare und ihr Dienst im Gastland. Referate der Jahrestagung 1997 des afem. edition afem - mission reports 5. Verlag fuer Kultur und Wissenschaft: Bonn, 1998 = Evangelikale Missiologie 15 (1999) 1: 13-22.

141 Ethelbert Stauffer. "Maertyrertheologie und Taeuferbewegung". *op. cit.*, p. 546.

142 Juu ya mtazamo wa Paulo kuhusu Msalaba na Mauaji ya mashahidi wa Imani, tazama: John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. *op. cit.*, pp 47-73.

wengi watakavyo kuonekana ni wazuri kwa mambo ya mwili, ndio wanaowashurutisha kutahiriwa; makusudi wasiudhiwe kwa ajili ya msalaba wa Kristo, hilo tu." (Gal. 6:12; pia angalia mstari wa 14).[143] 'Neno la Msalaba' ni 'upuuzi' kwa wasioamini (1 Kor. 1:18), ni kikwazo kwa Wayahudi na upuuzi kwa mataifa (1 Kor. 1:23), lakini ni kiini cha historia ya wokovu. Hivyo, moyo wa ujumbe wa mitume ni "Yesu Kristo, naye amesulubiwa." (1 Kor. 2:2). ".. bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulubiwa;" (1 Kor. 1:23). Hivyo ujumbe wa Msalaba ni utukufu wa injili na vilevile upuuzi wake (1 Kor. 1:17-25; Gal. 6:11-14). Theolojia ni ama theolojia ya Msalaba ('theogia Crucis') au hakuna theolojia kabisa, kama ambavyo Martin Luther[144] na John Calvin[145] wamesisitiza.

"Theologia Crucis inafundisha: "Bwana aliyefufuka ni Bwana aliyesulubiwa,"[146] lakini hatupaswi kupindua kifo cha Yesu Msalabani kuwa ushindi wa kibinadamu. Alfred de Quervain aliunda ukweli huu, "Si kwa sababu ya mapambano yake ya utukufu na ushindi, si kwa sababu ya wema wake, Kristo ni Bwana, lakini ni kwa sababu ya utii wake na imani katika hukumu."[147] "Kifo hiki si tu kinapungukiwa nuru ya kitamaduni na ya kibinadamu ya kifo cha Sokreti; pia kinapungukiwa kila kitu tunachofikiria kuwa ni cha kupendeza, cha kujenga au kuwa na uelewa juu ya ushindi."[148] "Asili ya sulubisho la Kristo siyo (tukizungumza kibinadamu) fedheha yake na ukosefu wake wa utukufu, bali ukweli kwamba Kristo alikufa kama Mwenye dhambi kwa ajili ya wenye dhambi."[149]

---

143 Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*, p. 33-34.

144 Walther von Loewenich. Luthers theologia crucis. Luther-Verlag: Bielefeld, 1982[6] . Von Lowevenich anadhihirisha kwamba theolojia ya Luther ya Msalaba haikutambua tu kazi yake ya kwanza (kr. 14-15) lakini pia mtazamo wake juu ya mateso yote halisi ya Mkristo (kk. 135-144). Robert. A Kelly. "The Suffering Church: A Study of Luthers Theologia Crucis". Concordia Theological Quarterly 50 (1986): 3-17, anaonesha kwamba theolojia ya Msalaba ni sababu kwamba mateso ndio kiini cha kazi ya Luther. Robert Kolb. For all the Saints. Changing Perceptions of Martyrdom and Sainthood in the Lutheran Reformation. *op. cit.*, hata hivyo, anaonesha jinsi wanatheolojia wa Kilutherani wa Baada-Matengenezo walivyosahau kipaumbele hiki. Kwa makusanyo ya hoja za Luther juu ya mateso, tazama; Otto Michaelis. Protestantisches Maertyrerbuch. *op. cit.*, pp. 217-245. Ethelbert Stauffer. "Maertyrertheologie und Taeuferbewegung". *op. cit.*, pp. 550-553, anadhani kwamba Luther anafupisha, anapitia upya na kutathmini theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani iliyotengenezwa katika karne zilizopita. Luther mwenyewe alitarajia kuuawa kama shahidi wa imani. Katika mwaka 1523, wakati watawa wa kiume wa kambi ya Augustine, Heinrich Voes na Johann von Essen walipochomwa moto juu ya miti (mti ulionyooka kama fito) huko Bruessel, aliyajadili mauaji yao kwa kirefu na akatamka wazi kwamba kifo chao kilipaswa kumpata yeye kwanza *Ibid.*, p. 551.

145 *Ibid.*, p. 218.

146 Alfred de Quervain. Die Heiligung. Ethik Erster Teil. Evangelischer Verlag: Zollikon, 1946[2] [1942[1]]. p. 151.

147 *Ibid.*, p. 152.

148 *Ibid.*, p. 151.

149 *Ibid.*, p. 151.

D. Kanisa Chini ya Mateso

24. Hakuna Kanisa bila Mauaji ya Mashahidi wa Imani

Hoja: "Mauaji ya mashahidi wa imani ni sehemu ya Kanisa,[150] **sehemu ya kiini chake kabisa,**[151] **na mateso ni alama ya umisheni** na Kanisa kati ya kupaa kwa Kristo na kurudi kwake,[152] kwa kuwa "... imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi" (Matendo ya Mitume 14:22). Paulo anaandika "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu **watateswa**"[153] (2 Tim. 3:12). Kutoka Agano la Kale anachota mafundisho, "Lakini kama vile siku zile yule aliyezaliwa kwa mwili **alivyomtesa** yule aliyezaliwa kwa Roho, ndivyo ilivyo na sasa" (Gal. 4:29). Yesu mwenyewe aliwaonya wanafunzi wake, "...Mtumwa si mkubwa kuliko Bwana wake. Ikiwa **walinitesa** mimi, ninyi," (Yohana 15:20). Kabla ya kuwatuma huko nje wanafunzi kwenda kuhubiri (Mat. 10:16-42), alizungumza walau kwa uwazi kabisa juu ya mateso ya vikwazo ambayo yalikuwa karibu yamefungwa kwa majaliwa yao katika "ufunuo wake (Yesu, *nyongeza ya mtafsiri*) wa shahidi wa imani"[154] (Marko 13). Petro anaelezea mateso siyo kama pingamizi jipya la imani, bali, kinyume chake, kuwa ni kitu cha kutegemewa na hata kuthaminiwa, "**Wapenzi, msifikiri kuwa ni jambo geni kuhusu majaribu makali ambayo yanawapata ili kuwajaribu ninyi, kana kwamba ni jambo geni liwapatalo: Lakini furahini, kwa kadri mlivyo washiriki wa mateso ya Kristo; kwamba, wakati utukufu wake utakapofunuliwa, mweze kufurahi tena kwa furaha izidiyo sana**" (1 Pet. 4: 12-13).

Martin Luther alisisitiza hoja hii kwa kusema, "Hata kama anafundisha tu Neno la Kristo, kila mkristo mwaminifu ni lazima awe na watesaji wake."[155] Mwumini anapaswa kuchukua "mashindano makubwa ya maumivu" (Ebr. 10:32), ya msalaba (Ebr. 12:2), ya upinzani wa wasioamini (Ebr. 12:3), ya mateso (Marko 10:30; Matendo ya Mitume 8:1; 13:50; Warumi 8:35; 2 Kor. 12:10; 2 Tim.

---

150 Oda Hagemeyer. "Theologie des Martyriums". Benediktische Monatsschrift 60 (1984) 309-315, here p. 309.

151 Peter Beyerhaus. Die Bedeutung des Martyriums fuer den Aufbau des Leibes Christi. *op. cit.*, p. 131; Karl Rahner. Zur Theologie des Todes. *op. cit.*, pp. 73-106 [*Ibid.*, 1965[5]]. See p. 91: "Hivyo mauaji ya mashahidi wa imani ni sehemu ya kiini cha Kanisa".

152 Tokunboh Adeyemo. "Persecution: A Permanent Feature of the Church". Evangelical Ministries/Ministères Evangélique (Association of Evangelicals of Africa and Madagascar) Mar-Aug 1985: 3-9; Tokunboh Adeyemo. De gemeente zal altijd vervolgd worden. n. d.

153 Juu ya vyanzo vingine vya 'dioko', 'persecute" tazama:. O. Knoch. "dioko". col. 816-819 in: Horst Balz, Gerhard Schneider (Ed.). Exegetisches Woerterbuch zum Neuen Testament. 2 Vols, Vol. 1. W. Kohlhammer: Stuttgart, 1992[2]; Guenther Ebel, Reinier Schippers, Lothar Coenen. "Bedraengnis, Verfolgung". pp. 60-64 in: Lothar Coenen et.al,. (Ed.). Theologisches Begriffslexikon zum Neuen Testament. Vol. 1. R. Brockhaus: Wuppertal, 1967; Guenther Ebel, Reinier Schippers. "Persecution, Tribulation, Affliction". pp. 805-809 in: Colin Brown (Ed.). The New International Dictionary of New Testament Theology. Regency/Zondervan: Grand Rapids (MI), 1976. Vol. 2.

154 Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*, p. 30.

155 Martin Luthers Saemtliche Schriften. *op. cit.* Vol. IV, p. 263.

12:3; mateso (Marko 10:30, 112:10-12; 1 Timotheo 3:11; 2 Thes. 1:4) – hayo ndio 'yote', pamoja na Paulo (2 Tim. 2:10), kwa ajili ya imani yake.

25. Chuki dhidi ya Mungu

Hoja: "Mateso ni matokeo ya chuki ya ulimwengu dhidi ya Mungu na ufunuo wake katika Kristo."[156] (Mat. 10:22; Marko 13:13; Yoh. 15:18kk; Ufu. 12:13). "Mateso ya Wakristo huibuka kutokana na mgogoro wa ndani kati ya mfumo wa maisha wa dunia hii na ujumbe wa Kristo na Kanisa lake."[157] Kama Martin Luther anavyoliweka 'Wakati mtu awapo Mkristo na kuanza kuikiri imani yake kwa maneno yake na maisha yake, dunia hukasirika na kuanza kumtesa, kumwumiza ..."[158]

Yesu, ambaye kwa kurudia anadhihirisha kwamba; kumtegemea yeye na baba yake daima huchochea mwitikio bila tafakari katika dunia inayochagua kuishi pasipo Mungu, anauita mwitikio huu 'chuki'.[159] "Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi. Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungeliwapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia" (Yohana 15: 18-19). Mwitikio huu huakisi uhusiano wa karibu kati ya maisha ya mwumini na maisha ya Kristo.

Ulimwengu unamchukia Yesu, kwa sababu "Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi; bali hunichukia mimi, kwa sababu mimi naushuhudia ya kuwa kazi zake ni mbovu" (Yohana 7:7). Kwa kinywa cha Daudi, Mungu alisema, "**Walinichukia bila sababu**" (Yohana 15:25; Zaburi 13;19). Hata familia ya mtu mwenyewe inaungana na ulimwengu katika kumkana (Mat. 10:21-22 + 35-37), kwa kuwa "Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu, lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, **ataokolewa**" (Mat. 10:22).Yohana, aliyeandika maneno mengi juu ya chuki ya ulimwengu kwa Wakristo, anahitimisha, "Ndugu zangu, msistaajabu ulimwengu ukiwachukia" (Yohana 3:13).

26. Chuki ya Ulimwengu kwa Mungu ina asili katika chuki ya Shetani

Hoja: "Mzizi wa chuki ya ulimwengu ni chuki ya zamani ya Shetani, Mfalme wa dunia hii,"[160] (Yohana 12:31; 14:30; 16:11). Ufunuo unamweleza Shetani kama Joka ambaye amekuwa akilitesa Kanisa daima tangu kuzaliwa kwa Kristo, "Na joka yule alipoona ya kuwa ametupwa katika nchi,

156 Tokunboh Adeyemo. "Persecution: A Permanent Feature of the Church". S. 23-36 in: Brother Andrew (Ed.) Destined to Suffer? *op. cit.*, p. 23.

157 Heinrich OEhler. "Christenverfolgungen". p. 333 in: Friedrich Keppler (Ed.). Calwer Kirchenlexikon. Vol. 1. Calwer Verlagsb.: Stuttgart, 1937.

158 Martin Luthers Saemtliche Schriften. *op. cit.*, Vol. XII, p. 542.

159 Werner Stoy. Mut fuer Morgen: Christen vor der Verfolgung. Brunnen Verlag: Giessen, 1980². pp. 104-105.

160 Peter Beyerhaus. Die Bedeutung des Martyriums fuer den Aufbau des Leibes Christi. *op. cit.*, p. 133.

alimtesa mwanamke yule aliyemzaa mtoto mwanaume" (Ufu. 12:13). Wakati Yohana anapotuambia, "Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya Uzima" (Ufu. 2:10; angalia pia 3:13), tunatambua kwamba, ingawa Shetani ndiye chanzo cha mateso yote, yuko chini ya utawala wa Mungu na atashindwa katika ushindi wa mwisho wa Mungu.

Ibilisi ni "Mwuaji" na "Mwongo" (Yohana 8:44), 'asiyefaa' (Kigiriki 'beliar'; 2 Kor. 6:15), ambaye huunda 'uasi' (2 Kor. 6:14). Yeye ni "mfalme wa uwezo wa anga, na roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi': ndiye hupanga "kawaida ya ulimwengu huu" (Efe. 2:2). "Mkuu wa ulimwengu huu" (Yohana 16:11; 12:31), Yeye ni 'mfalme' wa mapepo, " malaika wa kuzimu; jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni, na kwa Kiyunani analo jina lake Apolioni (Ufu. 9:11; angalia mistari ya 1-11), ambayo yote humaanisha 'mharibifu'. Yeye ni "mkuu wa giza hili" (Efe. 6:12), 'Mshitaki' (Ufu. 12:10), "Yule joka...yule mkubwa , nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na shetani.' (Ufu. 12:9), ambaye husambaza 'mafundisho ya mashetani' (1 Tim. 4:1). Kwa sababu hujigeuza awe kama "malaika wa nuru", watumishi wake daima ni "mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo" (2 Kor. 11:13-14).

Shetani hufanya kazi wakati ambapo Mungu huruhusu. Kabla ya ushindi wa Yesu Msalabani, alikuwa na nafasi katika chumba cha kiti cha enzi cha Mungu (Ayubu 1:6-12; 2:1-7; Zek. 3:1-2), lakini hukumu ilimwangukia yeye na pepo wake wachafu, wakati Yesu alipokufa, alitupwa chini duniani. Kuonekana kwa Yesu tayari kulikwishaashiria mwisho wa utawala wa Ibilisi juu ya pepo (Ufunuo 20:1-3).[161] Katika Mathayo 12:28, Yesu anasema, "Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia". Wakati wale sabini waliporudi wakifurahia mafanikio ya umishenari wao, anafurahi pamoja nao, "Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme. Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru. Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni" (Luka 10:17-20). Ufunuo 12:9 na 13 umeelezea anguko la Shetani na pepo wake wachafu kwa maneno yafuatayo, "Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye". Yeye ni "...nyota iliyotoka mbinguni, imeanguka juu ya nchi" (Ufunuo 9:1), na joka ambaye "...mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi'. (Ufu. 12:4).

Tangu mwanzo wa uimarishaji wa ufalme wa Mungu, Roho Mtakatifu huhakikisha juu "... ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa" (Yohana 16:11). "...akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo" (Kol. 2:15). Shetani na nguvu zake hawezi kukwepa moto wa milele (Mat. 25:41 na Ufu.

---

161 Wanatheolojia wengi wa Baada- na Wasomilenia wanaamini kuwa malaika mwenye funguo za kuzimu kuwa ni Yesu katika ushindi wake dhidi ya Shetani pale juu ya Msalaba. Hata hivyo, Wabaadamilenia huona hili kama tukio lijalo na ni malaika wa 'kawaida'

20:10), kama Maandiko yanavyotuhakikishia, "Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu" (Yuda 6); "Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu" (2 Petro 2:4). Kifungu hiki cha mwisho yawezekana kinarejea katika Zaburi 107:10-11, "Waliokaa katika giza na uvuli wa mauti, wamefungwa katika taabu na chuma, kwa sababu waliyaasi maneno ya Mungu, wakilidharau shauri lake Aliye Juu."

Maandiko matatu ya mwisho yanadhihirisha tatizo la Shetani – alikuwa amepokea hali ya mamlaka toka kwa Mungu (Kwa ujumla, mamlaka yote hutoka kwa Mungu), lakini alidai zaidi – alitaka kuwa kama Mungu! Ninatumia maneno yaliyotumiwa katika Mwanzo kuelezea Anguko la mwanadamu (Mwanzo 3:5), ambamo Shetani anajaribu kumshawishi Mwanadamu kufanya kufuru ile ile, kubadili mamlaka ya Ki-Mungu yaliyotolewa katika agano la Mungu kwa mamlaka yake binafsi – uongo mharibifu kabisa, kama Adamu alivyogundua mapema! Fikiria kuwa Ezekieli 28:11-19 na Isaya 14:12-18 ni ufafanuzi wa Shetani na viongozi wa wanadamu, inatupa picha mfululizo ya (kiburi dhidi ya Mungu), ambayo inajaribu kuvuka mipaka iliyowekwa na Mungu na kuwa Mungu.

Yesu pekee ndiye awezaye kuahidi, "....nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda" (Mat. 16:18), kwa sababu tayari amemshinda Shetani!

27. Roho Mtakatifu – Faraja Katika Mateso

Hoja: Roho Mtakatifu, 'Mfariji' (Yohana 16:16+26) huwapa Wakristo nguvu kuvumilia Mateso,[162] **na hata kufurahi katika hali zilizo ngumu kabisa.** "Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni heri yenu; kwa kuwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia" (1 Petro 4:14).[163] Roho wa Utukufu, ambaye alikaa juu ya Masihi (Isaya 11:2) huleta utukufu wake kwa wale ambao wanaonekana kupoteza utukufu wote, kama vile Stefano, ambaye Luka anamwelezea kama, "...akijaa Roho Mtakatifu" (Matendo ya Mitume 7:55), wakati wa utetezi wake na kuuawa kwake,[164] kama alivyouona Utukufu wa Mungu huko Mbinguni.

Roho Mtakatifu ni "Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu" (Yohana 14:17; angalia pia 15:26 na 16:7). Yeye

162 Kwa ajili ya mafunzo ya kina, tazama: William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. University Press of America: Washington D.C., 1981 [Diss. Basel, 1977]; Tazama pia: Karl Holl. "Die Vorstellung von Maertyrer und die Maertyrerakte in ihrer geschichtlichen Entwicklung" [1914]. pp. 68-102 in: Karl Holl. Gesammelte Aufsaetze zur Kirchengeschichte. Vol. 2: Der Osten. J. C. B. Mohr, 1928; Marc Lods. Confesseurs et Martyrs: Successeurs des prophètes dans l'église des trois premiers siècles. Cahiers Théologique 41. Delachaux & Niestle: Neuchatel, 1958; and Eduard Christen. "Martyrium III/2.". *op. cit.*, pp. 214-215 und Werner Stoy. Mut fuer Morgen. *op. cit.*, pp. 46.

163 Juu ya 1 Petro 4:14, tazama: William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom, *op. cit.*, pp. 64-65.

164 *Ibid.* pp. 36-43. Matendo 6:5 pia humwelezea Stefano kama mtu aliyejaa imani na Roho (Matendo 6:8).

ndiye aliye tofauti kati ya Wakristo na ulimwengu wetu wa uasi, na mtu pekee awezaye kuushinda ulimwengu (Yohana 16:8). Anashuhudia kwamba Shetani tayari amekwisha kushindwa (Yohana. 16:11).

Katika Luka 21:12-15, Yesu anatangaza kuwa atatoa hekima kwa wanaoteseka watakaposimama mbele ya mahakimu, hekima ambayo itakuwa ushuhuda. Nani atakayetoa hekima hii kama si Roho Mtakatifu?. Kifungu sambamba katika Mathayo 10:19-20 huzungumzia juu ya 'Roho wa Baba yenu' atakayeshuhudia mbele za mahakimu wenu. William Carl Weinrich anatoa angalizo kuwa Yesu alizungumza mara chache juu ya kazi za Roho Mtakatifu, lakini alipofanya hivyo, mara nyingi alimwelezea kama Msaidizi na Mfariji katika mateso (Mat. 10:17-20; Marko 13:9-11; Luka 21:12-19).[165] Haishangazi kwamba Paulo anafuata mfano wa Bwana katika orodha ya mateso yake kwa kuuelekeza uvumilivu wake kwa Roho Mtakatifu (2 Kor. 6:6). Katika Wafilipi 1:19, anaandika, "Maana najua ya kuwa haya yatanigeukia kuwa wokovu wangu, kwa sababu ya kuomba kwenu, na kuruzukiwa Roho wa Yesu Kristo". Anawakumbusha Wathesalonike, kuwa "Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiishia kulipokea neno katika dhiki nyingi, pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu." (1 Thes. 1:6-7).[166]

Kanisa la Kwanza lilikuwa likifahamu daima kuwa ni Roho Mtakatifu pekee anayeweza kuwapatia wanaoteswa hekima na nguvu za kuvumilia. Kwa mujibu wa Tertullian,[167] Roho huambatana nasi kifungoni;[168] 'Roho Mtakatifu, Mwalimu'[169] huwaanda Waumini kwa ajili ya mateso yao. Barua iliyoandikwa mwaka 177 BK. kutoka katika makanisa ya Lyon na Vienne humtaja raia Mrumi aliye kiongozi huko Gaul, ambaye alitoa msaada kwa Wakristo na yeye mwenyewe alihukumiwa kwa uingiliaji kati wake: "Yeye, aliye mfariji wa Wakristo, aliyekuwa na Mfariji, Roho wa Zekaria, ndani yake mwenyewe, kama utimilifu wa pendo lake unavyoonesha wazi..."[170] Maelekezo ya kikanisa ya Hippolyt (Mwanzoni mwa karne ya 3 BK.) yanalishauri kanisa lisiweke mikono juu ya waamini wanaotarajiwa kuwekwa wakfu kuwa wahudumu au wazee wa kanisa, iwapo wamewahi kufungwa au kuteswa, kwa sababu tayari wamekwishapokea heshima ya uzee (au kasisi, *nyongeza ya mtafsiri*) kupitia ushuhuda wao: wanapaswa kuchukuliwa kuwa ni Wakarismatiki*, kwa kuwa Roho Mtakatifu amekwishawapa ushuhuda huko mahakamani.[171]

---

165 Ibid, pp. 55-56.

166 *Ibid.*, pp. 57-58.

167 Baada ya kuwa amekuwa Mkatoliki.

168 Tertullian, An die Maertyrer 1,3, in: Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 104-107.

169 *Ibid.*, pp. 113.

170 Waraka kwa Makanisa ya Vienne na Lyon, katika: Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, p. 235 [5th. Book, Ch. 1, V.10].

171 Theofried Baumeister. "Maertyrer und Verfolgte im fruehen Christentum". Concilium 19 (1983) 3: 169-173, hapa uk. 170; Text Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 135 (Hippolyt, Apostolische Tradition, Absatz 9).

28. Furaha Katika Mateso

Hoja: Uwepo wa Roho Mtakatifu na faraja ya Mungu humwezesha mwamini kufurahi hata chini ya mateso.[172] "**Lakini furahini, kwa kadri mlivyo washiriki wa mateso ya Kristo; kwamba, wakati utukufu wake utakapofunuliwa, mweze kufurahi tena kwa furaha izidiyo sana**" (1 Petro 4:13; Angalia pia 1 Petro 1:6). Petro alijifunza hili kutoka kwa Bwana wake, aliyesema, "Heri ninyi watakapowashutumu na **kuwatesa** na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu" (Mathayo 5:11). Martin Luther akiandika katika namna ile ile, asema "Hatuna sababu ya kulalamika, wakati ulimwengu unapotutesa na kutuua, bali kufurahi na kuchangamka."[173] Ushauri huu ni wa kivitendo zaidi – Je, Luka hatuambii kuwa Paulo na Sila waliomba na waliimba sifa kwa Mungu ndani ya gereza (Matendo ya Mitume 16:25)? Je, umeshagundua kuwa Waraka kwa Wafilipi, waraka wa Agano Jipya unaojishughulisha zaidi na mateso kuliko nyaraka nyingine zote, pia ni barua ya furaha? "Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini" (Wafilipi 4:4).[174]

29. Kumtumaini Mungu Pekee

Hoja: Katika mateso, tunajifunza kutojitegemea wenyewe, bali kumtumaini Mungu pekee. Paulo anaandika, "Naam, sisi wenyewe tulikuwa na hukumu ya **kifo ndani ya** nafsi zetu ili tusijitumainie nafsi zetu, bali tumtumaini Mungu, awafufuaye wafu" (2 Kor. 1:9). Somo hili halikukusudiwa tu kwa wale wanaokabiliana na mateso, bali kwa kanisa la ulimwengu wote, vinginevyo kanisa lifumbe macho kwa mustakabali wa wanaoteswa.

Kwa sababu Mungu kamwe hatawaacha watoto wake wanaoteswa, Paulo anaiweka wakfu sura nzima ya 2 Wakorintho (2 Wakorintho 1:3-11) kwa faraja aliyoipokea kutoka kwa Kristo na toka kwa Baba katika mateso yake mwenyewe. Daima anasisitiza faraja na msaada Mungu anaoutoa. "Lakini Bwana alisimama pamoja nami akinitia nguvu" (2 Timotheo 4:17)

Mambo mawili hapa ni muhimu:

1. Hakuna kitu na hakuna mtu anaweza kumtenga Kristo na mwamini (Warumi 8:31-39), hata kama ni mateso (mstari wa 35).[175]

---

172 Tazama: Thomas Schirrmacher. "Gruende fuer die Fruehdatierung der Offenbarung vor 70 n. Chr." pp. 129-154 in: David Chilton. Die grosse Truebsal. Reformatorischer Verlag Beese: Hamburg, 1996 na maandiko yaliyonukuliwa kwa ajili ya ukanushi.

173 Martin Luthers Saemtliche Schriften. *op. cit.*, Vol. IX, p. 758.

174 Juu ya somo la mateso katika Waraka kwa Wafilipi, tazama: Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 176-182; Harry W. Tajra. The Martyrdom of St. Paul. *op. cit.*, pp. 58-72; William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 55-56 n. d.

175 Tazama hoja za Clemens wa Alexandria juu ya kifungu hiki katika: Clemens of Alexandria, Teppiche IV, 14, 96, 1-2, katika Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 133+135 (Nr. 49).

2. Mungu hataruhusu mateso kuwa yasiyobebeka; kwa kuwa anajua barabara ni jinsi gani mtu awezavyo kustahimili. "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili (1 Wakorintho 10:13).[176]

E. Tabia chini ya Mateso

30. Kamwe Usipanie Mateso

Hoja: Mkristo hapaswi kutafuta mateso. Tofauti na tabia ya mara kwa mara ya waamini wa Kanisa la Kwanza kutafuta mateso kwa ajili ya malipo na baraka zake, ni lazima kukumbuka kuwa ni haki maalumu ya Mungu, siyo yetu, kupanga ni nani apitie mateso ya mauaji ya mashahidi wa imani. Mwamini hana haki ya kuyatafuta mateso.

Tabia ya kutafuta mauaji ya mashahidi wa imani ya kawaida mahali pote kama mwaka 107-108 BK., kama Ignatius, Baba wa Kanisa na Askofu wa Antiokia,[177] aliyeuawa chini ya mfalme Trajani, aliwasihi waamini wa Rumi wasizuie kuuawa kwake, jambo ambalo wangeweza kufanya.[178] Mababa wengine wa Kanisa, kama vile Cyprian[179] na wapinzani wa Wadonatisti*, walifikiri tofauti na kusisitiza ukwepaji wa mauaji ya mashahidi wa imani.[180] Maelezo ya awali

---

176 Paulo haweki mpaka wa ahadi hii kwa hali za mateso - inahusika na majaribu yote, lakini iko katika hali ya jumla kwa asili yake, hivyo twaweza kuitumia katika mateso.

177 Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 262-263+272-274 (juu ya Ignatius, tazama kr. 260-289); Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 49-55; William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 111-222; Hans von Campenhausen. Die Idee des Martyriums in der Alten Kirche. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1936[1]; 1964[2]. pp. 71-73; Werner Stoy. Mut fuer Morgen. *op. cit.* pp. 39-40 und I. Bria. "Martyrium". *op. cit.* p. 267; See also the positive representation in: Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 54-60, especially p. 57. Maoni ya zamani, kwamba Ignatius hakutofautisha mauaji yake na yale ya Yesu au aliamini kifo chake kuwa dhabihu kwa ajili ya wengine, ni lazima yakataliwe: tazama; William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 111-115.

178 Tazama Waraka wake kwa Warumi: "Die Sieben Ignatius-Briefe". pp. 111-225 katika: Joseph A. Fischer (Ed.). Die Apostolischen Vaeter. Koesel: Muenchen, 1981[8]. pp. 182-193, hususani 7,2 (p. 191): "na katika pendo anatamani kifo", vile vile 2,1-4,3 + 6,1-3; na 'An die Trallianer' 1,1 (p. 179).

179 Tazama sehemu za waraka wa Cyprian kwa Fortunatus katika: Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp 152-161 (Nr. 57); ulio kamili zaidi katika: Edelhard L. Hummel. The Concept of Martyrdom According to Siant Cyprian of Carthage. The Catholic University of America Studies in Christian Antiquity 9. The Catholic University of America: Washington, 1946.

180 Juu ya ukanaji wa makusudi wa mauaji ya mashahidi wa imani, tazama: Bernhard Kriegbaum. Kirche der Traditionen oder Kirche der Maertyrer? Die Vorgeschichte des Donatismus. Innsbrucker theologische Studien 16. Tyrolia-Verlag: Innsbruck, 1986. pp. 77-81 n. d. na Donald W. Riddle. "From Apokalypse to Martyrology": Anglican Theological Review 9 (1926/27): 260-280, here, p. 271.

yaliyopo hata leo ya mauaji ya mashahidi wa imani,[181] "Mauaji ya shahidi wa imani ya Polycarp" (kama 155 -157 BK.) yanafikiria kuwa Baba wa Kanisa alikufa kinyume cha ridhaa yake kama ilivyokuwa katika suala la Yesu.[182] Clemens wa Aleksandria anaandika, "Tunawakemea wale wanaotupilia mbali maisha yao"[183] na anaongeza kwa uwazi, "Tunasema juu yao kuwa, wakiwa wamechagua kuondoka katika maisha haya kwa njia hii, hawafi kama mashahidi wa imani ..."[184]

Katika hali hii, jambo hili ni sawa na utumwa. Paulo, aliyewaamuru wafungwa kufanya kazi kwa nguvu na kuthibitisha imani yao kama watumwa, aliweza pia kuandika, "Kila mtu na akae katika hali ile ile ambayo alikuwa nayo alipoitwa. Je, uliitwa u mtumwa? Usione ni vibaya lakini kama ukiweza kuwa na uhuru, afadhali kuutumia" (1 Kor. 7:20-21).

Biblia inamwelezea mwanadamu kama mtumwa wa dhambi, aliyenaswa katika uasi wake dhidi ya Mungu. Wakati anapokubali hukumu ya Mungu na kifo cha dhabihu ya Kristo juu ya Msalaba, anaitwa na Mungu katika maisha mapya. Msamaha wa dhambi humkomboa kwa maisha mapya, lakini maisha haya mapya na Mungu hayabadilishi hali zote moja kwa moja na kwa haraka. Hata wakati bado ni mtumwa – bado aweza kumtumikia Mungu kwa utimilifu (jambo ambalo halihusiani na kuukubali utumwa - Paulo anapinga utumwa na anawashauri Wakristo kuwaacha huru watumwa wao katika 1 Kor. 7:21 na katika Waraka wa Filemoni,[185]), lakini imani katika Kristo hurekebisha desturi zetu tunazo zithamini. Si kazi inayofanya maisha kuwa ya thamani, bali Mwumbaji na Mwokozi, anayetupa sisi kazi zetu. Nguvu ya Ukristo imelala katika hitaji la haki kutoka kwa wengine katika msingi wa haki ya Mungu, lakini, uhuru mbali na hali za nje, huendelea kumshukuru na kumtukuza Mungu hata wakati haki inapokataliwa. Uhuru wa ndani unatangulia uhuru wa nje.

Kwa njia ile ile, Mkristo anapaswa kuwa imara chini ya mateso, lakini kufurahia zaidi pale anapoweza kuyaepuka, au pale yafikiapo mwisho - kitu ambacho ni uhalalisho kwa kujitoa kwetu kupinga mateso ya ndugu zetu wa kiume na wa kike. Tunaweza kuchukua hatua kuepusha, kukomesha au

181 Albert Ehrhard. Die Kirche der Maertyrer. *op. cit.* p. 37. Pia tuna waraka wa 156 BK. kutoka katika kanisa la Smyrna kwenda kwa kanisa huko Philomelium katika Firijia Mkuu (Greater Phrygia) juu ya tukio lilelile, ambalo Eusebius alilitumia, tazama Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. Tazama Albert Ehrhard. Die Kirche der Maertyrer. *op. cit.*, p. 37, zugleich ist ein Brief aus dem Jahr 156 n. Chr. der Gemeinde in Smyrna an die Gemeinde von Philomelium in Grossphrygien ueber dasselbe Ereignis, dass Eusebius uebernommen hat: Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, pp. 206-215 (4. Book, Ch. 14-15). Tazama chini kwa maandiko zaidi.

182 Martyrium des Polykarp 1,2 = S. 2-5 in: Herbert Musurillo (Ed.). The Acts of Christian Martyrs. Clarendon Press: Oxford, 1972, 'Martyrium des Polykarp' pp. 2-21;. William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp.166-167.

183 Klemens von Alexandrien, Teppiche IV, 4, 17, 1-4, in: Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 131 (Nr. 47).

184 *Ibid.* (Teppiche IV, 4, 17, 1).

185 Herbert M. Carson. The Epistle of Paul to the Colossians and Philemon. The Tyndale New Testament Commentary. Wm. B. Eerdmans: Grand Rapids (MI), 1979 (toleo-rudufu tangu 1960). hususani kk. 21-24.

kuyanyoshea kidole mateso. Katika mahubiri yake ya kwanza juu ya mateso, Yesu alisema, "Angalieni, mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa - mwitu; basi iweni na busara kama nyoka, na **msio na madhara kama njiwa**" (Mat. 10:16). Wakristo hawapaswi kumkana Bwana wao, lakini wanapaswa kuangalia njia za busara za kuepukana na mateso!

31. Ni Halali Kukimbia Mateso

Hoja: Agano la Kale na Jipya huweka wazi kuwa Waamini wanaweza kukimbia mateso yaliyopo popote pale duniani.[186]

Yesu aliondoka Yudea kueleka Galilaya wakati Yohana Mbatizaji alipokamatwa (Mat. 4:12), na baadaye alibaki huko wakati Wayahudi walipotaka kumwua (Yohana 7:1). Alijificha wakati Wayahudi walipojaribu kumpiga mawe (Yohana 8:59; 10:39). Pia Mungu alikuwa amewaamuru wazazi wake kukimbilia Misri ili kumlinda kutoka kwa Herode (Mat. 2:13-18). Wakristo katika Kanisa la Kwanza walikimbia kutoka Yerusalemu (Matendo ya Mitume 8:1) na Paulo alikimbia kutoka Dameski (Matendo ya Mitume 9:25; 2 Wakorintho 11:32-33) na kutoka Antiokia (Matendo ya Mitume 14:5-7),[187] Katika Ufunuo 12:6, kanisa lilikimbia kutoka kwa Ibilisi mpaka katika nyika. Hata Yesu anawaelekeza wanafunzi wake kukimbia "Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine; kwa maana ni kweli nawaambia, Hamtaimaliza miji ya Israeli, hata ajapo Mwana wa Adamu" (Mat. 10:23) ambapo Cyprian, Askofu wa Carthage baadaye ananukuu.

Agano la Kale pia linaeleza hali zinazofanana na hizo.[188] Obadia aliwaficha manabii 100 kutoka kwa Malkia Yezebeli katika mapango mawili (1 Wafalme 18:4+13). Waumini wengine 7000 pia walifichwa katika 1 Wafalme 19:1-18; Rum. 11:3-4). Pia Eliya alimkimbia Malkia yule yule mpaka Mlima Horebu (1 Wafalme 19:1-18) na Nabii Uria alijaribu kumkimbia Mfalme Yehoyakimu (Yeremia 26:20).

Katika hali chache maalumu, waamini walikwenda kukutana na kifo. Yesu na Paulo wote walirudi Yerusalemu ili wakamatwe (Matendo ya Mitume 10:19-25) na kufuatana na mapokeo ya kanisa la kwanza, Petro, aliyekuwa ameondoka Rumi, alirudi ili auawe, baada ya kuwa aliitwa arudi kwa maono.[189] Hata hivyo, ni 1. watu maalumu katika historia ya wokovu 2. ni hali maalumu katika historia ya wokovu 3. waliamriwa moja kwa moja na Mungu, (kwa mfano, Matendo ya Mitume 20: 22-23).

---

186 Werner Stoy. Mut fuer Morgen. *op. cit.*, pp. 40-42.

187 Matendo 20:3 pia yaweza kuonesha kwamba Paulo alikuwa akiepa hali ngumu.

188 William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, p. 1.

189 Carsten Peter Thiede. Simon Peter. The Paternoster Press: Exeter (GB), 1986. p. 185-194.

Jambo la kipekee katika Kanisa la Kwanza lilikuwa ni uhuru wa maaskofu na wazee kukimbia,[190] suala lililosababisha mabishano makubwa.[191] Yesu akionya juu ya 'mtu wa mshahara' aliyewaacha kondoo wake kwa mbwa mwitu (Yohana 10:11-13),[192] ilieleweka kama katazo la kukimbia, lakini maelekezo ya Yesu kuhusu kukimbia (angalia juu) huruhusu. Cyprian alirejea kwa Mathayo 10:23 alipokimbia kutoka Rumi, akiliongoza kanisa lake kutokea eneo la maficho, jambo lililomletea upinzani wa hali ya juu kutoka kwa kanisa (kundi la waamini) la Rumi.[193] Askofu mmoja aliyekuwa maarufu sana aliyebaki na kuuawa, alikuwa ni Polycarp, ambaye mfano wake ulibeba uzito katika hoja juu ya kukimbia mateso,[194] ambapo Cyprian na Athanasius walikuwa ni maaskofu maarufu waliokimbia mateso.[195] Hatimaye kanisa lilichukua msimamo kuwa askofu hapaswi kukimbia kwa sababu za hofu au woga, lakini anaweza kufanya hivyo kama ni kwa manufaa ya kanisa lake, 'Mgongano wa Wajibu', wa zamani'[196] kama unavyohalalishwa na Cyprian, Athanasius na Augustine,[197] waliofundisha kuwa maamuzi yangeweza tu kufanywa kufuatana na mwongozo wa Roho katika hali halisi.[198]

---

190 Tazama: Bernhard Koetting. "Darf ein Bischof in der Verfolgung die Flucht ergreifen?". pp. 220-228 katika: Ernst Dassmann (Ed.). Vivarium: Feschrift Theodor Klauser zum 90. Geburtstag. Jahrbuch fuer Antike und Christentum, Ergaenzungsband 11. Aschendorff: Muenster, 1984, kwa ajili ya ufupisho ulio bora kabisa.

191 *Ibid.* p. 221-222.

192 *Ibid.*, p. 221.

193 *Ibid.*, pp. 223-224 and Adolf von Harnack. Die Mission und Ausbreitung des Christentums in den ersten drei Jahrhunderten. VMA-Verlag: Wiesbaden, n. d.(repr. from 1924[4]). p. 215; Tazama pia waraka wa Cyprian kwa Fortunatus; sehemu zake katika Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 152-161 (Nr. 57); kwa ukamilifu zaidi katika: Edelhard L. Hummel. The Concept of Martyrdom According to Siant Cyprian of Carthage. *op. cit.*

194 Alvyn Pettersen. "'To Flee or not to Flee': An Assessment of Athanasius's De Fuga Sua". pp. 29-42 in: W. J. Sheils (Ed.). Persecution and Toleration. Taarifa zilizosomwa katika ... Ecclesiastical History Society. B. Blackwell: Oxford, 1984. p. 29.

195 *Ibid.*, and Bernhard Koetting. "Darf ein Bischof in der Verfolgung die Flucht ergreifen?". *op. cit.*, pp. 221-226. Ibid. hiyo pia hutaja mifano zaidi.

196 Ibid, p. 224 and Alvyn Pettersen. "'To Flee or not to Flee': An Assessment of Athanasius's De Fuga Sua". *op. cit.* Athanasius alikuwa na sababu za kisisasa na kitheolojia kwa kukimbia kwake kutoka kwa Waariani. (kr. 31-33) na akatoa mifano ya kibiblia kwa ajili ya mambo aliyoyajali kitheolojia. Hata hivyo, aliona ukimbiaji wakati mwingine kuwa ni makosa. Katika kutafakari kwake tena juu ya jambo hilo, tazama makala yake, 'De Vita Antonii' and his Letter at the Feast', *Ibid.*, pp. 37-40.

197 Bernhard Koetting. "Darf ein Bischof in der Verfolgung die Flucht ergreifen?". *op. cit.*, pp. 221+226-227.

198 Tazama Adolf von Harnack. Die Mission und Ausbreitung des Christentums in den ersten drei Jahrhunderten. *op. cit.*, pp. 214-216.; Michael Slusser. "Martyrium III/1.". *op. cit.*, pp. 209.

32. Si Mateso yote ni kwa Ajili ya Kristo

Hoja: Si mateso yote ni kwa ajili ya Kristo: wakati Wakristo wanapotenda uharifu, wanapaswa kuadhibiwa na kuteseka kama wengine.

Ahadi ya Yesu, "Heri ninyi watakapowashutumu na **kuwatesa** na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu." (Mat. 5:11) imewekewa mipaka kwa maneno "kwa uongo, kwa ajili yangu". Paulo anatukumbusha kuwa Serikali inapaswa kutuadhibu kama inavyofanya kwa wakosaji wengine (Rum. 13:4). Na Petro anatusihi "Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo. Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mema, ikiwa ndiyo mapenzi ya Mungu, kuliko kwa kutenda mabaya" (1 Petro 3:16-17). "Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine. Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo" (1 Petro 4:15-16; angalia rejea kuhusu mateso katika mistari ya 12-14).

33. Msaada kwa Wadhaifu

Hoja: Kanisa la Kwanza lilijikita zaidi na mustakabali wa wale walioshindwa chini ya mateso,[199] lakini kanisa la sasa limeachilia mbali jambo hili lililopo hata sasa. Karibu mavuguvugu yote ya migawanyiko katika karne nne za kwanza[200] (Wanoviti*, Wameliti* katika Misri na Wadonatisti katika Afrika) ilichimbukia katika makundi ambayo ama yalikataa kuwarejesha waumini walioanguka (Kwa kilatini 'lapsi' au 'tyraditores' – kati ya 303-305 BK.; kwa Kigriki 'parapeptokes'), hata baada ya toba, au waliobatilisha matendo maalumu ya wachungaji na maaskofu walioanguka. Kanisa la Kwanza lenyewe – na madhehebu makubwa – yalikataa fundisho la Kidonatisti[201] na walikubaliana

---

199 Adolf von Harnack. Die Mission und Ausbreitung des Christentums in den ersten drei Jahrhunderten. *op. cit.* pp. 214-216.; Michael Slusser. "Martyrium III/1.". *op. cit.* p. 209.

200 Albert Ehrhard. Die Kirche der Maertyrer. *op. cit.* pp. 122-267 und Ivo Lesbaupin. Blessed are the Persecuted: The Early Church Under Siege. Orbis Books: Maryknoll (NY), 1987 [Original Portugiesisch]; Spire (Hodder & Stoughton): Sevenoaks (GB), 1988. pp. 41-43, ambacho hujumuisha migawanyiko ya kienyeji, kufuatia Gerhard Besier. "Bekenntnis - Widerstand - Martyrium als historisch-theologische Kategorie". pp. 126-147 in: Gerhard Besier, Gerhard Ringshausen (Ed.). Bekenntnis, Widerstand, Martyrium: Von Barmen 1934 bis Ploetzensee 1944. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1986. p. 130.

201 Hakuna makusanyo ya maandiko ya kina yaliyo kwa ajili ya au kinyume na Udonatisti, lakini tazama: Hans von Soden; Hans von Campenhausen (Ed.). Urkunden zur Entstehungsgeschichte des Donatismus. Kleine Texte fuer Vorlesungen und UEbungen 122. de Gruyter: Berlin, 1950^{2}. 56 pp. Maandiko mengi juu ya vuguvugu hilo yanaanzia karne ya 19 hivi na yako katika Kilatini, kuna mafunzo na makusanyo machache ya kisasa. Tazama: Bernhard Kriegbaum. Kirche der Traditionen oder Kirche der Maertyrer? Die Vorgeschichte des Donatismus. Innsbrucker theologische Studien 16. Tyrolia-Verlag: Innsbruck, 1986; Hendrik B. Weijland. Augustinus en de kerkelijke tucht. J. H. Kok: Kampen, 1965; William H. C. Frend. The Donatists Church. Clarendon Press: Oxford, 1971^{1}; *Ibid.* & Oxford University Press: New York, 1985^{3}; Emin Tengstroem. Donatisten und Katholiken:

na maoni ya Augustine Aurelius[202] na Askofu Optatus[203] na mafundisho ya Maandiko, kuwa Wakristo waliokwepa mateso wanaweza kupokelewa katika makanisa wakati wanapotubu.[204]

Tuwe wenye rehema[205] kwa wale walio dhaifu sana kusimama, kama alivyokuwa Cyprian,[206] na kutambua hekima ya kuepa mateso, na kufikiri juu ya uwezekano kama kukimbia[207] au kukaa kimya.

Pengine Petro ni mfano mzuri unaojulikana wa 'lapsi', aliyekuwa dhaifu kutokana na hofu ya maisha yake (Mat. 26:69-75; Marko 14:66-72; Luka 22:56-62; Yohana 18:15-18+25-27: Angalia pia maonyo katika Mat. 26:31-35; Marko 14:27-31; Luka 22:31-34; Yohana 13:36-38). Awali Petro alimkana Bwana ("Ndipo akaanza kulaani na kuapa akisema, Simjui mtu huyu! Na mara akawika jogoo." (Mat. 26:74 = Marko 14:71), lakini alitubu na kupokelewa tena kwenye ushirika wa watu wa Mungu. (Angalia mwisho wa habari hapo juu). Pia Petro

Soziale, wirtschaftliche und politische Aspekte einer nordafrikanischen Kirchenspaltung. Studia Graeca et Latina Gothoburgensia XVIII. EBA: Goeteburg, 1964; Daniel Voelter. Der Ursprung des Donatismus, nach den Quellen untersucht und dargestellt. Mohr: Freiburg/Tuebingen, 1883 (very critical of Augustin and the church); Ferdinand Ribbeck. Donatus und Augustinus oder der erste entscheidende Kampf zwischen Separatismus und Kirche. Baedeker: Elberfeld, 1858; Wilhelm Thuemmel. Zur Beurteilung des Donatismus. M. Niemeyer: Halle, 1893 (anasisitiza tofauti ya lugha na ujamii). Ambavyo bado vinastahili kusomwa ni: Chester D. Hartranft. "Introductory Essay". S. I-XXXV in: Aurelius Augustinus. The writings against the Manichaeans and against the Donatists (Ed. von J. R. King und Chester D. Hartranft). A Select Library of the Nicene and Post-Nicene Fathers of the Christian Church (Ed. von Philipp Schaff). Serie 1, Vol. 4 Wm. B. Eerdmans: Grand Rapids (MI), 1979 (Nachdruck von 1887) [Tazama pia www.ccel/fathers2npnf/ und auf CDROM Christian Classics Ethereal Library 1998. CCEL (Wheaton College: Wheaton, IL, 1998].

202 *Ibid.*, pp. 130-131. Toleo maarufu la kale la maandiko ya Agostino dhidi ya Wadonatisti ni: Aurelius Augustinus. Scripta contra Donatista. Corpus scriptorum ecclesiasticorum Latinorum 51. Tempsky: Wien, 1908. Kwa toleo la Kiingereza, tazama: Aurelius Augustinus. The writings against the Manichaeans and against the Donatists (ed. by J. R. King and Chester D. Hartranft). A Select Library of the Nicene and Post-Nicene Fathers of the Christian Church (ed. by Philipp Schaff). Serie 1, Vol. 4 Wm. B. Eerdmans: Grand Rapids (MI), 1979 (repr. from 1887) [tazama pia www.ccel/fathers2npnf/ und auf CDROM Christian Classics Ethereal Library 1998. CCEL (Wheaton College: Wheaton, IL, 1998)].

203 Toleo la Kilatini la kitabu chake dhidi ya Wadonatisti limerudiwa kuchapwa kwa mfululizo tangu mwaka 1549. Toleo la mwisho ni: Optatus. De schismate Donatistarum. Ed. von Karl Ziwsa. Corpus scriptorum ecclesiasticorum Latinorum 26. Tempsky: Vindobonae, 1893; Reprint: S. Optati Milevitani libri VII septem ... Mfululizo uleule:. Johnson: New York, 1972; In English: Milevitanus Optatus. Against the Donatists. Translated Texts for Historians 27. Liverpool University Press: Liverpool, 1997; Optatus. The Work of St. Optatus Bishop of Milevis against the Donatists. no publisher: London, 1917; hakuna toleo la Kijerumani lililopo kwa kadri nijuavyo.

204 Bernhard Kriegbaum. Kirche der Traditionen oder Kirche der Maertyrer? *op. cit.* pp. 18-43. Katika mjadala wake wenye utata wa funzo la kihistoria la vuguvugu la Udonatisti, Kriegbaum anadhihirisha kuwa asili za Udonatisti ni zenye kukanganya sana kuliko jambo la kawaida la mauaji ya mashahidi wa imani.

205 Tazama: Patrick Johnstone. "Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution". *op. cit.*, p. 7 and Gerhard and Barbara Fuhrmann. "Versteckte Christen". Missionsbote (Allianz-Mission) 5/1983: 9-10.

206 Tazama: Michael Slusser. "Martyrium III/1.". *op. cit.*, p. 209; or Edelhard L. Hummel. The Concept of Martyrdom According to Siant Cyprian of Cartharrge. *op. cit.* kwa ajili ya mafunzo zaidi.

207 Tazama makala juu ya kukimbia hapo juu.

anatuonesha mahusiano ya karibu kati ya hofu ya mateso na kujiamini kupita kiasi. Kumbuka pia Yesu alikuwa amekwishaomba kwa ajili ya wanafunzi wake, "Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu" (Yohana 17:15), na kwa ajili ya Petro (Luka 22:31-32) kwamba Mungu angeweza kumwezesha kuitunza imani wakati wa mateso na wakati wa kushindwa kwake yeye binafsi.

34. Kuomba kwa Ajili ya Mtesaji

Hoja: Kufuatia desturi za Agano la Kale (Kwa mfano, Ayubu 31:29; 42:8-9), Agano Jipya linatusihi kuomba kwa ajili ya neema ya Mungu kwa ajili ya Watesaji.

Yesu anawasihi wanafunzi, "**Wapendeni adui zenu, wabarikini wale ambao wawalaani ninyi, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi, na waombeeni wale ambao wawaonea ninyi na kuwatesa**" (Mat. 5:44, [*angalizo toka kwa mtafsiri*: mstari huu katika Biblia ya Kiswahili, Union Version 1997, umekatwa], angalia pia mistari ya 45-48); "Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, Wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi, wabarikieni wale ambao wawalaani ninyi, waombeeni wale ambao wawaonea ninyi" (Luka 6:27-28). Paulo anaielezea amri ileile kwa maneno yanayofanana, "Tukitukanwa twabariki, **tukiteswa** twastahimili" (1 Kor. 4:12).

Ushuhuda wenye kuvutia kupita yote wa Shahidi wa Imani anayekufa ni maombi ya Yesu kwamba Mungu atakuwa na rehema juu ya watesi wake. Aliomba, "Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo" (Luka 23:34). Shahidi wa kwanza wa imani aliye Mkristo, Stefano, aliomba "Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii" (Matendo ya Mitume 7:60). Maombi yote yalisikiwa, kwa sababu baadhi ya wauaji waliokolewa baadaye (Ofisa wa Kirumi katika Luka 23:47; Paulo katika Matendo ya Mitume 9:1-18). Historia ya Kanisa[208] hujumuisha maelezo mengi ya mashahidi wa imani wanaokufa kama vile Polycarp,[209] ambao wanaomba kwa ajili ya watesi wao.[210]

---

208 Tazama: Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, p. 245 [5. Book, Ch. 4, V.5].

209 Tazama: Martyrium des Polykarp 14,1-3 + 15,1 = pp. 12-15 katika: Herbert Musurillo (Ed.). The Acts of Christian Martyrs. Clarendon Press: Oxford, 1972, 'Martyrium des Polykarp' pp. 2-21, pia katika Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 78-81, und in Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, p. 212 [4. Book, Ch. 15, verse 33-35]. Juu ya mauaji ya shahidi wa imani Polycarp, tazama: Hans-Werner Surkau. Martyrien in juedischer und fruehchristlicher Zeit. *op. cit.*, pp. 126-134 na kumbukumbu zinazohusu vyanzo. Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, pp. 206-215 (4. Book, Ch. 14-15); tazama pia nyaraka za Polycarp, ambazo kwazo anawasilisha mtazamo wake mwenyewe juu ya mauaji ya mashahidi wa imani: "Die beiden Polykarp-Briefe". pp. 227-265 in: Joseph A. Fischer (Ed.). Die Apostolischen Vaeter. Koesel: Muenchen, 1981[8].

210 Tazama: Eusebius, Kirchengeschichte, 5, 2, 5-7 (Letter to the churches in Vienna and Lyon), in *Ibid.*, pp. 90-93 na katika Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, p. 246.

Kanisa la sasa lina mifano yake, Katika mwaka 1913, Mwinjilisti wa Kiindonesia, Petrus Octavianus,[211]alimwelezea mmishenari katika eneo la Toradya, Celebes ya Kusini. Watu watano wa kikabila walitaka kumwua, lakini walimruhusu aombe kwanza. Aliomba kwa sauti kuwa waokolewe. Watatu kati ya wauaji walikamatwa huko Java, na waliokolewa walipokuwa gerezani na walirudi Toradya, ambapo walianzisha kanisa ambalo baadaye (1971) lilikuja kuwa kanisa la nne kwa ukubwa katika Indonesia likiwa na waumini zaidi ya 20,000. Pia tusiwasahau wamishenari watano waliouawa kwa risasi na Aucas. Baadhi ya wauaji baadaye walikuja kuwa nguzo za kanisa la Aucan.[212]

35 Wauaji Huwa Waamini

Hoja: Wengi walioanza kama watesaji wa Wakristo baadaye wao wenyewe huwa waamini.

Tumekwishaona mifamo miwili tayari. Mfano hasa unaojulikana sana ni, Paulo, ambaye mara kwa mara hurejewa kwa mateso yake ya awali kwa Kanisa. (1 Kor. 15:9; Gal. 1:13+23; Flp. 3:6; 1 Tim. 1:13. Angalia pia Matendo ya Mitume 9:4-5; 22:4+7-8; 16:11+14-15). Anajieleza mwenyewe kuwa "mwenye kukufuru, na mtesaji, na mwenye kujeruhi" (1 Tim. 1:13), na akiandika kuhusu mwitikio wa Wakristo waliosikia kuokolewa kwake, "...ila wamesikia tu ya kwamba huyo **aliyetutesa wakati uliopita**, sasa anaihubiri imani ile aliyoiharibu **kwanza**. **Na** wakamtukuza Mungu kwa ajili yangu" (Wagalatia 1:23-24). *Tunapoomba kwa ajili ya waamini wateswao, tunapaswa kuwajumuisha watesaji,* ambao pengine wataokolewa au mioyo yao itafanywa migumu kwa sababu ya ushuhuda wa mashahidi wa imani. Hawataachwa bila kuguswa.

F. Umisheni na Mauaji ya Mashahidi wa Imani

36. Matunda ya Mauaji ya Mashahidi wa Imani

Hoja: Damu ya mashahidi wa imani ni mbegu ya Kanisa. Nukuu hii inayojulikana sana kutoka kwa Baba wa Kanisa Tertullian[213] imetufikia kupitia maandishi ya Augustine na Wanamatengenezo. Ilitangulia kuwaonya Wafalme wa Kirumi kuwa upinzani wao utalipanua tu Kanisa.[214] "Kadri mnavyozidi kutufyeka, ndivyo tunavyozidi kuongezeka: damu ya Wakristo ni mbegu."

---

211 Petrus Oktavianus. "Die Narde ausschuetten". pp. 120-128 in: Otto Riecker (Ed.). Ruf aus Indonesien, Haenssler: Neuhausen, 1973[3] [1971[1]]. p. 126.

212 Gruppe Elisabeth Elliot. Die Moerder - meine Freunde. CLV: Bielefeld, 1999 (Mama Elliot ni mjane mmojawapo wa wamishonari waliouawa kama mashahidi wa imani).

213 Juu ya theolojia ya Tertullian ya mauaji ya mashahidi wa imani, tazama: William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 223-272.

214 Adolf von Harnack. Die Mission und Ausbreitung des Christentums in den ersten drei Jahrhunderten. *op. cit.*, pp. 506-510.

("semen est sanguis Christianorum"; *Apologia* 50:12kk. 'Mbegu ya kanisa ni damu ya mashahidi wa imani' kimsingi ni tafsiri sahihi zaidi.[215])

Wakati Yesu akiwaonya wanafunzi wake juu ya mateso yajayo (Luka 21:12-21), alikuwa ametabiri, "Na hayo yatakuwa ushuhuda kwenu,"[216] (Luka 21:13).[217] Katika Waraka wa Wafilipi, Paulo anaonesha wazi kuwa kufungwa kwake na mateso yake hayazuii Injili bali yanaisukuma mbele (Wafilipi 1:12-26). "Lakini, ndugu zangu, nataka mjue ya kuwa mambo yote yaliyonipata yametokea zaidi kwa kuieneza Injili" (Wafilipi 1:12).

Kanisa la Kwanza mara kwa mara lilirejea maneno ya Yesu juu ya kifo chake katika Yohana 12:24; "Amini, amini, nawaambia, Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi." Kwa mfano, mwandishi mmoja anasema, "Huoni, kuwa, kadiri wanavyouawa, ndivyo wanavyoongezeka? Hii si kazi ya mwanadamu, bali uweza ya Mungu; hizi ni ishara za uwepo wake."[218] Martin Luther alielezea wazo lile lile kwa maneno yafuatayo, "Chini ya mateso, Ukristo hukua, lakini mahali amani na utulivu vinapotawala, Wakristo huwa wazembe na wasiojali."[219]

Na hasa, mateso ya kwanza yaliyopangwa katika Yerusalemu yalisababisha tu kusambaa kwa Wakristo katika eneo lote la Dola ya Rumi! Wamataifa wa mwanzo waliokolewa katika Antiokia, siyo na mitume bali na Wakristo wa 'kawaida' waliokuwa wamekimbia kutoka Yerusalemu (Matendo ya Mitume 7:54-8:8).[220] Mkutano wa Kimataifa juu ya Uinjilisti wa Dunia wa Lausanne (1974) ulibainisha, "Mateso ni dhoruba inayoruhusiwa kusambaza mbegu ya Neno, inayosambaza wapanzi na wavunaji, juu ya mashamba mengi. Ni njia ya Mungu ya kupanua ufalme wake."[221] Mateso yamekuwa moja kati ya sababu kubwa katika kueneza Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo.[222]

Matunda ya mateso hujionesha yenyewe katika njia tofauti. Wakati mwingine, Wakristo huimarishwa (Flp. 1:12), na wakati mwingine, Injili inaweza kuhubiriwa kwa watu ambao vinginevyo wasingeweza kuisikia (kwa mfano, Flp. 1:13 "**kikosi kizima cha Askari**"). Kutawanyika kwa Wakristo husambaza injili

---

215 Hans von Campenhausen. "Das Martyrium in der Mission". *op. cit.*, pp. 79-80.

216 Ushuhuda huu haumaanishi tu kwamba watu wataokolewa, lakini pia waweza kuonesha ushuhuda wenye kujieleza dhidi ya mtesaji, na hata uthibitisho wa upinzani wake kwa Mungu.

217 F. Kattenbusch. "Der Maertyrertitel". Zeitschrift fuer neutestamentliche Wissenschaft 4 (1903): 111-127, hier p. 112.

218 Letter to Diognet 7,8-9, repr. in: Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 103 (Nr. 40).

219 Martin Luthers Saemtliche Schriften. *op. cit.*, Vol. XIII, pp. 1078-1079.

220 Kipekee tazama Billy Kim. "God at Work in Times of Persecution (Acts 7:54-8:8)". pp. 57-59 in J. D. Douglas (Ed.). Let the Earth Hear His Voice: International Congress on World Evangelization Lausanne, Switzerland. World Wide Publ.: Minneapolis (MN), 1975.

221 *Ibid.*, p. 57.

222 *Ibid.* p. 58; See also B. Dyck. "Verfolgung foerdert Gemeindewachstum". Dein Reich komme (Licht im Osten) 2/1983: 5 juu ya Ethiopia, kama mfano.

katika maeneo mapya (Angalia Matendo ya Mitume 11:19-21 na 8:1). Wakati mwingine mateso hufanya mahubiri na ushuhuda wa waamini kutenda kazi kwa ubora zaidi. Katika karne tatu za mwanzo, maaskari na maofisa waliokuja kuwa Wakristo mara nyingi walikuwa katika hatari, lakini hesabu ya waamini katika jeshi iliongezeka kwa kwa kiwango kikubwa ajabu (ukianzia katika Agano Jipya!).[223]

Mfano wa hivi sasa ni China. Hatuwezi kuhesabu idadi ya Wakristo kwa usahihi katika China, kwa kuwa Serikali na vyanzo rasmi vya kikanisa kimataifa vinadanganya juu ya idadi hiyo. Hakuna sensa, na hatuna daftari la usajili la makanisa ya nyumbani. Katika gazeti lake la lugha ya Kijerumani, "China Insights," (Utambuzi wa China). Tony Lambert wa Overseas Mission Fellowship (zamani China Inland Mission), anayechukuliwa kuwa mjuzi wa takwimu za Ukristo wa China,[224] alifikia hitimisho kuwa takwimu zake ni za chini sana. Baada ya kupitia takwimu mpya za Serikali katika mwaka 1997, anaamini kuwa idadi ya milioni 18.7 hadi 39 aliyoifikiri mwaka mmoja kabla, inapaswa kuongezwa hadi milioni 33 , ambayo kwayo milioni 20 hadi 30 ni Wainjili.[225] Hii ingemaanisha kuwa China ni ya pili kwa idadi ya Wainjili duniani kote, baada ya Marekani yenye (Milioni 49). Brazili yenye (Milioni 13), Nigeria (Milioni 5), Kenya (milioni 4) na Korea Kusini (takribani milioni 4) Wakristo wa Kiinjili wana sababu chache za kutosha kujihusisha na kanisa kubwa lililo kimya, Kanisa la China.[226] Jarida la *Idea* linakisia idadi ya Wakrsito kuwa kubwa zaidi kwa mwaka 1999.[227] Wakati ambapo kumekuwa na makisio ya Waprotestanti milioni moja na Wakatoliki milioni tatu katika China mwaka 1949, kuna Waprotestanti takribani milioni 13 katika makanisa yaliyosajiliwa, Waprotestanti milioni 40-60 katika makanisa ya nyumbani, Wakatoliki milioni 4 katika makanisa rasmi ya Kikatoliki na milioni 8 Wakatoliki wa chini kwa chini.

Johan Candelin alisema vema kabisa kuhusiana na hali ya sasa ulimwenguni, kwamba si siku zote ni kweli, kuwa mateso huzaa kukua kwa kanisa, lakini katika nchi nyingi ulimwenguni mateso hukua kwa sababu makanisa yanayokuwa kwa haraka zaidi kuliko mengine ulimwenguni yako katika nchi ambamo hakuna uhuru wa kidini.[228] Hili ni jambo la kutunzwa akilini mwetu pia.

---

223 Adolf von Harnack. Die Mission und Ausbreitung des Christentums in den ersten drei Jahrhunderten. *op. cit.*, p. 580.

224 Tazama pia: Tony Lambert. The Resurrection of the Chinese Church: A Unique Study of the Miraculous Survival of the Church in China. Hodder & Stoughton: London, 1991.

225 Tazama: Global Chinese Ministries. June 1999. pp. 1-2, distributed by UEMG, 35325 Muecke, kwa ajili ya takwimu zaidi za kina juu ya majimbo binafsi.

226 Tazama: Bruder David, Dan Wooding, Sara Bruce. Gottes Schmuggler in China. R. Brockhaus: Wuppertal, 1981.

227 Idea Spekrtum 40/1999: 9.

228 Johan Candelin. "Persecution of Christians Today". S. 16-24 in: Konrad-Adenauer-Stiftung (Hg.). Persecution of Christian Today: Christian Life in African, Asian, Near East and Latin American Countries. Documentation October 28, 1999 Conference Venue ... Berlin. Konrad-Adenauer-Stiftung: Berlin, 1999 = Johan Candelin. "Christenverfolgung heute". S. 17-26 in:

37. Matunda si Kitu cha Kuja Chenyewe Tu

Hoja: Mateso hayaongozi kanisa moja kwa moja kufanya likue au liwe safi, au kuwa na imani yenye nguvu.

Uzoefu wa Kanisa la Ujerumani chini ya Awamu ya Tatu (Third Reich) na chini ya Ukomunisti, kwa mfano, haujaongoza kuelekea kwenye marejeo ya mateso mazito wala kwenye uamsho au kukua kwa kanisa. Hata pale mauaji ya mashahidi wa imani yanapozaa matunda, hata hivyo, matokeo yake hayajileti yenyewe, bali mara zote ni kwa sababu ya rehema ya Mungu.

Mfano wa Yesu wa mpanzi (Mat. 13:3-8+20-22) huonesha mateso na shinikizo kama tu kitu hatari kwa imani kama ulivyo utajiri na ubinafsi. Kipi ambacho ni hatari zaidi kwa imani; mateso au utajiri? Wakristo wa Magharibi wanapenda kutukuza mateso, na waamini walio katika mateso wanapenda kutukuza uhuru na utajiri. Mbali na wale wanaopokea neno la Mungu na wale wanaolikataa, mfano wa Yesu unaonesha makundi mawili zaidi ya watu, ambao wako wazi kwa ajili ya neno, lakini huangukia mbali: "Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda. Hata alipokuwa akipanda, mbegu nyingine zilianguka karibu na njia, ndege wakaja wakazila; nyingine zikaanguka penye miamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara zikaota, kwa udongo kukosa kina; na jua lilipozuka ziliungua; na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka. Nyingine zikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea, ikazisonga; nyingine zikaanguka penye udongo mzuri, zikazaa, moja mia, moja sitini, moja thelathini." (Mat. 13:3-8) "...Naye aliyepandwa penye miamba, huyo ndiye alisikiaye lile neno, akalipokea mara kwa furaha; lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikitukia dhiki au **mateso** kwa ajili ya lile neno, mara huchukizwa. Naye aliyepandwa penye miiba, huyo ndiye alisikiaye lile neno; na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno, likawa halizai." (Mathayo. 13:20-22). Imani ya mtu anayeteseka chini ya mateso na shinikizo, imani ya mwingine imesongwa na mambo ya dunia na udanganyifu wa utajiri. Hili linatuhusu hata sisi nasi, kana kwamba limezungumzwa mwaka wa 2000 na siyo miaka 2000 iliyopita! Kamwe Yesu hatukuzi mateso na vitisho vyake wala utajiri na hofu zake. Vyote ni majaribu ya mazito kwa imani yetu. Katika hali zote, tunahitaji kulishika neno la Mungu na kuzaa matunda.

Hatupaswi kuwa na husuda kwa wengine, lakini tunajifunza kutoka kwao. Sisi tunaofurahia uhuru tunapaswa kujifunza kutoka kwa wale wanaoteseka, kwamba Ukristo sio dini ya 'hali nzuri,' lakini tunaweza kuvumilia chini ya matokeo ya kuogofya sana. Mbali na hayo, tunaweza pia kutumia utajiri wetu na muda wetu kuisaidia familia ya imani inayoteseka. Kwa upande mwingine, Wakristo walio katika mateso wanaweza kujifunza kutoka kwetu kuwa amani na utajiri pekee havileti furaha au kuleta urahisi wa kuishi kwa mujibu wa ukweli wa Biblia. Imani yetu haitegemei hali, bali uaminifu kwa Mungu, anayetujaza na

---

Konrad-Adenauer-Stiftung (Hg.). Verfolgte Christen heute: Christen in den Laendern Afrikas, Asiens, des Nahen Ostens und Lateinamerikas. Dokumentation 28. Oktober 1999 Internationale Konferenz ... Berlin. Konrad-Adenauer-Stiftung: Berlin, 1999, toleo lililofupishwa: Johan Candelin. "Mundtot Gemachten Stimme geben: Christenverfolgung heute". Confessio Augustana 1/2000: 13-18

Roho wake Mtakatifu, anayetupa nguvu za kumtumikia yeye na kufanana zaidi na Kristo.

38. Mauaji ya Mashahidi wa Imani Huambatana na Umishenari wa Ulimwengu

Hoja: Mauaji ya mashahidi wa imani ni sehemu ya umishenari wa Ulimwengu, kwa kuwa "Umisheni huongoza kuelekea kwenye mauaji ya mashahidi wa imani; na mauaji ya mashahidi wa imani huwa ni Umisheni."[229]

Hans Campenhausen anafikia hitimisho hili katika kujifunza kwake juu ya Kanisa la Kwanza. Yesu aliwatuma Sabini[230] na wale Kumi na Wawili kwa maneno "Angalieni mimi nawatuma kama kondoo[231]kati ya mbwa-mwitu; basi iweni na busara kama nyoka, **na msio na madhara kama njiwa**." (Mat. 10:16; Luka 10:3 angalia hotuba yote juu ya mateso[232]; Mat. 10:16-42). Karl Rahner anatumia kanuni hiyo hiyo, "Kanisa na Umisheni huthibitishana kila moja."[233] Kutawanyika kwa Kanisa la Kristo ulimwenguni kote daima kumeambatana na damu ya mashahidi wa imani na umishenari ulimwenguni na ni 'umisheni chini ya msalaba'[234] Hata kwa wazi zaidi ni aina ya mateso yasiyo na majuto. "Kadiri Kanisa linavyohubiri Injili, daima litakabiliana na kukataliwa, mateso na kifo"[235] Haishangazi kwamba baada ya kumwongoza kwa Kristo na kumwita kuwa mwinjilisti, Anania alimtahadharisha Paulo kuwa huduma yake ingekuwa na matokeo makubwa, lakini pia ingemletea mtume mateso makubwa: "Lakini Bwana akamwambia, Nenda tu; kwa maana huyu ni chombo kiteule kwangu, alichukue Jina langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli. Maana nitamwonyesha yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya Jina langu" (Matendo ya mitume 9:15-16). Kwa hiyo, Elimu ya umisheni ni lazima itoe kipaumbele katika suala la mateso kuliko ilivyofanya hapo nyuma, tukichukulia kama vielelezo vyetu wana-umisheni kama vile Karl Hartenstein[236] na Gerge

229 Hans von Campenhausen. "Das Martyrium in der Mission". *op. cit.*, p. 71.

230 Tazama Theofried Baumesiter. "Maertyrer und Verfolgte im fruehen Christentum" *op. cit.*, p. 172.

231 Luka anawarejea wao kama kondoo.

232 Peter Mayer. "Zeugnis und Leiden des Juengers Jesu - nach Matth. 10". pp. 2-16 in: Urgemeinde und Endzeitgemeinde - Missionarische Existenz in Zeugnis und Leiden: Vier Referate der Jahrestagung des Arbeitskreises fuer evangelikale Missiologie (AfeM). Idea Dokumentation 3/1988.

233 Karl Rahner. Zur Tehologie des Todes, *op. cit.*, p. 93.

234 Bruno Her, akinukuriwa katika: Ingrid Kastelan. "Verfolgung ist letztendlich Verheissung". idea 45/1977 (7.11.). pp. I-II, here p. I (on the AEM conference,"Gemeinde in Bedraengnis" 2.-6. Nov., 1977 in Burbach-Holzhausen).

235 I. Bria. *op. cit.*, 268.

236 Tazama: Christof Sauer. Mission und Martyrium: Studien zu Karl Hartenstein und zur Lausanner Bewegung. *op. cit.*; Christof Sauer. "Die Bedeutung von Leiden und Martyrium fuer die Mission nach Karl Hartenstein". pp. 96-109 in: Fritz H. Lamparter (Ed.). Karl Hartenstein: Leben in weltweitem Horizont: Beitraege zu seinem 100. Geburtstag. edition afem - missions scripts 9. Verlag fuer Kultur und Wissenschaft Schirrmacher: Bonn, 1995; Karl Rennstich. "Urgemeinde und Endzeitgemeinde:

Vicdeom[237], walioyachukulia mateso ya wamishenari na ya kanisa linalochipuka kama sehemu muhimu ya theolojia yao ya umisheni.

39. Shahidi wa Imani kama "Shahidi"; 'Ushuhuda' wa mashahidi wa imani

Hoja: Uhusiano baina ya Neno la Kigriki familia 'ushuhuda' (martys') na kifo cha Wakristo kwa ajili ya imani yao, halikuchimbukia katika Kanisa la Kwanza, bali ni Ufunuo wa Yohana Mtume, ambaye anazungumzia juu ya "roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ushuhuda (Kigriki, 'Martyria) waliokuwa nao" (Ufunuo 6:9) na juu ya Antipas, aliyeuawa huko Pergamo "Shahidi Mwaminifu" (Ufunuo 2:13). Shahidi wa imani ni shahidi wa mateso ya Kristo, "Shahidi mwaminifu" (Kigriki, 'martys'), (Ufunuo 1:5; 3:14).[238] Mashahidi wawili katika sura ya 11 wanakufa kwa ajili ya imani yao, na Ufunuo 17 inamweleza Kahaba wa Babeli "amelewa kwa damu ya watakatifu na kwa damu ya mashahidi wa Yesu" (mstari wa 6). Uhusiano wa karibu kati ya neno la Kigriki familia na mauaji ya waamini katika Ufunuo uko wazi kabisa, kwamba wengine huamini maana ya baadaye "martyr" ndio ilikuwa imekusudiwa,[239]ingawa wengine hawakubali.[240] Herman Strathmann, akiandika juu ya Ufunuo 2:13, anadhihirisha kizungumkuti kwa kuonesha kuwa Antipas hakuwa shahidi kwa kufa, bali aliuawa kwa sababu alikuwa shahidi.[241] Paulo anatumia neno linalofanana na hilo katika Matendo ya Mitume 22:20 "Na damu ya Stefano shahidi wako ilipomwagwa" hata Theofried Baumeister yuko tayari kukubali vifungu hivi kama matumizi ya awali ya neno katika maana hii.[242] Stefano aliuawa kwa sababu ya ushuhuda wake, lakini Matendo ya Mitume 22:20 hulihusisha wazo la kifo na ushuhuda kwa karibu sana.

Missionarische Existenz in Zeugnis und Leiden." pp. 17-27 in: Urgemeinde und Endzeitgemeinde - Missionarische Existenz in Zeugnis und Leiden: Vier Referate der Jahrestagung des Arbeitskreises fuer evangelikale Missiologie (AfeM). Idea Dokumentation 3/1988. pp. 20-25.

237 Tazama: Georg Vicedom. Das Geheimnis des Leidens der Kirche. Theologische Existenz heute NF 111. Chr. Kaiser: Muenchen, 1963; Johannes Triebel. "Leiden als Thema der Missionstheologie": Der Beitrag Georg Vicedoms zum Thema im Kontext gegenwaertiger Stimmen. Jahrbuch fuer Mission 20 (1988): 1-20.

238 I. Bria. "Martyrium". *op. cit.*, . 266.

239 Kwa mfano, Hans von Campenhausen. Die Idee des Martyriums in der Alten Kirche. *op. cit.*, 1936[1]; 1964[2]. pp. 42-46; Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 43-49; Walter Bauer. Griechisch-deutsches Woerterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments ... Walter de Gruyter: Berlin, 1971[5]. Col. 977; 1988[6]. Col. 1002; See also: F. W. Danker. "Martyr". p. 267 in: Geoffrey W. Bromiley. (Ed.). The International Standard Bible Encyclopedia. Vol. 3. Wm. B. Eerdmans: Grand Rapids (MI), 1986. Kwa mujibu wa: Theofried Baumeister. "Maertyrer und Verfolgte im fruehen Christentum". *op. cit.*, p. 170, karne ya pili Kanisa lilifasili vifungu husika katika Ufunuo kwa njia hii.

240 Kwa mfano: Johannes Beutler. "martyreo", "martyria", "martys" *op. cit.*, pp. 966-967; Allison A. Trites. The New Testament Concept of Witness. Society for New Testament Studies - Monograph Series 31. Cambridge University Press: Cambridge, 1977. pp. 154-174.

241 Hermann Strathmann. "martys, martyreo, martyria, martyrion". *op. cit.*, p. 499.

242 Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 31-32. Kwa mujibu wa: Theofried Baumeister. "Maertyrer und Verfolgte im fruehen Christentum". *op. cit.*, p. 170, karne ya pili Kanisa lilifasili vifungu vya Ufunuo kwa njia hii.

Vilevile vifungu vingine huhusisha mauaji ya mashahidi wa imani na ushuhuda. Katika Waebrania 11:4, Mungu anaipa damu ya Habili. "ushuhuda wa haki". Katika Luka 21:12-15, Yesu anatangaza kuwa tamko la mwamini mahakamani litachukuliwa kama 'ushuhuda' na ya kwamba Roho Mtakatifu angetoa hekima iliyo muhimu. Wote Yohana (Ufunuo 1:5; 3:14) na Paulo (mara nyingi, lakini angalia 2 Tim. 6:13; Kol. 1:20-21; Flp. 2:8) wanathibitisha kuwa Yesu alishuhudia na kudhihirisha kwa njia ya kifo chake. Wengi wanaona uhusiano wa karibu kati ya 'ushuhuda mzuri' wa Yesu mbele ya Pilato (1Tim. 6:13) na neno 'martyr'[243].

Mwaka 1998, F. Kattenbusch[244] alianzisha mdahalo mzito[245] wa maana ya neno 'martyrs'. Je, Agano Jipya lilitumia istilahi ya Kigriki 'shahidi' kumaanisha 'mashahidi wa imani', au matumizi haya yalikuwa ni matokeo ya baadaye?[246] Katika mwaka 1936, Hans von Campenhausen kwa nguvu alitetea wazo kwamba Kanisa la Kwanza limechota maana zake mbili ('martys' kwa pamoja kama 'shahidi' na 'shahidi wa imani') kutoka Agano Jipya.[247] Wakosoaji wa baadaye wa mtazamo huu, kama vile Norbert Brox,[248] wanaelewa 'shahidi' humaanisha 'mhubiri anayeshuhudia'. Brox haoni uhusiano kati ya wazo la 'shahidi' na 'shahidi wa imani' katika istilahi ya Kigriki.[249] Waandishi wengi wengine wanafuata wazo lake, ingawa wachahce wanalitumia inavyopasa.[250]

---

243 Walter Bauer, Kurt und Barbara Aland. Griechisch-deutsches Woerterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments ... Walter de Gruyter: Berlin, 1988[6]. Sp. 999 = Walter Bauer. Griechisch-deutsches Woerterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments ... Walter de Gruyter: Berlin, 1971[5]. Col. 974 and Hermann Strathmann. "martys, martyreo, martyria, martyrion". *op. cit.*, p. 507.

244 F. Kattenbusch. "Der Maertyrertitel". *op. cit.*, pp. 111-127; Tazama pia makala inayofuata ya E. Hocedez. "Le concept de martyr". Nouvelle Revue Théologique 55 (1928): 81-99 + 198-208.

245 Norbert Brox. Zeuge und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 114-131; anatoa maelezo yaliyosheheni.

246 F. Kattenbusch. "Der Maertyrertitel". *op. cit.*, pp. 112+114 anakubaliana kwa msingi wa Luka 21:13 na Waebrania 12:1, lakini kwa tahadhari tu.

247 Hans von Campenhausen. Die Idee des Martyriums in der Alten Kirche. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1964[2] [1936[1]]. hususani. kk. 21-29+42-46 (Katika Utangulizi wake wa toleo la mwaka 1964[2], Campenhausen anarudi nyuma kwa kiwango fulani, pasipo kutoa sababu zozote na pasipo kukirudufu kitabu chake. Tazama: Hans von Campenhausen. "Das Martyrium in der Mission". pp. 71-85 katika: Heinzguenter Frohnes, Uwe W. Knorr (Ed.). Die Alte Kirche. Kirchengeschichte als Missionsgeschichte 1. Chr. Kaiser: Muenchen, 1974; See also Ernst Guenther. Martys: Die Geschichte eines Wortes. Bertelsmann: Guetersloh, 1941.

248 Dhidi ya von Campenhausen: Norbert Brox. Zeuge und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 115-117 + 92-105 (kwa rejea zilizo katika Ufu.) na Allison A. Trites. The New Testament Concept of Witness. *op. cit.* Allison A. Trites. "martys and Martyrdom in the Apocalypse". Novum Testamentum 15 (1973): 72-80; Johannes Beutler. Martyria: Traditionsgeschichtliche Untersuchungen zum Zeugnisthema bei Johannes. Frankfurter theologische Studien 10. Knecht: Frankfurt, 1972 (an excellent summary of Brox Ibid, pp. 32-33); Johannes Beutler. "martyreo", "martyria", "martys" *op. cit.*

249 Norbert Brox. Zeuge und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 230-236.

250 Kwa mfano,. Johannes Beutler. "martyreo", "martyria", "martys". *op. cit.* na Werner Stoy. Mut fuer Morgen. *op. cit.*, pp. 67-68.

'Mhubiri' ni maana moja tu inayowezekana ya "shahidi". Maneno ya Kiebrania na Kigriki kwa shahidi yote yanatokana na mazingira ya kisheria.[251] 'Shahidi' katika Agano la Kale daima alieleweka kuwa shahidi katika mahakama ya sheria, hivyo basi shahidi wa imani aweza kuwa shahidi wa Mungu mbele ya wanadamu au shahidi[252] katika Hukumu dhidi ya watesi,[253] bila ya kuwa 'mhubiri'. Nehemia 9:26 waziwazi inawawasilisha manabii kama mashahidi wa mateso, walioondoshwa kwa chuki ya Wayahudi, "...waliwaua manabii wako walioshuhudia dhidi yao ili wakugeukie." Baadaye dini ya Kiyahudi ikalichukua wazo hilo, "Wakati ule ule, kifo cha watakatifu ni ushuhuda wa ajabu dhidi ya wauaji, inalenga zaidi ya yenyewe kuelekea siku zijazo"[254]

Matendo ya Mafarisayo na Masadukayo hushuhudia dhidi yao wenyewe, Yesu anawaambia 'Hivi mwajishuhudia wenyewe, ya kwamba ninyi ni wana wao waliowaua manabii' (Mat. 23:31)[255]. Hivyo, Maandiko hufundisha yote, ushuhuda wa maneno na ushuhuda wa matendo. Yesu anayaelezea maneno yake mwenyewe kama ushuhuda (Yohana 5:36; 10:25; 10:37-38)[256]. Shahidi wa imani hashuhudii tu kwa kutoa ushuhuda, bali pia kwa kifo chake.[257] Katika Luka 21:13, Yesu anatangaza, "Na hayo yatakuwa ushuhuda kwenu."[258] Wauaji ama watashupazwa zaidi au wataletwa katika toba kwa ushuhuda wa shahidi wa imani. Wakati mwingine Mungu huwaita wanadamu kuwa mashahidi katika vita yake dhidi ya mwanadamu, na hata dhidi ya watu wake mwenyewe. Otto Michel

---

251 Hermann Strathmann. "martys, martyreo, martyria, martyrion". *op. cit.* 479.

252 Kwa mujibu wa Gerhard Besier. "Bekenntnis - Widerstand - Martyrium als historisch-theologische Kategorie". *op. cit.*, p. 128, wakati mwingine tofauti ilifanywa kati ya 'martyria', iliyotumiwa katika Injili-fanani kuonesha wito wa shahidi kwa ajili ya uongofu, na 'martyrion' kumaanisha ushuhuda dhidi ya watesaji. (Mk 1:4 hususani; 6:11; Mt 24:14), wakati wote si kitu kilicho sawa. Tazama: Walter Bauer. Griechisch-deutsches Woerterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments ... Walter de Gruyter: Berlin, 1971[5].Col. 975-976 = Walter Bauer, Kurt and Barbara Aland. Griechisch-deutsches Woerterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments ... Walter de Gruyter: Berlin, 1988[6]. Col. 1000-1001. Kuhusu 'martys' katika matumizi ya kisheria katika Mk 14:63 = Mt 26:65, tazama: Hermann Strathmann. "martys, martyreo, martyria, martyrion". *op. cit.* p. 493. Istilahi zote, 'martyrion' und 'martyria', baadaye zilitumika kumaanisha mauaji ya mashahidi wa imani.

253 Norbert Brox. Zeuge und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 27-29 anatafuta maana ya 'ushuhuda kwa ajili ya mashtaka' katika Hukumu ya Mwisho katika Mathayo na Marko tu, na katika Yakobo 5:3 hurejea kwa vitu vya dunia hii. Ethelbert Stauffer. Theologie des Neuen Testamentes. Bertelsmann: Guetersloh: 1941[1]. p. 316, hata hivyo, anaonesha kwamba Agano la Kale na Dini ya Kiyahudi ya baadaye pia vilikuwa vikifahamu wazo la mtumishi wa Mungu kama shahidi kwa ajili ya mashtaka katika mashtaka ya kisheria ya Mungu dhidi ya mwanadamu.

254 Ethelbert Stauffer. "Maertyrertheologie und Taeuferbewegung". *op. cit.*, p. 545 juu ya Dini ya Kiyahudi kabla ya wakati wa Yesu.

255 Johannes Beutler. "martyreo", "martyria", "martys". *op. cit.*, p. 959.

256 Ceslas Spicq. Theological Lexicon of the New Testament. Hendrickson: Peabody (MA). [Original: Fribourg/CH, 1978/1982]. 3 Vols, Vol 2, pp. 447-452 ("martys").

257 Kipekee zaidi Hans von Campenhausen. Die Idee des Martyriums in der Alten Kirche. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1936[1]; 1964[2]. p. 55.

258 Kiekee zaidi F. Kattenbusch. "Der Maertyrertitel". *op. cit.*, p. 112.

anaamini wazo hili kuwa chanzo cha wazo la shahidi wa imani katika Agano la Kale na Jipya.[259]

Allison A. Trites anafafanua hatua tano katika maendeleo ya neno 'Martys'. 1. Shahidi katika mwenendo wa kisheria 2. Shahidi katika mwenendo wa kisheria ambaye anahukumiwa kwa sababu ya ushuhuda wake. 3. Kifo kama sehemu ya ushahidi. 4. 'Martys'= 'martyr', lakini likijumuisha wazo la 'shahidi' 5. 'Martys'= 'martyr', lakini likiweka kando wazo la 'shahidi'[260].

Trites anachukulia kuwa maneno mengine ya neno familia 'martys' yalitumiwa katika ngazi ya kwanza na ya pili ya maendeleo[261] lakini neno 'martys' lenyewe tayari lilifikia ngazi ya tatu mwishoni mwa wakati wa Agano Jipya.[262] Hii ingemaanisha kuwa neno 'martys' bado lilikuwa halina mana ya 'martyr'; lakini tayari lilikuwa limeshahusishwa nalo kwa uzito sana [263].

Ningekubaliana na Oda Hagemeyer,[264] ambaye anahitimisha kuwa Agano Jipya halilitumii neno hilo kumaanisha 'a martyr' (shahidi wa imani), bali kwamba maana yake inahusishwa kwa karibu sana na ushuhuda wa imani, kwamba tayari tunaweza kugundua hatua za mwanzo katika maendeleo ya matumizi ya baadaye. Herman Strathmann anaandika, 'Karne ya pili inaona maendeleo zaidi ya hatua za mwanzo bayana katika Agano Jipya, zaidi ya yote katika kazi zenye mtazamo wa Yohana'.[265] Kwa mujibu wa Strathmann, matumizi ya Agano Jipya kumaanisha 'shahidi' si zaidi wala pungufu kuliko yale ya hatua za awali[266] katika maendeleo ya maana ya baadaye ya 'martyr'.

Brox ameonesha kuwa Agano Jipya na Kanisa la Kwanza huendelea kutumia 'martys' katika maana yake ya kawaida 'shahidi'.[267] "Kama ilivyo kwa 'martys', chini ya mbinyo wa uzoefu wa Kanisa, neno 'martyria' pia lilikuza uhusiano wa karibu katika kesi ambazo kifo kilithibitisha uaminifu wa shahidi na ushuhuda wake. Neno lilichukua taswira nzuri ya mauaji ya mashahidi wa imani.[268]

---

259 Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.*, p. 20.

260 Allison A. Trites. "martys and Martyrdom in the Apocalypse: A Semantic Study". Novum Testamentum 15 (1973): 72-80, here pp. 72-73.

261 *Ibid.* p. 77.

262 *Ibid.* p. 80.

263 *Ibid.* p. 77.

264 Oda Hagemeyer. "Theologie des Martyriums". Benediktische Monatsschrift 60 (1984) 309-315. hapa ni kr. 310-311.

265 Hermann Strathmann. "martys, martyreo, martyria, martyrion". *op. cit.*, p 511.

266 *Ibid.*, p. 508; sawa na F. W. Danker. "Martyr". p. 267 katika: Geoffrey W. Bromiley. (Ed.). The International Standard Bible Encyclopedia.Vol. 3. Wm. B. Eerdmans: Grand Rapids (MI), 1986 na Otto Hiltbrunner. "Martys". p. 1059-1060 katika: Konrat Ziegler, Walther Sontheimer (Ed.). Der Kleine Pauly: Lexikon der Antike. 5 Vols. Vol. 3. dtv: Muenchen, 1979 [toleo-rudufu 1975] hutaja

267 Norbert Brox. Zeuge und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 196-230; Tazama ufupisho wake, kr. 231-236.

268 Hermann Strathmann. "martys, martyreo, martyria, martyrion". *op. cit.*, p. 507.

Haijulikani wazi ni kumbukumbu gani ilitumia kwanza neno hilo kumaanisha mauaji ya mashahidi wa imani. Theofried Baumeister, anaamini kuwa *The Sherpherd of Hermas* (Mchungaji wa Herma) bado inapungukiwa neno sahihi[269]. Clemens wa Rumi anaweza kuunganisha ushahidi wa mdomo na mauaji ya mashahidi wa imani kwa ukaribu,[270] lakini bila kutumia neno 'martyr' katika maana hiyo. Anambuni Petro kama 'shahidi' au 'shahidi wa imani' na anataarifu kuwa, "baada ya kushuhudia, alijipatia nafasi katika utukufu uliyomstahili"[271] Kuhusu Paulo, Clemens anaandika; '...na akatoa ushuhuda mbele ya mtu maarufu, hivyo ndivyo alivyoondoka kutoka katika ulimwegu huu.'[272] Je, Clemens anatumia neno 'ushuhuda' kumaanisha tamko la mitume au vifo vyao?[273]

Wakati mwingine kati ya Ignatius na 'Mauaji ya Polycarp', Baumeister anaona kuzaliwa kwa istilahi ya zamani ya shahidi wa imani (martyr). Anachukulia 'Mauaji ya Polycarp' (2.1), yaliyoandikwa mnamo 160 BK.[274] kuwa ushahidi wa kwanza wa matumizi ya neno 'ushuhuda' kumaanisha mauaji ya mashahidi wa imani [275]. Mfano wa mwanzo kabisa unaokubalika ulimwenguni, matumizi yake katika kumbukumbu hii huonekana kuakisi matumizi ya jumla. Katika waraka wa Makanisa kutoka Vienne na Lyon, 177 BK., matumizi haya yanaonekana kuwa ya kawaida; Kristo anaitwa "shahidi wa imani wa kweli na mwaminifu"[276]

Hata tangu karne ya pili, kwa Mkristo kuamua kufa kwa ajili ya imani yake ilichukuliwa kuwa hali ya juu kabisa ya mateso.[277] Kanisa lilitofautisha kati ya

---

269 Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 257.

270 Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 45, Note. 6 on Klemens of Rom, (1.) Klemensbrief 5,4+7.

271 (1.) Klemensbrief 5,4, "Der Klemensbrief". pp. 1-107 in: Joseph A. Fischer (Ed.). Die Apostolischen Vaeter. Koesel: Muenchen, 1981[8] p. 31.

272 Klemensbrief 5,7, *Ibid.*, p. 33.

273 Ninaona mbadala wa pili kuwa na uwezekano, kwa kuwa Petro anapata utukufu moja kwa moja baada ya ushuhuda wake; Tazama pia: F. Kattenbusch. "Der Maertyrertitel". *op. cit.*, p. 112 na Walter Bauer, Kurt and Barbara Aland. Griechisch-deutsches Woerterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments ... Walter de Gruyter: Berlin, 1988[6]. Col. 999.

274 Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 75.

275 Walter Bauer, Kurt and Barbara Aland. Griechisch-deutsches Woerterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments ... Walter de Gruyter: Berlin, 1988[6]. Col. 999.

276 Brief der Gemeinden von Vienne und Lyon (177 A. D.), in Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p. 91; see also Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, pp. 233-245 [5. Book, Ch. 2-3].

277 Maelezo zaidi katika The Shephard of Hermas, Parabel IX, 29; tazama: Theofried Baumeister. "Maertyrer und Verfolgte im fruehen Christentum". *op. cit.*, p.169.

'mtu anayeungama' (Kilatini, 'confessor', Kigriki, 'homologetes'),[278] ambaye alihukumiwa kwenda jela kwa ajili ya imani, lakini bado alikuwa akiishi, na hata anaweza kuachiwa huru; na shahidi wa imani. Cyprian, alitofautisha kati mashahidi wa imani, waungamaji waliokuwa wakiteswa, na 'mwaminifu' (Kilationi, 'stantes') ambao bado walikuwa hawajapata nafasi ya kuthibitisha imani yao mbele ya wenye mamlaka.[279] Utofautishaji huu, ambao ulianza kufifia baada ya Cyprian,[280]si wenye makosa. Kweli ni wenye kusadia, lakini bado haupatani na istilahi ya Agano Jipya, ambayo haiwaundi tu Wakristo wanaouawa kwa ajili ya imani yao, bali pia wale walio katika hofu ya kifo au aina nyingine za mateso.

40. Ushindi na Kushindwa kwa Manabii Vyote Huenda Pamoja

Hoja: Katika maagano yote, ushindi na miujiza husimama pamoja na kushindwa, mateso na kifo.[281]

Mwandishi wa Waebrania anaileza miujiza na ushindi wa manabii wa Agano la Kale (Ebr. 11:32-25) na kushindwa na kuuawa kwao (Ebr. 11:35-38). Maisha ya Yesu na wanafunzi wake hayana tofauti, kwa kuwa aliwatuma kama ambavyo yeye alitumwa (Yohana 17:18; 20:21). Wanashiriki katika kutumwa kwake, nguvu ya ufufuo wake, ushindi wake, udhaifu wake na kuuawa kwake ('theologia crucis'). Mungu anamkomboa Petro kwa njia ya mwujiza, kwa mfano (Matendo ya Mitume 12:7-11), lakini anaruhusu Yakobo kuuawa katika wimbi la mateso yale yale (Matendo ya Mitume 12). Yesu anatabiri kuuawa kwa Petro, lakini anamwepusha nayo Yohana (Yohana 21:15-23).[282] Yeremia anasimulia juu ya ukombozi wake akiuhusisha na kuuawa kwa Uria (Yeremia 26:23-24). Ni juu ya mamlaka ya hekima ya Mungu kuamua ni barabara gani watoto wake wanapaswa kupita. "Mapenzi yako yatimizwe!" (Mat. 26:42; Luka 22:42; Angalia pia Mat. 26:39, "kama utakavyo wewe" au Matendo ya Mitume 21:14; "Mapenzi ya Bwana na yatendeke")

Daima Mungu hutuma malaika kuwapa tahadhari, kuwalinda au kuwakomboa huru wanaoteswa (mfano; Yesu wakati wa utoto wake, Mat. 2:13-15; Petro na Yohana, Matendo ya Mitume 5:19-20; Petro, Matendo ya Mitume 12:11; marafiki watatu wa Daniel, Dan. 3). Wakati mwingine, Mungu huwasaidia watoto wake kwa matetemeko ya ardhi ya kimiujiza au wanyama hatari sana (Ebr. 11:33-35; Matendo ya Mitume 16:26; Daniel 6).

---

278 Maelezo zaidi katika Eusebius von Caesarea. Kirchengeschichte. *op. cit.*, p. 244 [5. Book., Ch. 4, V.3]; Tazama pia Theofried Baumeister. "Maertyrer und Verfolgte im fruehen Christentum". *op. cit.*, p. 170.

279 Tazama Johannes Herzog. "Maertyrer". *op. cit.*, p 167.

280 *Ibid.*

281 Tazama kichwa cha habari cha kitabu cha Herbert Schlossberg, Called to Suffer, Called to Triumph: 18 True Stories by Persecuted Christians. Multnomah: Portland (OR), 1990.

282 Tazama Otto Michel. Prophet und Maertyrer. *op. cit.* p. 27.

Yohana alijichukulia mwenyewe kama 'mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo' (Ufunuo 1:9) na hivyo anahubiri mateso na uwezekano wa kukombolewa, na ushindi wa mwisho wa Kanisa.

41. Udhaifu wa Mkristo ni Nguvu Yake

Hoja: Nguvu ya Mkristo hulala katika udhaifu wake, kama udhaifu wa Yesu Kristo ulivyomaanisha ushindi wake juu ya ulimwengu na juu ya Shetani. Kanuni hii hutenda kazi kwa kanisa zima ulimwenguni, na kwa Mkristo mmoja mmoja.

Mara nyingi Paulo aliutumia ukweli huu, ambao Yohana aliutumia katika Ufunuo kwa kanisa zima na kwake binafsi. Kitabu cha Wakorintho wa Pili hurejea juu ya ukweli huu mara kwa mara.[283] "Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na **mateso**, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu" (2 Wakorintho 12:9-10). Ikiwa andiko hili linawasilisha, 'udhaifu' wa Paulo kama 'utukufu' wake wa kweli; basi uko wazi zaidi katika 2 Wakorintho 11:23-30, ambao katika huo Paulo 'anajisifu' kwa ajili ya wahudumu wa Kristo walioridhika na vipawa vyao maalumu na mafanikio: "Wao ni wahudumu wa Kristo? (Nanena kiwazimu), mimi ni zaidi; katika taabu kuzidi sana; katika vifungo kuzidi sana; katika mapigo kupita kiasi; katika mauti mara nyingi. Kwa Wayahudi mara tano nalipata mapigo arobaini kasoro moja. Mara tatu nalipigwa kwa bakora; mara moja nalipigwa kwa mawe; mara tatu nalivunjikiwa jahazi; kuchwa kucha nimepata kukaa kilindini" (2 Wakorintho 11:23-25). Anahitimisha kwa maneno, "Ni nani aliye dhaifu, nisiwe dhaifu nami? Ni nani aliyekwazwa nami nisichukiwe? Ikinibidi kujisifu, nitajisifia mambo ya udhaifu wangu" (2 Kor. 11:29-30). Mwanzoni mwa waraka (2 Kor. 6:4-5), anarejea kwenye mateso - siyo ushindi wake - kama uthibithisho wa ofisi yake: "Bali katika kila neno tujipatie sifa njema, kama watumishi wa Mungu; katika saburi nyingi, katika dhiki, katika misiba, katika shida; katika mapigo, katika vifungo, katika vitina, katika taabu ..."

Fumbo hili linapendekeza tathmini mpya kabisa ya mateso ya waamini na kushindwa kwa wazi, ama kwa ajili ya udhaifu binafsi au upinzani wa dunia inayowazunguka. Hivyo Paulo anaandika "wala hamwaogopi adui zenu, katika neno lolote; kwao hao ni ishara madhubuti ya kupotea, bali kwenu ninyi ni ishara ya wokovu, huo utokao kwa Mungu" (Wafilipi 1:28. Angalia mazingira katika mistari ya 27-30).

42. Kufunuliwa kwa Wana wa Mungu

Hoja: 'Kufunuliwa kwa wana wa Mungu' (Rum. 8:10; angalia pia mistari ya 18-25), somo muhimu katika Agano Jipya litatokea wakati

---

283 Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 169-176.

wa Hukumu ya Mwisho, wakati Mungu atakapowafunua wale walio wake na wasio wake.

Haki yetu, ukweli wa kisheria ulioimarishwa kwa muda mrefu, utafunuliwa kwa watu wote katika nguvu zote, kwa ulimwengu usioonekana na unaooonekana. "Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo" (1 Yohana 3:2). Paulo anaandika, "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu" (Wakolosai 3:1-4).

Kwa sababu nyingi, wakati mwingine Wakristo huona vigumu kuukubali ukweli wa ufunuo wa utukufu na mamlaka yetu. Hatuwezi kuchukua wazo kwamba kutakuwa na siku ya hukumu na kisasi, wakati yale yote yaliyotendwa kwa waamini yatathibitishwa na kuadhibiwa. Na kilicho kigumu kumeza ni wazo kuwa rufaa ya haki inayofanywa kwa Mungu katika 'Zaburi ya Kisasi' au katika Ufunuo (kwa mfano Ufunuo 6:10) itatoshelezwa. Lakini ni kwa vipi Mkristo anaweza kuukataa ukweli uliohubiriwa wazi mara kwa mara katika Biblia? Wakristo wengi wana matatizo, kwa sababu:

1. Awali ya yote, hawachukulii ghadhabu ya Mungu kwa umuhimu mkubwa.

2. Hawaichukui nafasi yao ya kisheria kwa umuhimu mkubwa, kwa kuwa wanahukumu vitu vyenye ushahidi wa yale wanayoyaona au waliozoelea.

3. Wamepoteza au wamezimisha matumaini yao katika ushindi wa mwisho wa Mungu wenye kuonekana dhahiri na katika Neno lake.

4. Wanajihusisha tu na wokovu wao binafsi, si wa ulimwenguni unaobaki. Hawajihushi na Umisheni, uchumi, siasa wala historia.

Utazamiaji mabaya wa mtu binafsi au wa kitamaduni ulio wazi kwa Wainjili; si tu unaleta kukanganyikiwa kuhusu kufunuliwa kwa hukumu ya mwisho. Pia hatuoni umuhimu wa kivitendo katika unabii kuhusu hali ya siku zijazo ya Uumbaji (kwa mfano, Warumi 8:15-39). Iwapo twajali unabii huo kwa ujumla, tunaupeleka hadi katika Umilele.

43. Kilio kwa Ajili ya Haki

Hoja: Agano la Kale na Agano Jipya mara kwa mara hudai hukumu ya haki kwa wale wanaolitesa Kanisa, na huendelea kuonya kuwa hukumu ya kutisha inawangojea wale wanaompinga Mungu na Kanisa lake (hasa Zaburi 5; 7; 10; 35; 59; 83; 109; 137; 139; 10)[284]

---

284 Cornelis van der Waal. Het Verbondsmatig Evangelie. Buitjen & Schipperheijn: Amsterdam, 1990. pp. 144-149 = Cornelis van der Waal. The Covenantal Gospel. Inheritance Publ.: Neerlandia (CAN), 1990. pp. 127-131 and Werner Stoy. Mut fuer Morgen. *op. cit.*, pp. 50-51.

Matamanio haya yako wazi zaidi katika maombi ya mashahidi wa imani katika Ufunuo 6:10 "**...Hata lini, Ee Bwana, mtakatifu na wa kweli, hutahukumu na kulipa kisasi cha damu yetu juu yao wakaao juu ya nchi?**" Hii si rufaa tu kwa ajili ya kisasi binafsi, wala haidai kazi ya kivitendo ya kidunia au kuhalalisha nguvu yoyote ya kibinadamu katika neno au tendo. Wakristo wanajua kuwa Mungu amekwisha kuahidi, "Kisasi ni juu yangu mimi; mimi nitalipa," (Warumi 12:19). Tukiwa tumehakikishiwa kisasi cha Mungu, tunaweza kuwabariki wale wanaotutesa (Warumi 12:14)! Rufaa hii kwa ajili ya haki huelekeza kwenye uhakika ujao kuwa Mungu atawafunua wote waliokuwa sawa na wote waliokuwa wamekosea: 'Hata na sisi twaona fahari juu yenu katika makanisa ya Mungu kwa ajili ya saburi yenu, na imani mliyo nayo katika **mateso yenu yote** na dhiki mnazostahimili. Ndiyo ishara hasa ya hukumu **ya Mungu iliyo ya haki**, ili mhesabiwe kuwa **mwaustahili ufalme wa Mungu**, ambao kwa ajili yake mnateswa." (2 The. 1:4-5; Angalia pia mistari ya 3-12).

Mpaka kufikia hapo naweza kukumbusha, kuwa shahidi wa imani (martys)] ni shahidi, kwa sababu atashuhudia dhidi ya[285] watesi wake mbele za Mungu![286]

Kwa kweli, Mungu anaweza kuadhibu watesaji wa Kanisa lake hapa duniani na kwa wakati huu. Kwa mfano, Ufunuo wa Yohana huelezea anguko la Kahaba wa Babeli hapa duniani. Hatuhitaji kujaza kitabu na mifano ya hukumu ya Mungu kwa watesaji.[287]

44. Kwa nini Wasio na Mungu Hufanikiwa sana?

Hoja: Agano la Kale mara kwa mara huuliza kwa nini wasio na Mungu hufanikiwa (hususani Zaburi 73:1-28; Yer. 112:1-4; Zab. 1-15; Ayubu 21:6-16; Mhu. 8:10-14) Swali hili lenye hamasa linahitaji majibu kamili ya kibiblia.

Yeremia 12:1-4 ni mfano bora. Kwanza nabii anauliza kwa unyeyekevu, 'Wewe u mwenye haki, Ee BWANA, nitetapo nawe, lakini nitasema nawe katika habari ya haki. Mbona njia ya wabaya inastawi? Mbona wote watendao hila wanakaa salama?" Anauliza, ingawa anajua jibu vizuri kabisa na analihusisha katika mistari inayofuata. Mambo matatu ni muhimu:

1. *Anafahamu kuwa mafanikio ya wenye dhambi huja si kwa bahati, bali kutoka kwa Mungu*: "Umewapanda, naam, wametia mizizi, wanakua, naam, wanazaa matunda; katika vinywa vyao u karibu, bali katika mioyo yao, u mbali" (Yeremia 12:2). Ukweli kuwa, "Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga" (Yakobo 1:17) ni kweli kwa wasioamini, kwa kuwa Mungu "huwaangazia jua lake waovu na wema,

285 Katika Yakobo 5:3, kutu, taswira ya kudumu kwa muda mfupi kwa vitu vya duniani, itashuhudia dhidi ya kutokuamini.

286 Norbert Brox. Zeuge und Maertyrer. *op. cit.*, pp. 27-29, analipata wazo hili hususani katika Mathayo na Marko.

287 Kama vile; Samuel Clarke. A Looking-Glass for Persecutors. W. Miller: London, 1674.

huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki" (Mathayo 5:45; angalia pia Matendo ya Mitume 14:17).

2. *Yeremia anadai kuwa wasio na Mungu wanapokea hukumu wanayostahili*, "uwakokote kama kondoo waendao kuchinjwa, ukawaweke tayari kwa siku ya kuchinjwa" (Yeremia 12:3).

3. *Mbali na mafanikio ya sasa ya baadhi ya wasioamini, anaikiri kanuni ya laana na baraka inayotangazwa katika Kumbukumbu la Torati 27-32*. "**Hata lini nchi itaomboleza, na mimea ya kila shamba kukauka, kwa ajili ya waovu wakaao ndani yake? Wanyama wanaangamizwa na ndega pia; kwa sababu walisema, Hatauona mwisho wetu**" (Yeremia 12:4).

Zaburi ya Asafu (Zaburi 73) inatoa mfano mwingine ambapo Asafu karibu ajikwae (mstari wa 2), kwa sababu aliyaonea wivu mafanikio ya waovu (mstari wa 3). Watafanikiwaje namna hiyo, japo wanamdhihaki Mungu na wanapata utajiri kwa dhuluma (mistari ya 4-15)? Mtunga zaburi anajitahidi kuelewa (msitari wa 16. Angalia pia mistari ya 20, 21), "Hata nilipoingia katika patakatifu pa Mungu, nikautafakari mwisho wao" (mstari wa 17), hukumu (mistari ya 16-20+27) upweke na hofu, (mstari wa 19). Asafu hajaelewa kila kitu, lakini anahitimisha katika mistari ya 23 na 24, "Walakini mimi ni pamoja nawe daima, umenishika mkono wa kuume. Utaniongoza kwa shauri lako, na baadaye utanikaribisha kwa utukufu." Mafanikio ya utu wa nje ni kitu cha pili, kwa kuwa anahitimisha, "Wala duniani sina cha kupendeza ila wewe" (Mstari wa 25).

Kitabu cha Mhubiri kinashughulikia tatizo lile lile na kinakuja kwenye hitimisho lile lile: "**Tusikilize hitimisho la mambo yote: Mhofu Mungu, na utunze amri zake; kwa kuwa ndilo jukumu zima la mwanadamu. Kwa maana Mungu ataleta kila kazi hukumuni, na kila jambo la siri, liwe zuri, au liwe ovu**" (Mhubiri 12:13-14).

G. Kinyume cha Dini ya Mafanikio

45. Ukristo si Dini ya Mafanikio (Warumi 5:1-5)

Hoja: Ukristo si dini ya mafanikio ambayo haijali matatizo na isiyojua chochote kuhusu magumu.

Nini thamani ya imani isiyo na majibu ya magumu ya maisha? Ni kwa kiwango gani ahadi zake zina thamani, kama haziwezi kuthibitishwa katika maisha ya kila siku? Ukristo wa kibiblia haujaribu kuturidhisha na ahadi hewa zilizoahirishwa mpaka baada ya maisha haya, kama ilivyo ajabu kwa" "tumaini la utukufu wa Mungu" (Warumi 5:2). Ahadi za kibiblia za amani na tumaini zinafanya kazi hapa na sasa, mbali na giza lote la maisha. Tukichukua makadirio ya Wakristo 165,000 wanaokufa kwa ajili ya imani yao kila mwaka, kama Ukristo haukuwa na majibu kwa madhila na giza la dunia hii, tungepaswa kuhitimisha kuwa huku ni kushindwa.

Katika kitabu cha Warumi, baada ya kujadili hitaji la kiulimwengu la mwanadamu kwa ajili ya wokovu katika Kristo, Paulo anatambulisha matatizo, mateso na magumu ya maisha (Warumi 5:1-5), kwa kuwa Ukristo siyo tu dini ya utajiri.[288] "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu. Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini, na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi" (Warumi 5:1-5).

Kumbuka kwamba Paulo hajitukuzi tu katika utukufu wa Mungu, kana kwamba mwamini anaweza tu kuishi maisha ya namna hii, lakini pia kufurahia katika dhiki (mstari wa 3), na anapata maana ya kiroho katika matatizo na mateso ya wale waliokwisha hesabiwa haki. Matatizo yanatupa uzoefu (mstari wa 4), unaokuza tumaini letu la jumla na halali katika utukufu wa Mungu pamoja na na tumaini binafsi, linalopatikana kupitia saburi na uthabiti, tumaini lisilomfadhaisha mwamini kinyume na dhiki! Amani na Mungu haimwinui mwamini juu ya matatizo yote! Kinyume chake, Mkristo huyachukulia yote kwa umuhimu mkubwa kama anavyoyapitia na akiwa na kipawa cha amani na haki. Adolf Schlatter, anaandika kuhusu kifungu hiki, akisema, "Mbali na tumaini lijalo, Paulo anawasilisha hali ya sasa ya Kanisa, mbinyo, manyanyaso, majaribu kutoka katika dunia inayotuzunguka. Tuna amani na Mungu, lakini mgogoro na vita dhidi ya dunia ... utukufu usiotosheleza, kama unajumuisha tu tumaini..."[289]

Saburi na uthabiti ulioelezwa na Paulo si mafaniko ya mwanadamu! Paulo angeweza kufurahi tu katika dhiki ambazo huzalisha tumaini, "kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi" (Warumi 5:5). Schlater alilielezea hili kwa maneno yafuatayo, "Mwamini huyakabili magumu ya nafasi yake, kwa sababu Mungu humpa pendo lake."[290]

46. Theolojia ya Injili ya Utajiri na Afya ni ya Kuhojiwa

Hoja: Warumi 5:1-5 inakanusha mafundisho yanayotoa ahadi ya utajiri, afya nzuri na furaha tu kwa Wakristo 'wazuri' pasipo matatizo au mateso yoyote.

Ni kweli Mungu anaweza kutoa vitu hivi vyote kwa wale wanaotii amri zake, vitu ambavyo vinatumika kwa manufaa ya Viumbe. Hakika, hukusudia kufanya hivyo na atafanya (Mat. 6:25-34), lakini kwa kulingana na mpango wake. Hata hivyo, hii "Injili ya Utajiri na Afya" ya Kikristo, humnyima mwamini vipengele

288 Kama Martin alivyoonesha daima. Tazama: Walther von Loewenich. Luthers theologia crucis. Luther-Verlag: Bielefeld, 1982[6].

289 Adolf Schlatter. Gottes Gerechtigkeit: Ein Kommentar zum Roemerbrief. Calwer Verlag: Stuttgart, 1975[5]. p. 178.

290 *Ibid.*, p. 179.

mbalimbali vya jinsi ya kutumia imani yake na matokeo ya imani: Uvumilivu, tumaini na uthabiti; mambo matatu ambayo Bwana wetu Yesu Kristo pia alipaswa kujifunza, yeye aliye kielelezo chetu (Ebr. 5:8). Ni kwa kiasi gani tunapaswa kujifunza hayo!

Alfred Yeo katika Mkusanyiko wa Maandiko ya Muungano wa Kiinjili juu ya mateso katika Asia anaanza kwa maneno, "Ni uongo[291] kuulinganisha Ukristo na afya, utajiri, mafanikio na safari laini".

47. Kujikana na Kuteseka

Hoja: Kujikana[292] na kuteseka ni masuala muhimu katika maadili ya Kikristo na vipengele muhimu vya imani ya kweli na matendo.

Mara nyingi mateso huambatana na upungufu wa mahitaji ya msingi ya binadamu kama chakula, mavazi na nyumba (kwa mfano, 1 Kor. 4:11; 2 Kor. 6:5; 11:23-27; Flp. 4:12).

"Petro, aliyekataa kuamini kuwa Kristo ni lazima ateseke, alikuwa wa kwanza katika Kanisa "kuudhiwa tangu mwanzoni kabisa kwa mateso ya Kristo"[293] Petro ni mfano wa Mkristo anayekimbia machungu, kwanza anakana mateso ya Bwana wake ("Hasha, Bwana, hayo hayatakupata" Mat. 16:22; Marko 8:32), kisha anajaribu kuyazuia kwa nguvu (Yohana 18:10), hatimaye anajiinua mwenyewe na anashindwa (angalia juu). Kumbuka, kuwa Petro huyu huyu, aliyekataa wazo la mateso kwa nguvu sana, baadaye chini ya Mfalme Nero alikuja kuwa moja kati ya mashahidi jasiri kabisa na mashahidi wa imani wa Yesu Kristo!

48. Pigana Vita Vizuri vya Imani

Hoja: "Yesu aliwaahidi wafuasi wake mgogoro na mateso, si amani."[294]

Hivyo Paulo anamsihi mtumishi mwenzake Timotheo, "Piga vita vile vizuri vya imani" (1 Tim. 6:12) na analisihi kanisa linaloteswa "**Simameni imara katika roho moja, kwa nia moja mkipambana pamoja kwa ajili ya imani ya Injili; na msitishwe chochote na washitaki wenu, ambao kwao ni ishara ya upotovu, bali kwenu ni ishara ya wokovu, na ya Mungu. Maana kwa ajili yenu mmepewa kwa niaba ya Kristo, sio tu kumwamini yeye, bali pia kuteseka kwa ajili yake; mkiwa na mgogoro uleule mliouona ndani yangu, na sasa nasikia u ndani yangu**" (Flp. 1:27-30).

---

291 Alfred Yeo. "Introduction". pp. 1-2 in: Bong Rin Ro (Ed.). Christian Suffering in Asia. Evangelical Fellowship of Asia: Taichung (Taiwan), 1989. p. 1.

292 Werner Elert. Das christliche Ethos: Grundlinien der lutherischen Ethik. Furche-Verlag: Hamburg, 1961². pp. 338-345, Chapter "Der Verzicht".

293 Christof Sauer. Mission und Martyrium. *op. cit.*, p. 59, citing Dietrich Bonhoeffer.

294 *Ibid.*, p. 98.

49. Mauaji ya Mashahidi wa Imani ni Upinzani dhidi ya Mashambulizi ya Roho

Hoja: Mateso na kifo cha mashahidi wa imani ni upinzani mkuu wa imani dhidi ya dai la ulimwengu la kuwa na nguvu si tu juu ya mwili bali pia juu ya roho na dhamiri ya mwanadamu. Hofu ya Mungu, yeye ambaye anaweza kuangamiza mwili na roho katika Jehanamu, hushinda hofu ya wale wanaoweza kuangamiza mwili tu (Mat. 10:28).[295] Pindi tupatapo mateso, Yesu hutusihi "Nanyi kwa subira yenu mtaziponya nafsi zenu" (Luka 21:19).

50. Tamasha Mbele ya Ulimwengu Usioonekana

Hoja: "Shahidi wa imani hutazamwa na kusubiriwa katika ulimwengu usioonekana."[296]

Paulo aliwachukulia mitume kuwa ni "tamasha kwa ulimwengu; kwa malaika na wanadamu" (1 Kor. 4:9). Kutoka makao ya mbinguni, roho za mashahidi wa imani hutazama mustakabali wa Kanisa, hususani Kanisa linaloteswa (Ufu. 6:9-11), "wingu kubwa la mashahidi" (Ebr. 12:1, angalia uhusiano na mauaji ya mashahidi wa imani katika unabiii wa mashahidi wa imani wa Agano la Kale na mateso ya Yesu katika Ebr. 11:39-12:2).[297] Tukiwa tunafahamu juu ya watazamaji wa mbinguni na kukumbuka kuuawa kwao inatukumbusha kuutazama mfano wa Yesu (Ebr. 12:1-12).

51. Maono ya Makao ya Mbinguni

Hoja: Mateso yana thamani ndogo sana yakilinganishwa na utukufu wa milele na tuzo ya Mungu huko mbinguni. Mungu atazawadia mateso ya muda mrefu, uaminifu na imani [298] na tumaini, mambo ambayo ni maadili ya shahidi. Tuzo hizi zinaoana na kanuni ya Biblia kuwa wanyenyekevu watakwezwa na Mungu (1 Pet. 5:6; Yakobo 4:10). Kama Yesu alivyopitia ambaye "alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno" (Flp. 2:8-9). Ufunuo 20:4-6 huwasilisha kutukuzwa kwa mashahidi wa imani, wanaotawala na Kristo baada ya vifo vyao,

---

295 Friedrich Graber. Der Glaubensweg des Volkes Gottes: Eine Erklaerung von Hebraeer 11 als Beitrag zum Verstaendnis des Alten Testamentes. Zwingli Verlag: Zuerich, 1943. p. 262.

296 Christof Sauer. Mission und Martyrium. *op. cit.*, p. 112.

297 Tazama F. Kattenbusch. "Der Maertyrertitel". *op. cit.*, p. 114.

298 Neno la Kigriki, 'pistis' laweza kumaanisha 'imani/tegemea' na 'uaminifu/utegemewa'. Tazama tofauti katika 1 Pet. 1:5-9. Linatumika kumaanisha 'imani' katika 2 Thes. 1:3-4; Ufu. 2:19; 14:12; 2 Tim. 3:10; 4:6-7, linatajwa pamoja na 'subira' ('hypomone'). Katika Ufu. 13:10, humaanisha 'Uaminifu', likitajwa pamoja na 'subira'. Tumaini na subira vinaunganishwa katika 1 Thes. 1:3 na Warumi 15:5. Saburi na uvumilivu (Kol. 1:11), na imani na mateso vyote ni vipawa vya Mungu (Flp. 1:29)!

kama jibu lao la mwisho kwa mateso ya Kanisa la Kristo, ambalo Yohana analielezea katika Ufunuo kwa kushangaza sana.[299]

Paulo alikuwa akielewa ukweli wa kazi ya umishenari, ambayo bado inaambatana na mateso, chuki, mateso ya mwili na mahitaji muhimu sana, lakini alielewa kuwa magumu na matatizo ya sasa hayana nguvu yakilinganishwa na utukufu wa milele (Rum. 8:18).[300] Si kwamba mtume alikataa ukweli au umuhimu wa magumu hayo. Badala yake, alikiri umuhimu wake, lakini aliyachukulia kutokuwa na umuhimu yakilinganishwa na utukufu wa milele tulioahidiwa. Uhusiano kati ya magumu ya sasa na tuzo zijazo unaweza kulinganishwa na fedha; mapato yetu binafsi yanaweza kuwa juu, na yenye umuhimu mkubwa kwetu, lakini yakilinganishwa na mabilioni yanayohitajika ya bajeti ya serikali ya Shirikisho, akaunti zetu za benki si chochote. Katika 2 Timotheo 4:6-8, Paulo anakinzanisha kufa kwake kulikokuwa kunakuja (mstari wa 6 "wakati wa kufariki kwangu") na tuzo ya mbinguni (mstari wa 8 "taji ya haki").

Kwa kurudia Biblia huahidi tuzo ya kitajiri ya Mungu kwa waamini wanaopitia mateso (Mat. 19: 27-29). Barua za Yohana kwa makanisa huelekeza ahadi kwa "Yeye ashindaye"[301] (Ufu. 2:7+11+26; 3:5+12+21; 21:7). Waandishi wengi wa Biblia wanawatia moyo waumini wanaoteswa kwa mtazamo wa lengo la mbinguni. Mwandishi wa Waebrania anaandika, "Basi na tutoke tumwendee nje ya kambi, tukichukua shutumu lake. Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao" (Ebr. 13:13-14). Utukufu ujao huko mbinguni na tumaini la tuzo mara zote yamekinzanishwa na mateso ya dunia. Mwelekeo wa Waebrania 12 ni kuwa, tunapaswa kumwiga Yesu, ambaye kwa kudhamiria alibeba mateso kwa ajili ya fidia ya mbinguni iliyokuwa mbele yake (angalia pia 1 Petro 1:11). Petro pia anaandika, "**Lakini furahini, kwa kadri mlivyo washiriki wa mateso ya Kristo; kwamba, wakati utukufu wake utakapofunuliwa, mweze kufurahi tena kwa furaha izidiyo sana**" (1 Petro 4:13). Clemens wa Alexandria wakati fulani alisema kuwa Petro "... akiwa ameshuhudia (yaani aliuawa kama shahidi wa imani) alijipata nafasi sahihi katika utukufu."[302]

---

299 Ulrich Kellermann. "Das Danielbuch und die Maertyrertheologie der Auferstehung". p. 51-75 in: J. W. Van Henten (Ed.). Die Entstehung der juedischen Martyrologie. Studia Post-Biblica 38. E. J. Brill: Leiden, 1989. p. 65. Kellermann barabara anaona uwiano wa Dan. 7 na Ufu. 1: 20 (kr. 65-66); tazama pia Theofried Baumeister. Die Anfaenge der Theologie des Martyriums. *op. cit.*, p 227.

300 Katika waraka unaohusu mashahidi wa imani wa Lyon na Vienne (Eusebius Kirchengeschichte p. 234 [5. Book, Ch. 1, V.6]) mashahidi wa imani wanachorwa kama mifano ya ubatili wa maisha haya ukilinganishwa na utukufu ujao. Tazama pia William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 205-206.

301 Brother Andrew. "How Should Christians Regard Persecution?". p. 13-21 in: Brother Andrew (Ed.). Destined to Suffer? African Christians Face the Future. Open Doors: Orange (CA), 1979.

302 (1.) Klemensbrief 5,4, in "Der Klemensbrief". p. 1-107 in: Joseph A. Fischer (Ed.). Die Apostolischen Vaeter. Koesel: Muenchen, 1981[8] p. 31.

52. Maandiko Hayaweki Mpaka Kuwa Mateso Yatokee Katika 'Siku za Mwisho' tu

Hoja: Somo la mateso halipaswi kuwekewa mpaka wa kujadiliwa katika mambo yahusuyo siku za mwisho tu,[303] au kuangukia kwenye hali mbaya wakati matarajio ya kurudi kwa Kristo yanapofadhaishwa.[304] Maandiko huahidi 'dhiki' na mateso kwa Wakristo wa nyakati zote. Kwa hiyo vizazi vingi viliamini mateso ya wakati wao kuwa dalili ya kurudi kwa Kristo.[305] Badala yake 'Dhiki Kuu'[306] siyo hatua ya pekee ya historia, wala maandiko hayafundishi mafundisho juu ya Unyakuo Kabla ya Dhiki Kuu bila mashaka namna hiyo kwamba tunaweza kutegemea katika kukwepa mateso,[307] kama makanisa mengi ya Ulaya yanayofundisha.[308] Horst Englemann anaandika, "Tunapoyatumia mahubiri ya kinabii ya Yesu (Mathayo 24) kwetu wenyewe na si kwa wakati mwingine wowote wa historia ya wokovu, tunatambua kuwa jambo hili linalingana na mpango wa Mungu. Kadiri Siku za Mwisho zinavyokaribia (zilianza na Ufufuo wa Yesu Kristo: (Matendo ya Mitume 2:16kk; 1 Kor. 10:11b), kadiri upinzani dhidi Kristo unavyoongezeka ndivyo mbinyo kwa Wakristo unavyozidi."[309]

Theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani kipekee ni kiini cha fasili ya maandiko ya kinabii. Ujumbe wa manabii unapewa umuhimu wa kwanza dhidi

---

303 Bila kutarajia, kazi bora kabisa ya Kiinjili ya Kijerumani juu ya somo hili; Werner Stoy. Mut fuer Morgen: Christen vor der Verfolgung. Brunnen Verlag: Giessen, 1980[2], iliyosheheneshwa kwa nguvu sana wazo la Kurudi Mara ya Pili, kwamba, baada ya miaka ishirini, imepitwa na wakati kwa ukweli kuwa Urusi ya Kikomunisti haitawali tena vielelezo bora vya Kiinjili. Tatizo sawa na hilo liko pia kwa; Larry W. Poland. The Coming Persecution. Here's Life Publ.: San Bernardino (CA), 1990, ingawa waraka huu ulichapwa miaka kumi baadaye!

304 Franz Stuhlhofer. 'Das Ende naht!': Die Irrtuemer der Endzeitspezialisten. Brunnen: Giessen, 1992; Dwight Wilson. Armageddon Now!: The Premillenarian Respone to Russia and Israel Since 1977. Institute for Christian Economics: Tyler (TX), 1991[2] (repr. from Baker Book House: Grand Rapids (MI), 1977[1]), pp. 86-122; Gary DeMar. Last Days Madness: The Folly of Trying to Predict When Christ Will Return. Wolgemuth & Hyatt: Brentwood (TN), 1991; Gary North. Rapture Fever: Why Dispensationalism is Paralyzed. Institute for Christian Economics: Tyler (TX), 1993; Otto Friedrich. The End of the World: A History. New York, 1982 (Mafunzo ya kihistoria ya kina juu ya somo hili). Kwa mifano zaidi ya vielelezo na utabiri mbalimbali wa Kiinjili, tazama; Timothy P. Weber. Living in the Shadows of the Second Coming: American Premillennialism 1875-1982. pp. 177-203; Joel A. Carpenter. The Renewal of American Fundamentalism. Diss.: Baltimore (MD), 1984. pp. 93-133.

305 Mfano bora wa Mprotestanti ni Martin Luther. Ethelbert Stauffer. "Maertyrertheologie und Taeuferbewegung". *op. cit.*, p. 574 anadhihirisha hali ilivyo miongoni mwa Waanabaptisti.

306 Kwa mtazamo mbadala, tazama David Chilton. Die grosse Truebsal. Reformatorischer Verlag Beese: Hamburg, 1996 kikiwa na kiambatisho cha Thomas Schirrmacher. "Gruende fuer die Fruehdatierung der Offenbarung vor 70 n. Chr." pp. 129-154: Engl. Kwa asili bila kiambatisho: David Chilton. The Great Tribulation. Dominion Press: Fort Worth, Texas, 1987.

307 Paul A. Marshall. Their Blood Cries out. *op. cit.*, pp. 157-160 ("In Search of Armageddon") pamoja na mifano.

308 *Ibid.*, pp. 159-160. Wengi wa wale waandikao juu ya Kurudi Mara ya Pili, kama vile Dave Hunt, anatumia jambo hili kama usuli wa maonyo yao wenyewe, lakini wanafanya kwa uchache kuwasaidia Wakristo wanaoteswa.

309 Horst Engelmann. Gemeindestruktur und Verfolgung. *op. cit.*, p. 10.

ya masuala ya wendo (utaratibu wa kupanga miaka na matukio kwa mfuatano) au utimilifu wa moja kwa moja. Ahadi kuwa mashahidi wa imani walioteswa hapa duniani watatawala na Kristo haitapotea, kwa mfano, katika mdahalo juu ya Milenia.

Horst Englemann[310] anafupisha sababu tano muhimu zinazowazuia Wakrsito wa Kimagharibi kutojifunza somo la mateso:

1. Kijiografia: "Mambo hayo hayatatokea hapa."

2. Kihistoria: "Mambo ya aina hiyo hayatatokea tena."

3. Kitheolojia: "Hatutapita katika Dhiki Kuu, kwa sababu tutanyakuliwa kabla haijaanza."

4. Kiroho: "Kuna Wakristo wengi hapa, kwa hiyo tutaepushwa na aina hii ya mateso."

5. Kihalisia: "Tuna mambo mengi ya kutilia mashaka."

H. Serikali na Mateso

53. Kuna Aina Nyingi za Mateso

Hoja: Agano Jipya hutaja aina nyingi za mateso kama vitangulizi vya mauaji ya mashahidi wa imani.[311]

Ya kwanza ni dhihaka (Ebr. 11:36) na dharau (Marko 9:12) ambayo pia Yesu anaieleza kwenye Mahubiri Mlimani "Heri ninyi watakapowashutumu na **kuwatesa** na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu" (Mat. 5:11). Wayahudi walimzuia Yesu kuzungumza, wakasambaza tuhuma juu yake, wakamkamata kinyume cha sheria, wakamtesa, na wakamuua kikatili - kwa mujibu wa mpango wa Mungu wa kumwinua yeye (Matendo 2:22-36; Flp. 2:6-11).[312] Alijeruhiwa kwa ajili yetu (Isaya 53:4-10).

Paulo anataja hatari za kila siku na wanyama wakali kama njia za mateso katika 1 Wakorintho 15:30-32. Katika 2 Wakorintho 6:4-5, anaandika, "bali katika kila neno tujipatie sifa njema, kama watumishi wa Mungu; katika saburi nyingi, katika dhiki, katika misiba, katika shida; katika mapigo, katika vifungo, katika fitina, katika aibu, katika kukesha, katika kufunga..."

Waraka kwa Waebrania hutaja aina mbalimbali za mateso waliyoteseka Wakristo wa karne ya kwanza: "Lakini zikumbukeni siku za kwanza, ambazo,

---

310 *Ibid.*, p. 29, imejikita katika Patrick Johnstone. "Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution". *op. cit.*, pp. 3-7 na Dan Kyanda. "The Attitude of the Prepared Christian". pp. 97-104 katika: Brother Andrew (Ed.). Destined to Suffer? African Christians Face the Future. Open Doors: Orange (CA), 1979.

311 John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. *op. cit.*, pp. 1-12.

312 Tokunboh Adeyemo. "Persecution: A Permanent Feature of the Church". pp. 23-36 in: Brother Andrew (Ed.). Destined to Suffer? *op. cit.*, p. 25.

mlipokwisha kutiwa nuru, mlistahimili mashindano makubwa ya maumivu; pindi mlipotwezwa kwa mashutumu na dhiki, na pindi mliposhirikiana na wale waliotendewa hayo. Maana mliwaonea huruma wale waliokuwa katika vifungo, tena mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu, mkijua kwamba nafsini mwenu mna mali iliyo njema zaidi, idumuyo." (Ebr. 10:32-34, angalia pia mistari inayofuata). Manabii wa Agano la Kale walivumilia zaidi mateso mbalimbali: "Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa. Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora; wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani; walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji, waliteswa, wakitendwa mabaya (watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao), walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi" (Ebr. 11:35-38). Utofauti wa njia hauna kikomo. Aina nyingine siyo kali sana, kama vile dharau, kutengwa, kuzingirwa na magenge, kudunishwa kwa Wakristo, na alama zao na mafundisho yao hadharani ulimwenguni. Aina hizi, ingawa zinahusiana na mauaji ya mashahidi wa imani kwa asili, zinapaswa kutofautishwa kutoka njia ambazo ni kali zaidi kama kujeruhiwa kimwili, mateso na kuuawa, hususani pale serikali inapohusishwa.

54. Istilahi ya Shahidi wa Imani Haipaswi Kutumiwa Vibaya Kisiasa

Hoja: Tunapaswa kuepuka kuitumia vibaya istilahi ya shahidi wa imani kisiasa na kuifasili katika maneno ya kitauwa, kwa kuwa mateso yanaweza kusababishwa na maadili ya Kikristo au na nafasi ya kisiasa.

Theolojia ya Kikatoliki ya hivi karibuni, hususani Theolojia ya Ukombozi, wakati mwingine hutumia istilahi shahidi wa imani kwa mashahidi wa kisiasa (yaani, watu waliouawa kutokana na siasa zao - political martyrs, *nyongeza ya mtafsiri*) na wapiganaji wenye kupinga jambo (resistance fighter).[313] Kwa upande mwingine, ni sawa kabisa kwamba mauaji ya mashahidi wa imani yana mwelekeo halisi wa kisiasa, zaidi ya yote pindi ukosoaji wa watawala uanzishapo mateso. Baadhi ya manabii wa Agano la Kale kama vile Danieli au Yohana Mbatizaji walikuwa na jumbe za wazi za kisiasa; na hata Yesu alirejea dhahiri kwenye siasa, ingawa somo lenyewe si lenye umuhimu wa kwanza. Athanasius, Thomas Becket, Dietrich Bonhoefer, Martin Luther King – kwa kutaja wachache – wanaelezwa kwa uwazi kama mashahidi wa imani.

Kwa sababu serikali ya Mpinga Kristo ('mnyama') iliowatesa "watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu Kristo" (Ufu. 14:12),

313 Concilium 19 (1983) 3, hususani. Karl Rahner. "Dimensionen des Martyriums: Plaedoyer fuer die Erweiterung eines klassischen Begriffes". Concilium 19 (1983) 3: 174-176; Leonardo Boff. "Martyrium". Concilium 19 (1983) 3: 176-181; Johannes Baptist Metz, Edward Schillebeeckx. "Martyrium heute". Concilium 19 (1983) 3: 167-168; James Cone. "Martin Luther King". Concilium 19 (1983) 3: 230-236; makala zote zinapatikana kwa Kiingereza katika Johannes Baptist Metz, Edward Schillebeeckx (Ed.). Martyrdom Today. T. & T. Clark: Edinburgh & Seabury Press: New York, 1983.

itashindwa. Wale wanaomtii Joka watateseka mateso yale yale (Ufu. 12:17). Serikali inapotosha jukumu lake pale inapowaadhibu wale wanaotii amri za Mungu na kumwamini Kristo (Tazama mtiririko! Serikali inapaswa kuadhibu uovu. Wakristo, Watunzao Sheria ya Mungu, hawapaswi kuingia katika mgogoro na serikali!)

Hata hivyo, hatupaswi kuipanua istilahi hii ili kufanya upingaji wa kisiasa kuwa kigezo, ili kwamba yule anayeitwa shahidi wa imani hahitaji kuwa Mkristo kabisa, na mawazo yake ya kisiasa hayapaswi kukubaliana na Maandiko.[314]

55. Kinyume na Ukamilifu wa Mamlaka

Hoja: Kanisa la Kristo huteseka, kwa sababu mahubiri yake ya ufalme mkamilifu na hukumu huufanya ubora wa mamlaka ya mwanadamu uhojiwe.[315]

Kwa kawaida, Serikali huchukulia mashaka haya kama changamoto kwa mamlaka yake. Kadiri serikali inavyokuwa ya kimabavu na kitaifa, ndivyo inavyozidi kuogopa wazo la imani katika Kristo ambalo hupita mipaka ya dunia hii na utamaduni wake na mipaka ya kitaifa.[316] Kitabu cha Danieli kinatia mwanga juu ya jambo hili, hususani katika ndoto ya Nebukadneza (Dan. 2), na katika maono yake Danieli mwenyewe (Dan. 7-12). Mambo mengi ya msingi katika somo la ndoto hizi yanahusu mateso ya waamini.[317] Wafasili wengi wa Kiinjili hukubali kuwa picha aliyoiona mfalme katika Sura ya 2 na Wanyama Wanne katika Sura ya 7 zinatoa picha ya mfuatano wa tawala za dunia za Babeli (dhahabu, simba) Umedi na Uajemi (fedha, dubu), Uyunani au Ugiriki (shaba, chui) na Rumi (chuma, mnyama wa kutisha). Kila ndoto inarudia ahadi kuwa Mungu atauimarisha Utawala wake wa milele mahali pa utawala wa Rumi - ahadi iliyotimizwa katika Kanisa la Agano la Jipya. Kitabu chote kinapenyezwa na wazo kuwa, mbali na nguvu za falme za kipindi cha siku za Danieli, ufalme wa Mungu utadumu milele.

Ndoto ya Nebukadneza huishia pale ambapo jiwe kutoka mbinguni linateketeza sanamu (Dan. 2:34-35), linakua na kuwa 'mlima mkubwa', na "likaijaza dunia yote" (Dan. 2:35; angalia mstari wa 45). Danieli anasema, "Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali atavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele" (Dan. 2:44). Enzi ya Tawala za Kibinadamu iliisha na Warumi. Chini ya utawala wa Kirumi, Ufalme wa Mungu ungeanza na kukua kuijaza dunia yote. Hakuna taifa moja, si Wayahudi au mataifa mengine yoyote ya ufalme wowote, lingeweza kuutambua Ufalme huu (kama wegi wanavyofasili kifungu "wala watu

314 Gerhard Besier. "Bekenntnis - Widerstand - Martyrium als historisch-theologische Kategorie". *op. cit.*, pp. 139-143, anataja watetezi kadhaa wa wazo hili kinzani.

315 Imejikita kwa Georg Vicedom. Das Geheimnis des Leidens der Kirche. *op. cit.*, p. 24.

316 Patrick Johnstone. "Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution". *op. cit.*, pp. 3-4 huuona Utaifa (Nationalism) kama mpinzani mbaya kabisa wa Mwili wa Kristo.

317 *Ibid.*, p. 10.

wengine hawataachiwa enzi yake"). Kweli Yesu alianzisha Ufalme wake katika kipindi cha utawala wa Kirumi kwa wanafunzi wake na kanisa lake. Mara kwa mara alikuwa amekwishatabiri katika mifano mingi kuwa ufalme huu utakuja kuijaza dunia (kwa mfano, Mat. 13:24-35).

Kwa njia ile ile, Danieli anaziona tawala za dunia zinazowakilishwa na mnyama (Dan. 7:9-14 inaelezea maono; 7:17-27 ni fasili). Mungu ndiye mwenye kuamua mwisho wa tawala hizi kutoka katika kiti chake cha enzi mbinguni (Dan. 7:9-12), na mwisho wa falme hizi huja, wakati Mwana wa Adamu (Dan. 7:13, jina la baadaye liliobuniwa kwa Yesu) anaingia mbinguni (Kupaa kwa Yesu) na anapokea "mamlaka na utukufu , na ufalme ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa" (Dan. 7:14) kutoka kwa Mungu. "Na ufalme na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii." (Dan. 7:27).

Nabii Danieli anatangaza kuwa Mungu ataziondoa tawala za watu wa mataifa na utawala wa Kiyahudi wa Mungu, na badala yake ataweka utawala ulioanzishwa na Masihi, Serikali ambayo haitamilikiwa na taifa lolote, mtawala yeyote wa kibinadamu au kikundi chochote cha dini. Akizungumzia dola ya Rumi, utawala wa chuma katika ndoto ya Nebukadneza, Danieli anaandika, "Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele" (Dan. 2:44). Katika maono mengine, Masihi katika wakati huu anapokea "mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa" (Dan. 7:14). Tamko kuwa 'Ufalme' huu wa milele unapaswa kutumikiwa na kutiiwa na mataifa yote, "watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu" (Dan. 7:27) yawezekana halirejei kwa Wayahudi bali kwa Kanisa (kama ilivyo katika Efe. 2:6; Luka12:32; angalia pia Efe. 1:20-21). Hivyo, Kanisa la Agano Jipya lile ambalo halitegemeani na taifa moja; kwa kulitegemea linavuka na kushinda mipaka yote ya kitaifa. Ukweli kwamba watu wa Mungu hawahusiani na serikali ya taifa yoyote, bali wanahusiana na mataifa yote, ni kero kubwa kwa falme na serikali za wanadamu.

56. Raia Waaminifu

Hoja: Wakristo ni raia waaminifu, wanaotafuta ustawi wa serikali yao, nchi na watu wao, lakini wakati wowote Serikali inapojaribu kuwalazimisha kutomheshimu Mungu, ni lazima wamtii Mungu kuliko mwanadamu.[318]

---

318 Tazama; Edwin L. Frizen, Wade T. Coggins (Ed.). Christ and Caesar in Christian Missions. William Carey Library: Pasadena (CA), 1979, hususani. Earle E. Cairns. "Under Three Flags". pp. 3-45; David H, Adeney. "The Preparation of Missionaries to Cope with Political Change". pp. 49-53; T. Grady Mangham. "Aftermath to Persecution". pp. 61-73; Abram J. Wiebe. "Special Problems with Islamic Governments": pp. 95-102.

Baba wa Kanisa Tatian alielezea wazo hii kwa maneno yafuatayo; 'Mfalme ananiamuru mimi kulipa kodi: Ninajiandaa kulipa. Mungu ananiamuru kutumika na kutii: Nakubaliana na huduma hiyo. Ni lazima nimheshimu mwanadamu katika mtindo wa kibinadamu, lakini ni Mungu pekee anayepaswa kuhofiwa.... Ni pale tu ninapoamriwa kumkana yeye, sitatii; kisha ni bora nife...'[319] Si jambo la kushangaza, matamko mawili ya mara kwa mara katika kumbukumbu za uchunguzi wa kina katika kipindi cha Kanisa la Kwanza ni, kwa kuwa mtuhumiwa ni Mkristo, na kuwa anasisitiza utii wake kwa Serikali na kwa sheria zake.[320] Waraka wa Diogenetes, ulioandikwa katika kipindi hiki, unanukuu, "Wanawapenda wote - lakini wanateswa na wote. Hatujui chochote juu yao - na bado tunawahukumu..."[321] na 'Ingawa wanafanya mema, wanaadhibiwa kama watenda maovu."[322]

Mpango wa Mungu kwetu ni "amani wala si mabaya" (Yeremia 29:11), lakini mipango hii inafanana kwa ukaribu sana na amri, 'Kautakieni amani mji ule" (Yeremia 29:11). Changamoto hii inaihusu serikali ya kipagani, kwa kuwa inatoa taswira ya ndoto za utumwa wa Israeli huko Babeli.

Tabia ya Mkristo kwa serikali ina pande mbili, kwa kuwa "Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu" (Matendo ya Mitume 5:29; 4:19). Kwa upande mmoja, tunaweza tukarejea kwenye sheria ya Mungu ili kupinga madai ya serikali ya kuwa yenye uwezo wote. Kwa upande mwingine, tunaitii serikali yetu, hata kama inazidisha mamlaka yake. Tunapinga pale tu ambapo mamlaka zinajaribu kutulazimisha kutotiii sheria ya Mungu, au pale ambapo ni lazima tutetee maisha yetu na haki za wengine. Kwa sababu Mungu anaamuru hilo, Mkristo ni lazima alipe kodi, hata kama ni kubwa kupita kiasi, lakini bado tunaweza kunyooshea kidole kiwango kikubwa cha kuwa ni cha uonevu. Kwa njia ile ile tunapaswa kupinga dhidi ya ongezeko la usajili wa kitakwimu unaofanywa na serikali yetu (Usajili huo mara nyingi umefanywa dhidi ya Wakristo katika nyakati za mateso!) japo bado unajibu maswali ambayo yamefanywa wakati wa sensa. Kwa kweli ni vigumu kutangulia kukisia ni kwa kiwango gani tunaweza kushirikiana na serikali wakati wa mateso na lini tunapaswa kuanza kupinga. Migogoro ya kusikitisha kati ya makanisa yaliyosajiliwa na yale yasiyosajiliwa katika Muungano wa Kisovieti au katika China inatokana na tatizo hilo. Kama Yesu alivyosema wakati wa mara yake ya kwanza kuzungumzia mateso, "basi iweni na busara kama nyoka , na **msio na madhara kama njiwa**" (Mat. 10:16). Kwa vile kauli hizi zinatumika kwenye mahusiano yetu na Serikali, mtu binafsi anapaswa

---

319 Tatian, Rede an die Griechen 4,1, in: Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 85+87 (Nr. 34).

320 Gerhard Besier. "Bekenntnis - Widerstand - Martyrium als historisch-theologische Kategorie". *op. cit.*, pp. 129-130.

321 Schrift an Diognet 5,11, in. Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 99 (Nr. 39).

322 Schrift an Diognet 5,16, in. Theofried Baumeister. Genese und Entfaltung der altkirchlichen Theologie des Martyriums. *op. cit.*, pp. 101 (Nr. 39).

kuamua mwenyewe, kwa muda gani anaweza kushirikiana na lini anapaswa kupinga.[323]

Wakristo ambao bado wanafurahia uhuru wa kidini wanapaswa kuzingatia kwa mara nyingine jambo hili kwa namna ya mtu mmoja mmoja, kwamba juhudi zetu kwa Wakristo wanaoteseka, zinasaidia au la! Wakristo wengi wamekwishaachiwa kutoka magerezani kwa sababu ya juhudi hizo, lakini wakati mwingine upenyezi kutoka nje unaweza kuleta madhara. Hakuna ufumbuzi bayana; tunapaswa utumia muda wetu kukusanya taarifa kutoka vyanzo vya kienyeji, kujifunza mazingira kwa undani na kufikiri kwa umakini kabla ya kuanza kutenda. Hili si tatizo jipya; Mababa wa Kanisa na Wanamatengenezo walishughulikia jambo hili pia. Calvin wakati fulani aliyaandikia makanisa yaliyokuwa katika mateso kuwa alikuwa hajawahi kuyaandika hapo awali kwa hofu ya kuifanya hali yao kuwa mbaya zaidi.[324]

57. Kuomba kwa ajili ya Maisha ya Amani

Hoja: Maombi ni silaha muhimu: "Basi, kabla ya mambo yote nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu" (1 Tim. 2:1-3). Maombi siyo radhi ya kitauwa kukwepa wajibu, ili tuweze kuishi maisha ya utulivu na kitauwa! Kinyume chake, katika maombi, kanisa hujipenyeza kihalisia katika siasa, kwa sababu tunataka kumtumikia Mungu katika amani ya kweli.

1 Timotheo 2:1-5 hupendekeza kuwa, Paulo anazungumzia kipekee maombi wakati wa ibada. Maombi kwa wenye mamlaka na kwa ajili ya amani siku zote yamekuwa na nafasi katika liturujia. Kwa kawaida, maombi hayo hayapaswi kuongoza katika kuwatukuza viongozi wetu, bali yanapaswa kupinga maonevu na ukosefu wa umoja katika jamii, ambayo kipekee hujumuisha mateso ya Wakristo na vipingamizi vya kutekeleza imani yetu. Kwa mfano, Kanisa la Agano Jipya katika Yerusalemu, liliomba kuwa Petro afunguliwe kutoka gerezani. "Nao waliposikia, wakampazia Mungu sauti zao kwa moyo mmoja, wakisema, Mola, wewe ndiwe Mungu, ndiye uliyefanya mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo; nawe ulinena kwa Roho Mtakatifu kwa kinywa cha babaetu Daudi, mtumishi wako, Mbona mataifa wamefanya ghasia, na makabila wametafakari ubatili? Wafalme wa dunia wamejipanga, na wakuu wamefanya shauri pamoja juu ya Bwana na juu ya Kristo wake (Zaburi 2:1-2). Maana ni kweli, Herode na Pontio Pilato pamoja na Mataifa na watu wa Israeli, walikusanyika katika mji huu juu ya Mtumishi wako mtakatifu Yesu, uliyemtia mafuta ili wafanye yote ambayo mkono wako na mashauri yako yamekusudia tangu zamani yatokee. Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote, ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu. Hata walipokwisha kumwomba Mungu,

323 Werner Stoy. Mut for Morgen, *op. cit.*, p.58.

324 Waraka wa Calvin wa 10 Juni, 1552, katika: Otto Michaelis. Protestantisches Maertyrerbuch. *op. cit.*, p. 218.

mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri" (Matendo ya Mitume 4:24-31). Kanisa halipaswi kutegemea ama serikali au upande wa upingaji, bali kwa Yule Anayetawala watawala wote.

58. Kupinga Serikali

Hoja: Tunahitaji tathmini mpya ya wale wanaovunja sheria za Serikali kwa ajili ya Injili.[325]

Petro na mitume walihubiri Injili kinyume na marufuku ya Serikali (Matendo ya Mitume 4:19-20; 5:29) na mara kwa mara matokeo yalikuwa kukamatwa na kuadhibiwa (Matendo ya Mitume 12:1-2; 12:3). Katika kukabiliana na upinzani wa Kirumi, Wakristo walirejea kwa Kristo kama Bwana (Kigriki 'kyrios') na mfalme (katika kupinga amri ya mfalme. Matendo ya Mitume 17:6-7; 4:12). Makuhani wa Israeli pia walipinga wafalme waliohujumu mamlaka ya kichungaji: "Wakamzuia Uzia mfalme" (2 Nya. 26:18). Mayaya wa Misri hawakutii amri ya Farao ya kuwaangamiza watoto wa Waisraeli, na hata walidanganya ili kuwalinda watoto (Kutoka 1:15-20). Mama yake Musa Yokebedi alimwokoa mtoto wake kinyume cha sheria kwa hila, na akamdanganya binti Farao (Kutoka 2: 3-9). Rahabu aliwaokoa wapelelezi wa Kiyahudi kwa kudanganya, wakati alipopinga amri ya mfalme (Yosh. 2). Badala ya kuhukumu ukosefu wao wa uaminifu, Agano Jipya linawawasilisha kama vielelezo vya imani vinavyopaswa kuigwa! (Ebr. 11:31; Yakobo 2:25). Mara kwa mara Danieli na rafiki zake wanakataa kutii amri za watawala (Dan. 3:12+17, 6:13-14). Kumbuka kuwa mifano hii haiuhusu tu uabudu sanamu au ukanaji wa Injili, bali uvunjaji wa Sheria ya Mungu (uuaji, n.k.). Hata hivyo, upingaji huu unachukulia kuwa Serikali imetutaka kuiasi Sheria ya Mungu.

Hususani pale watawala wawili wanapopingana, tunagundua kuwa amali zinazolindwa na Sheria zina vipaumbele tofauti (Theolojia ya Kikatoliki ya Rumi huzungumzia 'mgogoro wa wajibu'). Mfano wa wazi ni jibu la Petro kwa mamlaka za Kiyahudi zilizowazuia mitume kuhubiri injili: "Petro na Yohana wakawajibu wakawaambia, Kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe" (Matendo ya mitume 4:19). Amri ya Mungu ya kuhubiri Injili ilipingana na amri ya Mungu ya kutii mamlaka. Danieli na rafiki zake walisimama katika mkanganyiko kama huo, lakini walikataa pale ambapo Nebukadneza alipowaamuru kuabudu sanamu yake (Dan. 3). Kwa namna ile ile, Danieli alikataa kutii amri ya Dario kwa kugeuza desturi ya maombi yake, ingawa

---

325 Bruder Andrew. "Wir brauchen eine neue Sicht der leidenden Kirche". Geoeffnete Tueren. Rundbrief Geoeffnete Tueren (Frutigen, Schweiz). Febr 1980. pp. 1-3, here p. 1-2 and W. Elwyn Davies. "When is it Legitimate to Disobey Government Edicts?". pp. 87-94 in: Edwin L. Frizen, Wade T. Coggins (Ed.). Christ and Caesar in Christian Missions. William Carey Library: Pasadena (CA), 1979. Kwa mjadala wa kina zaidi, tazama: Brother Andrew. The Ethics of Smuggling. Coverdale House Publ.: London, 1974; kwa uhakiki kinzani dhidi ya mtazamo huu, tazama: Greg L. Bahnsen. "Brother Andrew, The Ethics of Smuggling ...". The Journal of Christian Reconstruction 2 (1975/1976) 2 (Winter): Symposium on Biblical Law. pp. 164-169.

kutotii kwake kulimfikisha kwenye tundu la Simba. Amri ya kupiga marufuku kuabudu sanamu ina uzito mkubwa kuliko wajibu wetu kwa serikali.

Biblia huelezea migogoro mingi ya kimaadili. Katika Marko 2:23-23 (= Mat. 12:1-7; Luka 6:1-5). Yesu anahalalisha kitendo cha wanafunzi wake cha kupura ngano siku ya Sabato kwa kumrejea Daudi, aliyeruhusu kula Mikate ya Wonyesho, kwa sababu alikuwa na njaa (1 Sam. 21:4-7). Amri ya kulinda uhai na kutahiri zilikuwa muhimu zaidi kuliko sheria ya Sabato. Katika Mathayo 12:5, Yesu anauliza, "Wala hamkusoma katika torati, kwamba siku ya Sabato makuhani hekaluni huinajisi Sabato wasipate hatia?" Anataja sheria kadhaa za Biblia zilizo muhimu zaidi kuliko sheria ya Sabato, (huduma ya makuhani, kuokoa maisha, kuwanywesha mifugo, n.k.). Yesu anaonesha wazi kuwa makuhani huinajisi Sabato, lakini hubaki "bila hatia" kwa kufanya hivyo (Mat. 12:5).

Theolojia ya Matengenezo[326] kwa ujumla ilichukulia kuwa, wakati tunapotakiwa kufanya uamuzi kuhusu sheria za Mungu, mara zote kuna uamuzi sahihi; kutii sheria kuu, ambayo hufanya udhuru kwa ile ndogo,[327]ambayo inaonekana kufaa, kwa kuwa sheria za Kibiblia zinaona kuwa mtu binafsi anaweza kufanya ipasavyo na vyema katika mazingira yoyote, na kwa kuwa Maandiko yanatupa mifano kadhaa ya migogoro ya kimaadili (angalia chini). Sifahamu tukio lolote katika Biblia ambapo mtu hakuwa na chaguo isipokuwa kutenda dhambi, na angeweza tu kuamua kati ya uovu mdogo na ule mkubwa zaidi. Ikiwa mtu alitiwa hatiani kwa kudanganya ili kuokoa maisha, Biblia isingeweza baadaye kumfanya awe kielelezo cha kuigwa katika imani!

Theolojia ya Kilutheri, ambayo inachepuka kutoka katika msimamo wa Luther mwenyewe, huchukulia kuwa mtu siku zote ni wa kulaumiwa pale anapovunja Sheria ya Mungu, ingawa amri kuu inapaswa kuwa kigezo cha uamuzi huo. Kwa mfano, Walter Kuenneth huchukulia uuaji wa mtu katili unakubaliwa katika hali fulani kubwa, lakini anaamini kuwa muuaji bado anahitaji msamaha wa dhambi.[328] Hans-Joseph Wilting amesisitiza nguzo za msimamo wa Kilutheri kutoka katika wazo kuwa Mkristo, kama mwanadamu, bado ni mwenye dhambi, hivyo hawezi kamwe kutenda pasipo kutenda

---

326 E. g. John M. Frame. The Doctrine of the Knowledge of God: A Theology of Lordship. Presbyterian & Reformed: Phillipsburg (NJ), 1987. p. 137-139 "Hierarchies of Norms".

327 Baadhi ya wanatheolojia wasio wa Matengenezo wanashiriki katika mtazamo huu, kwa mfano; Norman L. Geisler. "Graded Absolutism". pp. 131-137 katika: David K. Clark, Robert V. Rakestraw. Readings in Christian Ethics. Vol. 1: Theory and Method. Baker Books: Grand Rapids, 1994; Norman L. Geisler. Christian Ethics. Baker: Grand Rapids, 1989. pp. 116-122 n. d.

328 Walter Kuenneth. Der Christ als Staatsbuerger. TVG. R. Brockhaus: Wuppertal, 1984. p. 96. Uchambuzi bora kabisa na wa kina juu ya mtazamo huu waweza kupatikana katika; Helmut Thielicke. Theologische Ethik. Vol. 2: Entfaltung, Part 1: Mensch und Welt. J. C. B. Mohr: Tuebingen, 1959². pp. 56-327.

dhambi.[329] Luther mwenyewe, katika kupinga wanatheolojia wa Kikatoliki wa siku zake, alichukulia uongo ulio muhimu kuwa si dhambi.[330]

Wazo kuwa mwanadamu ni lazima asubiri ufunuo maalumu kutoka kwa Mungu au ni lazima atende dhambi katika mgongano wa kimaadili, haliungwi mkono na Maandiko, bali liliimarishwa kupitia mifumo ya kitheolojia ambayo hairuhusu hitimisho jingine lolote linalowapinga wenyewe. Biblia haitupi ushahidi kuwa mtu anaweza kuwa katika hali ambayo kabisa haiwezi kufanya mapenzi ya Mungu, bali ni muhimu afanye dhambi. Najua hakuna jaribio kuhalalisha wazo hili kwa kurejea mifano halisi ya Kibiblia. Je, ilikuwa ni dhambi hasa, hata kosa dogo, kwa Petro kukataa kutii mamlaka waliomkataza kumtii Mungu kwa kuhubiri Injili? Je, alitenda dhambi kuliamini Agizo Kuu kuwa na umuhimu kuliko utii kwa mamlaka?

Migongano hiyo ya kimaadili ni ya kawaida zaidi kuliko tunavyofikiri; ni sehemu ya maisha ya kila siku. Kila mwanadamu hutathmini maadili yanayogongana kila siku. Uwepo wa taasisi nne halali za kiagano (familia, Serikali, Kanisa na Uchumi) huongoza kwenye umuhimu huo. Tangu ninapoamka asubuhi, ni lazima niamue namna ya kutimiza wajibu wangu kama mume, baba, mchungaji, mwajiri na raia, na hivyo ni lazima nitathmini daima mahitaji ya kila wajibu. Ni mara chache kutimiza wajibu wote kwa mara moja, lakini wajibu wote huo bado ni maagizo ya Mungu kwangu. Katika hali ya kawaida, tunao muda wa kutosha kukidhi matakwa ya wajibu wetu mbalimbali, na matokeo ya maamuzi yetu yana uzito kidogo. Siyo mpaka hali ya kushitusha inapoinuka, kama vile vitisho vya maisha, ndipo tunakuwa tunaumia kujua mchakato huu.

Kazi na mapumziko kwa pamoja ni amri za Mungu. Mungu alitoa mfumo wa siku sita za kufanya kazi na moja kwa mapumziko, lakini bado ni juu yangu kuamua ni wakati gani ninafanya kazi kwa malipo na ni wakati gani nifanyapo bila malipo, ni wakati gani nipumzike na wakati gani nilale, na ni muda kiasi gani natumia kupumzika na kufanya kazi. Maamuzi hayo si kwamba daima hayaonekani au ni rahisi. Kila wakati – mteja huamua ni bidhaa gani anunue, na hujali ni kiasi gani cha fedha anahitaji kwa ajili ya mahitaji mengine ya kifedha, analinganisha machaguo yake kwa mujibu wa mfumo wake wa maadili, na mara anajikuta yuko katika mgogoro wa wajibu. Wenye hali nzuri wana migogoro michache ya namna hiyo kuliko wale wanaopungukiwa utajiri na yule ambaye ni lazima aamue ni mahitaji gani muhimu ambayo ni lazima ayaepuke. Maamuzi ya kununua chakula kwa ajili ya watoto badala ya yeye wenyewe, kwa urahisi ni ufumbuzi wa mgongano wa kimaadili.

---

329 Tazama; Martin Honecker. Einfuehrung in die Theologische Ethik. Walter de Gruyter: Berlin, 1990. p. 238 und Hans-Josef Wilting. Der Kompromiss als theologisches und als ethisches Problem. Patmos: Duesseldorf: 1975. pp. 11-46 on Helmut Thielicke und pp. 47-64 on Wolfgang Trillhaas. Kwa kuwa Wilting anajadili tu wanatheolojia wa kisasa wa Kilutheri, mawazo mengine juu migogoro ya kimaadili haizingatiwi.

330 Axel Denecke. Wahrhaftigkeit: Eine evangelische Kasuistik. Vandenhoeck & Ruprecht, Goettingen, 1971. pp. 251-253 and William Walker Rockwell. Die Doppelehe des Landgrafen Philipp von Hessen. N. G. Elwert'sche Verlagsbuchhandlung: Marburg, 1904. pp. 178-180.

59. Mateso ya Wakristo Yanaweza Kukua kuwa Mauaji ya Kimbari

Hoja: Mateso ya Wakristo Yanaweza Kukua na kuwa Mauaji ya Kimbari.

Mauaji ya Waarmenia[331]na Waasiria (Waashuru)[332] huko Uturuki ni mfano mmojawapo. Katika nyakati za hivi karibuni, serikali ya Kiislamu ya Sudani[333] imekuwa ikayatisha makabila ambayo kwa sehemu ni Wakristo na sehemu nyingine ni ya waabudu mababu.

Uangamizwaji wa Wakristo Waarmenia unaofanywa na Waislamu wa Kituruki na Kikurdi mwanzoni mwa Karne ya Ishirini ilikuwa ni moja ya mauaji ya halaiki katika historia ya sasa hadi Awamu ya Tatu (Third Reich) ilipojaribu kuwaangamiza Wayahudi. Uturuki ilianza kuwachinja Waarmenia katika Karne ya Kumi na Tisa, lakini wimbi kubwa la mauaji, ambalo pia lilijumuisha makundi mengine ya Kikristo, lilikuwepo kabla Vita ya Kwanza ya Dunia. Kiasi cha Waarmenia milioni mbili waliuawa na Waturuki kati ya 1877 na 1939. Ikikanushwa na Serikali ya Uturuki, habari hii imepuuzwa hapa Ujerumani, ambayo ndiyo iliyolifunza jeshi la Uturuki, ikitoa maafisa wa Kijerumani, na kushiriki chini kwa chini katika oparesheni hii. Katika makusanyo yake bora ya kumbukumbu juu ya somo hili, ambamo kwayo anawasilisha orodha ya kina yenye ushahidi, anaelezea chanzo na matokeo ya suala hili na anachunguza ushiriki wa Ujerumani; Wolfgang Gust, Mtoa habari wa *Spiegel*, anahakikisha kuwa mauaji ya kikatili ya taifa la zamani kabisa la Kikristo duniani (Ubadilishaji wa dini wa familia inayotawala katika mwaka 301 BK.) yaliyofanywa na Serikali ya Kiislamu hayatasahuliwa kamwe. Kitabu hiki ni chenye umuhimu unaohusiana nasi leo, siyo tu kama rejea ya vita ya Armenia na Aserbardschan kwa ajili ya Caucasian Berg-Karabach, bali pia katika rejea ya usafishaji wa daima wa makundi ya kikabila unaofanywa na serikali za Kiislamu dhidi ya watu walio Wakristo (kwa mfano kusini mwa Sudani).

60. Mateso ya Wakristo Mara Nyingi yamekuwa Sehemu ya Mauaji ya Halaiki

Hoja: Mateso ya Wakristo Mara Nyingi Yamekuwa Sehemu ya Mauaji ya Halaiki.

Ujamaa wa Kitaifa na Ukomunisti ni mifano mizuri. Vyote hivi vilipinga imani ya Kikristo kwa nguvu na kushambulia dini nyingine na utaifa mbalimbali

---

331 Wolfgang Gust. Der Voelkermord an den Armeniern: Die Tragoedie des aeltesten Christenvolkes der Welt. Carl Hanser Verlag: Muenchen, 1993; tazama pia mkusanyiko wa kumbukumbu wa: Tessa Hofmann, Gerayer Koutcharian (Ed.). Voelkermord, Vertreibung, Exil, Menschenrechtsarbeit fuer die Armenier 1979-1987. Gesellschaft fuer bedrohte Voelker: Goettingen, 1987 na mapitio yangu ya Querschnitte 2 (1989) 4 (Oct-Dec): 8; na Caroline Cox, John Eibner. Ethnische Saeuberung und Krieg in Nagorni Karabach. Christian Solidarity International: Binz (CH), 1993[1]; 1995[2]. pp. 20-31.

332 Gabriele Yonan. Ein vergessener Holocaust: Die Vernichtung der christlichen Assyrer in der Tuerkei. Pogrom Taschenbuecher 1018. Gesellschaft fuer bedrohte Voelker: Goettingen, 1989.

333 Tazama; Cal R. Bombay. Let my People Go! The true Story of Present-Day Persecution and Slavery. Multnomah Publ.: sisters (OR), 1998.

pia.Tuna makadirio ya uhakika ya wastani wa mamilioni ya wahanga wa Ujamaa na Kitaifa,[334] lakini wahanga wa Ukomunisti hawakufanyiwa uhakiki mzuri. Kuna makadirio mbalimbali ya kutegemewa juu ya takwimu hizi,[335] mengi kutokana na vyanzo vya kidunia. Tathmini hii kimsingi, hushughulika tu kipekee na kanda na nyakati maalum. Takwimu ya kina ingepaswa kwanza kuelezea ni serikali zipi na mavuguvugu yapi yanayopaswa kufasiliwa kama ya Kikomunisti. Makala bora ya Jean-Pierre Dujardin katika toleo la 1978 la gazeti la Paris *Figaro* linatupatia muhtasari mzuri wa hali ya utafiti na maandishi yaliyopo.[336] Kwa mujibu wa Dujardin, idadi ya wahanga katika Muungano wa Urusi ilikuwa zaidi ya 70,000,000. Watu 24,000,000 walikufa wakati wa Kitisho cha Stalini, na watu 7,800,000 wakati wa maangamizi ya watu wa Ukraine. Kadiri ya watu 500,000 waliuawa chini ya manyanyaso ya Kambi za Nchi za Mashariki na serikali za Baltic. Hesabu ya wahanga wa Jamhuri ya Watu wa China imekadiriwa kufikia 63,000,000 (mwaka 1978), lakini hesabu ya wahanga wa Kisovieti haiwezi kuwa chini zaidi. Makadirio mengine yako juu mara mbili zaidi, lakini nimechagua kutaja hesabu za chini tu. Tukichukua wahanga wa serikali ndogo na zenye maeneo madogo, kama vile Cambodia[337] (2,500,000), tunapaswa kuongeza mamilioni kadhaa. Kazi nyingine ya Kifaransa ijulikanayo kama "Kitabu Cheusi cha Ukomunisti" (Black Book of Communism) cha mwaka 1997,[338] ambacho kimekuwa kigezo cha rejea, kinakadiria takwimu kamili ya wahanga wa Ukomunisti kufikia kiasi cha milioni 95.[339]

61. Mateso ya Wakristo chini ya Ujamaa wa Kitaifa

Hoja: Mateso ya Wakristo chini ya Ujamaa wa Kitaifa[340] yanaonesha kuwa mateso hayo pia yanawezekana katika nchi za

---

334 Mkusanyiko wa kina ulio bora zaidi waweza kupatikana katika Wolfgang Benz (Ed.). Dimension des Voelkermords: Die Zahl der juedischen Opfer des Nationalsozialismus. Quellen und Darstellungen zur Zeitgeschichte 33. R. Oldenbourg: Muenchen, 1991.

335 Kwa ajili ya ufupisho mzuri wa historia ya mateso ya Wakristo katika Kambi ya Mashariki ya awali, tazama: Rudolf Freudenberger et. al. "Christenverfolgungen". *op. cit.*, pp. 51-62.

336 Jean-Pierre Dujardin. "N'oublions jamais ...". Figaro Nr. 7/78 vom 18. Nov., 1978 (Tafsiri ya Kijerumani inapatikana kutoka kwa Hilfsaktion Maertyrerkirche/Voice of Martyrs).

337 Haijumuishi wale ambao walikufa baada ya mwaka 1978. Makadirio ya hivi karibuni kabisa ("Der rote Schrecken". Focus 48/1997: 168-170) yanafikia katika idadi ifuatayo: China mil. 65, USSR: mil. 20, nchi nyingine za Kikomunisti: mil. 9,44.

338 Stéphane Courtois et. al. (Ed.). The Black Book of Communism. Harvard University Press: Cambridge (MA) & London, 1999; Stéphane Courtois et. al. (Ed.). Das Schwarzbuch des Kommunismus: Unterdrueckung, Verbrechen und Terror. Piper: Muenchen, 1998[5] (French original 1997); See the review and summary in Eckhard Jesse. "Das Schwarzbuch des Kommunismus". Mut Nr. 374 (Oct 1998): 10-25.

339 Stéphane Courtois et. al. (Ed.). Das Schwarzbuch des Kommunismus, *op. cit.*, p. 16.

340 Rudolf Freudenberger et. al. "Christenverfolgungen". *op. cit.*, pp 48-51; Walter Adolph (Ed.). Im Schatten des Galgens: Zum Gedaechtnis der Blutzeugen in der nationalsozialistischen Kirchenverfolgung. Morus Verlag: Berlin, 1953 (mashahidi wa imani wa Kikatoliki tu); Gerhard Besier, Gerhard Ringshausen (Ed.). Bekenntnis, Widerstand, Martyrium: Von Barmen 1934 bis Ploetzensee 1944. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1986. pp. 11-165;. Juu ya mashahidi wa

Magharibi. Miongoni mwa mamilioni ya wahanga wa Ujamaa wa Kitaifa walikuwa 4,000 wengi wakiwa viongozi wa Kikatoliki. Wachungaji elfu tatu wa Bekennende Kirche (Kanisa Linalokiri) walifungwa gerezani.[341]

Nimechagua kazi za msingi kati ya mafuriko makubwa ya machapisho yaliyopo, ili kuelezea matatizo yaliyohusika katika mjadala. Kitabu cha Georg May cha kumbukumbu juu ya upinzani wa Kikatoliki dhidi ya Ujamaa wa Kitaifa na jaribio la Manazi kulifuta Kanisa Katoliki la Rumi[342] kinawaaacha wasomaji na msukumo wenye kukanganya. Kwa upande chanya, kumbuka kwamba:

Kwa msingi wa vyanzo mbalimbali asilia, May anawasilisha mtazamo wa Kinazi juu ya Kanisa Katoliki, hatua zilizochukuliwa dhidi ya Kanisa na hata kiwango cha kupinga cha Kanisa Katoliki, kitu kilichosababisha mauaji yasiyohesabika ya mashahidi wa imani, na hasa miongoni mwa makuhani. Kanisa Katoliki lilikuwa na mashahidi wa imani wengi waliouawa kuliko Waprotestanti.

May anaeleza imani binafsi ya Hittler na mtazamo wake juu ya Ukristo, ambao unaonesha kuwa Ujamaa wa Kitaifa wenyewe ulikuwa ni dini, na siyo wazimu wa kisiasa.

May anaonesha kuwa Makanisa ya Kiserikali ya Kiprotestanti hudiriki kudanganya historia kwa kuadhimisha vifo vya mashahidi wa imani na wapinzani wachache wa Kiprotestanti, hali inayotoa picha kuwa upinzani wa kidini ulikuwa wa Kiprotestanti, na kwamba upinzani wa Kiprotestanti ulikuwa umesambaa pote. Kipekee, Uliberali, ambao ni Ukristo kinzani umejaribu kuboresha heshima yake katika jambo hili.

Kazi ya May ina mtazamo hasi pia, kwa kuwa anatumia kitabu chake kuthibitisha ukuu wa Ukatoliki dhidi ya Uprotestanti.

Ametelekeza kitendo cha Kanisa Katoliki kuungana na Hittler, na anatoa picha kuwa Kanisa zima liliwapinga Manazi kuliko ya kuwa na ushiriki katika mafanikio ya chama. Ili kufanya hivyo, May anajitahidi kuonesha kuwa Hittler, anayejulikana kuwa aliliacha Kanisa Katoliki, kamwe hakuwahi kuwa Mkatoliki.

---

imani wa Kiprotestanti, tazama; Margarete Schneider (Ed.). Paul Schneider - Der Prediger von Buchenwald. Haenssler: Neuhausen, 1981[1]; 1996[4]; Rudolf Wentorf. Der Fall des Pfarrers Paul Schneider. Neukirchener Verlag: Neukirchen, 1989; Georges Casalis. "Theologie unter dem Zeichen des Martyriums: Dietrich Bonhoeffer". Concilium 19 (1983) 3: 236-240 = "Theology Under the Sign of Martyrdom: Dietrich Bonhoeffer". pp. 80-84 katika: Johannes Baptist Metz, Edward Schillebeeckx (Ed.). Martyrdom Today. *op. cit.*, Georg Huntemann. Der andere Bonhoeffer. R. Brockhaus: Wuppertal, 1989; Christoph Strohm. Theologische Ethik im Kampf gegen den Nationalsozialismus: Der Weg Dietrich Bonhoeffers mit den Juristen Hans von Dohnanyi und Gerhard Leibholz in den Widerstand. Heidelberger Untersuchungen zu Widerstand, Judenverfolgung und Kirchenkampf im Dritten Reich 1. Chr. Kaiser: Muenchen, 1989; tazama pia Hans-Joachim Ramm. Stets einem Hoeheren verantwortlich: Christliche Grundueberzeugungen im innermilitaerischen Widerstand gegen Hitler. Haenssler: Neuhausen, 1996.

341 Rudolf Freudenberger et. al. "Christenverfolgungen". *op. cit.*, p. 49.

342 Georg May. Kirchenkampf- oder Katholikenverfolgung: Ein Beitrag zu dem gegenseitigen Verhaeltnis von Nationalsozialismus und christlichen Bekenntnissen. Christiana-Verlag: Stein am Rhein, 1991.

Pia anashindwa kuelezea kwa nini Hittler hakutengwa (Kanisa la Kiprotestanti lilikuwa lisilojali pia katika jambo hili).

Ukosoaji wa nguvu wa May dhidi ya Kanisa la Kiprotestanti umeshindwa kutofautisha kati ya kambi mbalimbali, kama vile Wakristo wa jina na waamini wanaotenda sawa na ushawishi wa imani zao. Kwa vile lawama zake hakuna mahala znapojishughulisha na mafundisho ya msingi ya Kiprotestanti, bali ni kwa ajili ya ukosefu wa upinzani, mjadala wake hauwapi Waprotestanti nafasi, na hivyo unazima hata majadiliano binafsi na baadhi ya watu ambao pengine wangeweza kuchukulia kwa umakini maonyo ya May.

Kwa Waprotestanti wanaoamini Biblia, kitabu hicho ni mfano mzuri wa tabia ya wanatheolojia wanasili* wa Kikatoliki kuelekea malengo ya Matengenezo ya Kanisa, kwa kuwa May hajaribu kutofautisha kati ya uhalalishaji wa Kibiblia wa Matengenezo ya kanisa na Uprotestanti wa utamaduni wa kiliberali wa sasa. Huu ni udhaifu mkubwa wa kitabu: Kushindwa kote kwa Kanisa la Kiprotestanti chini ya Ujamaa wa Kitaifa kunatupiwa lawama kuwa kunatokana na mafundisho ya Kiprotestanti, wakati kushindwa kwa kanisa Katoliki kunahalalishwa na ukanaji kuwa watu hao walikuwa ni Wakatoliki wazuri na watendaji. Manazi maarufu wa Kiprotestanti wananukuriwa kana kwamba walikuwa Waprotestanti halisi, lakini Manazi maarufu wa Kikatoliki wanaoeshwa tu kama Wakristo wa majina. Katika hali hii, May anaigiza kuwa Wakatoliki wote wazuri alimpinga Hittler, wakati Waprotestanti wengi walimuuunga mkono. Inasikitisha kwamba, dhamira hii ya hoja ya utetezi imekifanya kitabu kuwa chenye mawazo ya kibinafsi mno. Ama sivyo kingeweza kuwa kazi bora na ufahamu wake wa kitaalamu ungeweza kuwafaidisha sana Waprotestanti.

I. Huruma ya Kivitendo

62. Wakati Mmoja Anapoteseka ...

Hoja: "Mauaji ya Mashahidi wa imani huliita Kanisa la Kristo kuimarisha umoja wake."[343]

Agano la Jipya huuchukulia umoja huu kama kipengele muhimu cha Sheria ya Kristo ya Upendo, na siyo chaguo kwa ajili ya kundi moja la waamini wahusika. "**Wakumbukeni hao walio kifungoni, kana kwamba mmefungwa pamoja nao; na hao wanaosumbuka kwa dhiki, kana kwamba ni ninyi wenyewe pia mkiwa katika mwili**" (Ebr. 13:3). Mkristo kamwe hateseki peke yake, bali daima kama sehemu ya Mwili wa Kristo, "Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho pia" (1 Kor. 12:26). Hivyo Paulo anamwagiza Timotheo "**Kwa hiyo vumilia magumu, kama askari zuri wa Yesu Kristo**" (2 Tim. 2:3). Anawandikia Wafilipi, "Lakini mlifanya vema, mliposhiriki nami katika dhiki yangu" (Flp. 4:14). Anateseka kwa ajili ya Waefeso na anayachukulia dhiki zake kuwa utukufu wao (Efe. 3:13).

---

343 Peter Beyerhaus. Die Bedeutung des Martyriums fuer den Aufbau des Leibes Christi. *op. cit.*, p. 140.

Hatupaswi kuruhusu hali yetu tulivu itupofushe kushindwa kuona matatizo ya Wakristo wengine. Kwa vile hii kwa kawaida inahitaji mfumo mzuri wa mawasiliano, jumuia za kimishenari, taasisi za haki za binadamu, muungano wa kimataifa wa makanisa, mahusiano binafsi na waumini kutoka nchi zingine na mifumo ya kimataifa kama vile Shirikisho la Kiinjili Ulimwenguni ni muhimu kabisa.

"Kanisa linalotelekeza mashahidi wake wa imani, kamwe haliwezi kuwaombea, kamwe halichukui nafasi zao au kuwajali, linaharibu si tu ushirika wa kiroho wa Mwili wa Kristo; bali pia linamsaliti Kristo, Kichwa cha Mwili, ambaye huteseka na washiriki wake."[344] Akizungumzia wafuasi wake na watumishi wanaoteseka, Yesu alisema, "Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika; nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia" (Mat. 25:34-36+40; angalia pia mistari ya 32-40; na 41-45).

Maombi ni njia ya kwanza kushiriki mizigo ya wengine. "Maombi ya kanisa husaidia kuokoa kutoka katika kifo wale wajumbe wa imani wanaojaribiwa kupita uweza wao, ambao wamepoteza matumaini ya kuishi"[345] (2 Kor. 1:8-11; angalia pia Flp. 1:19). Huruma ya kivitendo ni sehemu inayofuata ya msaada wetu, kama Kitabu cha Waebrania kinavyotukumbusha "Zikumbukeni siku za kwanza, ambazo, mlipokwisha kutiwa nuru, mlistahimili mashindano makubwa ya maumivu; pindi mlipotwezwa kwa mashutumu na dhiki, na pindi mliposhirikiana na wale waliotendewa hayo. Maana mliwaonea huruma wale waliokuwa katika vifungo, tena mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu, mkijua kwamba nafsi mwenu mna mali iliyo njema zaidi, idumuyo" (Ebr. 10:32-34; angalia mistari ya 32-29). Mwandishi wa Waebrania anaangalia pande mbili za mashindano makubwa ya maumivu: Baadhi ya waamini huteseka moja kwa moja, wengine huteseka kwa kushiriki mateso ya wengine. Wengine huteswa, na wengine huwa 'washiriki wenzi' wao. Wengine walipoteza mali zao, na wengine wakateseka pamoja na wafungwa. Mungu anatutarajia kujisikia kibinafsi kuwa waathiriwa wa mateso ya ndugu zetu wa kike na wa kiume katika Kristo!

Amri ya Kibiblia hujumuisha msaada halisi wa wa kijamii na kisiasa.[346] Mithali 24:11 hutuasa, "Uwaokoe wanaochukuliwa ili wauawe; nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe" na Mithali 31:8 huongeza, "Fumbua kinywa kwa ajili yake aliye bubu; uwatetee watu wote walioachwa peke yao".

---

344 *Ibid.*, p. 141.

345 Christof Sauer. Mission und Martyrium, *op. cit.*, p. 108.

346 Christof Sauer. Mission und Martyrium, *op. cit.*, p. 108.

63. Kujipenyeza kwa Mwili wa Kristo kwa Ajili ya Mashahidi Wake wa Imani Hufunua Hali Yake wenyewe

Hoja: "Namna kanisa linavyojishughulisha na mauaji ya mashahidi wa imani, kama tunajisikia sote kuathiriwa, na tunateseka na wanaoteseka (1 Kor. 12:26) au kwamba hatuguswi na dhiki zao, hudhihirisha hali halisi ya ushirika wa Kanisa."[347]

Wakristo waliojaliwa kuishi katika nchi zenye uhuru wa kidini hawapaswi kustarehe katika mafanikio yao, bali wanapaswa kuwasaidia ndugu zao wa kike na wa kiume katika imani. Tunafurahia uhuru wa kidini tu kwa sababu wengine, si tu Wakristo, waliupigania. Mungu atatulipa kazi zetu katika Umilele, lakini mara kwa mara kazi hizo husababisha mafanikio ya kidunia. Kielelezo cha tabia ya Paulo katika kifungo, ambayo "Lakini, ndugu zangu, nataka mjue ya kuwa mambo yote yaliyonipata yametokea zaidi kwa kuieneza injili;" (Flp. 1:12) ina matokeo, kwa kuwa "Na wengi wa hao ndugu walio katika Bwana, hali wakapata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kuthubutu kunena neno la Mungu pasipo hofu" (Flp. 1:14).

64. Ushirika ni Sehemu Halisi ya Kukumbuka Waamini Wanaoteseka

Hoja: Ushirika (Meza ya Bwana, Misa) ni sehemu halisi kuwakumbuka Wakristo wale wanaoteswa kwa ajili ya imani yao, kwa kuwa mitazamo yote ya msingi ya Mwili wa Kristo - ushirika na dhabihu – huhusiana kwa karibu sana na mauaji ya mashahidi wa imani.

Kwa upande mmoja, kama Ushirika unavyoashiria dhabihu ya mwili na damu ya Yesu, inalenga kwenye kuuawa kwake. Kwa upande mwingine, pia tunakumbuka kwamba Wakristo wote ni sehemu ya Mwili wa Kristo: "Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je! Si Ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja" (1 Kor. 10:16-17). Siwezi kuzidisha msisitizo kwenye usihi wa Paulo, "Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho" (1 Kor. 12:26). Hivyo ningeyasihi makanisa kutafuta njia tofauti za kuwakumbuka wanaoteswa wakati wanapoadhimisha Ushirika, ama wakati wa maombi ya dua, katika maneno ya utangulizi au kwa kusoma maandiko yenye kuhusiana na jambo husika.

65. Kuwakumbuka Mashahidi wa Imani katika Ibada

Hoja: Wakati Mwili wa Kristo unapokutana kuabudu, ni lazima uwakumbuke wale ambao wameteseka kwa ajili ya Kristo na wale ambao bado wanaendelea kuteseka.

---

347 Eduard Christen: " Martyrium III/2 *op. cit.*, p. 215.

Kuanzia na Matengenezo ya Kanisa, 'kalenda ya mashahidi wa imani' ya Kiprotestanti imekuwa ikipatikana ili kutusaidia katika maombi yetu ya mashahidi wa imani.[348] Cha kwanza katika kumbukumbu hizi za mashahidi wa imani, ambacho hukumbusha kumbukumbu za kiliturujia za mashahidi waliomwaga damu wa hapo zamani, ni kile cha John Foxes (1516 – 1587) 'Original Actes and Monuments of These Latter and Perilious Days' (Matendo Asilia na Kumbukumbu za Siku Hizi za Baadaye na za Hatari) (mwaka 1563), baadaye kilijulikana kama 'The Book of Martyrs' (Kitabu cha Mashahidi wa Imani) ambacho kilikuwa na ushawishi mkubwa kwa Waanglikana, Wanauzamo (Wapyuritani), Wanamatengenezo (Reformed) katika Bara[349] na kwa *Evangelischen Namenskalendar*,[350] na hata sasa bado kinachapwa.[351] Kuna njia nyingine nzuri za kukumbuka mashahidi wa imani, kam vile sanamu kumi za mashahidi wa imani wa ukiri wote katika Westminister Abbey huko London.[352]

Uabudu wa mashahidi wa imani, ambao uliibuka katika karne za kwanza[353] na unaofanywa katika makanisa ya Ukatoliki wa Rumi na ya Kiothodoksi, ni kitu

348 Tazama hapo juu kwa ajili ya Vitabu vya Mashahidi wa Imani wa madhehebu mbalimbali. Kwa mjadala wa masomo ya theolojia ya mauaji ya mashahidi wa imani wa Kiprotestanti, tazama pia: A. G. Dickens, John M. Tonikn. The Reformation in Historical Thought. Harvard University Press: Cambridge (MA), 1985. pp. 39-57; Diana Wood (Ed.). Martyrs and Martyrologies. Taarifa zilizosomwa katika ... Ecclesiastical History Society. B. Blackwell: Oxford, 1993; James Michael Weiss. "Luther and His Colleagues on the Lives of the Saints". The Harvard Library Bulletin 33 (1983): 174-195; Robert Kolb. For all the Saints. Changing Perceptions of Martyrdom and Sainthood in the Lutheran Reformation. *op. cit.*

349 Tazama Robert Kolb. For all the Saints. *op. cit.*, pp. 5-6; N. Norskov Olson. John Foxe and the Elizabethan Church. University of California Press: Berkeley, 1973; John T. McNeill. "John Foxe: Historiographer, Disciplinarian, Tolerationist". Church History 43 (1974): 216-229; William Haller. The Elect Nation: The Meaning and Relevance of Foxe's Book of Martyrs. Harper: New York, 1963; William Haller. "John Foxe and the Puritan Revolution". pp. 209-224 Katika: Richard Foster Jones (Ed.). The Seventeenth Century: Studies in the History of English Thought and Literature. Stanford: Standorf University Press, 1951.

350 Evangelischer Namenkalender: Gedenktage der Christenheit. Evangelische Buchhilfe: Kassel, 1979 (16 pp.); Robert Lansemann. Die Heiligentage, besonders die Marien-, Apostel-, und Engeltage in der Reformationszeit ... Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1939; tazama pia orodha katika: Evangelisches Tagzeiten Buch. Vandenhoeck & Ruprecht: Goettingen, 1998[4], and Frieder Schulz. "Das Gedaechtnis der Zeugen: Vorgeschichte, Gestaltung und Bedeutung des Evangelischen Namenkalenders". Jahrbuch fuer Liturgik und Hymnologie 19 /1975): 69-104.

351 John Foxe. Book of Martyrs. W. Tegg: London, 1851 [1563]; John Foxe. Fox' Book of Martyrs. ed. by William Bryon Forbush. John C. Winston: Philadelphia (PN), 1926; toleo jipya kabisa: John Foxe. Foxe's Book of Martyrs and How They Found Christ: in Their Own Words. Christian Classic Series 3. World Press Library: Springfield (MO), 1998 [1563]; John Foxe. Foxe's Book of Martyrs. Thomas Nelson Publ.: Nashville (TN), 2000 [1563] (matoleo mengine yalio kamili na yaliyofupishwa yanapatikana).

352 T. Melhuish. "The 20th Century Martys: Westminster Abbey". Church Building Nr. 53, 1998: 18ff and Peter Sandner. "OEkumene der Maertyrer: Neue Statuen an der Westminster Abbey in London". Diakrisis 20 (1999) 3: 149-155 na kwa maelezo ya kina Andrew Chandler (Ed.). The Terrible Alternative: Christian Martyrdom in the Twentieth Century. Cassell: London, New York, 1998.

353 Thomas Schirrmacher. "Die Entstehung der christlichen Heiligenverehrung in der Spaetantike". Bibel und Gemeinde 90 (1990) 2: 166-175. Tayari iko katika Martyrium of Polykarp 22,1 [= p. 18-19 katika: Herbert Musurillo (Ed.). The Acts of Christian Martyrs. Clarendon Press: Oxford, 1972, 'Martyrium des Polykarp' pp. 2-21] ca. 155-157 A. D. inahusisha, kwamba mwili uliochomwa wa

kigeni kwa Uprotestanti, kama pia kisivyo cha Kibiblia, lakini kimesaidia kufanya kumbukumbu za mateso kuwa hai. Kuwasahau watakatifu na mashahidi wa imani kabisa, si njia mbadala! Isipokuwa tunapaswa kuwakumbuka kama vielelezo vya kuigwa vya imani,[354] na kuwafundisha washiriki wa kanisa juu yao, kwa mfano, katika madarasa ya ukiri wa imani (katekisimu).[355] Katika Utetezi wake kwa Ukiri wa Augsburg (Augsburg Confession), Philipp Melanchton anatoa sababu tatu kwa ajili ya kuadhimisha kumbukumbu ya mashahidi wa imani na watakatifu wengine:

1. Tunapaswa kumshukuru Mungu kwa mifano ya neema yake.

2. Mfano wa mashahidi wa imani napaswa kuimarisha imani zetu.

3. Tunapaswa kufuata mfano wa imani yao, upendo wao na uvumilivu.[356]

Kwa sababu hizi, kumbu kumbu ya mashahidi wa imani daima zimekuwa sehemu ya ibada katika makanisa ya Kiprotestanti.[357] John Calvin aliongeza maombi kwa ajili ya walioteswa katika kitabu cake cha Utaratibu wa Ibada wa Geneva.[358]

66. Elimu juu ya Mateso

Hoja: 'Maelekezo juu ya mateso ni moja kati ya mafundisho ya kimsingi ya kidogma (bubuso) katika makanisa machanga'[359]

"Kitabu bora kabisa juu ya mateso ni Biblia".[360] Kama tulivyoona, vifungu vingi vya Agano Jipya viliandikwa kuwaandaa Wakristo kwa ajili ya mateso au

Polycarp uliabudiwa. Baada ya kifo chake, huduma za ibada zilifanywa kwenye kaburi lake. [*Ibid*., pp. 12-13].

354 Martin Scharfe. "Der Heilige in der protestantischen Volksfroemmigkeit". Hessische Blaetter fuer Volkskunde 60 (1969): 93-106.

355 Kwa ajili ya makusanyo ya Wasifu wa mashahidi wa imani wa sasa wa Kiinjili, tazama: Haralan Popoff. Tortured for His Faith: A Epic of Christian Courage and Heroism in Our Day. Zondervan: Grand Rapids (MI), 1970[1]; 1975[2]; Herbert Schlossberg. Called to Suffer, Called to Triumph: 18 True Stories by Persecuted Christians. Multnomah: Portland (OR), 1990.

356 Tazama ufupisho, *Ibid*.,p. 101 to Article 21 "Von der Anrufung der Heiligen" der Apologia der Confessio Augustana,. in: Horst Georg Poehlmann et. al. (Ed.). Unser Glaube: Die Bekenntnisschriften der evangelisch-lutherischen Kirche. Ausgabe fuer die Gemeinde. GB Siebenstern 1289. Guetersloher Verlagshaus: Guetersloh, 1986. pp. 347-357 [Abschnitte 271-280].

357 Robert Kolb. For all the Saints. Changing Perceptions of Martyrdom and Sainthood in the Lutheran Reformation. *op. cit*., pp 148-158.

358 Jean Calvin. Calvin-Studienausgabe. Vol. 2: Gestalt und Ordnung der Kirche. Neukirchener Verlag: Neukirchen-Vluyn, 1997. pp. 137-225 "Genfer Gottesdienstordnung (1542) mit ihren Nachbartexten", here p. 169; Juu ya matazamo wa Calvin kuhusu mauaji ya mashahidi wa imani, tazama pia: Jean Calvin. Calvin-Studienausgabe. Vol. 3: Reformatorische Kontroversen. Neukirchener Verlag: Neukirchen, 1998. pp 267-367 'Gegen die Irrtuemer der Anabaptisten' (1544), here pp. 366-367, and Hans Scholl's introduction,. pp. 267-277, here p. 271.

359 Horst Engelmann. Gemeindestruktur und Verfolgung. *op. cit*., p. 9.

360 Preparing Believers for Suffering and Persecution: A Manual for Christian Workers. Hope: Bulawayo (Zimbabwe), o. J. (ca. 1979). 15 pp. p. 6.

kuwatia moyo chini ya mateso. (Kwa mfano, Paulo,[361] alimfuata Kristo katika mauaji ya mashashidi wa imani, kama walivyofanya waandishi wengi wa Agano Jipya). Tunayo mahitaji makubwa ya machapisho mazuri[362] na makabrasha ya kina ya kufundishia Biblia juu ya somo hili.[363]

Kwa kadri liturujia inavyohusika, kuna njia nyingi za kuwandaa Wakristo kwa ajili ya mateso:[364] kujifunza mistari muafaka kwa moyo, nyimbo, maombi na sehemu za huduma za ibada.[365] Katika nchi nyingi, Wakristo wamejuta kwa uchungu kwa kutoandaliwa vizuri kwa ajili ya mateso.[366]

"Pia tunahitaji 'kichocheo kipya kwa ajili ya nguvu ya maombi'".[367] Tungeweza kutumia maombi ya kanisa la Yerusalemu, yalioongoza kwenye mwujiza wa ukombozi wa Petro,kama kielelezo (Matendo ya mitume 4:23-31, msingi wake ni Zaburi 1:1-2).[368]

67. Tunahitaji Wakiri Imani

Hoja: Kanisa la Yesu Kristo linahitaji watakatifu na mashahidi wa imani majasiri, waume kwa wake waliodhamiria kukiri imani yao hata kwa gharama yoyote - chuki ya jamii, uhasama mkubwa wa Serikali na wa makundi ya kidini, na hata upinzani wa Kanisa lisiloongozwa vema.

Uzoefu wa Kanisa la Ujerumani chini ya Unazi na Ukomunisti unaonesha ulazima huu. "Toka katika uchanga wake, daima Kanisa limekuwa kanisa la kukiri imani yake."[369] Kama Kanisa haliwezi kukiri imani yake, linakuwa lenye kudanganywa kwa urahisi, na hugeuka kuwa mtesi.

---

361 John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. *op. cit.*, pp. 107-118.

362 Patrick Johnstone. "Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution". *op. cit.*, p. 6.

363 Kwa kina: Thomas Schirrmacher. Gottesdienst ist mehr: Plaedoyer fuer eine liturgische Gottesdienstgestaltung. Theologisches Lehr- und Studienmaterial 2. Verlag fuer Kultur und Wissenschaft: Bonn, 1999.

364 Kwa kina: Thomas Schirrmacher. Gottesdienst ist mehr: Plaedoyer fuer eine liturgische Gottesdienstgestaltung. Theologisches Lehr- und Studienmaterial 2. Verlag fuer Kultur und Wissenschaft: Bonn, 1999.

365 Kwa maelezo mazuri kwa ajili ya Katekisimu, bila kutaraji yamepitwa na wakati, tazama: Manfred Fermir. Christen in der Verfolgung. Anregungen: Arbeitshefte fuer den Religionsunterricht ... 3. R. Brockhaus, 1979.

366 Kwa mfano katika Korea, tazama Peter Pattison. Crisis Anaware: A Doctor Examines the Korean Church. OMF Books: Sevenoaks (GB), 1981. pp. 232-239.

367 Bruder Andrew. "Wir brauchen eine neue Sicht der leidenden Kirche". *op. cit.*, pp. 1-3, here p. 2; tazama pia: Bruder Andrew. And God Changed His Mind. Chosen Books: Old Tappan (NJ), 1990; Chosen Books: Grand Rapids (MI), 1999].

368 William Carl Weinreich. Spirit and Martyrdom. *op. cit.*, pp. 32-34.

369 Johannes Wirsching. "Bekenntnisschriften". pp. 487-511 katika: Gerhard Krause, Gerhard Mueller (Ed.). Theologische Realenzyklopaedie. Vol. 5. Walter de Gruyter: Berlin, 1980. p. 487.

68. Ustahimilivu ni Muhimu

Hoja: Uwezo wa kustahimili chini ya magumu – hususani Kanisani na umishenarini – ni moja kati ya alama muhimu sana za uongozi wa kiroho na ni maandalizi ya moja kwa moja kwa ajili ya mateso.[370]

Kwa sababu hofu ya mateso, hususani miongoni mwa viongozi, ina matokeo mabaya kiasi hicho kwa ajili ya Mwili wa Kristo, ustahimilivu ni lazima ushiriki jukumu kubwa zaidi katika mafunzo ya kitheolojia na katika uchaguzi wa watendakazi wa kanisa. Kwa sababu makuzi ya tabia huhitaji mifano ya kuigwa, lengo hili laweza tu kufikiwa kupitia kujihusisha kwa walimu na wanafunzi katika makanisa ya mitaa au katika taasisi halisi. Uvumilivu, ustahimilivu na dhamiri ya kujitoa dhabihu haviwezi kufunzwa darasani au kwa kushiriki katika miradi ya muda mfupi, bali tu chini ya wajibu wa muda mrefu.

69. Muundo wa Kanisa na Mateso

Hoja: Katika kuanzisha makanisa mapya, uongozo unapaswa kujaribu kuimarisha miundo inayoweza kuhimili mbinyo na inayoweza kuendelea kutimiza wajibu wao wa kiroho chini ya mateso.[371]

Makanisa ya nyumbani[372] na makanisa madogo madogo ni muhimu,[373] kwa sababu yanafanya kazi bila uendeshaji kutoka taasisi kubwa.[374] Tunahitaji mafunzo zaidi juu ya somo hili.

70. Tunahitaji Mawazo Yenye Uhalisi

Hoja: Utambuzi wa mateso ya ndugu zetu wa kiume na wa kike katika Kristo unapaswa kuwa sehemu ya maisha ya kila siku ya makanisa yetu. Tunapaswa kuanza kulifanya kuwa jambo muhimu

---

370 Patrick Johnstone. "Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution". *op. cit.*

371 Horst Engelmann. Gemeindestruktur und Verfolgung. *op. cit.* und John S. Pobee. Persecution and Martyrdom in the Theology of Paul. *op. cit.* pp. 107-118 "Persecution and the Church". Kwa Ukatoliki, tazama: Walbert Buehlmann. "Die Kirche als Institution in Situationen der Christenverfolgung". Concilium 19 (1983) 3: 217-220 = "The Church as Institution in the Context of Persecution". pp. 58-62 katika: Johannes Baptist Metz, Edward Schillebeeckx (Ed.). Martyrdom Today. *op. cit.*

372 Met Q. Castillo. The Church in Thy House. Alliance-Publishers: Malina (Philippinen), 1982 (kwa ushirikiano na Ushirika wa Kitheolojia wa Asia [Asia Theological Fellowship]); Thomas S. Gosslin II. The Church without Walls. Hope Publ.: Pasadena, 1984.

373 "Preparing 3rd World Believers for Church Growth under Persecution". *op. cit.*, p. 7 and Preparing Believers for Suffering and Persecution: A Manual for Christian Workers. Hope: Bulawayo (Zimbabwe), n. d. (ca. 1979). 15 pp. p. 9 ("Every Christian home must become a church." Herbert Schlossberg. A Frangrance of Oppression: The Church and Its Persecutors. Crossway Books: Wheaton (IL), 1991. p. 161 huona mashirika ya makanisa ya kimtaa (congregationalists associations) yenye makanisa machahche kuwa ni ya muhimu.

374 Preparing Believers for Suffering and Persecution. *op. cit.*, p. 9.

katika miradi yetu na makundi yote ya kazi, lakini tunahitaji mawazo yenye uhalisi ili kusaidia kulitambua lengo hili.

- Acha nihitimishe kwa mawazo machache kwa ajili ya uongozi wa kanisa. Washiriki wanaweza kuleta mapendekezo chini ya uangalizi wa uongozi.
- Nilipokuwa mtoto, daima nilivutiwa na ukumbi wa ibada wa Kituo cha Kimataifa cha WEC huko Bulstrode jijini London. Sitasahau picha za wamishenari ambao wametoa maisha yao katika Kongo ya Ubeligiji (Zaire) kwa ajili ya imani yao.[375] Kwa nini tusitundike picha hizo mahali popote? Wamishenari waliopigwa risasi hadi kufa na Wahindi wa Ki-Auca walichorwa hata katika stampu za kutumia barua![376]
- Omba kwa ajili ya Wakristo wanaoteswa kila Jumapili, au mara kwa mara wakati wa ibada. Maombi yanaweza kuwa ya jumla, kwa nchi maalumu, au kwa ajili ya mwamini maalumu. Fanya hii iwe sehemu ya utamaduni wako wa ibada.
- Hubiri juu ya jambo hili angalau mara moja kwa mwaka. Pia hubiri juu ya 'Gharama ya Kumfuata Kristo'. Vifungu vizuri vya Maandiko vyaweza kuwa: Luka 21:12-15; Heb. 10:32-39; 1 Pet. 2:13-17; Mat. 5:10-16; 2 Thes. 1:3-12; Gal. 1:23-24; Marko 10:29, 30; 2 Kor. 2:9-10; 2 Kor. 4:7-12; Rum. 8:35-39; Yohana 15:18-21; Matendo ya Mitume 16:13-34.
- Usikwepe maandiko ambayo hutaja mateso au yanayoelezea maisha ya mashahidi wa imani kama vile, Stefano, Paulo, Yeremia. Unapohubiri katika vifungu hivyo ambavyo hujishughulisha na mateso, ingiza jambo hili katika mahubiri.
- Hakikisha kuwa kila kusanyiko la maombi katika kanisa lako au eneo lako huombea angalau hitaji moja halisi la baadhi ya waamini wanaoteswa.
- Je, kuna Wakristo wengine katika eneo lako ambao wanatoka katika nchi ambazo Wakristo wanateswa? Mwombe atoe ushuhuda. Yawezekana mshiriki mmoja wa kanisa anaweza kutoa habari juu ya somo hili baada ya kuitembelea nchi hiyo.
- Shirikiana na bodi ya umisheni au mashirika ya haki za binadamu kuandaa huduma za ibada, mikutano ya kanisa au mikutano ya kikundi kidogo juu ya wanaoteswa.

---

375 Tazama: Idoti und David M. Davies. With God in Congo Forests During the Persecution Under Rebel Occupation as Told by an African Pastor. Worldwide Evangelization Crusade: Bulstrode, Gerrards Cross (GB), 1971.

376 Tazama: Idoti und David M. Davies. With God in Congo Forests During the Persecution Under Rebel Occupation as Told by an African Pastor. Worldwide Evangelization Crusade: Bulstrode, Gerrards Cross (GB), 1971.

- Itumie kwa faida Siku ya Kimataifa ya Maombi kwa Kanisa Linaloteswa (International Day of Prayer for the Persecuted church-IDOP) katika mwezi Novemba kufanya uwasilishaji (mahubiri) juu ya mateso au kualika msemaji mgeni. Jaribu kuitoa wiki ya nyuma au inayofuata kuongeza kwa kina uelewa katika vikundi vya vijana, vikundi vidogo vidogo kanisani au mikutano ya maombi.
- Wape wasiriki wako kanisani jukumu la kulitaarifu kanisa kila mara juu ya mateso. (Tumia majarida ya kimishenari au mtandao, n.k. kukusanya marejeo).
- Mfanye mwamini mmoja awajibike kwa mambo kama vile haki za binadamu, uhuru wa kidini au mateso ya Wakristo. Mtu huyu anapaswa kufanya mawasiliano na makundi yanayofanya kazi kanisani kwa upande mmoja, na vyama vya kimishenari na taasisi za haki za binadamu kwa upande mwingine.
- Lipatie kanisa lako majarida sawia au machapisho kutoka bodi za kimisionari na taasisi za haki za binadamu.
- Andaa matukio ya kiuhamasishaji juu ya somo hili au utunze nafasi kwa ajili yake katika ubao wa matangazo ya kanisa.
- Ulipe kanisa kijarida juu ya jambo hili, ongeza taarifa kwenye barua za kanisa mara kwa mara au uweke kwenye mbao za kanisa za matangazo.
- Waandikie Wakristo wanoteswa na familia zao na makanisa yao. Vyama vya kimishenari na taasisi za haki za binadamu zinaweza kukupa anuani zao.
- Unga mkono maombi kwa Wakristo wanoteswa na andika kwa serikali na balozi mbali mbali.
- Waandikie wanasiasa wako na balozi za nchi zinazohusishwa. Waandikie wanasiasa na balozi katika nchi hizi. Vyama vya kimishenari na taasisi za haki za binadamu zinaweza kukupa anuani na taarifa.
- Wasiliana na mwakilishi wa Wilaya ya uchaguzi au jimbo a uchaguzi au viongozi wengine wanaowajibika kijamii na uwape taarifa juu ya Wakristo wanoteswa.
- Litie moyo kanisa lako kushiriki katika harakati hizi.
- Angalau mara moja kwa mwaka, toa matoleo ya Jumapili kwa kundi linalojihusisha (kanisani kwako, vyama vingi vya kimishenari, taasisi za haki za binadamu).

Kiambatanisho 1: Haki za Binadamu na Imani ya Kikristo

(Imetafsiriwa katika Kiswahili na Emmanuel Buganga)

Imechapwa kwa Kirusi katika jarida la Academy of Science of Russia. POISK: Ezemedel' naja Vsesojuznaja Gazeta [Journal of the Russian Academy of Science=Jarida la Taaluma ya Sayansi ya Kirusi]. Na. 48 (446) 22-28. Novemba 1997. uk. 13; ilichapwa tena katika gazeti la Russian Teacher's Association (Chama cha Walimu cha Urusi): Utschitjelskaja Gazeta (Russiche Lehrerzeitung). Na. 2 (9667). 3.1.1998. S. 21+ Na. 3 (9668) 20.1.1998 uk.. 22. Iliandikwa kwa ajili ya Conferenz Evangelikaler Publizisten (Kongamano la Waandishi wa Habari wa Kiinjili na Watu wa Vyombo vya Habari) la Muungano wa Kiinjili wa Ujerumani.

Binadamu kama Kiumbe na Mfano wa Mungu

Desemba 10, 1948, Muungano wa Kisovieti ulisaini Azimio Kuu la Haki za Binadamu lililopitishwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Azimio linasema kwamba binadamu wote wana utu sawa (Kifungu 1) na kuzuia ubaguzi wote wa ujamii, rangi, jinsi, lugha, dini au ushawishi wa kisiasa (kifungu 2). Kwa sababu watu wote wana haki ya kuishi na kuwa huru (kifungu 3), utumwa (kifungu 4) na mateso (kifungu 5) vinazuiliwa. Wote ni sawa mbele ya sheria na wanaweza kuhukumiwa tu kwa mujibu wa sheria zilizowekwa, baada tu ya kuwa wamesikilizwa katika Mahakama ya sheria (kifungu 7-11). Wote wako huru kuhamia na kuchagua mahali pa makazi yao (kifungu 13) na kuomba ukimbizi katika nchi nyingine (kifungu 14). Kila binadamu yuko huru kuchagua mwenzi, na familia, kama 'kiini asilia na cha msingi katika jamii', ni lazima alindwe na Serikali na jamii (kifungu 16+26). Pia Azimio linataka haki ya umiliki mali binafsi (kifungu 17), haki ya uhuru wa dhamiri na dini, ambao unajumuisha haki ya mtu kubadili imani yake (kifungu 18), haki ya kutoa maoni na kupata habari (kifungu 19), haki ya kujumuika na kuunda vyama (kifungu 20), haki ya kupiga kura (kifungu 21). Kila mmoja ana haki ya kupewa usalama katika mambo ya kijamii (kifungu 22+25+28), kufanya kazi kwa malipo ya haki (kifungu 23) na kupata elimu (kifungu 26).

Kwa ukaribu likihusishwa na wazo la haki za binadamu, kuna dai kuwa watu wote wana haki sawa kutendewa kama binadamu - bila kujali ujamii wowote, dini, jinsi, ushawishi wa kidini, au heshima ya kijamii au kiuchumi iwezavyo kuwa. Nini ni msingi wa usawa wa binadamu, kama si ukweli kwamba wote waliumbwa na Mungu katika hali ya usawa? Hivyo, hoja ya Kikristo kwa haki za binadamu ni lazima ianze na historia ya Biblia ya Uumbaji, "Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa

mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba" (Mwa. 1:26-27). Ukweli kwamba Binadamu aliumbwa katika mfano na sura ya Mungu unamfanya ashiriki jukumu kubwa katika mahusiano na binadamu, mtu kwa mwenzake, Kwa mfano, Mwa. 9:16 inamhitaji mwuaji kuadhibiwa kwa kuwa uuaji huharibu mfano au sura ya Mungu.

Uumbaji upo kwa ajili ya utukufu wa Mungu na una maana yake kutoka kwa Mungu. Ukweli huu unashikilia zaidi "Taji ya Uumbaji", Binadamu aliumbwa kwa mujibu wa amri ya Mungu ya Uumbaji ili kutimiza jukumu alilopewa na Mungu. Mungu alimfanya awe mtawala juu ya dunia, bali pia alimpa wajibu wa kuhifadhi viumbe wa dunia. Mtunga Zaburi aandika, "**Umemfanya kuwa mtawala juu ya kazi za mikono yako, umeviweka vitu vyote chini ya miguu yake; kondoo na ng'ombe wote pia, na wanyama wa kondeni**" (Zab. 8:6-7).

Kwa sababu hii, haki za binadamu hujumuisha tu yale mapendeleo ambayo Mungu amempa Binadamu, hakuna haki nyingine ambazo binadamu anaweza kuchagua au kudai mwenyewe, kwa matakwa yake mwenyewe.

Kwa hiyo Wakristo hawawezi kujiambatanisha moja kwa moja na orodha ya haki za binadamu zilizotengenezwa na nchi za Magharibi badala ya zile za Biblia. Maandiko hueleza haki za taratibu za Kimahakama zilizopangwa kwa mujibu wa sheria zilizoelezwa vema, kwa kusikiliza mashahidi, kwa mahakimu ambao hawajapewa rushwa na kwa ulinzi wa kisheria, kama tutakavyoona. Hata hivyo, milolongo hiyo ya kisheria haiwezi kujibainisha na utekelezaji wa haki za Kimagharibi. Fikiri ingekuwa hivyo- ingejibainisha na mfumo upi? Mfumo wa Kijerumani, Kiingereza, Kifaransa au Kimarekani? Sote tunajua kuwa mifumo hii ni tofauti sana! Kuna nafasi kubwa kwa aina ya mifumo ya kisheria ambayo hutofautiana kwa sababu za kitamaduni na mapokeo ya kihistoria ya watu wake, lakini bado zinatoa hakikisho la haki za binadamu.

Mizizi ya Kikristo ya Haki za Binadamu

Hakuna yeyote awezaye kubisha ukweli kwamba haki za binadamu zilizotolewa kumlinda mtu, zinatoka katika fikra za Kikristo. Kwa uwazi, Azimio Kuu la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa la Desemba 10, 1948 linadhihirisha mizizi yake katika Ukristo. Ukomeshwaji wa utumwa na mateso, kanuni ya usawa mbele ya sheria, haki ya kupumzika na kuburudika kama zinayoonekana katika Sabato au pumziko la Jumapili - zinatokana na mapokeo ya Kikristo na wala si bahati au serikali ambazo zinakubali haki hizi na kuzitia nanga (kuziweka kuwa sehemu) katika katiba zao nyingi kwa wingi katika nchi za Kikristo. Hata Karl Marx alikubali hili, kwa sababu alipinga haki za binadamu kwa kuwa ni zao la Ukristo (kwa mfano, Kazi za Marx na Engels, Kitabu cha 1 = Marx and Engel Works, Vol. 1).

Hakuna serikali wala hakuna mfumo wa kisheria uwezao kuendelea kuwepo pasipo kuwa na amali chache za kawaida, na kwa umuhimu kabisa amali zilizokitwa katika vitu visivyoonekana. Mfumo wa kisheria hukubali mfumo wa

amali, kwa kuwa sheria huchukuliwa kutoka katika viwango vya maadili vilivyotangulia kuwepo na nje yake yenyewe.

Hakikisho la utu wa binadamu huona kwamba Binadamu ni zaidi ya kile anachokielewa juu yake mwenyewe. Hawezi kueleweka kwa njia na nyenzo za sayansi asilia. Yeye yu wazi kwa vitu visivyoonekana. Serikali ya kisiasa, yenye mfumo wa kisheria, hutegemea mahitaji ambayo yenyewe haiwezi kudhamini.

Mwako au Msamaha na Toba?

Kwa mujibu wa falsafa za Mwako katika karne ya kumi na nane, ambazo zilijaribu kuanzisha haki za binadamu pasipo Mungu na kinyume cha Kanisa; Mema yote, ukijumuisha haki za binadamu zingeweza kuchotwa kutoka katika Asili na kutoka katika Fikra. Utambulishi wa Rousseau wa 'Fikra' na 'Asili' ni wa kipekee katika mawazo ya Mwako. Hata hivyo, jaribio la kuziweka haki za binadamu katika Asili zimeshindwa kwa kuwa hakuna mtu yeyote awezaye kukubaliana juu ya maana ya 'Asili' au juu ya jinsi sheria zake zinavyoweza kuvumbuliwa. Wolfgang Schild, profesa wa sheria ya jinai anaaandika, "Mwako hauwezi na haupaswi kuwa neno la mwisho, neno letu la mwisho. Ufikra na utendaji wake ni lazima uchukuliwe katika mipaka yake, kama sivyo maisha ya kijamii yenye thamani ya utu wa Binadamu hayawezekani. Tena, hata sheria ya adhabu kipekee haiwezi kujizuia yenyewe kwa njia ya fikra ili kupata amani na utaratibu kwa gharama yoyote ile: inahitaji utambuzi wa utu wa binadamu - hata wa mtu aliyetenda kosa baya kabisa la jinai - kama msingi wake na mpaka wake".

Mawazo kwamba binadamu angeweza kuboreshwa kwa elimu, na kwamba magonjwa ya binadamu yangeweza kutatuliwa kwa Mwako, ni tatizo la kimsingi la falsafa ya Kigriki, ya Uyumanisti na ya Mwako. Njozi za Uyumanisti katika elimu hudai uwepo wake kwenye wazo kuwa maadili yangeweza kukuzwa kupitia elimu, kwa kuwa unadhani kwamba mtu hufanya makosa tu kwa sababu yeye ni mjinga au kwa sababu hufikiri kimakosa, sio kwa sababu dhamiri yake ni yenye uovu na kwa sababu yeye hawezi kufanya jema kwa nguvu zake mwenyewe. Falsafa hizi hujaribu kupunguza mtazamo wa kimaadili na wa kiwajibu wa mawazo, maneno na matendo kwa suala la maarifa, ambayo humfanya binadamu kuwajibika, pindi tu ajuapo kile afanyacho.

Hata hivyo bado tunashangazwa kujifunza kwamba madaktari huvuta sigara kwa wingi kama watu wa kawaida wafanyavyo, kwamba watu wanaendeleza mitindo ya maisha isiyo salama kwa afya, na kwamba wanawake daima wanaendelea kupata mimba kinyume na mafuriko ya taarifa juu ya uzazi wa mpango. Sote twajua kutoka katika maisha yetu wenyewe, kwamba kujua jibu sahihi, na hata kushawishiwa nalo, hakuhakikishi kwa njia yoyote kuwa twaishi ipasavyo. Mwanasiasa ambaye anatetea kwa nguvu ndoa ya mke mmoja kama msingi wa jamii bungeni, haoneshi umuhimu wa uaminifu wa ndoa katika maisha yake binafsi, na wala hana kinga dhidi ya uzinzi au talaka.

Biblia hufundisha kwamba dhambi ya mtu huathiri sio tu mawazo yetu, bali pia ubinadamu wetu wote, na kwamba zaidi ya yote, dhamiri zetu ambazo zinapingana na Mungu hutuongoza kutenda na kufikiri kimakosa, hivyo basi

kuna upungufu katika mawazo na kujali kwetu zaidi. Ni lazima tuondoe utu wa kale ulioshikwa na dhambi hapo kale. Wakristo huamini kuwa ni Mungu yeye mwenyewe alikufa kuchukua nafasi ya Mwanadamu, wakati Kristo alipokufa juu ya Msalaba kwa ajili ya ukosefu wetu wa upendo na ubinafsi wetu. Wakati tunapokubali kwamba hatuwezi kujiokoa wenyewe kwa nguvu zetu na kwa fikra zetu, bali twategemea utimilizi wa Kristo wa adhabu yetu, twaweza kushinda dhamiri zetu zilizo ovu kwa imani iliyo katika Yesu, na kufanya upya dhamiri zetu na fahamu zetu kwa namna ya mapenzi ya Mungu (Rum. 1:20-25; 12:13). Ufanywaji upya wa kweli hutokea wakati nguvu ya Mungu hufanya kazi katika utu wetu wa ndani; sio kupitia kampeni za kielimu, bali kwa upendo wa Mungu na Msamaha.

Haki za Binadamu Hutangulia Serikali

Utu wa binadamu na haki za binadamu ni sehemu ya mtu kama kiumbe cha Mungu. Hivyo, Serikali haiumbi haki za binadamu, huzifuma na kuzilinda. Kwa kuwa haki ya kuishi iko katika asili ya binadamu, mtu hazipokei kutoka kwa serikali, na hakuna Serikali yenye haki kuamua kwamba raia wake hawana tena haki ya kuishi, bali wanaweza kuuawa kwa matakwa ya mtawala. Wala serikali haiwezi kutoa haki ya kuwa na familia, kwa kuwa Serikali haimiliki familia, yenyewe inakubali tu jukumu lililowekwa katika utaratibu wa Uumbaji kulinda ndoa na familia.

Kwa hiyo kuna haki zilizokuwepo kabla ya serikali, na kuna haki zilizo juu ya Serikali, haki zichukuliwazo kutoka katika asili, na zote kutoka katika asili ya mwanadamu na kutoka katika aina mbalimbali za jamii ya mwanadamu. Serikali ni lazima iheshimu haki hizi na kukubali mipaka iliyowekwa kwa haki hizi za asili za Mungu kwa mtu, familia mwajiri (au mwajiriwa!) na za makundi mengine ya jamii ya mwanadamu.

Kwa kuwa haki za binadamu zina mizizi katika mfumo maadili unaoelezwa na Serikali, kwa usawa mfumo huu huzuia rufaa za kimakosa kwa haki za binadamu, kwa sababu unalinda utu wa binadamu na wengine. Kwa mfano, hakuna mtu mwenye haki ya kuonesha utu wake kwa kuua au kuchoma mali kwa makusudi ili kupata malipo ya bima.

Haki za binadamu huchukulia Serikali kuwa na nguvu zenye mipaka na sheria halali kwa watu wote, sheria ambayo inaweka mipaka ya nguvu ya serikali. Kama jambo hili lisingekuwa hivyo, ni hakika mtu angepokea haki zake kutoka kwa serikali. Hivyo mtu angekuwa tu na haki na madai ya ulinzi ambayo serikali yake ingemhakikishia. Huu ndio mtazamo wa Kishoshalisti, ambao hautoi nafasi kwa changamoto au kujisahihisha kwa serikali ambayo ilijitangaza yenyewe kuwa Mungu.

Maana ya Warumi 13

Andiko muhimu kabisa juu ya jukumu la Serikali ni sura ya kumi na tatu ya Waraka kwa Warumi, ambao uliandikwa na mtume Paulo, aliyeuleta Ukristo Ulaya na Asia katika karne ya kwanza B.K. “Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu;

kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu. Hivyo amwasiye mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu; nao washindanao watajipatia hukumu. Kwa maana watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema, bali kwa sababu ya matendo mabaya. Basi wataka usimwogope mwenye mamlaka? Fanya mema, nawe utapata sifa kwake; kwa kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu kwako kwa ajili ya mema. Lakini ufanyapo mabaya, ogopa; kwa maana hauchukui upanga bure; kwa kuwa ni mtumishi wa Mungu, amlipizaye kisasi mtenda mabaya kwa ajili ya ghadhabu. Kwa hiyo ni lazima kutii, si kwa sababu ya ile ghadhabu tu, ila na kwa sababu ya dhamiri. Kwa sababu hiyo tena mwalipa kodi; kwa kuwa wao ni wahudumu wa Mungu, wakidumu katika kazi iyo hiyo. Wapeni wote haki zao; mtu wa kodi, kodi; mtu wa ushuru, ushuru; astahiliye hofu, hofu; astahiliye heshima, heshima" (Warumi 13:1-7).

Kifungu hiki huonesha wazi kuwa hakuna mtu apingaye serikali kwa kanuni zinazoweza kupinga mamlaka ya Mungu. Kinyume chake: anapinga sheria ya Mungu, na ana haki ya kuchukuliwa hatua za kisheria (Rum. 13:2). Kwa kuwa Serikali inalo jukumu la kuzuia na kuadhibu uovu, Wakristo wanapaswa kufanya wema, kama wanataka kuepuka mgongano. Ikiwa Mkristo anafanya makosa anapaswa kuadhibiwa kwa haki na Serikali. Kwa kuwa Serikali, kama mtumishi wa Mungu, inao wajibu wa kulipa kisasi (13:4). Matokeo yake, Mkristo hulipa kodi yake na hutoa heshima inayostahili kwa maofisa wa serikali (13:6-7).

Lakini swali ni kuwa, ni nani anayetoa maana ya kipi kizuri au kibaya? Je, Paulo aliliacha hili mikononi mwa Serikali? Je, Serikali yaweza kutangaza kitu chochote kizuri na kulazimisha kwa raia wake? Hapana. Wakati alipoongea juu ya uzuri, anaufasili kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu, na kuufasili ubaya kama kitu kile ambacho kilihukumiwa na sheria ya Mungu. "haki huinua taifa, bali dhambi ni aibu ya watu wowote" (Mith. 14:34).

Hivyo Biblia hutupa mipaka na maelekezo yaliyo wazi kwa kodi, huduma za kiulinzi na kwa polisi. Kwa mfano, Yohana Mbatizaji aliwaambia watoza ushuru na mapolisi (mtu yule yule alitumika kama polisi na mlinzi), "Msitoze kitu zaidi kuliko mlivyoamriwa" na "Msidhulumu mtu, wala msimshitaki kwa uongo; tena mtoshewe na mshahara wenu" (Lk. 3:12-14).

Kutoka katika matamko haya ya Paulo twaweza kuchota mawazo mawili muhimu:

1. Serikali yaweza tu kuhukumu kile watu wafanyacho, sio kile wanachofikiri. Inahusika kwa matendo mema au mabaya, kwa kufanya. Si kazi ya serikali kudhibiti dhambi zote, bali zile tu ambazo kazi zake zaweza kuchunguzika na zinaweza kuharibu utaratibu wa umma, ambao Serikali ina wajibu wa kuuendeleza na kuulinda.

2. Serikali haiwezi kutofautisha kati ya Wakristo na watu wengine, yaani waamini wa imani tofauti, iwapo wanaelekeza imani zao katika hali ya amani. Kwa kuwa Mungu huzuia upendeleo katika mambo ya kisheria, Wakristo

ni lazima waadhibiwe kwa ukali uleule sawa na wasio waumini pindi wavunjapo sheria. Serikali haiwezi kutofautisha kati ya Wakristo na washirika wa vikundi vingine vya kidini, kwa kuwa yaweza kuhukumu tu kwa msingi wa matendo.

Haki za binadamu ni za kiulinzi, zinadumu si zaidi sana katika kufasili upendeleo mbalimbali kwa mtu, bali kuipa mipaka nguvu ya Serikali na ya taasisi nyingine ambazo hujishughulisha na maisha ya watu. Kwa sababu hii, Paulo anaweka mipaka ya majukumu ya Serikali kwa nyanja maalumu za maisha, badala ya kuipa haki ya kuratibu na kuadhibu mawazo na maisha ya watu wote.

Serikali haipaswi kujipambanua na jamii, kama serikali za kishoshalisti ambavyo zimefanya tangu Mapinduzi ya Ufaransa. Katika serikali hizo, nyanja zote ukijumuisha familia na Kanisa ziko chini ya Serikali. Jamii ni zaidi ya Serikali. Serikali hazina mamlaka juu ya nyanja zote za kijamii.

Juu ya Utenganishi wa Kanisa na Serikali

Kama ambavyo Serikali haiwezi kulitawala Kanisa au dini, serikali yenyewe pia haiwezi kuwa chini ya kanisa au dini. Utenganishi kati ya Kanisa na Serikali haupingani na imani ya Kikristo, bali kwa asili yake huibuka kutoka katika imani hiyo, kwa kuwa Biblia inaifanya serikali kuwa na jukumu la kusaidia watu kuishi kwa amani, bila kujali chochote waaminicho. Ni wajibu wa kanisa na wa dini kuelekeza kwenye umilele, kutoa uimara wa maadili na kuchochea moyo wa mahusiano baina ya mtu na Mungu.

Hivyo, mwanahistoria Eugen Ewig huzungumzia fundisho la Agano la Kale la Mamlaka mbili. Eduard Eichmann, pia ni mwanahistoria, akiandika juu ya mgawanyo wa mamlaka katika Agano la Kale baina ya kuhani na mfalme anasema, “Sambamba na Maandiko Matakatifu mitazamo ya Agano la Kale imekuwa mali-shirika ya Mkristo wa Magharibi”.

Yesu alithibitisha utengano huu katika maneno, “mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na yaliyo ya Mungu mpeni Mungu’ (Mk. 12:17). Kwa sababu sheria hii imekuja kutoka kwa Mungu, ambaye yu juu ya mfalme, taasisi za kidini za Mungu zilizomo duniani, watu wa Mungu waliojiweka pamoja, hawako juu ya mfalme. Kipaumbele cha kwanza ni utii kwa Mungu, ambaye hutambua na kuweka mipaka ya kile kilicho cha Kaisari. Kaisari hana mamlaka ya kutambua na kuweka mipaka ya kile kilicho cha Mungu. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba mtawala ni tegemezi kwa Kanisa, kwa kuwa Mungu amekwisha kumpa wajibu kwa watu wote katika utwala wake, sio tu waamini wa kundi moja la kidini.

Utengano baina ya Kanisa na Serikali haumaanishi kwamba daima majukumu hayaingiliani, au kwamba taasisi hizo hazihitajiani. Kinyume chake, Kanisa laweza kuishauri serikali na kuifundisha Sheria ya Mungu, kama Yehoyada alivyomfundisha Yoashi, “Yoashi akafanya yaliyo mema machoni pa BWANA siku zake zote Yehoyada kuhani alizomfundisha” (2 Fal. 12:2). Ni jambo baya kwamba Kanisa la sasa limetupilia mbali huduma hii muhimu na linapendelea kujiunga na makundi mbalimbali na kulalamika.

Utenganishi wa Kanisa na serikali hauwi vita dhidi ya Ukristo hadi pale Serikali inaposahau jukumu lake katika Sheria ya Mungu na kuanza kuitesa imani.

Mungu Hana Upendeleo

Karne nyingi zilizopita katika Biblia, Mungu alifanya hatua halali za kisheria za haki za binadamu. Hakimu mwenye haki ni wa muhimu katika kuitambua haki, na Mungu ni mfano wa kwanza na asilia wa hakimu mwenye haki (Kumb. 10:17-18; Zab. 7:9+12; 9:5; 50:6, Tazama pia Zab. 75:3+8), "kwa maana BWANA ni Mungu wa hukumu" (Isaya 30:18). Yeye ni mlinzi wa haki. Wale wahukumuo kwa halali hutenda katika Jina la Mungu. Agano la Kale hutueleza juu ya mfalme mwenye haki Yehoshafati, "**Akawaambia mahakimu, zingatieni kile mfanyacho; kwa kuwa hamhukumu kwa ajili ya mtu, bali kwa ajili ya BWANA, ambaye yu pamoja nanyi katika hukumu. Hivyo basi sasa hofu ya BWANA iwe juu yenu; zingatieni na mfanye; kwa kuwa hakuna uovu kwa BWANA Mungu wetu, wala kujali nafsi za watu, wala kupokea zawadi**" (2 Nya. 19:6-7).

Hakimu ni lazima awe macho juu ya ukweli kwamba Mungu anamtazama na husimama upande wa mwenye haki, "Kuipotosha hukumu ya mtu mbele zake aliye juu, na kumnyima mtu haki yake, hayo Bwana hayaridhii kabisa" (Maombolezo 3:35-36).

Kwa sababu hii Biblia ina maelekezo mengi kuhusu haki, hatua za kisheria zimhusuzo binadamu. Kwa mfano, mashtaka huhitaji walau mashahidi wawili (Hes. 35:30; Kumb. 17:6; 19:15; Mat. 18:16; Yoh. 8:17; Ebr. 10:28; 1 Tim. 5:18), hivyo basi mashtaka yanaletwa na mashahidi wawili au watatu (Kumb. 10:17-18). Washitaki wenye vurugu hawapaswi kusikilizwa (Zab. 35:11).

Mahakimu wanaoongoza wanapaswa kutokuwa na upendeleo kabisa (Kumb. 1:16; 2 Nya. 19:7; Mith 18:5; 24:23; Ayu. 13:10; Kol. 3:25; Efe 6:9), kwa kuwa Mungu mwenyewe hana upendeleo (Kumb. 10:17-18). Ni mahakimu waovu tu walio na upendeleo (Isa. 10:1-2; 3:9).

Hukumu inapaswa kufanywa pasipo mawazo ya haraka haraka yasiyothibitishwa (1 Tim. 5:21), bali baada ya hakimu akiwa amekwishachunguza kwa makini uthibitisho wote (Kumb. 17:4). "Fanyeni hukumu za kweli", Mungu anasema katika Zekaria 7:9; hivyo basi hukumu haipaswi kubatilishwa.

"Pakiwa na mashindani kati ya watu, wakaenda maamuzini, na hao waamuzi wakaamua; na wampe haki mwenye haki, na wamhukumie makosa yule mwovu" (Kumb. 25:1). Rushwa haipaswi kuathiri maoni ya hakimu. "Asiye haki hutoa rushwa kifuani, ili kuzipotosha njia za hukumu" (Mith. 17:23). Mungu ni mfano mkuu. "Kwa maana BWANA, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa mabwana, Mungu mkuu, mwenye kuogofya, asiyependelea nyuso za watu, wala hakubali rushwa" (Kumb. 10:17). "Basi sasa hofu ya BWANA na iwe juu yenu; angalieni mkaifanye; kwa maana kwa BWANA, Mungu wetu, hapana uovu, wala kujali nafsi za watu, wala kupokea zawadi' (2 Nya. 19:7).

Kwa ujumla, Maandiko yanahalalisha zawadi zinapotolewa kwa furaha au kuwasaidia watu. Wakati mwingine Biblia inatambua kuwa zawadi zaweza kuwa muhimu, ikiwa watu wanatakiwa kufikia lengo halali. Mwalimu mwema anatueleza, 'Zawadi ya mtu humpatia nafasi, humleta mbele ya watu wakuu' (Mith. 18:16) na "kipawa cha siri hutuliza hasira; na rushwa bindoni humaliza ghadhabu kali' (Mith. 21:14). Mtu mwenye haki anapokabiliwa na maofisa mafisadi, hana tumaini la kufikia malengo ya kisheria kwa ukamilifu. Ikiwa hana nafasi ya kushinda ufisadi huu kwa njia yoyote ile, anaweza kupata haki zake kwa kutumia zawadi. Ni wakati tu anunuapo ufisadi, yeye mwenyewe anahukumiwa hatia ya ufisadi. Yule anayelazimishwa kuwapa rushwa wengine kwa hakika atajibidisha kuondoa ufisadi, hususani katika kanisa, au katika taasisi nyingine za kidini.

Kwa sababu hii, ni lazima kusiwepo na vipimo viwili linganifu, kama vile vifungu vya sheria vinavyohusu matajiri na vingine vinavyohusu wakulima. Agano la Kale lilihitaji mfumo sawa wa adhabu kwa ajili ya wananchi (wazawa) na kwa wakazi wageni (Kut. 12:49), "Msitende yasiyo haki katika hukumu, usimpendelee mtu maskini, wala kumstahi mwenye nguvu; bali utamhukumu jirani yake kwa haki" (Law. 19:15). Kwa sababu Mungu hulinda 'madai ya maskini' (Mith. 29:7) na 'maskini na wahitaji' (Mith. 31:9), Mithali 31:8-9 inatuamuru sisi "Fumbua kinywa chako, kwa ajili yake aliye bubu; uwatetee watu wote walioachwa peke yao; fumbua kinywa chako, uhukumu kwa haki; uwapatie maskini na wahitaji haki yao".

Hivyo Biblia hupima haki ya nchi kwa jinsi iwalindavyo walio dhaifu. Sio tu hali ya utajiri au daraja la viongozi iliyo muhimu, bali pia hali ya Kanisa la Kiserikali ni muhimu, tena hali ya vikundi vidogo vya Kikristo nayo pia ni muhimu. Sio tu hali ya mahakimu wenye fedha na mamlaka kulinda haki zao iliyo muhimu, bali pia hali za maskini, wajane na mayatima wawapo mahakamani.

Mungu ni Mwumba na Bwana wa wanadamu wote. Anatutarajia tutendeane sisi kwa sisi kama mfano (sura) wake na viumbe wake - binadamu wa kujishughulisha na binadamu, si wanyama kwa wanyama.

Kiambatanisho 2: Imani ni Haki ya Binadamu

Thomas Schirrmacher. "Glauben ist ein Menschenrecht". ai-Journal (Jarida la Amnesty International Germany) 8/2006:6-9

(Imetafsiriwa kwa Kiswahili na Joseph SM Ipimilo)

Katika nchi nyingi duniani, watu bado wanapitia mateso na kubaguliwa, kwa sababu wako katika kundi fulani la kidini. Uhuru wa kidini na haki za binadamu zina mahusiano ya karibu sana - nchi zinazozuia uhuru wa kidini kwa kawaida pia huvunja haki zingine za binadamu.

Donato Lama, Mfilipino Mkatoliki, amekuwa akifanya kazi huko Saudi Arabia kwa miaka kumi na mitano, wakati polisi wakipekua nyumba yake mwezi Oktoba 1995, walipata picha yake akiwa katika maombi. Wakimtia hatiani kwa kufanya uinjilisti, alikamatwa, na kutiwa gerezani pasipo mawasiliano na ulimwengu wa nje, akifungwa minyororo na kupigwa. Katika Desemba 1996, alihukumiwa kwenda jela kwa mwaka mmoja na nusu na viboko sabini.

Katika takwimu zake za nusu mwaka kwa mwaka 2000, Christian Organisation Open Door (Taasisi ya Kikristo ya Fungua Milango) iliitaja Saudi Arabia kuwa nchi yenye uhuru mdogo kabisa wa kidini. Taarifa ya 1999 ya Serikali ya Marekani juu ya uhuru wa kidini inasema hivi kuhusu Saudi Arabia: "Uhuru wa kidini haupo. Uislamu ni dini ya kiserikali na raia wote wanapaswa kuwa Waislamu. Serikali inazuia kitendo cha hadhara kwa dini nyingine. Ibada binafsi kwa watu wasio Waislamu zinaruhusiwa....Chini ya Shari´a (sheria ya Kiislamu), ambayo kwayo serikali huchota falsafa yake, kuongoka kwa Mwislamu kuingia dini nyingine kunachukuliwa ni uasi. Uasi wa umma ni kosa linalohukumiwa kwa kifo ikiwa mtuhumiwa hataikana imani yake mpya." (www.state.gov/g/drl/irf). Hata ikiwa kihalisia wachache wanashawishika ili kuwaongoa Waislamu - matukio hayo kwa uchache sana huwekwa hadharani - sheria hii huvunja ibara ya 18 ya Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (UNO, 1948), ambalo kwa uwazi linajumuisha haki ya kubadili dini. Wakristo kipekee wanatishwa na ukosefu wa uvumilivu wa Saudi Arabia dhidi ya dini nyingine. Wengi wa Wakristo huko Saudi Arabia ni wafanyakazi wa kigeni. Wafilipino wa Kikatoliki na Kiinjili, kipekee na mara nyingi hudunishwa, na huwekwa jela kwa miezi, wakiteswa na kufukuzwa nchini.

Ibara ya 18 ya Azimio la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (UNO, 1948)

"Kila mmoja ana haki ya uhuru wa mawazo, dhamiri na dini; haki hii hujumuisha uhuru wa kubadili dini yake au imani, na uhuru, ama akiwa peke yake au katika jamii pamoja hadharani au faragha, kudhihirisha dini yake au imani katika mafundisho, matendo, ibada au utii."

Si tu wasio Waislamu wanaoteseka – vikundi vya Kiislamu visivyokubaliana na shule ya Hanbalic yyy?, kama vile Washia na vikundi (sects) vya Kiislamu pia vinashambuliwa na polisi wa kidini 'Muttawwa'. Mateso hayo ya vikundi vya kidini mbali na dini ya serikali hutokea katika nchi nyingi. Tabia nyingine ya kidunia yaweza kuonekana huko Saudi Arabia vilevile. Kesi zinazoshughulika na uhuru wa kidini mara kwa mara huachwa mikononi mwa Polisi wa siri badala ya kupelekwa mahakamani.

Katika nchi ambazo huweka mipaka ya uhuru wa kidini, haki nyingine za binadamu hupuuzwa pia. Kuna mahusiano ya karibu kati ya mambo haya mawili. Mamilioni huteseka na uvunjwaji wa haki zao za kibinadamu kwa sababu tu wako kundi fulani la kidini.

Uhuru wa kidini ni haki ya msingi ya binadamu. Ibara ya 2 ya Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu linalaani ubaguzi wa ujamii*, rangi, jinsi, lugha, ushawishi wa kisiasa au kidini. Ibara ya 18 inafasili maana ya kilicho kwenye uhuru wa mawazo, dhamiri na dini (angalia juu).

Haki za binadamu na uhuru wa kidini vina chanzo kimoja, Katalogi za kwanza za haki za binadamu ziliundwa huko Ufaransa katika kupinga ukatili wa kanisa. Huko Marekani kimsingi zilibuniwa na watu waliokuwa wamekimbia mateso ya kidini huko Ulaya. Hitaji la uhuru wa kidini hatimaye limeshawishi kwa nguvu maendeleo ya wazo la haki za binadamu.

Kwa miaka mingi, suala la uhuru wa kidini lilikuwa umetiwa kivuli na mambo ya Kikomusiti. Tangu anguko la Umoja wa Kisovieti, hata hivyo, nchi za Kiislamu ambazo huwatesa raia wake kwa misingi ya kidini zimevuta hisia.

